# ULINGANUZI WA USEMI WA KISIASA KATIKA KAMPENI ZA URAIS NCHINI KENYA MIEZI MITANO KABLA YA CHAGUZI ZA MWAKA WA 2007 NA 2013

**KARIITHI FRANCIS M.**

**Ripoti hii ya Utafiti Imetolewa kwa Kitengo cha Shahada za Juu ili Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamifu katika Isimu Tumikizi.**

**CHUO KIKUU CHA LAIKIPIA**

**NOVEMBER 2015**

## UNGAMO NA IDHNINI

### UNGAMO

Ripoti hii ya utafiti ni kazi yangu mwenyewe na haijawasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo chochote kile.

Francis Kariithi M.

Sahihi………………………….. Tarehe…………………………..

MDK32/2183/11

IDHINI YA WASIMAMIZI

Ripoti hii ya utafiti imewasilishwa kwa ajili ya kutimiza baadhi ya mahitaji ya shahada ya Uzamifu katika Isimu Tumikizi katika Chuo Kikuu cha Laikipia kwa idhini yetu kama wasimamizi:

Prof. Francis Aswani

Sahihi……………………………… Tarehe……………………..

Idara ya Fasihi na Mawasiliano
Chuo Kikuu cha Laikipia

Prof. James Ogola Onyango

Sahihi……………………………… Tarehe……………………..

Idara ya Fasihi na Mawasiliano
Chuo Kikuu cha Laikipia

## HAKIMILIKI

Haki zote zimemilikiwa: Sehemu yoyote ya tasnifu hii isinakilishwe, kuhifadhiwa au kutumiwa kwa njia yoyote ile bila ya kibali kutolewa na mtafiti au Chuo Kikuu cha Laikipia.

©Hakimiliki, 2015

Francis Kariithi M

## TABARUKU

Ninaitabaruku kazi hii kwa mke wangu Irene Wangari, wanangu Rick Kariithi, Isaac Mwangi, Charles Gichuhi na aila yangu yote kwa kunihimiza na kuzivumilia kero zangu wakati wa kuishughulikia kazi hii.

# IKISIRI

Tangu maajilio ya vyama vingi vya kisiasa nchini Kenya lugha imekuwa ikitumiwa kama zana ya kisiasa na kijamii katika kukuza ushindani na kukolezea mikakati ya usemi wa kikabila ambao hunuiwa kutoa nafasi kwa mwanajamii kuyasimbua masuala fulani ya kijamii akilenga faida imrudie yeye. Kutokana na mabadiliko kadhaa ya kisheria ambayo yalitokea nchini Kenya baada ya uchaguzi wa 2007, haikuwa dhahiri ikiwa wanasiasa wangeusitiri usemi wao, kwa kuhofia kufunguliwa mashtaka endapo ingebainika kuwa usemi wao ungekuza chuki baina ya jamii mbalimbali nchini. Utafiti huu ulilinganua usemi wa wanasiasa miezi mitano kabla ya chaguzi za mwaka wa 2007 na 2013. Malengo ya utafiti huu yalikuwa kuzichunguza mada tofauti za usemi katika kampeni za urais nchini Kenya katika kipindi kilichokuwa chini ya utafiti huu. Utafiti huu vilevile ulijadili mikakati tofauti tofauti iliyotumiwa na wanasiasa katika kampeni za urais nchini Kenya; na kutathmini athari za usemi wa wanasiasa katika kampeni hizo. Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi (UHU): Usemi – Mkabala wa Kihistoria (UMK) ilimwongoza mtafiti, ambapo mbinu ya maelezo ndiyo iliyotumiwa kuichanganulia data. Wanasiasa waliolengwa walikuwa Raila Odinga, Uhuru Kenyatta na William Ruto. Data ilikusanywa kwa njia ya kimakusudi (usampulishaji wa matukio kiuhakiki) kutoka kwenye magazeti ya *The Daily Nation* na *The Standard* ambamo nukuu za usemi wa wanasiasa hao za miezi mitano kabla ya chaguzi za mwaka 2007 na 2013 zilichanganuliwa. Mada za Usemi katika kampeni zilikuwa msingi wa uchanganuzi wa data husika. Ilibainika kuwa uteuzi wa mada za usemi huongozwa na masuala nyeti ya kihistoria katika jamii kama vile ardhi na masuala mengine ibuka. Aidha, ilibainika kuwa wanasiasa huiteua mikakati mbalimbali ambayo malengo yake huwa ni kuishawishi jamii; isitoshe, imedhihirika kwamba usemi huo wa kisiasa ulikuwa na athari kadhaa; kama vile, kujikariri kwa masuala ya kihistoria, kuzalika kwa miungano ya kikabila, kuibuka kwa usemi wa kitabaka, kuibuka kwa usemi wa kidini na kuchipuka kwa usemi wa kuumbuana miongoni mwa matukio mengine mengi. Utafiti huu umeonyesha kuwa lugha ni kiashiria cha masuala ya jamii na hivyo hali za kisiasa, hivyo basi, lugha inaweza kuonekana kama nguvu ya kuendeshea mabadiliko ya kisiasa na kijamii. Inatarajiwa kwamba utafiti huu ni mchango katika kuukuza uwanja wa uchanganuzi wa usemi wa kisiasa hasa ulinganuzi wa usemi wa kisiasa. Mwisho, inatarajiwa kuwa matokeo yatachangia katika kuyaelekeza mashirika mbalimbali ambayo yamepewa majukumu kuhakikisha kuwa uwajibikaji na utangamano unaafikiwa nchini kwa kubainisha pale mpaka wa 'usemi wa chuki' unaanzia na kuishia.

## ABSTRACT

Since the advent of multiparty politics in Kenya, language has mostly been used as a political and social weapon, with politicians embracing varied strategies that are aimed at promoting a particular interpretation of a social issue. Following a number of constitutional changes that had taken place in Kenya, it was not clear whether politicians would have been more guarded in their choice of language for fear of being prosecuted for propagating hate speech. In view of the aforementioned, this study set out to undertake a Comparative Political Discourse Analysis during presidential election campaigns five months before both 2007 and 2013 elections. The objectives of the study were to investigate different Discourse Topics during the period under investigation; the study also discussed types of politician's political strategies during presidential election campaigns. The study also examined the impact of politician's political discourse during presidential election campaigns. The theory that guided the study was Critical Discourse Analysis (CDA): Discourse-Historical Approach (DHA). Descriptive method of analysis within the main DHA strategies was employed. Purposeful sampling strategy (Critical case sampling) was used to collect data of politician's reported utterances five months before 2007 and 2013 elections. The main players were; Raila Odinga, Uhuru Kenyatta and William Ruto because during both 2007 and 2013 elections campaign these personalities were among the most pronounced politicians who played a pivotal role during presidential campaigns. The data which was analyzed was collected from *The Daily Nation* and *The Standard* newspapers. The main Discourse Topics employed by the said politicians formed the basis of the analysis. The study found out that the general choice of discourse topics by politicians is guided by society's most salient historical issues such as the land question and vote rigging. The study also established that politicians use selected strategies whose objective is mainly to persuade the electorate. The study found out that this political discourse had several effects on society such as re-awakening the past; with respect to tribal affiliations, elites discourse, religious discourse, and character disparagement discourse just to mention a few. The significance of this undertaking is that; language can be seen as a purveyor of social issues and therefore political situations – and language can also be seen as a driving force directed at changing politics and society. It is hoped that these findings will contribute to the field of discourse analysis; more specifically, comparative political discourse analysis. Finally, the study may inform bodies charged with responsibilities of ensuring that Kenyans' dream of being cohesive and integrated is attained by spelling out where 'hate speech' starts and ends.

## SHUKRANI

Naichukua nafasi hii ya mapema kumrudishia Muumba wa vyote shukrani za kipekee kwa kuniongoza kupitia Roho wake ambaye daima amekuwa nami siku zote za maisha yangu katika ulimwengu huu.

Shukrani zingine zikiendee Chuo Kikuu cha Laikipia kwa kuyafanya masomo yangu kutengenea kupitia wahadhiri wote wa chuo hicho ambao utu wao ulijibainisha na kusheheni mwongozo wa kupigiwa mfano.

Shukrani jazila ziwaendee wasimamizi wangu Profesa Francis Aswani na Profesa James Onyango ambao daima walinihimiza na kuwa karibu nami nilipohitaji kuwaona. Utu wao na ushauri wao hauelezeki; Mola awajalie mazuri kutokana na mioyo yenu safi isiyokuwa na doa wala toa. Daktari Gwachi Mayaka, nakushukuru pakubwa kwa kunisuta na kunikumbusha umuhimu wa kuikamilisha kazi hii; Mungu ausetiri moyo wako huo safi.

Kwa jumla nazitoa shukrani zangu nyingi kwa wahadhiri wote idarani kwa kunifaa kwa njia moja au nyingine; Daktari Jacinta Ndambuki, Daktari Vicky Khasandi na Profesa Felicia Yieke nawashukuru.

Siwezi kumsahau mke wangu Irene Wangari ambaye pamwe na wanangu Rick, Isaac na Charles walikuwa sababu yangu kubwa ya kuishughulikia kazi hii ambayo niliiona kuwa yao. Naomba Ilahi aipe aila yangu moyo thabiti wa kuweza kustahimili yote; kwani 'Penye nia pana njia'. Siwezi kuwasahau kakangu Joseph na dadangu Mary kutokana na mioyo yao safi iliyosheheni upendo na himizo, Mungu aishiye azifanikishe ndoto zenu.

Mwisho, naichukua fursa hii kuwashukuru wote ambao walihusika katika kuhakikisha kuwa ndoto hii yangu imetimilika; huenda uliifanikisha kazi hii sirini; ni ombi langu kuwa Mungu aishiye atakutimizia yote utarajiyayo sirini kwa kuwa Mungu si Mfaki.

## YALIYOMO


UNGAMO NA IDHNINI .......... i

HAKIMILIKI .......... ii

TABARUKU .......... iii

IKISIRI .......... iv

ABSTRACT .......... v

SHUKRANI .......... vi

ORODHA YA GRAFU .......... xii

ORODHA YA MAJEDWALI .......... xiii

UFUPISHO WA MANENO .......... xiv

SURA YA KWANZA .......... 1

UTANGULIZI .......... 1

1. 1 Usuli wa Mada .......... 1

1. 2 Suala la Utafiti .......... 7

1. 3 Malengo ya Utafiti .......... 8

1. 4 Maswali ya Utafiti .......... 8

1. 5 Sababu za Kuiteua Mada .......... 8

1. 6 Umuhimu wa Utafiti .......... 9

1. 7 Upeo na Mipaka ya Utafiti .......... 10

1. 8 Ufafanuzi wa Istilahi .......... 12

SURA YA PILI .......... 14

TAHAKIKI ZA MAANDISHI .......... 14

2. 1 Utangulizi .......... 14

2. 2 Usemi wa Kisiasa .......... 14

2. 3 Itikadi .......... 14

2. 3. 1 Siasa na Itikadi .......... 16

2. 3. 2 Itikadi na Usemi wa Kisiasa ........ 16

2. 3. 3 Miktadha na Hali za Kisiasa ........ 17

2. 4.1 Maandishi ya Ulinganuzi wa Usemi wa Kisiasa ........ 19

2. 4. 2 Maandishi ya Mikakati ya Hila ........ 20

2. 4. 3 Maandishi ya Siasa za Kimbari ........ 24

2. 5. 1 Diskosi ........ 25

2. 5. 2 Matini ........ 25

2. 5. 3 Mwingilianomatini ........ 26

2. 5. 4 Uhusiano wa Mwingilianomatini na Mwingilianouneni ........ 27

2. 5. 5 Mada ........ 28

2. 6 Uchanganuzi Hakiki wa Usemi ........ 29

2. 6. 1 Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi ........ 30

2. 6. 2 Kanuni za Uchanganuzi Hakiki wa Usemi ........ 31

2. 6. 3 Usemi, matini, muktadha, ........ 31

2. 7 Misingi ya Nadharia ........ 32

2. 7. 1 Usemi-Mkabala wa Kihistoria ........ 33

2. 7. 2 Maelezo ya Kijumla Kuhusu Mikakati ya Uchanganuzi wa Usemaji ........ 34

2. 7. 3 Mkakati wa Unominishaji / Urejelezi ........ 35

2. 7. 4 Mkakati wa Uarifishaji ........ 35

2. 7. 5 Mkakati wa Mkabala ........ 36

2. 7. 6 Mkakati wa Ubishi ........ 36

2. 7. 7 Mikakati ya Uzidishaji na Upunguzaji wa Uzito ........ 37

2. 7. 8 Matumizi ya Topoi katika Uchanganuzi wa Ubishi ........ 37

2. 7. 9 Topoi ........ 37

2. 7. 10 Ubainishaji wa Topoi ........ 38

2. 7. 11 Upotoshaji katika Ubishi ........ 38

2. 7. 12 Vifaa vya Uchanganuzi na Kanuni za Usemi – Mkabala wa Kihistoria ......................... 38
SURA YA TATU ........................................................................................................... 40
MBINU ZA UTAFITI ................................................................................................... 40
3. 1 Utangulizi ............................................................................................................. 40
3. 2 Njia za Utafiti......................................................................................................... 40
3. 3 Muktadha wa Utafiti............................................................................................... 40
3. 4 Uteuzi wa Data....................................................................................................... 41
3. 5 Ukusanyaji wa Data................................................................................................ 42
3. 6 Kundi Lengwa........................................................................................................ 42
3. 7 Uchanganuzi wa Data............................................................................................. 43
3. 8 Matumizi ya Grafu ................................................................................................. 45
SURA YA NNE............................................................................................................. 47
UCHANGANUZI WA DATA NA UFASIRI.................................................................. 47
4. 1 Utangulizi .............................................................................................................. 47
4. 2 Uteuzi wa Mada ..................................................................................................... 47
4. 3 Mada za Usemi za Mwaka wa 2007 na 2013........................................................... 48
4. 3. 1 Mada ya Ukabila.................................................................................................. 49
4. 3. 2 Mada ya Ardhi...................................................................................................... 60
4. 3. 3 Mada ya Uchumi wa Nchi.................................................................................... 65
4. 3. 4 Mada ya Uwajibikaji............................................................................................ 70
4. 3. 5 Mada ya Wizi wa Kura ........................................................................................ 74
4. 3. 6 Mada ya Katiba ................................................................................................... 78
4. 3. 7 Mada ya Miungano ya Vyama ............................................................................. 82
4. 3. 8 Mada ya Viongozi wa Awali................................................................................ 88
4. 3. 9 Mada ya Ghasia za Uchaguzi .............................................................................. 94
4. 3. 10 Mada ya Umri wa Wagombeaji.......................................................................... 97

4. 3. 11 Mada ya Nchi za Kigeni ........ 101
4. 3. 12 Mada ya Mahakama ya Hague ........ 104
4. 3. 13 Mada ya Kura ya Maoni ........ 107
4. 3. 14 Mada ya Mitafaruku katika Vyama ........ 109
4. 3. 15 Hitimisho ........ 113
SURA YA TANO ........ 114
UFASIRI, MJADALA NA MAELEZO ........ 114
5. 1 Utangulizi ........ 114
5. 2 Mikakati ya Usemi katika Mwaka wa 2007 na 2013 ........ 114
5. 3 Mkakati wa Urejelezi/ Unominishaji katika Kampeni ........ 115
5. 4 Mikakati ya Uarifishaji ........ 128
5. 4. 1 Ujumuishaji ........ 130
5. 4. 2 Utatanishaji ........ 134
5. 4. 3 Ujenzi wa Siasa ........ 139
5. 4. 4 Uwekevishaji ........ 142
5. 5 Mikakati ya Ubishi kwenye Usemi katika Kampeni za Urais ........ 144
5. 5. 1 Utangulizi ........ 144
5. 5. 2 Matumizi ya Topoi katika Mkakati wa Ubishi ........ 145
5. 5. 3 Topoi za Ubaguzi ........ 145
5. 5. 4 Topoi za Hila/Wizi katika Upigaji Kura ........ 150
5. 5. 5 Topoi za kutahadharisha ........ 152
5. 5. 6 Topoi za Ufisadi ........ 156
5. 5. 7 Topoi za Kudhihaki ........ 158
5. 5. 8 Topoi za Nambari/idadi ya Wapigaji Kura ........ 160
5. 5. 9 Topoi za Mzigo/Uhalifu ........ 161
5. 5. 10 Hitimisho ........ 163

5. 6 Mkakati wa Mkabala ........ 164

5. 7 Uongezaji na Upunguzaji wa Uzito ........ 166

5. 8. Hitimisho ........ 173

5. 9 Athari za Usemi wa Kisiasa katika Kampeni za Urais ........ 173

5. 9. 1 Athari ya Usemi wa Raila ........ 176

5. 9. 2 Athari ya Usemi wa Uhuru ........ 186

5. 9. 3 Athari ya Usemi wa Ruto ........ 197

5. 9. 4 Hitimisho ........ 205

SURA YA SITA ........ 206

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 206

6.1 Utangulizi ........ 206

6. 2. Mada za Usemi kwenye Kampeni za Urais ........ 206

6. 2. 1 Aina ya Mikakati katika Kampeni za Urais ........ 209

6. 2. 2 Athari za Usemi wa Wanasiasa kwenye Kampeni ........ 210

6. 3 Hitimisho ........ 211

6. 4 Mapendekezo ........ 213

6.5 MAREJELEO ........ 215

CHETI CHA UTAFITI ........ 226

## ORODHA YA GRAFU

Grafu 1.1: Mada ya Ukabila katika mwaka wa 2007 na 2013…………………………………...59

Grafu 1.2: Mada ya Ardhi Mwaka wa 2007 na 2013…………………………………………64

Grafu 1.3: Mada ya Uchumi wa Nchi Mwaka wa 2007 na 2013……………………………...69

Grafu 1.4: Mada ya Uwajibikaji Mwaka wa 2007 na 2013…………………………………...73

Grafu 1.5: Mada ya Wizi wa Kura 2007 na 2013……………………………………………..77

Grafu1.6: Mada ya Katiba 2007 na 2013……………………………………………………...81

Grafu 1.7: Mada ya Miungano ya Vyama 2007 na 2013……………………………………...87

Grafu 1.8 :Mada ya Viongozi wa Awali 2007 na 2013………………………………………93

Grafu 1.9: Mada ya Mapigano 2007 na 2013………………………………………………....96

Grafu 1.10: Mada ya Umri wa Wagombeaji 2007 na 2013…………………………………100

Grafu 1.11: Mada ya Nchi za Kigeni 2007 na 2013…………………………………………103

Grafu 1.12: Mada ya Mahakama ya Hague 2007 na 2013…………………………………..106

Grafu 1.13: Mada ya Kura ya Maoni 2007 na 2013…………………………………………108

Grafu 1.14: Mada ya Mitafaruku ya Vyama 2007 na 2013…………………………………111

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 4.1: Baadhi ya Mitazamo Chanya na Hasi katika Usemi wake Raila 2007 na 2013……………………………………………………………………………………..119-120

Jedwali 4.2: Baadhi ya Mitazamo Chanya na Hasi katika Usemi wake Uhuru 2007 na 2013…………………………………………………………………………………….123- 124

Jedwali 4.3: Baadhi ya Mitazamo Chanya na Hasi katika Usemi wake Ruto 2007 na 2013……………………………………………………………………………………..127-128

## UFUPISHO WA MANENO

| | | |
|---|---|---|
| TKHB | : | Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu |
| TY | : | Tafsiri Yangu |
| TTHM | : | Tume ya Taifa ya Haki na Maridhiano |
| TUGBM | : | Tume ya Uchunguzi wa Ghasia Baada ya Uchaguzi Mkuu |
| PNU | : | Party of National Unity |
| ODM | : | Orange Democratic Movement |
| TW | : | Tume ya Waki |
| TUU | : | Tume ya Uwiano na Utangamano |
| UHU | : | Uchanganuzi Hakiki wa Usemi |
| KANU | : | Kenya African National Union |
| NARC | : | National Rainbow Coalition |
| UMK | : | Usemi Mkabala wa Kihistoria |
| UH | : | Uchanganuzi Hakiki |
| HKST | : | Halmashauri ya Kitaifa ya Sayansi na Teknolojia |
| TKSTU | : | Tume ya Kitaifa Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi |
| TNA | : | Muungano wa Kitaifa |
| TUMK | : | Tume ya Uchaguzi na Mipaka ya Kenya |
| CORD | : | Coalition of Reform and Democracy |
| URP | : | United Republican Party |
| ODM – K | : | Orange Democratic Movement - Kenya |
| UDF | : | United Democratic Forum Party |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1. 1 Usuli wa Mada

Maajilio ya vyama vingi nchini Kenya mnamo mwaka 1991 kuliibusha kujengeka kwa makundi mawili kinzani, lile la waliokuwa serikalini na lile la upinzani; mgawanyiko huo uliegemeza makundi hayo katika makabila yao (Kimenyi 1997; Muigai 1995). Hivyo basi uchaguzi wa mwaka 1992 ulijikita katika mtazamo wa kikabila; ukweli huo ulijikariri katika uchaguzi wa mwaka wa 1997, (Oyugi 1997; Orvis 2001; Apollos 2001).

Ushindani wa kisiasa nchini Kenya ulikuwa ukitekelezwa kupitia kwa usemi wa kikabila. Madai haya huenda yakawa na mashiko ikiwa itazingatiwa kuwa kampeni za urais husheheni mawazo ambayo hukuzwa kupitia propaganda chungu nzima na usemi wa chuki na ambapo mikakati ya kuwasilishia "madai" hayo huwa imesheheni propaganda ambayo huwa imefinyangwa ikizungukia masuala ya kijamii ambayo aghalabu huwa ya kihistoria au hata ibuka. Malengo ya wanasiasa huwa kufanikisha usimbuzi tarajiwa kwa wanajamii ili kufanikisha kampeni zao; jambo hili huwezekana kupitia lugha ambayo huwa nyenzo muhimu katika kuangazia mada tofauti tofauti ambazo wakati mwingi hugusia jamii pana.

Usemi wa kisiasa katika kampeni za urais nchini Kenya ulituhumiwa kuwa ulikuwa ukipelekea kuibuka kwa usemi wa uchochezi; jambo lililopelekea nchi ya Kenya kukumbwa na mapigano ya kikabila katika uchaguzi wa mwaka 1992 baada ya Kifungu cha 2B cha katiba kubatilishwa na kuifanya Kenya kuwa na vyama vingi vya kisiasa. Habwe (1999) akimnukuu Aristotle, aliangazia kuwa, "…binadamu ni kiumbe wa kisiasa". Kwa sababu siasa ni njia ya maisha kwa binadamu kulikuwa na haja ya kulinganua usemi wa kisiasa katika kampeni za urais miezi mitano kabla ya uchaguzi wa 2007 na miezi mitano kabla ya uchaguzi wa 2013 kutokana na tetesi kuwa uchaguzi wa 2007 ulishuhudia mapigano ya kikabila kutokana na madai kuwa usemi wa kiuchochezi kutoka kwa wanasiasa ulichangia kuzuka kwa ghasia; miaka mitano baadaye Kenya ikajikuta katika uchaguzi uliosadifiana na kuibuka kwa mabadiliko mengi yaliyojumuisha miongoni mwao kuzinduliwa kwa katiba mpya. Matukio kwenye kampeni miezi mitano

kabla ya uchaguzi wa 2007 na miezi mitano kabla ya uchaguzi wa 2013 yalikuwa yametokea nyakati mbili tofauti na kwa ajili ya mapito ya wakati pamwe na historia, umuhimu ulikuwapo wa kuupitia usemi wa wanasiasa katika kampeni za chaguzi hizo mbili.

Siasa zizungukiazo kampeni za urais nchini Kenya hudhihirisha kuibuka kwa masuala mawili makuu ambayo huchochea siasa za urais kuegemezwa kwenye suala la ukabila na lile la utabaka. Masuala haya mawili yalikuwa yakipelekea kutingwa kwa juhudi za kuwapo na uchaguzi huru na wa haki nchini Kenya; mielekeo hii ilikuwa ikisheheni matokeo hasi katika kukua na kukuza demokrasia nchini Kenya. Usemi wa kisiasa wenye kukitwa katika suala nyeti la ukabila lilikuwa bayana nchini Kenya (Tazama 4.3.1 kwa maelezo zaidi); kasi yake ilidaiwa ilikwenda kwa matao ya juu pale suala la siasa na vyama vingi lilipotokea kupata msukumo katika mwaka wa 1992. Kulikuwa na uwiano wa kina kati ya ukabila na mwelekeo wa matokeo ya upigaji kura hasa pale upigaji kura huo uliizungukia kura za urais. Wanasiasa walitafuta uungwaji mkono kupitia usemi wa kikabila kwa kukuza masuala yenye kuzua mhemko. Matokeo ya matumizi ya usemi wa kikabila yalikuwa kuzitenga jamii zilizochukuliwa kuwa ziliufaidi utawala tangulizi.

Ripoti ya Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu (Itarejelewa kama TKHB kwenye kazi hii) kuhusu ghasia za baada ya uchaguzi iliyotolewa mnamo tarehe 15 Agosti 2008 ilieleza kuwa, wanasiasa walichangia katika kuchochea ghasia hizo. Katika ibara ya 356 ya ripoti hiyo, maelezo yao yalikuwa dhahiri:

> Wakati wa kampeni, wanasiasa kutoka pande zote mbili za kisiasa walitumia matamshi ya chuki na maoni ya kuhamakisha ambayo yalichochea chuki na bezo miongoni mwa jamii mbalimbali (TY).
> (KNCHR 2008:356, 95).

Ripoti hii ilidhihirisha kuwa baadhi ya wanasiasa waliutumia usemi au maneno ambayo yalipochunguzwa kwa jicho pevu pasina shaka yalisemwa kuwa yalichangia kukuza mpando wa mhemko katika jamii fulani fulani nchini Kenya:

> Katika mkoa wa Bonde la Ufa wanasiasa kadhaa wanasemekana kuwa walichochea ghasia hizo katika kampeni za kisiasa kwa kuziuliza jamii asilia za mahali pale kuwatimua watu wasio wa jamii ya Kalenjin.

> Wanasiasa hawa waliitumia sitiari kama vile “kungoa madoadoa”. Sitiari kama hizi zilitumiwa katika mkoa wote wa Bonde la Ufa na wanasiasa wa jamii ya Kalenjin. Utumiaji wa nahau kama hii ulipelekea kufurushwa kwa jamii zisizo za Kalenjin kutoka mkoa wa Bonde la Ufa mnamo mwaka wa 1991. (TY)
> (KNCHR 2008:531,134).

Itakumbukwa kuwa, Tume ya Taifa ya Haki na Maridhiano (Itarejelewa kama TTHM) katika ripoti yake ilidokeza kuwa, ili kupelekea kuuthibiti utulivu na amani iliyokuwa imekwisha patikana nchini Kenya baada ya kipindi hicho cha giza baada ya uchaguzi wa 2007; wanasiasa walikuwa na jukumu la kuwapatanisha wananchi kabla ya kuelekea kwenye uchaguzi wa tarehe 4 Machi 2013. Kwa njia nyingine TTHM ilitahadharisha kuwa matumizi ya ‘lugha ya uchochezi’ baina ya makundi tofauti ingechochea uhasama na kurejesha mapiganoo nchini Kenya Barasa (2014).

Wanasiasa na usemi wao walikuwa wepesi wa kuitumia lugha yenye kubeba masuala ya kikabila. Katika mwaka wa 2010 tume hiyo iliwauliza mawaziri wawili na mkereketwa mmoja wa kisiasa kujiwasilisha mbele yao kutokana na dai la kutoa usemi ambao ulikuwa na chembechembe za kuweza kuzua uhasama baina ya jamii katika maeneo yao (*Saturday Nation* tarehe 30 Januari 2010). Washtakiwa hawa hatimaye walifikishwa mahakamani na ambapo kesi yao ilikamilika mwaka wa 2012. Mbunge mwingine ambaye tayari alitokea kufikishwa mahakamani alikuwa wa Mwea na ambaye alikumbwa na shtaka la kutoa usemi uliopelekea kutokea kwa mauaji ya watu wanne katika mpango wa makazi wa Ngariama huko Kirinyaga kusini *Daily Nation*, tarehe 27 Machi, 2010.

Maelezo hayo kwa jumla yaliafiki ukweli kuwa usemi wa wanasiasa ulikuwa na athari kubwa katika jamii. Asher (1992) alisema kuwa matamshi yanayotolewa na mtu huwa na tukio la ghafla au hasi ama chanya. Kutokana na maelezo hayo huwa ni matarajio ya kila mwananchi mzalendo kuwa wanasiasa wangekuwa vyombo vya kuzitangamanisha na kukuza demokrasia nchini Kenya kwa kuitumia lugha ambayo ingezitangamanisha jamii kwa jumla. Mapigano ya kisiasa nchini Kenya yalisababisha Tume mbili kuundwa katika mwaka wa 2008; Tume Huru ya Ukaguzi wa Uchaguzi (Itarejelewa kama THUU) na Tume ya Uchunguzi wa Ghasia Baada ya Uchaguzi Mkuu (Itarejelewa kama TUGBUM).

THUU na TUGBUM zilichunguza masuala yote kuhusiana na uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2007 na kutoa mapendekezo yake.

Tume ya Kriegler iliteuliwa na rais mstaafu Kibaki chini ya kifungu (102) cha sheria cha Tume ya Uchunguzi. Kuundwa kwa Tume hiyo kulihalalishwa kupitia Notisi nambari 1983, katika Gazeti la Serikali la tarehe 14 Machi 2008 la nchi ya Kenya. Tume yenyewe ilifutikwa baada ya makubaliano kati ya vyama vya PNU na ODM. Tume hiyo iliapishwa tarehe 20 Machi 2008 na kupewa jukumu la kuyashughulikia masuala kama vile:

1. Kuchunguza udhaifu wa katiba na masuala ya kisheria.
2. Kuchunguza muundo, uwezo, majukumu na uhuru wa walioijenga Tume ya Uchaguzi ya Kenya.
3. Kuchunguza mazingira ya uchaguzi, majukumu ya vyama vya kisiasa, mashirika yasiyokuwa ya serikali, vyombo vya habari na wachunguzaji wa uchaguzi.
4. Kuchunguza mipango na utekelezwaji wa uchaguzi wa 2007, ufunzaji wa masuala ya uchaguzi, usajilishaji wa wapigaji kura, usalama, utaratibu, kuhesabiwa kwa kura, maamuzi na utayarishaji wa matokeo na utatuzi wa ubishi. Miongoni mwa masuala mengine mengi. (Ripoti ya Kriegler 2007).

Tume ya Waki ilianza kazi yake tarehe 23 Mei 2008 baada ya Tume hiyo kuhalalishwa kupitia Notisi nambari 4473 kifungu cx-nambari 4 cha Gazeti la Serikali ya Kenya. Tume hiyo iliteuliwa chini ya kifungu cha sheria 102 za Tume ya Uteuzi ya Sheria za Kenya jukumu likiwa kuchunguza mapigano baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2007. Kando na tume hizo kulikuwa kumeshuhudiwa mabadiliko mengi nchini Kenya. Mabadiliko husika yalikuwa ni pamoja na kuzinduliwa kwa katiba mpya tarehe 27 Agosti 2010, kuingia kwa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai ya Hague nchini Kenya, kuundwa kwa Tume ya Uwiano na Utangamano (Itarejelewa kama TUU) nchini Kenya mnamo mwaka wa 2008 miongoni mwa matukio mengine mengi. Mabadiliko kama hayo hayakuwa na budi kuashiria kubadilika kwa siasa za nchi ya Kenya kwani, madai yalikuwa mengi kuwa mapigano ya baada ya kutangazwa kwa kura za urais nchini Kenya katika mwaka wa 2007 yalisalia kuwa suala nyeti.

Tukio la kubuniwa kwa Tume ya Uwiano na Utangamano nchini Kenya mnamo mwaka wa 2008 lilikuwa dhihirisho tosha kuwa usemi wa wanasiasa ulichukua nafasi muhimu katika siasa kwani huenda ungepelekea kuibuka kwa mielekeo chanya au hasi baina ya wananchi; ikumbukwe kuwa jukumu lake lilikuwa kushughulikia msukosuko wa ghasia za baada ya uchaguzi na masuala ambayo huenda yalizua mhemko miongoni mwa wananchi. Kubuniwa kwa tume hiyo kuliafikiana na matarajio kwenye Kifungu cha Sheria cha Tume hiyo cha mwaka 2008. Kifungu hicho kiliafikiana na matarajio ya sheria ya kanuni za adabu za mwaka huo wa 2008. Usemi wa kisiasa kimsingi hutumiwa kama ala katika utafutaji wa uungwaji mkono hasa wakati ushindani unapolenga na kutopenyeza katika jamii tofauti. van Dijk (2006) anasema kuwa hali za kisiasa haziibushi wanasiasa kuzungumza kwa njia fulani; lazima kuwapo na mwingiliano wa hali na matini husika. Mabadiliko ambayo yalikuwa yameshuhudiwa nchini Kenya yalikuwa mengi na ambayo yalizungukia suala la utawala na siasa. Kuzinduliwa kwa katiba mpya nchini, kuingia kwa Mahakama ya Kimataifa Jinai ya Hague nchini, kuundwa kwa Tume ya Uwiano na Utangamano (TUU), kuibuka kwa Tume ya Waki (Itarejelewa kama TW) miongoni mwa matukio mengine mengi yalichangia vipi katika kukuza au kufifiza usemi wa uchochezi wa wanasiasa katika kampeni za urais nchini Kenya? Ripoti ya Waki ilidai kwamba Agosti 2007 katika sehemu moja katika Mkoa wa Bonde la Ufa, wanasiasa mashuhuri wa ODM walipiga siasa za kupendelea "Majimbo" na ambapo msemaji mmoja aliiuliza jamii moja iondoe "madoadoa" kutoka katika mkoa huo ili kurahisisha kumuondoa aliyekuwa rais wa Kenya Mwai Kibaki kutoka kwa utawala na kuwang'oa Wakikuyu kutoka mkoa huo. Aidha, bila kutumiwa lugha siasa zitakosa kusawirika au kutelezekeka, Austin (1962) anaamini kuwa lugha ilikuwa na zaidi ya maana ya maneno na vishazi. Alizidi kusema kuwa maneno hayatumiwi kusema tu bali hutumiwa kutenda matendo (vitendoneni). Kutokana na kuwapo kwa matumizi ya lugha katika siasa wakati wa kampeni za kiti cha urais; kulikuwa kuna umuhimu wa kuyasaili maswali kama vile; kulikuwa na mwingiliano gani wa mada na usemi wa wanasiasa kabla ya uchaguzi wa mwaka 2007 na mapigano ya baada ya uchaguzi huo?

Katika mwaka wa 2013 kabla ya uchaguzi mkuu nchi ya Kenya ilikuwa katika njia panda kutokana na uwezekano wa wanasiasa kuyaegemea makabila yao na itikadi za vyama na

miungano yao katika kuhakikisha kuwa uchaguzi wa kiti cha urais ungetokea kuwapendelea. Itakumbukwa kuwa mfumo wa kisiasa nchini Kenya ulikuwa ukiyashuhudia mabadiliko mengi ambayo kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2013 ulikuwa umeshuhudia kuzinduliwa kwa katiba mpya katika mwaka wa 2010. Mwanzomwanzo wa mwaka wa 2013 haikuwa dhahiri vile hali za kisiasa zingetokea kutekelezwa na wanasiasa, hofu kuu iliyokuwapo ilikuwa; je uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2013 ungekumbwa na vita vya kikabila kama vile mambo yalivyokuwa katika mwaka wa 2008 baada ya kutangazwa kwa kura za urais katika uchaguzi mkuu wa 2007? Kwingineko kulikuwa na hofu kuu ya kutokea kwa mitafaruku ya kisiasa baina ya chaguzi mbili kuu mtawalia miongoni mwa wananchi wa Kenya. Wasiwasi mwingine uliokuwapo ni kuwa; je Kenya ilikuwa na uwezo wa kujizoazoa na kuwa na uchaguzi mkuu ambao haungeshuhudia mtafaruku kama ilivyokuwa katika mwaka wa 2008? Maswali kama haya yalihitajika kujibiwa kwani chaguzi za mwaka wa 2007 na mwaka wa 2013 zilikuwa chaguzi mbili tofauti, kila uchaguzi ukiwa ngambo yake swali kuu lilikuwa; Usemi wa wanasiasa katika mwaka wa 2007 uliegemezewa mada zipi za usemi tofauti na mwaka wa 2013? Kama ilivyokuwa katika uchaguzi wa mwaka wa 2007, uchaguzi wa 2013 uliibusha tetesi chungu nzima; matukio ambayo yalichangia kuwekwa kwa mikakati mbadala ya kuhakikisha kuwa ulaghai wa kisiasa ungetingwa katika uchaguzi huo wa mwaka wa 2013.

Kabla ya uchaguzi, woga na kiwewe kuhusu mapigano ya kisiasa yaliakisika kwingi. Kutoka mijini hadi mashambani na pia katika vyombo vya habari, Wakenya walikuwa na wasiwasi mwingi kuwa Kenya ingejitenga kwa misingi ya kikabila. Mitazamo hiyo ilichochewa na uzito wa uchaguzi huo wa mwaka wa 2013 miezi mitano kabla ya uchaguzi. Kama vile ilivyokuwa katika mwaka wa 2007 miezi mitano kabla ya uchaguzi mkuu, uchaguzi uliishia kuwa kinyanganyiro baina ya farasi wawili baina ya kiongozi wa jamii ya Kikuyu – Uhuru Kenyatta wa Muungano wa Jubilee na mpinzani kutoka jamii ya Luo – Raila Odinga kutoka muungano wa CORD.

*10th December 2012, (189)*

> *The battle would be between CORD and Jubilee… the rest are donkeys.*
>
> Kinyanganyiro kitakuwa baina ya CORD na Jubilee… wengine ni punda.

Kama ilivyokuwa katika mwaka wa 2007 uchaguzi wa mwaka wa 2013 ulizusha mabishano chungu nzima kwa kuwa vifaa vya kuukadiria ubora wa uchaguzi huo vilikosa kuafikia malengo yake ya kuzuia hila na wizi wa kura kama ilivyokuwa imeazimiwa baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2008.

Ili kuwa na uwelewa wa kina kuhusu vile usemi wa kisiasa nchini Kenya ulivyokuzwa na kuthibitiwa na wanasiasa kulikuwa kuna haja ya kupigia darubini tofauti katika usemi wa wanasiasa ulioziaka kampeni za urais baina ya chaguzi kuu mbili, ule wa mwaka wa 2007 na 2013, kwani usemi wa kisiasa huchochewa na mada ambazo huteuliwa na wanasiasa kama ilivyobainishwa na matokeo ya utafiti. Ili kuelewa tofauti baina ya usemi wa kisiasa kabla ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 na 2013 kulikuwa kuna haja ya kuvilinganisha vipindi hivyo viwili kwani kulishuhudiwa mabadiliko mengi mno baada ya mapigano ya kisiasa baada tu ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi mkuu wa urais ya mwaka wa 2007. Ikumbukwe kuwa siasa si suala tuli, hubadilika kutegemea mtazamo wa kihistoria, itikadi, masuala ibuka, miktadha na wahusika katika vipindi vya uchaguzi. Aidha, ulinganuzi wa usemi tarajiwa uliipata sampuli ya utafiti kwa kuulinganisha usemi wa wanasiasa kutoka kwa magazeti ya Daily Nation na The Standard kwa kuwa magazeti hayo yanayo historia ndefu nchini Kenya na kusambazwa na kusomwa kwake hufanywa zaidi ya magazeti mengine nchini Kenya; hivyo basi kulikuwa kuna uwezekano wa nukuu za usemi wa wanasiasa waliorejelewa kupatikana na hivyo kufanikisha usampulishaji.

**1. 2 Suala la Utafiti**

Usemi wa kisiasa ulikuwa umetuhumiwa kuwa ulikuwa ukichangia kutokea kwa mapigano ya kikabila nchini Kenya kila kulipokuwa na uchaguzi. Kutangazwa kwa kura za urais za mwaka wa 2007 na kuzuka kwa mapigano kulishuhudia kuibuka kwa mabadiliko mengi yaliyozungukia kuzinduliwa kwa katiba mpya, siasa na utawala. Hali hii ilileta swintofahamu ikiwamo baadhi ya wanasiasa wa hadhi kubwa nchini kufunguliwa mashtaka kwenye Mahakama ya Kimataifa ya Hague kutokana na madai kuwa usemi wao wakati wa kampeni za urais nchini Kenya ulikuwa wa uchochezi. Kwa misingi hii, ilikuwa si dhahiri ikiwa usemi wa wanasiasa nchini Kenya ulipunguza makali na uchochezi ikilinganishwa na madai mengi yaliyokuwapo. Utafiti huu ulilinganisha

usemi wa kisiasa katika kampeni za urais miezi mitano kabla ya chaguzi za mwaka wa 2007 na mwaka wa 2013.

### 1. 3 Malengo ya Utafiti

Shabaha kuu ya utafiti huu ilikuwa kulinganisha usemi wa kisiasa nchini Kenya katika kampeni za urais miezi mitano kabla ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 na miezi mitano kabla ya uchaguzi wa mwaka 2013. Ili kufanikisha hilo utafiti uliazimia:

1. Kuchunguza tofauti katika mada za usemi wa kisiasa katika kampeni za urais nchini Kenya miezi mitano kabla ya chaguzi za mwaka wa 2007 na 2013.
2. Kujadili mikakati ya usemi waliyoitumia wanasiasa katika kampeni za chaguzi za urais nchini Kenya katika mwaka wa 2007 na 2013.
3 Kutathmini athari za usemi wa wanasiasa katika kampeni za chaguzi za urais nchini Kenya katika mwaka wa 2007 na mwaka wa 2013.

### 1. 4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu wa ulinganuzi wa usemi wa kisiasa katika kampeni za urais nchini Kenya uliongozwa na maswali yafuatayo:

1. Kulikuwa na tofauti gani katika mada za usemi wa kisiasa katika kampeni za chaguzi za urais miezi mitano kabla ya chaguzi za mwaka wa 2007 na 2013?
2. Wanasiasa waliitumia mikakati gani ya usemi katika kampeni za chaguzi za urais nchini Kenya katika kampeni za chaguzi za mwaka wa 2007 na 2013?
3. Kulikuwa na athari gani za usemi wa wanasiasa katika kampeni za chaguzi za urais nchini Kenya katika mwaka wa 2007 na 2013?

### 1. 5 Sababu za Kuiteua Mada

Kama tafiti zingine, utafiti huu ulitokana na vichocheo kadhaa; kama vile, ilikuwa ni wazi kudai kuwa diskosi ya kisiasa ilikuwa haikosi kuwa na pengo kwani tafiti nyingi zimekuwa zikizungukia sarufi Habwe (1999); kulinganua diskosi ya kisiasa katika kampeni za uchaguzi wa urais nchini Kenya bila shaka kulichangia kuzielewa hila na

ushindani wa wanasiasa katika kampeni za urais nchini Kenya kwa kuzirejelea mada za usemi wa kisiasa. Kutokana na suala la ukabila kuwa "kidonda ndugu" nchini Kenya, kulikuwa na haja ya diskosi ya kisiasa kwenye kampeni za urais kuchunguzwa; hili lilipelekea kuzielewa siasa za urais kwani usemi wa kihistoria ungeweza kudhihirika dhahiri kule ambako huegemezwa katika kampeni za uchaguzi wa urais nchini Kenya. Pia, kutokana na nchi Kenya kukumbwa na mabadiliko mengi yaliyojihusisha na siasa na utawala, utafiti huu ulikuwa kigezo aula katika kubainishia kama mabadiliko yaliyoshuhudiwa nchini Kenya yalichangia katika kuusitiri usemi wa wanasiasa nchini Kenya au la.

Mojawapo wa kanuni za UHU ni kuwa; usemi ni wa kihistoria hivyo basi kutokana na mtazamo huo utafiti huu uliniwezesha kubainisha ni masuala yapi (mada za usemi) ya kihistoria ambayo wanasiasa walikuza na kukolezea usemi wao katika kampeni za urais nchini Kenya. Ni sawa kusema kuwa siasa zimepenya kabisa katika maisha ya binadamu na hivyo basi kuulinganisha usemi wa kisiasa kufuatia mabadiliko ya kisheria, siasa na utawala baada ya mapigano lilikuwa jambo zuri kwani mtafiti aliuafikia ukweli kuwa falsafa ya kisiasa hubadilika kila uchao. Vilevile mtafiti aliafikiana nao Fairclough na Wodak (1997:259) waliokuwa wamesema kuwa; sehemu muhimu za maisha ya jamii yanaendelea kuwa kitovu cha mchakato mzima wa vyombo vya habari, hasa runinga na kuwa tukio hilo linadhihirika vyema katika siasa. Kwa sababu njia nyingine inayotumiwa na wanahabari katika usambazaji wa matukio muhimu ya siasa hasa wakati wa kampeni ni kwa kuyatumia magazeti, kulikuwa na haja ya sampuli za usemi wa wanasiasa kukusanywa kutoka kwa magazeti.

**1. 6 Umuhimu wa Utafiti**

Lengo kuu la kijumla la utafiti huu lilikuwa ni kudadisi kama kulikuwa na tofauti katika usemi wa kisiasa miezi mitano kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2007 na miezi mitano kabla ya uchaguzi mkuu wa 2013, na hivyo basi kuwafaidi watafiti wa uchanganuzi wa diskosi ya kisiasa. Matokeo ya utafiti huu yanaweza kuzihamasisha jamii kwa kuitoa nafasi ya kuwaelewa wanasiasa wakati wa kampeni, na hivyo kuujenga utangamano ambao huwakwepa wananchi kila baada ya uchaguzi mkuu nchini. Aidha, kuna umuhimu mkubwa kwa jamii kuweka hadhari na kukadiria uzito wa usemi

wanaoutoa kwani huenda ukawa kichocheo cha kuibua mhemko baina ya makabila tofauti kwa kiwango kikubwa kwani utafiti huu uliafikiana naye Asher (1992) aliposema, "Neno linalotamkwa lina athari ya mara moja; uwezo wa ama kujenga au kubomoa" Kwa mapana na marefu yake, utafiti huu uliweza kudadisi na kuibua kuwa kulikuwa na mikakati mbadala iliyotumiwa na wanasiasa baada ya nchi ya Kenya kupitia mabadiliko mengi ya kisheria. Matokeo ya utafiti huu yameweza kubainisha kuwa usemi wa wanasiasa wakati wa kampeni hutokea kufufua masuala ya kihistoria kama vile usemi wa kikabila, usemi wa kihistoria, masuala ya ardhi, wizi wa kura na kadhalika.

Wakimnukuu Chilton (2007), Wodak na Meyer (2001:14) waliangazia kuwa Uchanganuzi wa Usemi Linganuzi ni kitengo kimojawapo kilichokuwa kikizua changamoto kwa waasisi wa UHU; na kuwa ingekuwa ni lazima kwa uwanja huo kushughulikiwa pasi na kuangaziwa kwa mitazamo ya Kiulaya ili kuipa sura ya kiulimwengu. Mtazamo wake Chilton bila shaka ulihitaji kuibua suala la kiusomi na hivyo kuchangia katika uwanja wa uchanaganuzi wa usemi; hasa usemi linganuzi.

**1. 7 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu ulijikita katika kuilinganisha diskosi ya kisiasa katika kampeni za urais miezi mitano kabla ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 na miezi mitano kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2013. Mtafiti alizichanganua matini kutoka katika magazeti mawili makuu nchini; "*Daily Nation*" na "*The Standard"* ambayo alitumainia kuwa yangehodhi usemi wa wanasiasa waliokuwa wamelengwa kwenye utafiti. Kutokana na historia ndefu ya magazeti hayo, uwezekano ulikuwa mwingi wa matukio mengi ya wanasiasa wakati wa kampeni kuripotiwa na waandishi wake. Matini tarajiwa zilikuwa zile zilizojitokeza kwenye kampeni za urais katika mwaka wa 2007 na pia katika kampeni za urais wa mwaka 2013. Ili kuupa utafiti huu mashiko mtafiti aliulinganisha usemi wa wanasiasa watatu katika chaguzi zote mbili ambao walikuwa; Raila, Uhuru na Ruto. Msingi wa kuchanganulia data ulikuwa tofauti za mada za usemi wakati wa kampeni za wanasiasa hao kwenye kampeni za chaguzi za urais katika vipindi vilivyokuwa chini ya utafiti wenyewe. Kutokana na kuwapo na nukuu nyingi za wanasiasa kutoka kwenye magazeti yaliyoteuliwa mtafiti alizidondoa nukuu husika kulingana na mada za usemi. Mada zilizoorodheshwa zilipewa nambari kama njia moja ya kujua idadi kamili ilyotumiwa na

mtafiti katika uchanganuzi wake. Kuenea na kusomwa kwa magazeti hayo na wananchi kulimvutia mtafiti kwani kulikuwa na uwezekano wa waandishi wa magazeti hayo kuyaangazia masuala na usemi mwingi wa wanasiasa uliojidhihirisha kwenye kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2007 na 2013. Changamoto ambayo ilitokea ilikuwa; usemi wa wanasiasa hao ulikuwa umenukuliwa kwa kiingereza ikikumbukwa kuwa wanasiasa waliitumia lugha ya Kiswahili wakati wa kampeni zao. Ilimbidi mtafiti kuutafsiri usemi huo kwa makini ili kuufanya kusalia na uasili wake ili kuhakikisha kuwa sampuli ilikuwa na mashiko.

### 1. 8 Ufafanuzi wa Istilahi

Ufafanuzi ufuatao wa istilahi umetolewa kwa maana na jinsi ulivyotumika katika kazi hii.

**Diskosi** – Hali ya kuwasiliana kwa misingi ya matumizi ya lugha pamwe na mwakilisho wa ishara za utabia.

**Itikadi –** Huu ni utaratibu wa maadili ambayo yalipendekezwa na vyama na miungano ya kisiasa ili kuwaongoza wanasiasa katika hatua zao za kuyafanya maamuzi yanayohusu jamii/kundi moja na mambo yote anayokumbana nayo katika maisha.

**Kutafuta Fadhila** – Hali ambapo mzungumzaji hulenga kunata makini ya msikilizaji, lengo likiwa faida imrudie yeye.

**Kuudhuru Uso –** Jambo lolote linalosemwa ambapo humdhuru mtu au humkirihisha na kuupuja utu wake.

**Madanganyo ya Upole –** Hali ambapo mtu humdanganya msikilizaji wake akiepuka kuudhuru uso wake.

**Mahitaji ya uso –** Matarajio kuwa mitazamo ya umma kuuhusu uso wa mtu itaheshimiwa.

**Matini-** Kifungu cha maandishi au usemi wa lugha.

**Mwingilianomatini –** Kuwapo kwa sifa mbalimbali za matini au usemi mmoja au zaidi katika mazungumzo ya wanasiasa.

**Mielekeo hasi** - Misimamo ambayo ni kinyume cha matarajio.

**Mikakati ya Usemi –** Katika kazi hii ilitumika kama njia au maarifa tofauti tofauti ya kuitumia lugha katika usemi wa kisiasa wakati wa kampeni za urais.

**Uchanganuzi Hakiki wa Usemi –** Katika kazi hii ilifumbata uchanganuzi wa matini zisizo dhahiri ili kuziweka wazi katika matumizi ya lugha.

**Usemi wa Kisiasa –** hatua yoteyote ya mtagusano wa jamii ambapo usemi/matini huwa kifaa kitumiwacho na wanasiasa ili kuishawishi jamii kuwaunga wanasiasa mkono.

**Uso Hasi –** Mkakati ambao hudhamiria kuutishia au kutoutishia uhuru wa msikilizaji kutoka kwa mwanasiasa.

**Uwezo** – Hii ni hali ambapo mwanasiasa huwaathiri watu wengine katika kutekeleza madhumini ya kisiasa.

**Topoi** – Imetumiwa kurejelea 'sheria za mahitimisho' ambazo huoanisha ubishi na yale yanayolengwa katika usemi wa wanasiasa.

**Usemi wa Chuki** – Ni usemi ambao husemwa kuwa unaweza kuzichochea jamii mbili na kusababisha kutokea kwa mapiganoo ya kikabila.

**Ilokusheni** – Ni kitendo kifanywacho katika kuzungumza au kuitumia lugha.

# SURA YA PILI

# TAHAKIKI ZA MAANDISHI

## 2. 1 Utangulizi

Sehemu hii ya mapitio ya maandishi ilidhamiriwa kutathmini kazi mbalimbali zilizohusiana na usemi wa kisiasa. Hili nililifanya kwa kuangalia maandishi ya kijumla; upande mmoja ulijikita katika maandishi kuhusiana na siasa, nao upande wa pili uliangazia nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi (UHU) pamwe na Usemi Mkabala wa Kihistoria (UMK). Kwa sababu hii ilikuwa kazi ya kiusomi ilinilazimu kubukua na kudurusu kazi tofauti tofauti ili kuupa utafiti huu mwelekeo.

## 2. 2 Usemi wa Kisiasa

Suala la siasa na jamii ni shilingi kwa ya pili. Akimnukuu Aristotle, Chilton (2008:4-5) alisema binadamu ni mnyama wa siasa… na kuwa shughuli za kisiasa haziwezi zikatekelezwa pasi na kuitumia lugha. Njia nyingine kama vile kulazimisha hutumiwa, lakini kutekelezekeka kwa siasa kumefungamanishwa na matumizi ya lugha. Ni wazi kusema kuwa matumizi ya lugha siyo njia ya pekee tu ambayo binadamu huingiliana kwayo, lakini ndiyo njia iliyobainika na kukua zaidi. Binadamu wanapoingiliana kwa kuzungumziana kunayo mambo anuwai ambayo watakuwa wakitekeleza. Suala la siasa nchini Kenya kama nchi nyingine yoyote iwayo ile, huegemea ushawishi; ushawishi ambao elementi muhimu itumiwayo ni lugha. Siasa katika kila masuala ya uchaguzi huongozwa na itikadi ambazo hufungamanishwa na mitazamo ya wanasiasa katika kipindi husika.

## 2. 3 Itikadi

Akimnukuu Thomson (1984:4), Barasa (2014:12) alisema kuwa '…kwa yakini itikadi huhusishwa na shughuli ya kuhimili ulinganifu wa uhusiano katika utawala ili kuthibiti mamlaka kwa kuficha, kuhalalisha au kubatilisha uhusiano huo; Barasa (2014) alizidi kusema kuwa kila wakati itikadi huwa zana au rasilimali ya makundi ya kijamii yenye uwezo. Kulingana naye van Dijk (2006) makundi yanayotawaliwa huweza kuwa na itikadi tofauti, kama vile itikadi za kukinza na itikadi za kiupinzani. Aidha, Dijk (2006) aliongezea kuwa itikadi hufungamanishwa na makundi ya kijamii, matabaka, hadhi, au

jamii zinazowakilisha matakwa yao. Kauli yake iliongezea kutaja kuwa kama zilivyo lugha, itikadi huwa na umuhimu wa kijamii. Alisema kuwa hamna itikadi za mtu binafsi, lakini kilichoko ni utumiaji wa itikadi fulani kutegemea mtazamo wa mtu binafsi. Makundi hayaelezewi kwa misingi ya kitambulisho cha itikadi pekee, lakini vilevile huelezewa kwa kuzingatia miliki ya muundo wa itikadi husika; kinyume na vile mitazamo mingi ya itikadi ilivyo katika tamaduni nyingi, si lazima itikadi ziwe na mtazamo hasi. Huwa na muundo na majukumu yaliyo sawa hata kama yanayajumuisha makundi yanayotawala au hata kutawaliwa, makundi 'mabaya' au makundi 'mazuri'. Hivyo basi, huenda kukawa na itikadi hasi vilevile itikadi chanya (ya jamii timilifu ya kufikirika), kutegemea mtazamo, thamani, au ushirikishwaji wa kikundi katika kutathmini masuala husika. Van Dijk alidai kuwa, si imani zote zinazohusisha makundi ya kijamii ambazo husheheni itikadi. Kwa hivyo, makundi tofauti kiitikadi au yanayopingwa yanahitajiwa kuwa na imani ya pamoja ili kuyafanya yaweze kuwasiliana. Shida za kiasili zilizoko katika ushirikiano baina ya itikadi na maarifa hutatuliwa kwa njia ya kijumla, maarifa ya utamaduni wa kijamii, kwa kugawanywa kulingana na vile jamii inavyoeleweka, hujumuisha hatua zote. Mojawapo wa mitazamo iliyoangaziwa katika mitazamo ya zamani ya itikadi ilikuwa yenye nguvu ya kiasili, kwa kuwa itikadi huchukua nafasi mwafaka katika uhalalishaji wa utawala mbaya kutoka kwa makundi yenye uwezo. Aidha, aina mojawapo nzuri ya mifano yenye itikadi yenye nguvu ni pale makundi yanayotawaliwa yanakubali kuwa itikadi za wanaowatawala kuwa za kweli au zenye mantiki. Aidha, itikadi hujenga kanuni za kijumla ambazo huthibiti mshikamano ambao huwakilisha makundi jumuishi ya kijamii. Kwa mfano, huenda itikadi ya mbaguzi wa rangi ikaithibiti mielekeo ihusuyo uhamiaji au kuithibitisha hatua fulani. Itikadi husimamia mojawapo wa sehemu ya kitambulisho cha kijamii au sura ya kikundi chenyewe.

Itikadi hujengeka katika kielelezo cha muundo wa kijamii ambao huhusisha idadi fulani za kategoria ambazo huwakilisha sehemu kubwa ya kikundi tambuzi cha kijamii, kama vile kutofautisha umiliki, vigezo vya kutofautisha uanachama, mifano ya hatua, malengo, kaida na thamani, urejelezi wa makundi, na rasilmali za kimsingi au mapendeleo. Nyingi ya itikadi na sio zote huwa na uhusiano katika hali ya kiushindani, migongano,

kutawaliwa na mikinzano baina ya makundi, hii ikiwa kama sehemu ya ushindani wa kijamii.

### 2. 3. 1 Siasa na Itikadi

Akiligusia suala la siasa na itikadi, van Dijk (2006) alisema kuwa kama kunazo taasisi ambazo zimefumbata itikadi kwa kina ni zile za kisiasa. Kulingana naye ni kuwa ni tukio lililo wazi kwa kuwa makundi kinzani huwa katika ushindani wa kiutawala kutokana na nafasi zao kuwa katika hali telezi kisiasa. Ili makundi hayo yaweze kuthibiti ushindani dhidi ya wapinzani wao huwa hawana budi kujipanga sawasawa na kumakinika kiitikadi. Akiwanukuu (Freeden, 1996; Ball and Dagger, 1999; Eatwell, 1999; Leach, 2002; Seliger, 1976), msomi huyo alisema kuwa shughuli zote za kisiasa kwa yakini hushughulikia itikadi, na utambuzi wa kisiasa na ambapo hujitambulisha na itikadi. Ushirikiano wa kijamii katika uwanja wa kisiasa, kama vile wanasiasa na makundi ya kisiasa, huwa na misingi yake katika miungano yao, usawa na tofauti katika itikadi zao.

### 2. 3. 2 Itikadi na Usemi wa Kisiasa

Akizungumzia itikadi na usemi wa kisiasa, van Dijk (2006) alihoji kuwa ikiwa uwanja wa kisiasa ulidhihirika kuwa wenye itikadi za kina, basi shughuli zote zihusuzo siasa ziliufuata mkondo huo, pamwe na usemi wake. Kwa yakini, itikadi za kisiasa hazijihusishi tu na uzalishaji na uwelewaji wa usemi wa kisiasa na shughuli zingine za kisiasa, lakini hujihusisha vilevile na uzalishwaji tena wa matukio hayo (Tazama 2.4.3). Iaminike kuwa usemi hufanya itikadi idhihirike kwa kuwa usemi ndiyo njia ya pekee inayoweza kuchangia katika kueleweka na kutekelezeka kwake. Shughuli zingine za kisiasa hudokeza tu matukio ya itikadi husika, kwa mfano katika ubaguzi kama vile wa kijinsia, rangi, au itikadi za kisiasa. Ni katika usemi ambapo tunahitajiwa kuelezea dhahiri kuwa matukio kama hayo hutokea 'kwa kuwa yeye ni mwanamke,' 'kwa kuwa yeye ni mtu mweusi,' ama, 'kwa kuwa hao ni wa mrengo wa kijamaa'. Kwa hivyo, kwa kiwango kikubwa itikadi za kisiasa hupatikana, huelezwa, hufunzwa, hukuzwa na hushindaniwa kupitia usemi.

### 2. 3. 3 Miktadha na Hali za Kisiasa

Mwingiliano baina ya usemi na itikadi za kisiasa hutafitiwa kwa msingi wa miundo ya usemi wa kisiasa, kama vile matumizi ya msamiati wa kibaguzi, miundo ya sentensi kama vile viwakilishi vya kauli tendi na visivyo tendi kama vile **sisi** na **hao**, istiari au topoi, ubishi, umaanisho na vipengele vingine vya usemi. Akiwanukuu Duranti na Goodwin (1992), van Dijk (2006) alishikilia kuwa, ilikuwa ni lazima usemi kutazamwa kwa misingi ya miundo ya muktadha. Alidai kuwa haikuwa murua kwa usemi wa kisiasa kuzingatia hali – zijulikanazo za viwakilishi vya kisiasa **sisi**. Ni muhimu kuzihusisha kategoria zingine kama vile, ni nani aliyesema hayo, lini, wapi na walikuwa na nani kwa kuangazia hali halisi za matukio ya kisiasa.

Usemi wa kisiasa hauelezewi kwa misingi ya miundo ya usemi wa kisiasa lakini vilevile kwa kurejelea miktadha ya kisiasa. Miktadha ya kisiasa huweza kuelezewa kwa kurejelea maeneo halisi kama vile bunge, katika mijadala au katika mikutano ambapo muda wa kuyatekeleza hayo huzingatiwa. Zaidi ya hayo, usemi wa kisiasa huweza kutekeleza majukumu ya kisiasa wakati wa utekelezaji wa vitendo vya kisiasa ambapo shughuli hizo huwa kama vile, za utawala, uundaji wa sheria au uandaaji makundi ya upinzani kukiwapo na malengo mahususi ya kisiasa kama vile kutetea au kuupinga mswada au kutaka kuchaguliwa. Mwisho, wahusika katika masuala ya kisiasa kwa yakini huwa hawashiriki pasina kumakinika katika hali za kisiasa, lakini huwa na uwelewa, huchangia katika kuzithibiti kaida na thamani za kisiasa sawia na itikadi za kisiasa. Matukio kama hayo yaegemezwayo kwenye miktadha ndiyo huwezesha itikadi za wahusika zioanishwe na usemi wao (Gumperz, 1982). Matini au usemi husheheni itikadi kimantiki, lakini wale ambao huwa na itikadi huwa watu, wanasiasa, waandamanaji – sio tu katika tukio kama hili la kijamii au usemi, lakini pia katika maeneo mengine.

Mitindo ya miktadha ndiyo huongoza usemi wa kisiasa. Usemi wa kisiasa huweza kukadiriwa kusheheni mambo kadhaa, huweza kuwa usemi wa ahadi au usemi wa kutishia kutegemea uwezo na uhusiano wa wahusika, nyadhifa zao za kisiasa (serikali au upinzani, chama changu au chako), vile vile ikiwa madhumuni yakiwa kusaidia au kudhuru kundi lengwa. Mitindo ya miktadha huweza kutawala viwango vyote vya mbinu katika usemi wa kisiasa, kama vile uchaguzi wa msamiati, viwakilishi, miundo ya kisintaksia, na uchaguzi

mwingine wa kisarufi ambao hutegemea vile hali zimeelezwa. Kwa hivyo, msamiati na muundo wa kisintaksia katika mijadala ya bunge huwa na urasmi mwingi kuliko mkutano wa kisiasa usiokuwa rasmi wa wafuasi wa chama au kurasa za maandishi za kipropaganda. Miundo ya miktadha huweza kuongoza kwa jumla mpango wa kielelezo wa usemi wa kisiasa, kama vile uzungushaji wa usemi, ufunguzi na ufungwaji wa mijadala katika bunge, muundo wa uneni katika mahojiano ya kisiasa, mipangilio ya ratiba ya chama, mipangilio ya matangazo ya chama katika majarida au mabango.

van Dijk (2006) aliangazia kuwa itikadi za kisiasa huonyesha namna matini na usemi wa kisiasa umesheheni miundo ya mikingamo ambayo huakisi ushindani au migongano ya wafuasi ya makundi ambayo huanihika kwa misingi ya kundi-ndani na kundi-nje. Miundo hii hudhihirika vyema katika mielekeo mahususi ya kisiasa – kama vile mielekeo ya ubaguzi wa rangi kuhusu uhamiaji… Ikiwa basi miundo ya mikingamo huwa dhahiri, yaliyomo kwenye usemi huchangia kwa kiwango fulani kuonyesha aina inayohusika ya mikingamo. Kulingana naye ni kuwa, tafiti nyingi kuhusu usemi wa kiitikadi husheheni mikakati ya kijumla ambayo huweza kutajwa kama mraba wa itikadi:

1. Kusisitiza uzuri wa mambo Yetu
2. Kusisitiza ubaya wa mambo Yao
3. Kutosisitiza ubaya wa mambo Yetu
4. Kutosisitiza uzuri wa mambo Yao.

Kulingana na msomi huyo mikakati hii ya kijumla inaweza kutumiwa katika viwango vyote vya matendo, maana, na katika aina ya matini na usemi. Kwa hivyo, hotuba za kisiasa, mahojiano, mipango, au propaganda kwa yakini hulenga mada za muungano au chama ‘chetu’, mazuri ambayo wameyafanya, na kuwahusisha wapinzani wao na mada hasi kama vile vita, machafuko, mihadarati, kukosekana kwa uhuru na mambo mengine mengi. Kulingana naye, maana au mada husheheni sura au muundo: maana inaweza kuboreshwa kwa njia nyingi kama vile mkazo, kutazama, mpangilio wa maneno, kuweka anwani, uainishaji wa mada, urudiaji na kadhalika. Mambo kwa kawaida huwa kinyume wakati wanasiasa hutelekeza masuala yote mabaya yawahusuyo. Masuala mabaya zaidi kuwahusu maadui zao – kama vile mashambulizi ya kiugaidi – yatawekwa katika ukurasa

wa kwanza kwa kuzingatia anwani hasi yenye maandishi makubwa… na huenda yakakolezwa wino.

### 2. 4.1 Maandishi ya Ulinganuzi wa Usemi wa Kisiasa

Habwe (1999) aliufanya utafiti wake akidhamiria kuyachunguza matamshi ya wanasiasa nchini Kenya ambapo alilenga kuangazia matatizo ya mshikamano, kuchukuana kwa matini za usemi wa kisiasa katika lugha ya Kiswahili na maana ya umaanisho; yaani kipragmatiki. Utafiti wake Habwe ulitafiti usemi wa wabunge na ambapo data yake ilikusanywa katika kampeni za ubunge katika miji mikubwa nchini Kenya kutokana na kutumiwa kwa lugha ya Kiswahili na watu wengi mijini. Utafiti huu ulitofautiana na wake Habwe (1999), kwani ulijikita katika kuulinganisha usemi katika kampeni za urais nchini Kenya katika vipindi viwili tofauti. Utafiti wake Habwe ulikuwa muhimu kwa mtafiti kwani ulinipa dira katika kuelewa umuhimu wa mada za usemi wa kisiasa katika uchanganuzi wa siasa nchini Kenya, ikizingatiwa kuwa falsafa ya siasa hubadilika kila uchao.

Lwaitama (1988), alitafiti hotuba za Kiswahili za kisiasa nchini Tanzania ambapo aliangazia mbinu za kiwakilishi cha nomino cha mtu binafsi kwa kuwachunguza wanasiasa wawili waliobobea katika siasa ambao walikuwa ni waheshimiwa marais wastaafu hayati Nyerere na Mwinyi. Alitambua kuwa matumizi badalia ya kiwakilishi nomino haikuwa ishara ya mbinu ya mtu binafsi bali pia ilitegemea muktadha wa matumizi. Utafiti wake Lwaitama ulikaribiana na huu na vilevile kutofautiana; kwani uliwahusu marais waliotawala, utafiti huu ulihusu kampeni za urais nchini Kenya. Tofauti iliyokuwapo ilikuwa kubwa kwani utafiti huu ulijikita katika kulinganisha usemi wa kisiasa nchini Kenya baina ya vipindi viwili tofauti, huku Lwaitama akiwalinganisha marais waliokuwa wamestaafu.

Utafiti mwingine uliofanywa na Lwaitama (1995) ulikuwa mpana zaidi ya ule wa kwanza; akinukuliwa na Habwe (1999) msomi huyo aliutumia mtazamo wa lugha hakiki katika kuzitafiti mbinu za uneni katika hotuba za marais wa hapo awali wa nchi ya Tanzania; waheshimiwa hayati Nyerere na Mwinyi. Masuala aliyoangalia ni pamwe na aina ya msamiati – nomino, vielezi, miundo ya sentensi kama vile ya usemi taarifa badala ya usemi halisi, kiwakilishi nomino cha mtu binafsi, zinavyotumiwa na wazungumzaji kama

mtindo wa mtu binafsi na ufaafu wa muktadha. Utafiti wake Lwaitama uliakisi sifa moja muhimu ya utafiti huu kwani ulichunguza mbinu za uneni katika siasa za wanasiasa hao; pale ambapo utafiti huu ulipiga hatua zaidi na kuchunguza Mada za Usemi pamwe na Athari ya matumizi ya mbinu tofauti tofauti katika usemi wa wanasiasa niliowateua katika kampeni za uchaguzi wa urais nchini Kenya.

### 2. 4. 2 Maandishi ya Mikakati ya Hila

Gitonga (1991) alitolea maelezo kufungamana na diskosi ya kisiasa nchini Kenya alipojikita katika sayansi ya kampeni za uchaguzi. Kile ambacho alikigusia ni suala la mbinu chafu zilizokuwa hazisheheni maadili zilipotumiwa na wanasiasa katika kampeni za uchaguzi ambazo zilikuwa pamoja na kuharibiana sifa, ghasia, uvumi, kusiribiana matope, vitisho, ufisadi, taarifa za wongo; kauli yake ilisema kuwa mbinu hizi zilielekezewa mgombeaji mpinzani, au wafuasi wake; maelezo yake yalizidi kudai kuwa mbinu hizi zilijumuisha kitendo chochote, kama vile namna ya utendaji au vile maneno yalivyokiuka sheria zilizowekwa, maadili, taratibu za itifaki na tabia za mienendo katika jamii husika. Mtafiti huyo alitokea kusema kuwa siasa kama hizo hazikufaidi bali zilikuwa zembefu, hafifu na hatari na hivyo basi alipendekeza kutekelezwa kwa siasa chanya ambazo zingesaidia katika kuiaka demokrasia. Utafiti huu ulilenga kulinganisha diskosi ya kisiasa kwa kuangazia kampeni za urais nyakati mbili tofauti nchini Kenya. Utafiti wa Gitonga ulilingana na huu kwa jinsi moja na kutofautiana kwa jinsi mbili; kwanza ulijikita katika kampeni za uchaguzi kama huu. Tofauti ni kuwa kipindi cha utafiti na kundi lengwa kilitofautiana na hiki, fauka ya hayo, utafiti huu ulijihusisha na ulinganuzi wa usemi kwenye kampeni za urais miezi mitano kabla ya chaguzi za mwaka wa 2007 na mwaka wa 2013. Ikumbukwe kuwa wakati wa utafiti huu mabadiliko mengi ya kisiasa yalikuwa yamekwishadhihirika nchini Kenya hivyo, kuibua haja ya kuelewa vile usemi wa siasa ulivyoathiriwa na matukio yaliyoibuka nchini.

Irungu (1999) alitafiti kuhusu sanaa ya hila za kisiasa za Kenya. Utafiti wake ulijikita katika kuchunguza mbinu zilizotumika wakati wa uongozi wa chama cha KANU kabla ya, na baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 1992. Mbinu ambazo alitokea kuzielezea zilihusiana na upachikwaji wa majina kwa viongozi, wafuasi, wapinzani au kundi lolote la watu. Ilithibitika kuwa majina hayo yalikuwa na uwezo wa kuvutia hisia chanya au hata

hasi miongoni mwa wananchi. Mfano mzuri ulikuwa ule ulioelekezewa jamii za Wajaluo na Wakikuyu; lililodhamiriwa lilikuwa kuzitenga jamii hizo mbili kutoka kwa makabila mengine nchini na kukuza uhasama dhidi yao. Makabila hayo yaliitwa "wakabila", Majaluo yalielezwa kuwa kundi lililoshikilia utamaduni na ukoo kikiki, ilhali Wakikuyu walisemwa kuwa wakabila, walafi wenye uchu wa pesa na wanyakuzi sugu wa ardhi. Mbinu zingine zilikuwa za kukuza chuki, propaganda na matumizi ya sitiari kama vile "kula" iliyomaanisha utumiaji wa uwezo wa kisiasa katika uendelezaji wa kabila lililokuwa katika uongozi. Utafiti wake Irungu ulinifaa pakubwa kwani uliangazia usemi wa kisiasa; tukio lililoufaa utafiti huu kwa kuwa ulijikita katika kuulinganisha usemi wa kisiasa nchini Kenya katika kampeni za urais kwa kulinganisha vipindi viwili tofauti. Utafiti wa Irungu ulinifaa kwani ulinipa nafasi ya kuweza kuona kuwa kulikuwa na mabadiliko ya usemi baina ya kipindi cha utafiti wake na kipindi kilichokuwa chini ya uchunguzi huu ikizingatiwa kuwa Kenya ilikuwa imekumbwa na mabadiliko mengi yaliyozungukia siasa, utawala na sheria.

Murungi (2000) alitalii diskosi ya kisiasa nchini Kenya kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2002; akimrejelea "mwasi wa chama cha kisiasa". Aliziangazia istilahi mbalimbali zilizotumiwa na chama cha KANU kumrejelea mtu aliyekihama chama chake cha kisiasa na kujiunga na chama kingine. Mtu kama huyo alipewa lakabu ya "msaliti, kahaba wa kisiasa, mhaini" au "mamluki". Mtu kama huyo alielezwa kuwa mwenye nia ya kuvuruga 'amani, upendo na umoja uliokuwapo'; kulingana naye, mtu kama huyo angeendewa na marafiki zake na kuraiwaraiwa kwa kuambiwa kuwa yeye ni mwema na kwamba alipotoshwa na watu "wakabila" na "waovu" katika upinzani waliokuwa na nia ya kusababisha "vurumai"; Murungi aliongeza kuwa; mwasi huyo angelazimishwa kukiri hadharani; "kwa hiari" kwamba alikuwa amepotea lakini wakati huo alikuwa amepatikana. Katika kipindi hicho diskosi ya kisiasa ilisheheni kauli kama "ukosefu wa maendeleo" ambazo hazikumaanisha barabara, maji, elimu wala vituo vya afya kwa wananchi bali zilimaanisha maendeleo ya kibinafsi ya kiuchumi ambayo ni pamoja na mashamba, magari ya kisiasa, nyama choma, pombe, wanawake na ufanisi wa rasilmali mbalimbali. Kutokana na rasilmali hizo mwasi angeweza kushawishiwa na kuwapuuza wapinzani na kuwaona kama waliofilisika na waliokwa hawana "ajenda ya maendeleo". Tofauti iliyokuwapo ni kuwa, utafiti huu ulichunguza usemi uliokuwa haujikiti katika

suala la vyama vingi pekee; lakini, uliotalii diskosi ya kisiasa iliyozungukia kampeni za chaguzi za urais nchini Kenya katika vipindi viwili tofauti.

Chilton na Schaffner (1997:206) katika van Dijk (1997) walimtaja binadamu kimsingi kama kiumbe mwenye lugha na kuwa binadamu alikuwa kiumbe wa kisiasa. Ili kuupa mtazamo wao mashiko waliurejelea msimamo wake Aristotle aliyekuwa amesema kuwa binadamu ni kiumbe wa kisiasa. Kuna elementi za ukweli katika maelezo yote mawili; kimsingi, walisema kuwa haiwezekani kuzishughulikia siasa pasina kuwapo na matumizi ya lugha. Katika mtazamo mpana, Chilton na Schaffner walishikilia kuwa wanenaji mashuhuri kama vile Isocrates, Plato, Cicero ambao walituhumu kuwa wanenaji wa umma walitokea kuwa na uwezo wa kuhadaa wananchi kwa kuyatumia matamshi yenye kughilibu. Katika elimu inayohusiana na lugha ni vizuri kutaja kuwa utafiti wa usemi – sanaa ya usemi shawishi – ilifikiriwa na waandishi wa Kiyunani na Kirumi kama mfano wa "sayansi ya kisiasa". Watoaji maoni wengi, na hasa watu wengi wa kawaida katika maisha ya kila siku wanao mtazamo kuwa wanasiasa na asasi za kisiasa huendelezwa na lugha "shawishivu" na "milikivu" ambayo kwa kawaida umma unao ufinyu wa kuielewa. Mtazamo wao Chilton na mwenzake ulikuwa muhimu katika utafiti huu kwani ulinganuzi wa usemi wa kisiasa nilioangazia uliegemea matumizi ya lugha ya wanasiasa niliowalenga.

Haugerud na Njogu (1991) katika Habwe (1999), walitafiti usemi wa kisiasa ambapo walisema kuwa usemi wa wanasiasa ulimaanishwa nao wanasiasa kwani walikuwa wenye mikakati ambayo waliwasilisha jumbe zao wakilenga faida iwarudie au nchi inufaike kutokana na matarajio yao. Kulingana na utafiti huo Habwe aliangazia kwamba utafiti huo ulikuwa na umuhimu mkubwa kwani ulisheheni mapatano katika tukio la kujisingizia. Utafiti huo ulikuwa tofauti na huu kwani uliangazia usemi wa wanasiasa pasina kujikita katika kipindi chochote mahususi na ambapo aliangazia kwa kiasi mikakati iliyotumiwa na wanasiasa.

King'ei (2001) katika Shitemi na wenzake (2001), aliangazia diskosi ya kisiasa nchini Kenya akirejelea unenaji wa kisiasa kwa kuzirejelea dhana mbalimbali na upendekezaji. Aliziangazia baadhi ya sifa muhimu zilizotawala matumizi ya diskosi ya kisiasa nchini;

hili alilifanya kwa kurejelea usemi, virai na maelezo kutoka vyombo vya habari. Alihoji kuwa wanasiasa walikuwa wajenzi wa kiisimu kwa kubuni mitindo ya usemi na kuunda maneno mwafaka ya kutosheleza hadhira na hali pana za kijamii. Alishikilia kuwa lugha ya wanasiasa nchini Kenya ilisheheni tasifida iliyofumwa katika maneno mazito na virai vilivyolenga kusitiri masuala nyeti huku yakitetea hadhi ya msemaji au wasemaji. Utafiti huu uliazimia kupiga hatua zaidi kwa kuuweka wazi usemi uliotumiwa na wanasiasa kwa kuirejelea nadharia ya UMK. Hili nilitarajia kuliangazia kwa kurejelea namna lugha inavyotumiwa na wanasiasa katika hali pana za kijamii.

Mutahi (2005) alitafiti kuhusu ghasia za uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2002 nchini Kenya ambapo aliangazia ghasia, mauaji, vitisho na uhamishaji wa jamii zilizofikiriwa kuwa wafuasi wa upinzani. Kulingana na matokeo ya utafiti wake wanasiasa wa chama cha KANU "walitabiri" kuwa nchi ingegawanyika kwa misingi ya kikabila ambayo ingechangia fujo na ghasia iwapo vyama vingi vingeruhusiwa kuibuka nchini. Akimnukuu Kagwanja (1998:70), alisema kuwa baadhi ya viongozi wa KANU hasa kutoka mkoa wa Bonde la Ufa walianza kutisha kutolewa kwa nguvu kwa watu wa mbari nyingine kutoka mkoa huo. Vile vile walianzisha wito wa kuanzishwa kwa mfumo wa utawala wa "majimbo" ili kuyalinda maslahi yao kutokana na watu kutoka nje.

Achieng' (2007) alitafiti ufasiri na uhusishaji wa diskosi ya kisiasa nchini Kenya ambapo alisema kwamba wanasiasa walikuwa na athari kubwa kwa jamii na wangewafanya wafuasi wao kuamini waliyosema; kwa hivyo, wao walitumia thamani ya lugha kikamilifu kuwasilisha jumbe katika mawasiliano. Alidhamiria kuchunguza misingi ya misululu ya utoaji na usimbuzi wa usemi wa wanasiasa na kubainisha uhusishaji wake katika jamii na kuelezea hali katika diskosi za kisiasa zilizopelekea kutokea kwa tafsiri nyingi katika usemi. Utafiti wake ulibainisha kwamba mitindo katika diskosi ya siasa ilikuwa na utata ambao ulitokea kuibusha tafsiri kadhaa. Usemi pia ulibainisha kuchangia katika kuyafanya majukumu ya jamii kama vile kudhihirisha ubaguzi wa kijinsia na ushindani wa utawala. Utafiti wake Achieng' ulikuwa muhimu katika kufanikisha utafiti huu kwani alibainisha kuwa usemi huhusishwa na matukio fulani ya kijamii na vilevile husheheni tafsiri kadhaa. Utafiti huu ulijikita katika kulinganua usemi wa kisiasa katika kampeni za chaguzi za urais nchini Kenya; utafiti wake ulikuwa muhimu kwani ulidhihirisha kuwa kulikuwa na

ubaguzi kama vile wa kijinsia; utafiti huu ulilenga miongoni mwa masuala mengine kujadili mikakati ya usemi waliyotumia wanasiasa katika kampeni za chaguzi za urais nchini Kenya baada ya Kenya kushuhudia mabadiliko mengi ya kisiasa, sheria na utawala kabla ya uchaguzi wa mwaka wa 2013.

Oduori (2009) alitafiti lugha na siasa katika mwaka wa 2005 ambapo alionyesha jinsi matumizi ya lugha ya wanasiasa yanavyodhihirisha mahusiano ya kiuwezo kati ya viongozi na wananchi na vilevile baina ya wanasiasa wenyewe; aidha utafiti wake uliangazia matumizi ya lugha na utawala ambapo kile kilichoangaziwa ni vile viongozi walivyotumia lugha katika kuendeleza utawala. Utafiti wake Oduori unatofautiana na huu kwani ulijikita katika kuangazia vile lugha ilivyodhihirisha mvutano baina ya viongozi wa kisiasa na vilevile athari zilivyoweza kuibushwa na usemi wa wanasiasa kwa juhudi ili kuleta utangamano wa kitaifa.

### 2. 4. 3 Maandishi ya Siasa za Kimbari

Jonyo (2003) aliangazia siasa za vyama vingi kwa kurejelea KANU na NARC kwa kuangazia umuhimu wa siasa za kimbari ambapo alibainisha kuwa siasa za vyama zilikitwa katika suala la mbari hasa tangu pale mabadiliko kuhusu vyama vingi zilipopata msukumo nchini Kenya katika mwaka 1991. Katika mwaka wa 2002 ukinzani katika siasa za Kenya ulikuwa kwamba Wakalenjin na Wakikuyu walikuwa wamekwisha itawala nchi ya Kenya kwani walikuwa wameshauonja urais na hivyo basi wakati wa mbari zingine ulikuwa umepiga hodi – wakati wa "kula". Kulikuwako na istilahi zingine zilizoibuka kama vile "nyumba ya mumbi" istilahi hiyo ilimrejelea Uhuru Kenyatta na kudai kuwa ndiye alikuwa anafaa kumrithi rais mstaafu Moi kwani angeweza kuzivutia kura za Wakikuyu. Kutoka Mkoa wa Magharibi, "Mwana wa mberi" nayo ilikuwa istilahi iliyokuwa ikimrejelea Musalia Mudavadi ambaye alikuwa ameshawishiwa kumwachia Uhuru Kenyatta nafasi ya kuwania Urais. Wanasiasa katika eneo la Mkoa wa Magharibi kama vile Cyrus Jirongo na Amukowa Anangwe waliitwa wasaliti na watu wa mbari zao. Kundi la mungiki na wafuasi wao walitumia istilahi ya "thaai" kama kiunganishi cha watu waliotarajiwa kuziunga juhudi zao mkono na yeyote aliyepinga pendekezo hilo alitishiwa maisha yake. Pamwe na istilahi hiyo kulikuwa na istilahi "Kiambu mafia" iliyokuwa imefumbatwa na wafuasi sugu wa Uhuru Kenyatta; bila shaka hivi vilikuwa baadhi ya

viashiria muhimu vya nafasi ya mbari katika siasa za Kenya. Utafiti huu ulikuwa tofauti na wake Jonyo kwani niliilinganisha diskosi ya kisiasa katika kampeni za chaguzi za urais nchini Kenya. Utafiti wake Jonyo ulikuwa muhimu sana kwani matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwa mwingilianomatini na mwingilianouneni ni mambo mawili ambayo kujitokeza katika usemi wa kisiasa; hili lilikuwa wazi kutokana na kujikariri kwa mapendekezo kutoka kwa wanasiasa (Raila *Standard 15th December 2007*) waliosema kuwa kulikuwa kuna haja ya jamii zingine kupewa nafasi kuiongoza nchi ya Kenya.

### 2. 5. 1 Diskosi

Habwe (1999) aliwanukuu Schiffrin (1994:5) na Stubbs (1983: 12) na kusema kuwa maandishi yalihusiana na diskosi na kuwa yalikuwa yakitumiwa kwa kipindi kirefu lakini tafsiri yake ilikuwa finyu. Hili lilifanyika kwa kuwa sababu ilikitwa kwenye mitazamo tofauti kufungamana na asili ya watafiti na hivyo basi kuchangia kuwapo na matumizi tofauti ya dhana hiyo moja. Johnstone (2008:1) aliangazia mtazamo sawa kwa kudai kuwa watu katika nyanja tofauti za kiusomi na taaluma walitumia neno uchanganuzi wa diskosi kwa kuegemea kile walichokifanya, vile walivyokifanya au hata yote (TY). Johnsone (2008:1) aliitaja diskosi kama hali ya kuwasiliana kwa misingi ya matumizi ya lugha japo kunao waliokuwa na mtazamo mpana zaidi wa “mwakilisho wa ishara za utabia” kwa namna yoyote (Blommaert, 2005:2). Kulingana naye, istilahi diskosi ilikuwa ikitumiwa kwa mbadilishano na neno matini, kutokana na mtazamo huo wakati mtu aliposhughulikia masuala ya matini alisemwa kuwa aliyashughulikia masuala ya diskosi vilevile (Stubbs 1983:9). Mtazamo huo hata hivyo ulitokea kupingwa nao Fairclough 1989; Leech 1983; Leech na Short 1981; na kwa mujibu wake Habwe (1999:30), aliurejelea mtazamo wao kama tata kidiskosi.

### 2. 5. 2 Matini

Matini ni sehemu ya diskosi. Hili ni wakati matini inaonekana kama sehemu jumuishi ya hali za kuwasiliana katika miktadha fulani. Habwe (1999:37) akimnukuu Petofi (1985:209) alizitolea hali nne katika kuelezea matini. Moja, alisema matini ni elementi za lugha. Pili, matini zingeweza kuwa huru katika viwango fulani, kwa mfano; irabu, sentensi huenda zingekuwa matini katika hali zake. Tatu, matini zingeweza kusheheni maana; hilo lilimaanisha kuwa matini haikuwa mfuatano wa ishara lakini ishara

zilizoingiliana na dalili. Na nne, matini zingeweza kujaliza majukumu fulani ya mawasiliano. Katika kuyafanikisha matumizi ya matini katika tasnifu hii mtafiti aliurejelea matini kama elementi za lugha kutokana na mtazamo huo kuyafumbata suala zima la utafiti huu.

**2. 5. 3 Mwingilianomatini**

Dhana ya mwingilianomatini huashiria mitazamo miwili ule wa usomaji na uandikaji matini kama njia ya kutazama matini kama mwingiliano wa matini za awali, waandishi, wasomaji na makongamano. Mitazamo mingi ya wasomi husema kuwa dhana hiyo hutumiwa kuelezea kuwapo kwa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi fulani ya kifasihi. Waasisi wengi husema kuwa mwingilianomatini huchukulia kwamba kila kazi kama vile za kifasihi zinahusiana na kazi iliyoandikwa kabla kwa namna moja au nyingine; yaani ni njia bainifu au wazi za mwingilianomatini kwa kunukuu au kudondoa, wizi wa kiuandishi na wigobezi. Thibault (1994) anauelezea mtazamo huo kwa kusema: 'matini zote, za kusemwa na kuandikwa, hutengenezwa na huwa na maana ambazo watumiaji wa matini huzihusisha ndanimwe na mwingiliano wazo na matini zingine katika mpango wa jamii. Inaaminika kwamba Kristeva (1986) aliibuka na istilahi ya mwingilianomatini kwa misingi ya kazi ya Bakhtin ya usemezano. Bakhtin (1986) alisema kuwa kila matini (au usemi) huwa mabadilishano ya mawazo, kwa mtazamo kuwa maana yake hupatikana kwa ushirikiano na matini zingine. Kristeva (1981) alisema kuwa matini fulani ni 'mabadiliko ya matini zingine, mwingilianomatini: katika nafasi ya matini fulani, mazungumzo kadhaa, yaliyochotwa kutoka kwa matini zingine, yaliyogawanywa na kufifiza matini nyingine.

Wasomi wengi akiwamo Fairclough (1992) huuona mwingilianomatini sio tu kama umbo ambamo matini huwa na uhusiano, lakini pia kama tabia za jamii ambayo huhusisha jambo fulani la kijamii lililoelekezwa kwa njia ya kutoa na kufasiri usemi. Kulingana na Fairclough (1992), mwingilianomatini huashiria vile matini zinaweza kubadilisha matini za awali na kuunda upya mapatano (ya tanzu, usemi), ili kuibua matini mpya. Yaani mwingilianomatini hujihusisha na jinsi matini zinavyotolewa kwa ushirikiano na matini za awali na vile matini hizo husaidia kutengeneza mapatano yaliopo katika kutoa matini mpya. Japo utafiti huu haukuwa wa kifasihi, Wamitila (2008:25) amesema kuwa matini za

kifasihi husomwa kwa kuhusishwa na matini nyinginezo kwa kuwa matini hiyo itakuwa imechota, kuinukuu, kuigeuza, kuiiga kwa namna ya kubeza au kuirejelea kwa njia moja au nyingine matini nyingine. Mitazamo ya wasomi hawa inayo mwangwi katika suala la ulinganishaji wa usemi wa kisiasa katika yale niliyokuwa nimelenga kufanya kutokana na kuhusishwa kwa mada za usemi wa kisiasa zinazoingiliana katika kampeni za urais miezi mitano kabla ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 na ule wa mwaka wa 2013. Mwanasiasa anayelizungumzia suala fulani huweza kuathiriwa na usemi fulani wa kisiasa kihistoria kwa kiasi fulani na kuifanya kazi hiyo kuwa sehemu ya 'maana ya kidalili' ya usemi wake. Mwanasiasa anaweza kuchota kutokana na chukulizi, mawazo au maoni yaliyopo kwenye usemi fulani (alionao mwanasiasa huyo) kuihusu mada hiyo au kaida za usemi unaohusika. Uwelewa huo huwa muhimu sana katika kulizungumzia suala lililokuwa limezunguziwa zamani na wanasiasa kabla ya hapo.

### 2. 5. 4 Uhusiano wa Mwingilianomatini na Mwingilianouneni

Reisigl na Wodak (2001:90) walisema kuwa UMK hudhukuru kuwapo kwa uhusiano wa mwingilianomatini na mwingilianouneni kwenye matini, tanzu na diskosi, pia na uziada wa lugha ya jamii/ubadilikaji wa kisoshiolojia, historia ya shirika au taasisi, na ujenzi wa hali. Wakiiangazia mitazamo hiyo, wasomi hao walitalii namna uhusiano baina ya diskosi, tanzu na matini, na siasa za kijamii hubadilika.

Mwingilianomatini kulingana nao Reisigl na Wodak (2001:90), humaanisha kuwa matini moja huingiliana na matini nyingine, siku za awali na siku za baadaye. Wanazidi kusema kuwa miingiliano hiyo hurasimishwa kwa njia tofauti, kama vile kwa kurejelewa kwa mada waziwazi au mhusika mkuu, kwa marejeleo ya matukio sawa; kwa kudokezwa au kuamsha hisia; kwa kubadilisha mijadala muhimu kutoka kwa matini moja na kuipeleka kwa matini nyingine na kadhalika. Wasomi hao waliangazia kuwa uhamishwaji wa elementi fulani za matini kwenda kwa miktadha mingine hujulikana kama umuktadhishaji. Elementi fulani ya matini ikitolewa kutoka kwa matini nyingine mahsusi, hujulikana kama hatua ya ufutajimatini. Ikiwa elementi hizo zitawekwe kwenye muktadha mpya, kile hushuhudiwa kulingana nao Reisigl na Wodak (2001:91), ni umatinishajitena. Kwa (kiasi), elementi mpya za maana hupatikana kwa kuwa maana hujengeka wakati wa matumizi. Mtazamo waliokuwa nao ni kuwa umuktadhishaji huweza kudhihirika wakati

wa kulinganisha hotuba ya kisiasa pale ambapo uchaguzi wa ripoti wa hotuba hutekelezwa kutoka kwenye magazeti.

Kulingana nao Reisigl na Wodak (2001:91), usemi mmoja huwa unaingiliana na usemi mwingine kwa njia tofauti. Wasomi hawa walisema kuwa, ikiwa wataafiki kuwa "usemi", kimsingi unao uhusiano na mada, wangeshikilia kuwa, usemi kuhusiana na kubadilika kwa hali ya anga mara nyingi ingerejelewa kama mada au mada ndogo za usemi mwingine kama vile fedha au afya. Usemi huwa wazi na huzalisha mada zingine ndogo katika maeneo mengine. Kutokana na kuingiliana kwa mitazamo ya wasomi hawa na utafiti nilioufanya, suala la mwingilianomatini na mwingilianounenii lilikuwa muhimu sana kwani itakumbukwa kuwa utafiti huu ulikuwa ulihusika na ulinganuzi wa usemi wa wanasiasa katika kampeni za urais nchini Kenya miezi mitano kabla ya chaguzi za 2007 na 2013. (Tazama 4. 3 hadi 4. 3. 14)

**2. 5. 5 Mada**

Akizungumzia muundo wa makro – kisemantiki akiirejelea dhana ya mada, van Dijk (2009:68) alisema kuwa alikuwa akihimiza Uchanganuzi Hakiki (UH) utangulize kwa uchanganuzi wa muundo wa makro – kisemantiki, yaani kwa kuangazia maana ya kijumla ya mada au dhamira. Aliongezea kuwa mtazamo huo ndio ambao hudhihirisha suala la kijumla kuhusu usemi; kwani huwa ni tukio la kimakusudi na huthibitiwa na mzungumzaji kwa makini; kwa kuwa hujumuisha habari muhimu za usemi, na kuelezea kwa jumla maudhui kwa muundo wa matukio katika akili; na kwa kiwango kikubwa huwakilisha maana au ujumbe ambao wasomi hutokea kukariri katika usemi. Msomi huyo alisema kuwa sababu za kuteua mada zilitokana na ukweli kuwa; mada zilikuwa na umuhimu mkubwa kwa kuwa ndizo zilizothibitiwa na wanenaji waliokuwa na uwezo mkubwa kwa kuwa zilitokea kuathiri miundo mingine mingi ya usemi (kama mshikamano wa jumla), na kuwa zilikuwa na athari dhahiri kwa wasikilizaji na kuibua uwezekano wa masuala hayo kujikariri kwa msingi wa uwezo wa kijamii.

Akiwarejelea (Brown na Yule 1983:73), Habwe (1999:21) alisema kuwa, alirejelea mada katika utafiti wake kuhusu hotuba za kisiasa kwa lugha ya Kiswahili kwa kuwa mada zilikuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu ya kuzingatia kanuni za mshikamano katika matini. Alisema kuwa kulingana nao Brown na Yule (1983) ni kuwa, elementi ambazo

huchochewa humfunga mzungumzaji kuongea kwa kuzingatia masuala ya wakati huo; yaani matukio yaliyoko kwenye fremu mlimo mada. Utafiti huu ulijifunga katika suala la kudondoa mada zilizosheheni kampeni za urais miezi mitano kabla ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 na kampeni za urais miezi mitano kabla ya uchaguzi wa mwaka wa 2013 kwani mada hizo ndizo zilizokuwa zinadhamiriwa kuibua tofauti katika masuala yaliyochochea kampeni za chaguzi hizo mbili. Kuibuka kwa mada zilizokuwa zinatofautiana katika chaguzi hizo mbili kulichangia kudhibitisha kuwa masuala ya kihistoria kama yanavyozungukia jamii huwa dira muhimu katika kuashiria namna matumizi na uchaguzi wa lugha huvutiwa na masuala ya kijamii. Katika utafiti huu mtafiti alikuwa anayo shabaha ya kuchunguza tofauti katika mada za usemi wa wanasiasa kutokana na umuhimu wa mada hizo kuziongoza kampeni za wanasiasa wakati wa uchaguzi mkuu.

**2. 6 Uchanganuzi Hakiki wa Usemi**

Kulingana nao Wodak na Meyer (2001:1) Uhakiki wa Lugha na Uchanganuzi Hakiki Usemi ni mifumo ambayo imekuwa ikitumiwa kwa kubadilishana; hata hivyo siku za hivi karibuni UHU imetokea kutumiwa zaidi na hivyo kurejelea ile nadharia iliyojulikana kama Uhakiki wa Lugha. Aghalabu, mizizi ya UHU imo kwenye elimu ya usemaji, matini za lugha, anthropolojia, falsafa, jamii saikolojia, sayansi tambuzi, elimu fasihi na isimujamii, vilevile, lugha tumikizi na pragmatiki. Japo taaluma zilizoshehenezwa kwenye mtazamo wa UHU ni tofauti, zote hushughulikia diskosi na inayo mikabala saba iliyo na ukuruba, Wodak na Meyer (2001:2), wakiwanukuu (van Dijk 2007; Wodak 2008) waliiona kama ambayo:

1. Huvutiwa na vipengele asili vya watumiaji halisi wa lugha (badala ya kufanya utafiti wa kidhahania na mifano iliyokarabatiwa/iliyobuniwa).

2. Mitazamo yake ielekezewe jamii pana na sio maneno au sentensi zilizo pweke, na hivyo basi kuibua misingi mipya ya uchanganuzi wa: matini, diskosi, mazungumzo, vitendo vya usemi, au matukio ya mawasiliano.

3. Huafiki upanuzi wa lugha kuzidi kiwango cha sarufi ya sentensi kuuelekeza utafiti kwa mtazamo wa mtagusano na matendo.

4. Huafiki upanuzi wa mtazamo wa ishara (kama vile elimu ishara n.k), kama njia ya kutangamana na kuwasiliana: kwa ishara, picha, filamu, mtandao wa mawasiliano na njia zingine anuwai za mawasiliano.

5. Huafiki mtazamo mpana tambuzi wa jamii au njia, na mikakati ya mitagusano katika jamii.

6. Huzingatia utafiti wa majukumu ya (jamii, utamaduni, hali na utambuzi) katika miktadha ya matumizi ya lugha.

7. Hufumbata uchanganuzi mpana wa matukio ya sarufi za matini na matumizi ya lugha kama vile: muwala, balagha, upole, usemi vitendo, mitagusano, mrejeosabiki, ishara, mada, mizunguko, miundo mikubwa ya lugha, na matukio mengine ya matini na diskosi.

**2. 6. 1 Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi**

Kulingana na van Dijk (1998) Uchanganuzi Hakiki wa Usemi (UHU; ilitumiwa katika utafiti huu kurejelea Uchanganuzi Hakiki Usemi) ni uwanja ambao unahusika na uchunguzi wa matini zilizoandikwa au kuzungumzwa ili kudhihirisha chanzo cha uwezo au utawala usio na msimamo, usiokuwa na usawa na unaopendelea, kudumishwa kwake na kuzalishwa tena baina ya miktadha fulani ya kijamii, kisiasa na kihistoria.

Kwa mtazamo sawa, Fairclough (1993) akitoa fasiri yake kuhusu (UHU), alisema kuwa, "…huu ni uchanganuzi ambao hulenga kuchunguza kwa utaratibu kile kinachosababisha ushirikiano usioeleweka na maamuzi baina ya (a) utekelezaji wa matukio pamwe na matini zisizo na msimamo, na (b) mitazamo mipana na miundo ya kijamii, ushirikiano na njia; za kuchunguza vile mazoea, matukio na matini zinavyozuka kutokana na itikadi na kuegemezwa na kushirikishwa katika ushindani wa utawala na kuchunguza vile utata wa ushirikiano baina ya usemi na jamii inakuwa sababu za kusaka mamlaka na utawala". Kwa ufupi, Uchanganuzi Hakiki Usemi unalenga kuweka wazi ukuruba uliopo wa masuala tata baina ya matendo ya diskosi, matendo ya jamii, miundo ya kijamii kwa mtu yeyote ambaye hajapambaukiwa na hali husika.

### 2. 6. 2 Kanuni za Uchanganuzi Hakiki wa Usemi

Kama vile kulivyo katika nadharia zingine, waasisi wa UHU wameangazia kanuni kadhaa ambazo kwa kawaida huwa nguzo za kuegemewa na wasomi; kanuni hizo huwa:

1) UHU hushughulikia matatizo ya kijamii
2) Ushirikiano wa mamlaka hufuata hoja maalum.
3) Usemi huhusisha jamii na utamaduni
4) Usemi hutekeleza majukumu ya kiitikadi
5) Usemi ni wa kihistoria
6) Ukuruba baina ya matini na jamii huleta suluhu
7) Uchanganuzi wa usemi hufasirika na kuelezeka
8) Usemi ni mfano wa matendo ya jamii

UHU hushughulikia uchanganuzi wa lugha na ishara kama kipengele cha mielekeo ya jamii pamwe na matatizo yao. Linalozingatiwa si lugha au matumizi ya lugha pekee lakini kwa kuzingatia sifa bainifu za lugha kulingana na miundo na mienendo ya utamaduni katika jamii. Wilson (1990:19). Amesema kuwa lugha ya kisiasa husanifiwa ili kuyaafikia malengo mahususi ya kisiasa na kuwafanya watu waamini katika mambo fulani. Maelezo kama haya yanatokea kuwa idhibati tosha kuwa masuala ya kijamii huzua mijadala nyeti. Nadharia ya UHU huchanganua masuala kama haya na kuchangia katika kusawiri picha wazi, kwani mabadiliko mapya ya kisiasa katika jamii husheheni elementi mbadala za itikadi na utamaduni katika jamii. Masuala kama haya hutumiwa na wanasiasa katika siasa zao ili kuithibiti jamii husika; na kuupunguza ushindani kutoka kwa wapinzani wake.

### 2. 6. 3 Usemi, matini, muktadha,

Matumizi ya nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi hupelekea kuchunguza sehemu tofauti tofauti za matukio katika jamii; hili linamaanisha kuwa utafiti wa lugha (simulizi, andishi, utazamaji) kwa yakini husalia kuwa sehemu ya shughuli hizo zote – hivyo basi

utafiti huu sharti ufumbate taaluma zaidi ya moja. Fauka ya hayo; Ili kuchanganua, kuelewa na kuelezea utata wa masuala yanayotafitiwa inalazimu kutiliwa maanani asili ya data inayopatikana kutoka mitazamo badalia ya uchanganuzi. UHU huthamini uhusiano katika mwingiliano wa matini na mwingiliano wa misimamo baina ya matamshi, matini, tanzu na usemi, pamwe na viziada lugha katika jamii, historia ya shirika au taasisi na hali husika. Kwa kuangazia mwingiliano wa haya yote, nilitalii vile mada za usemi, mikakati ya lugha na athari zinavyobadilika kwa misingi ya siasa za kijamii kwa ajili ya mapito ya wakati.

Kama ilivyotajwa, (Rejelea 2.4.3 na 2.4.4) Mwingiliano wa matini humaanisha kuwa matini zina uhusiano na matini zingine, sasa na vilevile siku za awali. Miingiliano kama hiyo hubainishwa kwa njia tofauti tofauti: kwa kurejelea mada waziwazi au hata mhusika mkuu; kwa kurejelea matukio asilia; kwa kudokeza au kuvuta hisia; kwa kuhamisha mijadala mikuu kutoka kwa matini moja hadi nyingine na kadhalika. Mwingiliano wa matukio hudhihirisha kuwa usemi unao uhusiano kwa njia tofauti; kwa mfano, mheshimiwa William Ruto aliposema ni **sisi** tuliomfanya awe Waziri Mkuu; na sasa ametuondoa nyumbani kwetu (jamii ya Wakalenjin walipohamishwa kutoka msitu wa Mau). Wakimnukuu (Girnth, 1996), Wodak na Reisigl (2001:90) walisema kuwa **eneo la tendo** husheheni sehemu ya ukweli wa jamii katika kijisehemu cha usemi. Maeneo tofauti ya matendo huelezwa na majukumu tofauti ya utekelezaji wa misimamo. Kwa ufupi, usemi kuhusiana na suala mahususi na huenda likatangulizia kuelezeka katika uwanja mmoja na kuendelea kuelezeka katika nyanja zingine; usemi kwa hivyo husambaa katika nyanja tofauti na kupishana au kuhusisha matamshi mengine.

### 2. 7 Misingi ya Nadharia

Maana si mfumo wa uundaji wa mawazo ya aina moja, ni suala lenye mitazamo badalia na telezi na lenye utata wenye kushangaza. Kuielewa maana tuli ya matini iliyonenwa au iliyozungumzwa kunahitaji ustadi wa kina katika enzi hii tuliyo nayo. Kwa yakini, mfichuo wa habari na njia za mawasiliano ni suala pana ambalo mtu hawezi kuwa na uhakika wa habari inayomzunguka. Ili kuyaafikia malengo ya utafiti huu, Nadharia ya UHU; Usemi – Mkabala wa Kihistoria (UMK ilitumiwa katika utafiti huu kusimamia Usemi Mkabala wa Kihistoria), ambayo ni kimelea cha nadharia ya UHU ilitumiwa kwa

sababu ingeweka wazi masuala ya kihistoria ambayo ni jumuishi katika mitagusano iliyozungukia siasa nchini Kenya; hasa katika kampeni za uchaguzi wa urais nchini Kenya baina ya vipindi vilivyokuwa chini ya uchunguzi huu.

### 2. 7. 1 Usemi-Mkabala wa Kihistoria

Wodak na Meyer (2001:26) wakimnukuu (Girnth, 1996) wanasema kuwa mtazamo huu hujaribu kuweka wazi nadharia ya usemi kwa kuioanisha na maeneo ya matendo, tanzu, usemi na matini. Usemi – Mkabala wa Kihistoria huegemezwa kwenye falsafa – mwelekeo wa kijamii katika Nadharia Hakiki. Hivyo basi dhana hii hufuata uhakiki ambao hufumbata mawazo matatu yenye ukuruba; haya ni kwa mujibu wa Wodak (2001:88). Kulingana na nadharia ya Usemi – Mkabala wa Kihistoria:

1. Matini au uhakiki usemi – asili hulenga kufumbua mtanziko wa matini – fiche, au miundo semi – mfiche isiyowiana na kweli kinzani na nafsi – kinzani.

2. Uhakiki wa uchunguzi – jamii huhusika na ufichuzi wa masuala yaliyo dhahiri na yaliyo fiche na shawishivu au yaliyo na hila. Hapa huwapo na kuegemea tajriba ya miktadha na kuzitumia nadharia za kijamii na vilevile nadharia zingine kutoka taaluma zingine ili kufanikisha usimbuaji wa matukio yasiyofuata mantiki.

3. Uhakiki wa masuala ya baadaye yenye kutumainiwa katika kufanikisha mawasiliano (kwa mfano, kwa kuelezea hatua dhidi ya matumizi ya lugha isiyo latifu au kwa kupunguza vizingiti vya matumizi ya lugha katika taasisi kama vile hospitali, skuli n.k).

Maelezo yalivyobainika kuhusiana na Usemi – Mkabala wa Kihistoria ilikuwa ni kulifanya suala linalotafitiwa kwa msimamo wa mtafiti mwenyewe liwe bayana na lithibitike kinadharia kwa fasili; yaani ni kwa nini masuala mengine husheheni mantiki kuliko mengine. Kulingana na Usemi – Mkabala wa Kihistoria lugha haina nguvu yoyote ikiwa pweke – ni njia ya kuwezesha na kudumisha utawala pale ambapo watu wenye “mamlaka” wanapoitumia, Wodak (2001:88). Tukio hili bila shaka hutokea kuelezea ni kwa sababu gani Usemi – Mkabala wa Kihistoria huihakiki na kuichanganua lugha hasa

inapotumiwa na wale walioko kwenye utawala kwani wanazo nafasi za kuimarisha hali za watu.

Utawala hufungamana na ushirikiano mzuri baina ya wahusika wenye nyadhifa katika jamii fulani au wanaotoka katika jamii tofauti. Wakimnukuu Weber (1980:28), Wodak (2001) anauona utawala kama uwezekano wa mtu binafsi kuwa na hiari katika ushirika dhidi ya hiari au mapenzi ya wengine. Njia zinazotumiwa kudumisha mamlaka huwa "vitendo vya nguvu"(kulazimishwa na vurugu), kuwatawala watu kwa vitisho au ahadi, kushirikisha utawala (matumizi ya mamlaka na kunyenyekea kwenye utawala) na kuwatawala kiustadi kwa kutumia mambo kama vile njia za kuzalisha mali, usafiri, silaha na kadhalika (Popitz 1992).

Mamlaka huhalalishwa au kuharamishwa kupitia usemi; kwa kawaida matini huwa njia ya kuendeleza mapambano ya kijamii kwani hudhihirisha ishara za kutofautiana kimsimamo na kupigania mamlaka na utawala. Ni kwa misingi hii ndio mtafiti alidhamiria kuangazia matumizi tofauti ya lugha yanavyotumiwa kuangazia hali na namna utawala humilikiwa. Mamlaka hufuata mpango sio tu kwa kutumia sarufi mbadala, lakini vilevile kwa mhusika kuongoza jamii kwa njia za tanzu katika matini, au kwa kutumia utaratibu fulani wa kuufikia umma.

### 2. 7. 2 Maelezo ya Kijumla Kuhusu Mikakati ya Uchanganuzi wa Usemaji

Utafiti wa kazi hii uliiegemea nadharia ya Wodak (2001) ya UMK ili kuibusha misimamo ya wanasiasa hao watatu katika usemi wao wakati wa kampeni zao za urais katika vipindi viwili nilivyokuwa nikivichunguza. Kulingana na msomi huyo, dhana ya mkakati ilitazamwa kama njia moja ambayo husheheni chembechembe pana na pia finyu za uhakika na dhamira yenye mipango ya mazoea ambayo hutumiwa kuafikia suala fulani la kijamii, kisiasa, kisaikolojia au lengo la kiisimu. Mikakati ya usemaji hupatikana katika hatua tofauti zenye utata katika utaratibu wa kiisimu. Katika kazi yao Reisigl na Wodak (2001) mikakati ya usemi imezungumziwa walipouchanganua usemi wa kiubaguzi na upinzani wa kisemiti kwa kuirejelea mikakati ya nadharia ya UMK. Katika kazi yake Wodak (2001); kumeorodheshwa aina tano za mikakati ya usemaji ambayo ni:

1. Mkakati wa Unominishaji / Urejelezi

2.Mkakati wa Uarifishaji
3.Mkakati wa mkabala
4.Mkakati wa Ubishi
5.Mikakati ya Uzidishaji na Upunguzaji wa Uzito

Mikakati inayohusu uwasilishwaji “wetu” na “wao” kama ilivyozungumziwa na Reisigl na Wodak (2001) inatumiwa kuchanganulia usemi wa ubaguzi, kama vile wa rangi, na usemi wa mitazamo ganda; kwa hakika inajaribu kuyajibu maswali yanayofumbatwa na mikakati mitano ya uchanganuzi wa usemaji kama vile ambavyo huchangia kuisawiri picha ya mitazamo miwili ya usemi ambayo huwa uwasilishwaji wetu chanya na wao hasi.

**2. 7. 3 Mkakati wa Unominishaji / Urejelezi**

Mkakati wa Unominishaji ni mkakati ambao huhusika na namna mtu anavyotajwa na kurejelewa kilugha. Mkakati huu wa kwanza hulenga kujenga na kuwakilisha wahusika wa kundi fulani la kijamii Wodak (2001). Ili kuyafanya maelezo ya mkakati huu kuwa bayana ni aula kusema kuwa mkakati wenyewe huwa kama picha ambayo hudokeza namna mhusika anavyotajwa ambapo tukio lenyewe huwakilisha usemaji na nafasi ya kundi husishwa na pia kundi lisohusishwa. Kwa yakini vifaa ambavyo hutumiwa kuashiria kutumiwa kwa mkakati huu huwa matumizi ya njia bainishi kiuwanachama, kwa kumrejelea mhusika kitamathali, kibayolojia, kiasilia na kwa matumizi ya sitiari za kumpuja mtu waziwazi au kwa njia isiyokuwa wazi.

**2. 7. 4 Mkakati wa Uarifishaji**

Baada ya kujengwa au kutambuliwa, wahusika wa kijamii awe mtu binafsi, kundi la wanachama au makundi husika huarifishwa kwa njia ya lugha. Mikakati ya uarifishaji wakati mwingine hutambuliwa kama jambo ganda na huweza kutathminiwa kitabia kwa mtazamo chanya au hasi kwa umbo la lugha lililowazi au linalojitokeza kwa kuelezewa. Mikakati hii hudhamiria aidha kutambulisha wahusika wa kijamii kwa njia ambayo huenda ikawa inazidisha au kupunguza namna wanavyosawiriwa kiunafiki au kwa kuthaminiwa kwa njia chanya au hasi (Reisigl na Wodak 2001). Mikakati hii haiwezi ikatenganishwa na mikakati ya unominishaji kwa urahisi. Kwa yakini, mikakati mingine ya urejelezi inaweza kuchukuliwa kwa njia mahususi kuwa mikakati ya uarifishaji, kwa

kuwa utambuaji wa mikakati ya urejelezi huhusisha umaanishaji dhahiri na pia udokezaji wa maana kwa kuelezea wahusika wa kijamii kwa njia ya kiunafiki au kwa kuwathamini.

### 2. 7. 5 Mkakati wa Mkabala

Barasa (2014) amesema kuwa Mkakati huu wa Mkabala hutumiwa na wanasiasa kama kiashiria cha kuisawiri picha kuhusu kina cha kuhusika kwa usemi wa wanasiasa. Tukio hilo huweza kutambuliwa ikiwa kutakuwa na nukuu, utoaji taarifa, matumizi ya simulizi au kwa kuelezewa. Wanenaji huweza kudhihirisha haya kwa kujihusisha (hujidhihirisha kwa ukwepaji, kwa urudiaji, au kwa kutenganishwa kama vile kwa alama za kuzidisha na ishara), au kutengwa (kwa matumizi ya kishazi kirejeshi, kishazi kihusishi, unominishaji au usemi wa taarifa).

### 2. 7. 6 Mkakati wa Ubishi

Utafiti huu uliweza kutathmini njia zilizotumiwa na wanasiasa kuiendelezea mijadala na ubishi wao katika kampeni za urais. Hili lilifanywa kama njia moja ya kutambulisha kuwa watu na makundi fulani ya watu katika jamii hujaribu kuyahalalisha madai yao kwa utaratibu mahususi katika matumizi yao ya lugha. Mkakati huu wa ubishi huwa una ukuruba wa kina na matukio ya ushawishi, hila na uhalalishaji usemi wa kibaguzi. Kama njia moja ya kuafikiana na utaratibu katika uchanganuzi wa ubishi; topoi hutumiwa. Barasa (2014) alitaja kuwa dhana ya topoi hutumiwa katika mkabala wa mbinu – pembuzi ambayo hudhihirisha ubishi kama utaratibu. Akiwanukuu Reisigl na Wodak (2001), Barasa (2014) alisema kuwa mkakati wa ubishi huthibitisha ishara chanya au hasi kuhusu mtu au kundi fulani la watu. Reisigl na Wodak (2001) walitilia mkazo hasa kwenye topoi wakisema kuwa, kwa kawaida hiyo ndiyo njia ambayo matukio chanya au hasi huthibitishwa kwayo. Walizidi kudhihirisha kuwa, topoi kwa kawaida hutumiwa katika usemi wenye upendeleo au kubagua ili kuhalalisha kutengwa kwa wahamiaji kwa kutumia mijadala yenye kusheheni ukweli wa kiasi kama vile, hao ni mzigo kwa jamii, “wana ghalama kubwa”, “utamaduni wao ni tofauti” na kadhalika. (Tazama 2.7.2 hadi 2.7.4, utambuaji na utumiaji wa topoi).

### 2. 7. 7 Mikakati ya Uzidishaji na Upunguzaji wa Uzito

Mikakati ya uongezaji wa uzito huwa upande mmoja, na mikakati ya upunguzaji wa uzito hutokea kwa upande wa pili. Mikakati hii husaidia kuvumishia na kupunguzia hadhi ya kihusishi kwa kuongezea au kupunguzia nguvu ya ilokusheni ya usemi wa ubaguzi wa rangi, usemi usiopendelea kisemiti, usemi wa kitaifa au usemi wa kikabila. Mikakati hii huchukua nafasi muhimu katika uwasilishaji usemi kutokana na utendakazi wake wa kutia makali au upunguzaji makali. Reisigl na Wodak (2001) waliutaja mkakati huu kama ambao huvumisha ufahamu wa ukubalifu wa vihusishi. Utafiti huu ulilenga kubainisha kama wanasiasa hao watatu waliutumia usemi uliokuwa wa kubagua na kama ulibeba chembechembe za uzito au la.

### 2. 7. 8 Matumizi ya Topoi katika Uchanganuzi wa Ubishi

Matumizi ya topoi katika kuchanganulia mkakati wa ubishi huegemewa sana pale usemi wenye chembechembe za kutenga na kubagua huwa umejitokeza Barasa (2014). Kwa sababu utafiti huu ulikuwa unahusu usemi wa kisiasa kulikuwa kuna haja ya kuelezea dhana ya topoi, namna topoi huweza kubainishwa katika usemi na nafasi ya upotoshaji katika uchanganuzi wa ubishi.

### 2. 7. 9 Topoi

Dhana ya topoi imezungumziwa na wasomi wengi lakini utafiti huu ulijikita kwenye maelezo ya kijumla yaliyokuwa yameafikiwa na wasomi wengi; Reisigl na Wodak (2001:75) waliuafiki mtazamo wake Keinpointer (1992:194) kwa kumnukuu:

> Topoi au loki inaweza kuelezewa kama sehemu ya ubishi inayohusiana na uwajibikaji, uwe wa ukweli au wenye 'kauli iliyohitimishika'. Huwa na uhusiano na yale yaliyomo au 'kanuni za mahitimisho' ambazo huunganisha mjadala au mijadala na hitimisho au madai. Kwa hivyo, huthibitisha mabadiliko kutoka kwenye mijadala kuelekea kwenye hitimisho".

Reisigl na Wodak (2001) waliongezea kusema kuwa wachanganuzi wa usemi lazima wakumbuke kuwa nafasi ya ubishi na upotoshaji ulio au usiokuwa na ukubalifu hausawiriki vyema hasa pale utabiri wa kibaguzi ni sehemu ya utaratibu wa ubishi.

### 2. 7. 10 Ubainishaji wa Topoi

Uchanganuzi wa mijadala ya ubishi yenye uhusiano wa yaliyomo unaweza kutekelezwa kinyume na orodha yao Reisigl na Wodak (2001) waliyoiona kuwa haijakamilika na kuwa haikukinzana. Barasa (2014: 69) alimnukuu Wodak (2006:74) aliyekuwa ameorodhesha topoi kwa njia ifuatayo: jambo liso maana, faida, kasoro, maelezo, tafsili ya jina, hatari na tishio, utu, haki, uwajibikaji, mzigo, upimaji, fedha, ukweli, sheria na haki, historia, nambari, utamaduni na dhuluma. Akimnukuu Zagar (2010), Barasa (2014) alisema kuwa hakuna orodha moja ya aina za topoi ambayo inaweza kutumiwa katika uchanganuzi wa usemi; aliongezea kusema kuwa topoi zaidi zinaweza kuongezewa kwenye orodha ya topoi za awali; aliongezea kusema kuwa, pia topoi zinaweza kudondolewa kwenye orodha. Kama njia moja ya kuafikiana na mtazamo wake Barasa (2014); utafiti huu ulizirejelea topoi chache ambazo mtafiti aliziteua pasina kufuata utaratibu mahsusi.

### 2. 7. 11 Upotoshaji katika Ubishi

Kulingana nao Reisigl na Wodak (2001:110) utaratibu wa ubishi huwa na mashiko au upotoshaji.  Wodak amesema kuwa kuna mantiki zenye kanuni kwenye mijadala shindani na inayojenga kuwezesha ubainishaji mzuri wa topoi kwenye upotoshaji. Kwa mujibu wa Reisigl na Wodak (2001) baadhi ya sheria za uteuzi wa dhana za upotoshaji huwa; uhuru wa kujadili, wajibu wa kutoa sababu, marejeleo sawa ya mkinzani katika usemi wa awali… na uwazi katika uwelezaji na tafsiri isiyo na kasoro; wasomi hawa walishikilia kuwa, ikiwa kanuni hizo hazitakuwa zimezingatiwa basi, madanganyo huwa yametokea. Hata hivyo, walikiri kuwa si kazi rahisi kutofautisha ikiwa utaratibu wa ubishi umetumiwa ipasavyo kama topoi au kama upotoshaji ikiwa mtu hana uwelewa wa muktadha wa awali. Mtazamo wao Reisigl na Wodak (2001:114) kuwa uchanganuzi wa topoi na upotoshaji wenye mfanano wa uhusiano wa yaliyomo hutegemea mada za kimakro. Mtazamo huo ulikuwa dira wakati wa kuzitofautisha topoi na upotoshaji kwenye utafiti huu.

### 2. 7. 12 Vifaa vya Uchanganuzi na Kanuni za Usemi – Mkabala wa Kihistoria

UMK huwa ya Pande-Tatu; baada ya;

(1) Kutambua yaliyomo au mada mahususi katika usemi,

(2) Mikakati ya usemaji huchunguzwa; hatimaye,

(3) Njia za lugha (aina) mahususi, muktadha – huru tambuzi wa lugha (kama ishara) huchunguzwa.

Ili kuweza kuafikiana na mtazamo malengo ya utafiti, maswali yafuatayo yalimuongoza mtafiti ili kuyaafikia malengo ya utafiti:

1) Wanasiasa katika kampeni za urais waliongozwa na mada zipi za usemi katika chaguzi zote mbili?
2) Mada za usemi husika ziliingiliana na kutofautiana vipi katika chaguzi zote mbili kwa mujibu wa itikadi za vyama na miungano?
3) Mada za usemi zilichochewa vipi na matukio ya kihistoria?
4) Ni mada zipi za usemi zilizoakisika katika uchaguzi fuatilizi?
5) Viwango vya wanasiasa katika kuziangazia mada za usemi fulani fulani zilitofautiana vipi?

Kama ilivyosemwa na Wodak (2001), (Tazama 2.5) kunayo mikakati kadhaa ambayo hutiliwa maanani wakati wa kuchanganua usemi na matini zinazoingiliana, Wodak (2001:94) aliangazia aina tano ya mikakati yenye kufuata mantiki na ambayo kwa yakini ilifungamana na suala la utafiti. Wasomi hawa walisema Kuwa, “mkakati” kwa jumla hufungamana na utaratibu wa kimataifa (kujumlisha hoja maalum) na ambapo hutumiwa ili kufanikisha kuyaafikia malengo ya kijamii, kisiasa, kisaikolojia au matumizi ya lugha.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3. 1 Utangulizi

Sura hii ilijikita katika kuangazia njia za utafiti zilizotumiwa na mtafiti ambapo alielezea ala tofauti tofauti zilizoegemewa katika ukusanyaji wa data na jinsi data husika ilivyochanganuliwa na kufasiriwa ili kufanikisha harakati za kuyajibu maswali ya utafiti.

## 3. 2 Njia za Utafiti

Tafiti nyingi katika nadharia ya UHU huchanganua "matini asili"; kwa kuangazia vile uasili huo huwa katika hali gani ya kijamii, na katika mwelekeo gani wa shida za kijamii; hata hivyo haya husalia kutokuwa wazi. Kutokana na mkabala huu mtafiti aliitumia njia ya kimaelezo kwa kuwa utafiti huu ulikuwa wa kiuchunguzi ukiazimia kuuchunguza usemi wa wanasiasa watatu wakati wa kampeni miezi mitano kabla ya chaguzi kuu za mwaka wa 2007 na 2013. Wanasiasa hao walikuwa Raila, Uhuru na Ruto. Orodho (2003) alisema kuwa ukaguzi wa kimaelezo hutumiwa katika utafiti wa kuelezea kwa kuwa humpa mtafiti nafasi ya kukusanya data, kuifupisha data, kuiwasilisha na kuifasiri akikusudia kuiweka wazi. Utafiti huu pia unaingiliana vyema na utafiti wa kimaktaba (Kimaandishi). Njia hii kama vile imeelezwa iliwasilisha uchanganuzi aula kwa kufasiri na kuelezea matokeo ya utafiti kuambatana na ulinganuzi wa usemi wa kisiasa katika vipindi vilivyokuwa chini ya utafiti huu. Kwa kuwa utafiti huu uliwalenga wanasiasa waliokuwa miongoni mwa wanasiasa waliokuwa na msukumo mkubwa katika siasa za nchi ya Kenya katika chaguzi mbili zilizokuwa zimelengwa; mtafiti aliongozwa na usemi wa kila mwanasiasa kama njia ya kuubainisha usemi wa wanasiasa hao kutoka kwa magazeti mawili makuu nchini Kenya ambayo ni *'The Standard'* na *'Daily Nation'*. Wanasiasa hao walikuwa Uhuru Kenyatta, William Ruto na Raila Odinga ambao walikuwa wameshiriki kikamilifu katika kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2007 na 2013.

## 3. 3 Muktadha wa Utafiti

Utafiti huu ulivilenga vipindi viwili tofauti vya uchaguzi wa kitaifa ambapo uchaguzi mkuu nchini Kenya hufanywa kila baada ya miaka mitano ikiwa hakuna jambo lolote

ambalo linaweza kuchochea kufanyika kwa uchaguzi mkuu kabla ya kutamatika kwa kipindi hicho. Kwa mujibu wa muktadha wa utafiti huu, uchaguzi ulifanywa katika mwaka wa 2007 na 2013 ambapo mtafiti aliikusanya data akiilenga miezi mitano kabla ya chaguzi zote mbili. Katika uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2007 mtafiti aliurejelea mwezi wa Agosti (2007), Septemba (2007), Oktoba (2007), Novemba (2007) na Desemba (2007) na kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2013 miezi mitano kabla ya uchaguzi huo mtafiti aliurejelea mwezi wa Oktoba (2012), Novemba (2012), Desemba (2012), Januari (2013) na Februari (2013).

### 3. 4 Uteuzi wa Data

Njia ya kimakusudi ilitumiwa katika kuiteua data ya utafiti, Patton (1990:169) alisema kuwa uwezo na mantiki katika usampulishaji wa kimakusudi hujihusisha na uchaguzi wa taarifa yenye kadhia nyingi ili kutekeleza utafiti wenye kina. Msomi huyo alizidi kusema kuwa jukumu la usampulishaji wa kimakusudi huwa ni kufanikisha uchunguzi wa habari za kina ambazo zinaweza kuakisika kwenye maswali ya utafiti unaolengwa. Kando na mtazamo wake Patton (1990) mtafiti alimrejelea Nwadito (1999) aliyesema kuwa njia hii ni bora pale mtafiti anaazimia kupata data ya kusudi fulani. Gal (1996) kwa upande wake alidokeza kuwa mtafiti anahitaji kwenda kwenye chanzo cha data bila wasiwasi ikiwa anafahamu kile anachokilenga. Chini ya usampulishaji wa kimakusudi mtafiti aliuegemea mtazamo wake Patton (1990:174) aliutaja kama usampulishaji wa matukio kiuhakiki kwa kuwa njia hiyo huvichunguza visa au habari zenye mashiko. Kulingana naye matukio yenye upeo mkubwa ni yale yanayoweza kutoa fununu ya jambo kwa njia ya kuacha shauku au kwa kuwa yana umuhimu katika mpangilio wa mambo kama yalivyo. Uhuru Kenyatta, William Ruto na Raila Odinga walirejelewa kwa kuwa walikuwa miongoni mwa wanasiasa waliokuwa na msukumo mkubwa katika vyama vyao, pia walijihusisha na kampeni za kiti cha urais katika chaguzi hizo mbili. Magazeti yaliyoteuliwa yalikuwa *Daily Nation* na *The Standard* kwa kuwa uenezwaji wake ulikuwa wa juu zaidi kutokana na kuwa na wasomaji wengi ikilinganishwa na gazeti la Kiswahili lijulikanalo kama Taifa Leo. Japo utafiti huu ulifanywa kwa lugha ya Kiswahili usampulishaji ulifanywa kutoka kwa magazeti ya *Daily Nation* na *The Standard* kwa kuwa kulikuwa na uwezekano wa matukio ya wanasiasa hao kupatikana humo.

### 3. 5 Ukusanyaji wa Data

Ukusanyaji wa data ya utafiti ulihusu usemi wa kisiasa katika kampeni za urais nchini Kenya. Ili kutokea na data yenye mashiko mtafiti aliutumia usampulishaji wa vigeu kimakusudi kwa kuyasoma magazeti ya *Daily Nation* na *The Standard* ambapo nukuu za wanasiasa husika zilikusanywa. Usemi uliolengwa ulikuwa wa Uhuru Kenyatta, William Ruto na Raila Odinga. Kuteuliwa kwa magazeti hayo kulitokana na imani kuwa matini tarajiwa zingepatikana na hivyo basi kufanikisha malengo ya utafiti. Kuteuliwa kwa magazeti hayo kulichochewa na imani kuwa magazeti hayo ndiyo yaliyokuwa na historia ndefu nchini Kenya, tena kiwango cha kuenea kwake na uwezekano wake kuhodhi habari na matukio mengi ya wanasiasa hao waliokuwa wameteuliwa kwenye utafiti. Kuteuliwa kwa Uhuru Kenyatta, William Ruto na Raila Odinga kulifanyika kimakusudi kutokana na imani kuwa wanasiasa hao walichukua nafasi za kina katika kampeni za vipindi vyote viwili. Niliongozwa na nukuu za kila mwanasiasa kuziafikia mada za usemi katika kuiteua data iliyojenga msingi wa kampeni za urais miezi mitano kabla ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 na miezi mitano kabla ya uchaguzi wa mwaka wa 2013 (Tazama 4.3 hadi 4.3.14). Baada ya kuyasoma magazeti hayo, mtafiti alizibainisha nukuu 206 alizozipa nambari na kuzitumia katika kuelezea matokeo ya utafiti; idadi ya nukuu za kila mwanasiasa iliweza kusawirika kwenye grafu ya kila mada (Tazama 4.3 – 4.3.14). Ukusanyaji wa data ulitekelezwa baada ya kupewa kibali na Halmashauri ya Kitaifa ya Sayansi na Teknolojia (HKST) inayojulikana sasa kama, Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi (TKSTU). (Tazama kiambatisho katika ukurasa wa 226).

### 3. 6 Kundi Lengwa

Kwa sababu siasa hasa katika uchaguzi mkuu huwakutanisha wagombeaji wa kiti cha urais kutoka katika vyama tofauti, mtafiti aliudondoa usemi wa wanasiasa na hatimaye kuiafikia mada kutokana na usemi kwa mujibu wa vipindi husika pamwe na wanasiasa husika; yaani, Uhuru Kenyatta, William Ruto na Raila Odinga kwenye chaguzi zote, ule wa 2007 na ule wa 2013. Uhuru Kenyatta aliteuliwa kutokana na kuhusika kwake katika kampeni zote mbili ambapo katika uchaguzi wa mwaka wa 2007 alinukuliwa akimpigia debe rais mustaafu Mwai Kibaki aliyekuwa katika chama cha PNU na katika mwaka wa 2013 mwanasiasa huyo alikuwa amejitosa kwenye kinyanganyiro hicho cha kiti cha urais kikamilifu na ambapo William Ruto aliyekuwa ameipinga miondoko yake wakati wa

uchaguzi wa mwaka 2007 alikuwa mshiriki wake wa karibu katika uchaguzi huo wa mwaka wa 2013. William Ruto aliteuliwa kutokana na misimamo yake iliyokuwa haitetereki kama ilivyodhihirika kutokana na kuwaunga mkono wapinzani wawili katika chaguzi mbili tofauti; mmoja katika kipindi kimoja na mwingine katika kipindi kingine tofauti. Usemi wa mwanasiasa huyo ulikuwa na umuhimu mkubwa kwa kuwa yeye pekee katika wanasiasa kwenye utafiti ndiye aliyekuwa amezipigia siasa zake akiwa katika ngambo mbili tofauti. Kama vile ilivyodhihirika nukuu za usemi wa mwanasiasa huyo ziliongozwa na itikadi katika chama au muungano ambao alikuwa anauhusudu baina ya vipindi hivyo viwili (Tazama 4.3 hadi 4.3.14). Raila Odinga aliteuliwa kwa kuwa alikuwa mwanasiasa aliyebobea katika siasa na kutokana na kuhusika kwake katika siasa akiwa katika upinzani kulikuwa na haja ya kuupigia usemi wake darubini baina ya vipindi hivyo viwili ikizingatiwa kuwa wapinzani wake walikuwa tofauti katika uchaguzi ule wa 2007 na 2013. Itakumbukwa pia kuwa mapigano yaliyotokea nchini Kenya katika mwaka wa 2008 baada ya rais mstaafu Mwai Kibaki kutangazwa kuwa mshindi yalidaiwa kusababishwa na usemi wa chuki kutoka kwa wanasiasa tajika kutoka katika muungano wa PNU na chama cha ODM. Ni vyema kukumbusha kuwa wanasiasa walioteuliwa na mtafiti walikuwa vigogo katika miungano na vyama katika kampeni zile za mwaka wa 2007 na zile za mwaka wa 2013.

### 3. 7 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa njia ya maelezo baada ya utambuaji wa mada za usemi na uelezaji wa sehemu muhimu za lugha kama zilivyotumiwa na kuwahusisha wanasiasa katika kampeni za urais. Mbinu hiyo ya maelezo ilitumiwa kwa kuizingatia nadharia ya Usemi – Mkabala wa Kihistoria ambayo ni kimelea cha UHU kwa kuirejelea mikakati husika. Kwanza, uchanganuzi ulijihusisha na kuziangazia Mada za Usemi za chaguzi zote mbili miezi mitano kabla ya uchaguzi ule wa 2007 na 2013 (Tazama 4.3 hadi 4.3.14), pili, mikakati iliyotumiwa na wanasiasa hao iliangaziwa kwa kuirejelea nadharia ya UMK yao Reisigl na Wodak (2001:94); (Tazama 5.2 hadi 5.5), na tatu, kutathmini athari ya usemi wa wanasiasa hao waliokuwa wameteuliwa kama asili ya data (Tazama 5.6 hadi 5.6.3). Kwa mujibu wa Reisigl na Wodak (2001) uchanganuzi wa data kuhusiana na utafiti huu uliyazingatia maswali matano ambayo yaliakisi sifa za mtazamo wao Reisigl na Wodak (2001:93):

1. Wanasiasa katika kampeni walitajwa na kurejelewa vipi kilugha?

2. Wanasiasa husika walihusishwaje na tabia zao, ustahilifu wao, sifa bainifu zao na usemi wao?

3. Ni kwa njia gani utaratibu wa mijadala na ubishi wa wanasiasa hao ulivyoafiki na kuhalalisha kutengwa, kuchujwa, kugandamizwa, kubaguliwa na kunyonywa kwa kundi moja na lile jingine?

4. Ni kwa mtazamo gani ambapo majina, sifa na mijadala kuhusiana na wanasiasa hao ilivyoendelezwa?

5. Je, usemi wa kubagua ulitolewa waziwazi, ulikuwa unazidisha au kupunguza uzito?

Kutokana na maswali hayo matano mtafiti aliichagua mikakati mitano ya usemaji ambayo hutumika kuelezea hali mbili tofauti za wahusika katika usemi ambazo ni; uwasilishwaji 'wetu' chanya na uwasilishwaji 'wao' hasi. Ili kuyaafikia malengo ya utafiti huu mtafiti aliichanganua data husika kwa kujikita katika kila lengo kama njia moja ya kuchochea matokeo yenye mashiko. Katika lengo la kwanza mtafiti aliuegemea mtazamo wao Wodak na van Dijk (2008:58) waliposema kuwa kama kunayo kategoria ambayo huwa lazima kuhusishwa katika utafiti wa mijadala katika bunge ni mada. Kwa kuwa mtazamo wao ulikuwa ukiakisika katika utafiti huu; mada za usemi zilirejelewa ili kuyaelewa masuala ya kihistoria yaliyotumiwa na wanasiasa kama nyenzo ya kuivutia jamii. Kulingana nao Wodak na van Dijk (2008:58) dhana ya mada za usemi husemwa (kimakro) kama kauli ambayo huhusisha maana ya matini au usemi kilimwengu. Kutokana na kuegemewa kwa mtazamo huo na mtafiti, mada za vipindi vyote viwili zilichunguzwa ili kubainisha mada zilizozijenga kampeni za wanasiasa hao katika uchaguzi ule wa mwaka wa 2007 na ule wa 2013. Utafiti ulibainisha kuwa mada za usemi zilichochewa na mambo kama vile, mgombeaji kiti alikwa nani, matukio ya kihistoria yalikuwa yapi, jamii iliyolengewa ujumbe ilikuwa gani na mwisho masuala ibuka katika jamii yalikuwa yapi. Lengo la pili

lilijadiliwa na mtafiti akiiangazia mikakati iliyotumiwa na wanasiasa hao katika vipindi hivyo viwili kwa kuongozwa na nadharia ya UHU; Usemi – Mkabala wa Kihistoria. Uchanganuzi wa mikakati uliegemezewa mitazamo yao Reisigl na Wodak (2001), ambapo mikakati iliyotumiwa ilikuwa mkakati wa Urejelezi, Uarifishaji, Ubishi, Mkabala na Uongezaji na Upunguzaji wa Uzito. Lengo la tatu la utafiti lilijikita katika kuzitathmini athari ambazo zilichochewa na usemi wa wanasiasa waliokuwa wameteuliwa kama asili ya data ya utafiti. Wanasiasa hao walikuwa Uhuru Kenyatta, William Ruto na Raila Odinga.

### 3. 8 Matumizi ya Grafu

Kastellec na Leoni (2007) katika kazi yao ya Utumiaji wa grafu badala ya majedwali katika sayansi ya kisiasa walisema kuwa lengo lao lilikuwa kuwahimiza wanasayansi wa kisiasa kwa kuangazia kuwa taarifa nyingi ambazo huwasilishwa kwa kutumia majedwali zinaweza kuwasilishwa vyema kwa njia ya grafu. Walisema kuwa ikiwa azimio ni kuipa hadhira ufahamu wa data ili kuweka msingi wa uchanganuzi wa takwimu fuatilizi, basi waliamini kuwa maelezo ya takwimu kwa matumizi ya grafu ni uchanganuzi ulio bora zaidi. Wasomi hao walizidi kusema kuwa grafu hurahisisha ulinganuzi wa vigeu ambavyo vinaweza kuwa muhimu katika ukadiriaji wa uchanganuzi usio tuli. Kastellec na Leoni (2007) walionyesha kuwa grafu hurahisisha ulinganuzi wa vigeu vya seti mbili au zaidi. Kwa kuwa mtafiti alikuwa akiulinganisha usemi wa wanasiasa katika kampeni, matumizi ya grafu kuambatana na mapendekezo yao Kastellec na Leoni (2007) yalifumbatwa.

Mtafiti alimrejelea van Dijk (2008:58) aliyesema kuwa, kama kuna kategoria za usemi ambazo hazina budi kujumuishwa kwenye utafiti wa majadiliano katika bunge ni kategoria za mada za usemi. Mada za usemi zimeelezwa kidhahania (kimakro) kama masuala yanayojumuisha maana ya kijumla (muundo wa kimakro – kisemantiki) ya matini au usemi. Kama njia moja ya kuyaafiki maelezo yake van Dijk (2008) ya umuhimu wa kategoria ya mada katika uchanganuzi wa majadiliano katika bunge, mtafiti alitumia grafu kama kiashiria kimoja cha kufanikisha uchanganuzi wa data iliyokuwa imekusanywa ambapo shabaha ya kwanza ya utafiti ilikuwa kuangazia tofauti katika usemi wa wanasiasa miezi mitano kabla ya chaguzi za mwaka wa 2007 na 2015. Kila mada iliyozungumziwa na wanasiasa walioteuliwa katika vipindi hivyo viwili ilionyeshwa kwa

njia ya grafu mseto ili kuchangia katika kuisawiri picha bora kuhusu mada zilizoenziwa na wanasiasa hao. Kabla ya matokeo hayo kuonyeshwa kwenye grafu umaratokezi wa kila mada ya usemi ulizingatiwa na mtafiti; idadi ya nukuu iliyoafikiwa na mtafiti ilikuwa 206. Grafu zote zilibeba matokeo ya wanasiasa wote watatu kila grafu ikiwaweka wanasiasa hao mkabala na mwingine. Grafu moja ilibeba mada aina moja ya usemi, upande mmoja ukiwa umejikita katika mwaka wa 2007 na mkabala na mwaka huo kulikuwa na mwaka wa 2013. Njia hii ilikuwa bora kwa kuwa kila mada ya usemi ilidhihirisha kuwa kulikuwa na tofauti ya kuenziwa kwa mada moja kuliko mada nyingine na wanasiasa hao katika kampeni zao. Magazeti yaliyotumiwa kama mkakati mmoja wa kuipata data yalionyeshwa katika kila grafu kwa pamoja kama njia moja ya kutofautisha umaratokezi wa kunukuliwa kwa wanasiasa hao katika kila mada ya usemi. Umbali wa kwenda juu kwenye grafu ulionyesha matokeo ya mwanasiasa kama alivyokuwa amenukuliwa kwenye gazeti moja kuwapiku wapinzani wake katika kuizungumzia mada moja ya usemi zaidi ya wenzake katika vipindi vya kampeni hizo.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI WA DATA NA UFASIRI

## 4. 1 Utangulizi

Ili kufanikisha uchanganuzi na ufasiri wa data ya utafiti huu uliowahusu Uhuru Kenyatta, Raila Odinga na William Ruto ilikuwa muhimu kwanza kuzingatia umuhimu wa kuzibainisha mada za usemi kwani utafiti wenyewe ulikuwa ukijihusisha na ulinganuzi wa usemi wa kisiasa katika kampeni za urais miezi mitano kabla ya chaguzi kuu mbili za urais ambazo zilikuwa zile za mwaka wa 2007 na 2013. Kwa kuwarejelea wasomi kadhaa, mtafiti ameuzungumzia umuhimu wa kuziangazia mada za usemi katika kampeni za wanasiasa hao. Kama njia moja ya kuisawiri picha safi kuhusiana na mada za usemi mtafiti amepiga hatua zaidi na kuzitumia grafu katika kila mada lengo likiwa kuweka msingi wa uchanganuzi wa data. Ni vizuri kutaja kuwa umaratokezi wa uteuzi wa mada moja au nyingine uliangaziwa na kila grafu kufungamana na mada za usemi. Kama ilivyobainishwa kila grafu iliwajumuisha wanasiasa hao watatu kwa kuangazia nukuu za kila mmoja wao.

## 4. 2 Uteuzi wa Mada

Akiwanukuu Brown na Yule (1983:89); Crystal na Davy (1969), Habwe (1999:181) alidai kuwa sifa moja muhimu inayotofautisha mazungumzo ya kawaida na aina zingine za usemi ni kuwa mazungumzo ya kawaida hayana mada moja ya kipekee ambayo huteuliwa mwanzoni mwa mazungumzo. Msomi huyo alishikilia kuwa uteuzi wa mada huafikiwa na washiriki kutegemea kanuni za uhusiano. Habwe (1999) alizidi kuangazia kuwa katika hotuba za kisiasa huwa kuna utata wa kiasi kwani kama sheria, mada huteuliwa kabla jambo kusemwa na kuwa ni kutokana na msingi wa mpango huo ndipo leseni katika usemi hutolewa. Aliwanukuu Haugerud na Njogu (1991) ambao walikuwa na mtazamo kuwa kundi lolote likipanga mkutano jambo ambalo huzingatiwa ni kule kulilenga jambo la kuzungumziwa katika mkutano huo. Msomi huyo aliongezea kuwa wazungumzaji tofauti wanapotokea kuhutubia mkutano ambao huwa umeyaafikia masuala ya kuzungumzia, aghalabu masuala mengine ibuka ambayo hayakuwa yamelengwa kuzungumziwa hupenyeza katika usemaji wa wahusika hao. Maelezo yake msomi huyo yaliasikika katika

utafiti huu ambapo katika kuangazia nukuu za wanasiasa niliowateua, mada za usemi zilichangia katika kuupa utafiti huu mashiko ikizingatiwa kuwa lugha iliyotumiwa pamwe na mikakati ya usemi ilizungukia mada za usemi. Itakumbukwa kuwa mtafiti alikuwa amemrejelea van Dijk (2008: 58) aliyekuwa amesema kuwa katika utafiti wa usemi wa majadiliano katika bunge kategoria za mada huwa muhimu kuzingatiwa. Mtazamo huo ulikuwa ukiakisika katika utafiti huu kwani ulizihusu siasa za wanasiasa na masuala ambayo yangewezesha kampeni zao kunoga. Ni vyema kuangazia kuwa kuzungumziwa kwa masuala yaliyofungamana na mada za usemi kuliingiliana vyema na matukio ya kihistoria katika chaguzi hizo mbili.

### 4. 3 Mada za Usemi za Mwaka wa 2007 na 2013

Akizungumzia siasa na lugha Chilton (2004:4), alimnukuu Hague *et: al* (1998), ambaye alimnukuu pia Miller (1991) aliyesema suala la siasa kwa yakini linahusu kujadiliana na kushawishi. Wazo hili linaashiria haja ya kuelezea vile matumizi ya lugha yanaweza kuathiri mamlaka, uhalali, makubaliano na yote yanayotambua asili ya siasa. Mada za Usemi zilizotumiwa na wanasiasa kuziaka kampeni zao miezi mitano kabla ya uchaguzi wa 2007 zilichochewa na masuala yaliyozungukia jamii, historia au hata kwa kuibuka. Ili kuiafikia mada fulani ya usemi niliangazia umaratokezi wa nukuu zilizoaangaziwa na wanasiasa niliokuwa nimewalenga ili kuyaafikia malengo yangu. Idadi za nukuu husika zilidondolewa kutoka kwenye magazeti mawili yaliyorejelewa; magazeti ya '*The Standard'* na '*The Daily Nation';* nukuu husika ziliwazungukia Uhuru Kenyatta, Raila Odinga na William Ruto. Kwa kawaida wanasiasa hulenga kuishawishi jamii, hivyo basi ushawishi wowote ule haujengwi kwenye ombwe tupu; hujengwa kwenye masuala yamhusuyo binadamu katika maisha yake ya kila siku; usemi wa kisiasa katika kampeni za urais miezi mitano kabla ya uchaguzi wa mwaka 2013 uliegemezwa kwenye masuala fulani ya 2007 ya kijamii. Kutokana na misingi hii ni wazi kusema kuwa siasa zilipigwa kwa misingi ya mambo yaliyoiathiri jamii hivyo kuibusha mada za usemi zenye kuzingatia matukio ya kihistoria yaliyozikumba jamii. Mada za usemi zilizojitokeza kwenye kampeni katika kipindi kilichotajwa zilihusu Ukabila, Ardhi, Mahakama ya Jinai ya Kimataifa, Uchumi, Katiba, Mchafuko ya Kisiasa ya mwaka wa 2007, Miungano ya Vyama, Ufisadi, Wizi wa Kura, Matokeo ya Kura za Maoni, kujiingiza kwa nchi za kimataifa katika siasa za Kenya, miongoni mwa masuala mengine mengi.

#### 4. 3. 1 Mada ya Ukabila

Onyango (2008:6), aliangazia kuwa ukabila ulikuwa umechangia kuibuka kwa mwingiliano wa kina kikabila, na ambapo tukio hili huwa la kiushindani na si la kushirikiana. Jambo hili lina mashiko ikiwa nukuu zao Uhuru, Raila na Ruto katika magazeti ya *'The Standard'* na *'The Daily Nation'* yataegemewa. Doane (2006) katika makala yake ya, 'Ubaguzi wa Rangi ni Nini? Usemi wa Ubaguzi wa Rangi na Siasa za Ubaguzi wa Rangi' alisema kuwa ushindani wa kisiasa hutekelezwa kwa njia ya usemi wa kiubaguzi wa rangi ambao alikuwa ameuelezea kama mkusanyiko wa matini na usemi wa kijamii kwa kuzingatia matukio ya ubaguzi wa rangi. Nukuu kuwahusu wanasiasa hawa zilitokea kuasikika katika uteuzi wao wa mada ya ukabila ambapo itikadi kuihusu mada hii ilisawirika vizuri katika kampeni za vyama husika katika mwaka wa 2007.

*Standard 15th December 2007, (1)*

> *We want to bury tribal politics and give every community equal chance to have a stub at the presidency. It should not be a reserve of certain families.*
>
> Tunataka tuzike siasa za ukabila na kuipa kila jamii nafasi sawa ya kuwa rais; haiwezi kuwa urais umetengewa familia fulani tu.
>
> (Tafsiri hii na zile zingine fuatilizi zimefanywa na mtafiti).

Kulingana na nukuu hii mwanasiasa huyo alitumia mada ya ukabila kama jukwaa la kuzikuzia kampeni zake kwani alielewa kuwa hiyo ilikuwa njia rahisi ya kuivutia ngozi kwake, ikizingatiwa kuwa wapinzani wake katika muungano wa PNU walichukuliwa kuwa wa jamii moja – ile ya mkoa wa Kati. Mada ya Ukabila na mitazamo ya kimbari iliakisika kwenye kampeni za mwaka wa 2007 kwa kiwango cha juu sana ikizingatiwa kuwa matumizi ya jumbe fupi kupitia simu za rukono yatazingatiwa. Onyango (2008:9) aliangazia haya kupitia arafa kutoka kwa wakereketwa wa ODM waliotokea kuuzungumzia ukabila kwa kuulinganisha na kuzuka kwa homa iliyotisha, tiba ikiweza kupatikana kwa ODM:

> *A Deadly Mountain Flu known as PNU, which affects the brain, has been reported in Central Kenya. The region is under quarantine. People in other parts of Kenya are advised to take ODM pills. One should take full orange for 3 months to avoid infection.*

Homa ya kutisha kutoka Mlimani yajulikanayo kama PNU, na ambayo yanaweza kuathiri ubongo yametokea Mkoa wa Kati. Eneo hilo limetengwa; watu wengine katika sehemu tofauti nchini Kenya wanashauriwa kumeza tembe 3 za ODM. Chungwa moja kwa muda wa miezi mitatu ili kuzuia kuambukizwa.

Akiurejelea ujumbe mfupi kutoka kwa wafuasi wa PNU ukilenga wafuasi wa ODM, msomi huyo aliisawiri picha iliyoonyesha kuwa ukabila kama tukio la kihistoria ulikuwa hai nchini Kenya. Arafa kutoka upande wa PNU zilibeba sifa hasi kwa wakereketwa wa chama cha ODM.

*Do you want to be ruled by Luo to take us back to joblessness? Safeguard the kingdom. Let us ALL come out and give all the votes to Kibaki so that we are not ruled by an uncircumcised man who will make us wear shorts and plunder all our wealth. It's your vote that will prevent our country from going back to Egypt. May our God bless you.*

Nyinyi mnataka mtawaliwe na Mjaluo ili aturejeshe nyakati za kukosekana kwa kazi? Tuilinde himaya hii yetu; SOTE tujitokeze na tumpigie Kibaki kura zetu zote ili tusitawaliwe na mtu ambaye hajatahiriwa kwani atatufanya tuvae kaptura na ataufuja utajiri wetu. Kumbuka ni kura yako itakayoizuia nchi hii kurejeshwa Misri. Mungu wetu akubariki.

Utafiti wake Onyango uliibua mtazamo kuwa mada ya ukabila katika harakati za uchaguzi wa mwaka wa 2007 ilikuwa imepenya na kuwanda kwingi nchini Kenya. Kama njia ya kuzisuta jamii nchini Kenya kuuhusu ukabila, Raila Odinga aliyatumia masuala ya awali ya kihistoria ya Ukabila ili kuakisi kuwapo kwa ukabila nchini Kenya:

*Nation 23rd August 2007, (2)*

*May the spirit of Waiyaki wa Hinga, Harry Thuku, Dedan Kimathi and J.M. Kariuki descend upon ethnic chauvinists who have not yet seen the light, and liberate them from their negative ethnicity, and imbue them with a new spirit of nationhood.*

Ni ombi langu kuwa walio na taasubi za ukabila washukiwe na roho za Waiyaki wa Hinga, Harry Thuku, Dedan Kimathi na J.M. Kariuki kwani

hawajaona mwangaza, ili wanasuliwe kutoka kwa misimamo hasi ya kikabila na kujazwa na roho mpya wa uzalendo.

Kulingana na nukuu hii ni wazi kuwa mwanasiasa huyo alidhamiria kuisuta jamii iliyoishi Mkoa wa Kati kwani wote hao aliowanukuu walikuwa mashujaa wa eneo hilo na ambao mwanasiasa huyo aliwaona walikuwa wakereketwa wa uzalendo nchini Kenya ambao aliwasawiri kama viongozi waliochukizwa na ukabila.

Uhuru Kenyatta alikuwa kiongozi wa wengi katika bunge baada ya kushindwa na mstaafu rais Mwai Kibaki katika kura za urais mwaka wa 2002 baada ya kupendekezwa kuipeperusha bendera ya KANU naye mheshimiwa rais mstaafu Daniel Moi. Hatua ya Moi kumpendekeza Uhuru Kenyatta iliwatamausha washiriki wa Moi ambao nao pia walikuwa wakikitupia kiti hicho jicho; kutamauka huko kuliwafanya washiriki wake Moi kuafikia msimamo sugu wa kumtema pamwe na mradi wake; hivyo basi Uhuru Kenyatta akawa anatambuliwa na wale ambao hawakuuafiki uteuzi huo kama “Mradi wa Moi”. Katika kura za mwaka wa 2007, Uhuru Kenyatta aliamua kutojitosa uwanjani kukipigania kiti cha Urais kilichokuwa kinakaliwa naye rais mstaafu Mwai Kibaki, na badala yake akaamua kumuunga mkono. Uamuzi huo haukuchukuliwa kwa urahisi kutoka pande zote; yaani kutoka kwa wanachama wa KANU, wanachama wa ODM, na rais mstaafu Daniel Moi ambaye aliona kuwa Uhuru alikuwa amekisaliti chama hicho alichokuwa mwenyekiti wake. Itakumbukwa kuwa katika harakati za kupinga katiba mpya kuzinduliwa katika mwaka 2006 kwenye kura ya maoni, Uhuru Kenyatta alishirikiana na Kundi la Chungwa katika kuupinga mswada huo wa katiba.

Tukio la Uhuru Kenyatta kutojitosa uwanjani kulizua mhemko miongoni mwa wanasiasa wa pande zote mbili, na kupelekea kuufanya usemi wake uliozungukia kampeni za urais kuwa finyu. Masuala yaliyozungumziwa naye Mwanasiasa huyo ni pamwe na Ukabila, rais mstaafu Moi, Mhemko kwenye chama cha KANU, Wizi wa Kura, Uchumi, Miungano ya Vyama, Kura ya Maoni, Katiba, rais mstaafu Kibaki, miongoni mwa mambo mengine. Mada ya Ukabila iliibuka katika kampeni za urais wakati Uhuru Kenyatta alipotokea kuiomba jamii yake kuitikia mwito wa kupiga kura pasi na kuligawanya eneo lao. Mwanasiasa huyo alitokea kulitumia eneo kama njia ya kujificha ndani ya suala hilo la ukabila.

*Daily Nation 8th September 2007, (3)*

> *I appeal that we vote as a bloc and make sure that we turn out in large numbers during the Election Day.*
>
> Nawasihi tupige kura bila kuzigawanya na tuhakikishe kuwa tumefanya hivyo kwa idadi kubwa siku ya Uchaguzi.

Kulikuwa na tetesi kuwa Uhuru Kenyatta alikuwa anakitupia kiti cha Naibu wa Rais jicho, tetesi zilizokuwa zinafungamanishwa na njama yake ya kumuunga rais mstaafu Kibaki mkono. Hali hii ilipelekea kuibuka kwa mada ya ukabila katika kampeni zake, na hivyo kuibua kampeni zilizoegemezwa kwenye suala hilo la ukabila.

*The standard 19th December 2007, (4)*

> *There is no way we are going to have a president and his deputy from the same tribe. It can never happen.*
>
> Haiwezekani rais na naibu wake wakatoka katika jamii moja. Haiwezekani kabisa.

Ili kuifutilia mbali dhana ya ukabila na suala la urithi kwenye hatua yake ya kumuunga rais mstaafu Kibaki mkono, Uhuru Kenya alionekana kuirejelea historia na kudhihirisha kuwa siasa hizo zilikosa usemezano na misimamo yao (ODM); tukio ambalo kwake lilikuwa likilenga kuitenga jamii fulani.

*The standard 26th November 2007, (5)*

> *If the arrangement was workable in Kenya, my late father Jomo Kenyatta would have handed over power to a Kikuyu. And similarly, retired president Moi would have done so to a fellow Kalenjin.*
>
> Kama mpango huo ungeweza kufanya kazi nchini Kenya, basi Hayati baba yangu Jomo Kenyatta angemwachia Mkikuyu uongozi; naye rais mstaafu Moi angefanya hivyo kwa Mkalenjin mwenzake.

William Ruto kama mwanasiasa alifanya miondoko yake iwarejeshe watu nyuma na kuisawiri picha ya kukumbukwa kuhusu vijana wa KANU wa mwaka wa 1992. Mwaka huo ndipo mizizi ya mwanasiasa huyo alipoota na kumwelekeza katika uwanja wa siasa kupitia chama cha KANU. Katika mwaka wa 2007, William Ruto alijiunga na chama cha ODM na kukitema chama chake cha awali alipokuwa amemuunga mkono Uhuru Kenyatta katika uchaguzi wa mwaka wa 2002. Mwaka huo mwanasiasa huyo alipata msukumo

mkubwa kutoka kwa wakaazi wa Mkoa wa Bonde la Ufa wa jamii ya Kalenjin japo kulikuwa na vuta ni kuvute kutoka kwa rais mstaafu Moi aliyekuwa ametamaushwa na miondoko yake Ruto ya kukitema chama cha Kanu; mwaka huo, alizicheza siasa zake akiwa katika chama pinzani, jambo hili liliibua tumbo joto katika chama cha KANU. Masuala aliyoyazungumzia katika kampeni yalilandana na yake Raila Odinga aliyekuwa kiongozi wa chama cha ODM; Masuala hayo yalizungukia, masuala ya Moi, Majimbo, Katiba, Uchumi, Miungano ya Vyama, Uwajibikaji, Ghasia za Kisiasa, chama cha Kanu, rais mstaafu Kibaki, miongoni mwa mambo mengine. William Ruto aliirejelea mada ya Ukabila kuhusiana na uteuzi kwenye nyadhifa mbalimbali na nafasi za kazi katika mashirika ya Kiserikali alipoangazia kuwa kuteuliwa kwa mtu serikalini kulitegemea alikuwa ni wa kabila gani. Kwa mujibu wa usemi wa mwanasiasa huyo, uteuzi serikalini uliegemezwa kwenye suala nyeti la ukabila.

*The standard 19th October 2007, (6)*

> *It is now clear that under this government, unless you belong to certain communities that are politically correct, you cannot land an appointment.*
>
> Sasa ni wazi kuwa mtu hawezi kuteuliwa katika wadhifa wowote serikalini kama yeye hajatoka katika kabila fulani.

Uteuzi wa mada kuhusiana na ukabila katika uchaguzi wa mwaka 2007 ulidhamiriwa kuzisuta jamii fulani zilizotuhumiwa kuwa zilikuwa zinapendelea kuziendeleza siasa zao kwa kujifungamanisha na makabila yao. Umaratokezi wa mada ya ukabila katika kampeni za urais uliashiria kupendelewa kwa mada hiyo na muungano husika. Kulingana na grafu kuihusu mada hiyo, ni wazi kuwa Raila Odinga na William Ruto waliipendelea sana mada hiyo ikilinganishwa na Uhuru Kenyatta.

Katika kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2013 Raila Odinga alinukuliwa akiusuta Muungano wa Jubilee kutokana na kile alichokiona kama hatua ya wapinzani wake kuwagawanya Wakenya kwa misingi ya kikabila. Alikumbusha kuwa yeye alikuwa amedhihirisha kuwa hakuwa mkabila kwani alitokea kumuunga rais mstaafu Mwai Kibaki mkono hapo awali katika uchaguzi wa mwaka wa 2002. Katika gazeti la *Daily Nation 24th February 2013,* mwanasiasa huyo alinukuliwa akisema kuwa yeye alikuwa tofauti na wapinzani wake kwani alikuwa hawagawanyi Wakenya kwa kuzingatia misingi ya

kikabila kama wapinzani wake kutoka muungano wa Jubilee. Mwanasiasa huyo alisema kuwa yeye pekee ndiye alikuwa na uwezo wa kuwaunganisha Wakenya ikiwa msimamo wake wa kusema 'Kibaki Tosha' ungeweza kuzingatiwa.

> *(7)*
>
> *Compared to my rivals in Jubilee who have been dividing Kenyans along tribal lines, I am the only one who can unite the country. I have sacrificed a lot politically for the sake of this country. In 2002, I said Kibaki Tosha; not because he was a Kikuyu but because he is a Kenyan.*
>
> Ikilinganishwa na wapinzani wangu wa Jubilee ambao wamekuwa wakiwagawanya watu katika misingi ya kikabila, ni mimi tu ninayeweza kuliunganisha taifa. Nimejitolea sana kisiasa kwa ajili ya taifa hili. Katika mwaka wa 2002 nilisema Kibaki Tosha; si kwa sababu alikuwa Mkikuyu lakini kwa sababu alikuwa Mkenya.

Raila Odinga aliangazia umuhimu wa utaifa akitaja kuwa wapinzani wake walikuwa wanayatumia makabila yao ili kuwawezesha kuutwaa ushindi. Alikumbusha kuwa Kenya ilikuwa ya watu wote hivyo basi mawakala wa ukabila hawakuwa na lao kwani siku za kupiga kura kwa misingi ya 'mtu wetu' zilikuwa zimepitwa na wakati.

*The Standard 15th February 2013, (8)*

> *The Jubilee leaders are busy bandying ethnic figures, but I am telling them they will be surprised by the outcome of the election. The country is for all of us.*
>
> Viongozi wa Jubilee wanafanya bidii kusambaza kuendeleza ukabila, lakini ninawaambia kwamba watashang'aa sana kuona matokeo ya uchaguzi. Nchi hii ni yetu sote.

Katika uchaguzi wa mwaka wa 2013 Uhuru Kenyatta alikuwa kwenye siasa kikamilifu kwani alikuwa kiongozi wa chama cha kisiasa cha TNA na hivyo basi kampeni husika zilimhusu vyema baada ya kuungana na chama cha URP chake William Ruto na kwa pamoja wakaujenga muungano wa Jubilee ambao lengo lao lilikuwa kuutwaa uongozi wa nchi ya Kenya katika uchaguzi wa 2013. Kwa hivyo, mwanasiasa huyo aliyazungumzia masuala mengi yaliyohusu nchi ya Kenya, masuala hayo yalikuwa na mwingiliano

mkubwa na yale yaliyozungumziwa na Raila, lakini ikidhihirika bayana kuwa kulikuwa na mkinzano wa moja kwa moja.

Mada ya ukabila ilitokea kuibuka katika kampeni za mwanasiasa huyo aliyekuwa akiwakemea wale waliokuwa wakisema kuwa haikuwa sawa kwa Mkikuyu kugombea kiti cha urais; alihoji kama katiba ya Kenya ilikuwa na kipengele kama hicho. Tukio hilo lilikuwa linapendekezwa na viongozi kutoka katika jamii zingine. Uhuru Kenyatta aliirejelea Katiba na kusema kuwa kila mmoja nchini Kenya alikuwa na haki zake kikatiba kuwania uongozi wa urais na kuwa hakuna yeyote ambaye angezuiwa kutekeleza haki yake hiyo ya kikatiba.

*The Standard 16th November 2012, (9)*

> *There are people who say that someone from the Kikuyu community should not become the president. Where is that written in the constitution? Everybody has a right to vie as well as elect whoever he likes.*
>
> Kuna watu wengine wanaosema kuwa mgombeaji wa kiti kutoka jamii ya Wakikuyu hastahili kuwa rais. Jambo hilo limeandikwa wapi kwenye katiba? Kila mtu ana haki ya kugombea na vile vile anaweza kumchagua yeyote ampendaye.

Wakati mmoja Uhuru Kenyatta aliyapuuzilia mbali maelezo kuwa muungano wa Jubilee ulikuwa wa kikabila kwa kuhoji kuwa waliokuwa wamesimama naye katika hafla moja ya kampeni walikuwa wanasiasa kutoka makabila mengine ikiwa wale waliokuwa na mawazo hayo wangeweza kuwatupia macho na kuona walikuwa wakiwawakilisha nani.

*Daily Nation 6th January 2013, (10)*

> *Look at the faces at the forefront of the alliance and see who they represent.*
>
> Tazama nyuso za wale walioko hapa mbele yenu kutoka muungano huu na uone wanawaakilisha nani.

Katika uchaguzi wa mwaka wa 2013 William Ruto alitokea kubadilisha msimamo wake wa hapo awali wa kumuunga mkono Raila Odinga na kuamua kuungana na Uhuru Kenyatta katika muungano wao wa Jubilee; Ruto akikiwakilisha chama cha URP naye Uhuru Kenyatta akikiwakilisha chama cha TNA. Kujitenga kwake na Raila Odinga kulisababisha kampeni kupigwa kwa njia tofauti na msimamo wake wa hapo awali akawa

anaivutia ngozi kwake akiielekezea Jubilee; hivyo basi, masuala yote aliyokuwa anayazungumzia yalikuwa yanakinzana na yake Raila Odinga. Masuala aliyoyazungumzia yalilandana na yake Uhuru Kenyatta kwa sababu malengo yao yalikuwa mamoja. Miongoni mwa masuala aliyozungumzia ni pamwe na ukabila, Mahakama ya Kimataifa ya Jinai ya Hague, ardhi, ufisadi, kura ya maoni, katiba, uchumi, machafuko ya baada ya uchaguzi mkuu, uwajibikaji, kuundwa kwa miungano ya kisiasa, katiba, kuingiliwa kwa masuala ya kisiasa na mataifa ya kigeni na umri wa wagombeaji kiti cha urais.

Mada ya upigaji wa kura nchini Kenya kwa misingi ya ukabila ilizua tumbo joto na kuwafanya wanasiasa kulizungumzia katika kampeni zao; hasa pale kampeni zilizungukia kiti cha za urais. William Ruto aliuzungumzia ukabila akisema kuwa waliodhania kuwa makabila hayo mawili; yaani, Wakikuyu na Wakalenjin hawangeweza kuungana na kupiga kura kwa kushirikiana, walikuwa hawajui walilokuwa wakilisema kwani kulingana naye, ajenda yao muhimu ilikuwa ni kuwaunganisha wananchi wa Kenya.

*The Standard 3rd December 2012, (11)*

> *Our opponents have been peddling lies that the two communities will never vote together. We are set to disapprove that this time around. We want to reconcile this country; we want to bring all Kenyans together so that we live in peace.*
>
> Wapinzani wetu wamekuwa wakieneza uvumi kuwa jamii hizi mbili haziwezi kupiga kura kwa ushirikiano; lakini, tutadhihirisha kuwa uvumi huo hauna nafasi wakati huu. Tunataka kuliunganisha taifa hili; tunataka kuwaleta Wakenya wote pamoja ili tuishi kwa amani.

Aliikumbusha jamii yake kuwa kutokana na wao kumuunga mkono Raila Odinga katika uchaguzi wa 2002, wao walikuwa wamesalia kuwa nje ya serikali kwa jumla ya miaka kumi; hili aliliona kama jambo ambalo lilisababishwa naye Raila Odinga ambaye walikuwa wameuunga ugombeaji wake wa urais mkono. Mwanasiasa huyo, (Raila) alionekana kama ndiye alikuwa amelisababisha tukio hilo la jamii ya Kalenjin kuwa nje ya serikali kwa kipindi hicho kwa sababu ya kauli mbiu yake ya ‘Kibaki Tosha’.

*The Standard 6th November 2012, (12)*

> *We supported that man in the last elections but we are now telling him bye. We have been in the opposition for 10 years because of his Kibaki Tosha slogan. If someone cheats you once, he is a liar, but when you are cheated for the second time, you become a fool yourself.*
>
> Sisi ndio tuliomuunga mtu huyo mkono katika uchaguzi uliopita, lakini sasa tunamwambia kwaheri. Tumekuwa nje ya serikali kwa jumla ya miaka 10 kwa sababu ya kauli mbiu yake ya Kibaki Tosha. Mtu akikudanganya mara moja yeye ni mdanganyifu, lakini akikudanganya mara ya pili, wewe utakuwa mpumbavu.

Mwanasiasa huyo wakati mmoja aliwasuta wale waliokuwa wakidhania kuwa jamii moja haingefanya kazi na jamii nyingine kuyasahau hayo kwani uchaguzi haungeegemezwa kwenye misingi ya ukabila bali ungeegemezwa kwenye misingi ya shida zilizokuwa zikiwakumba Wakenya na namna shida hizo zingetatuliwa.

*The Standard 25th December 2012, (13)*

> *If our competitors think this election will be defined by ethnicity, they are damn wrong. This poll will be defined by problems facing 40 million Kenyans and solutions for these problems.*
>
> Ikiwa wapinzani wetu wanafikiria kuwa uchaguzi huu utaamuliwa kwa misingi ya ukabila, wamekosea sana. Uchaguzi huu utaamuliwa kwa misingi ya shida zinazowakumba Wakenya milioni 40 na namna shida hizo zitakavyotatuliwa.

Suala kuhusu jamii ya Kalenjin lilimvutia Raila Odinga ambaye katika mwaka wa 2007 alikuwa ameungwa mkono kikamilifu na jamii hiyo ambayo inakalia Mkoa wa Bonde la Ufa. Kutokana na kuungwa kwake mkono hapo awali aliiona haja ya kurejea kwao kuwauliza kuungwa mkono tena kwani Ruto alikuwa ameutamatisha ushirikiano wake na Raila. Raila alimsuta Ruto akihoji kuwa watu wengine walidhania kuwa hangeweza kwenda kwa jamii hiyo ya Kalenjin bila kupelekwa na 'mtu huyo' akisema kuwa jamii hiyo ilimpenda na kuwa mambo hayangekuwa tofauti mwaka huo wa 2013.

*The Standard 6th October 2012, (14)*

*Others think I cannot go to the Kalenjin without them. Even in 2007, it is the community itself that drove them to support me because they loved me. This time round it is not going to be any different.*

Wengine wanafikiria kuwa siwezi kwenda kwa jamii ya Kalenjin bila wao kunipeleka. Hata mwaka wa 2007, ni jamii yenyewe ndio iliyowafanya wakubali kuniunga mkono kwa sababu jamii hiyo ilinipenda. Hata sasa haitakuwa tofauti kwani jamii hii itakuwa name.

Itakumbukwa kuwa wakati mmoja Raila aliiomba jamii hiyo msamaha kutokana na madai kuwa alikuwa amewakosea; kosa ambalo hakulitaja. Katika mwaka wa 2007 mwanasiasa huyo alikuwa amepewa lakabu "arap Mibei"; lililomaanisha yeye atokae ziwani.


*The Standard 30th October 2012, (15)*

*Forgive me, I am seeking forgiveness. If I erred, I am sorry I am a human being and I apologise as we were in the same team last time.*

Nisameheni, ninaomba msamaha. Kama nilikosea, poleni kwa kuwa mimi ni binadamu na ninaomba msamaha kwa kuwa tulikuwa katika timu moja wakati uliopita.

Suala la jamii ya Kalenjin lilichipuza katika kampeni za urais za mwaka wa 2012-13, baada ya William Ruto na Raila Odinga kutengana ambapo Raila aliusuta mtazamo wake Ruto aliouona kama ambao haukuwa na mashiko kwani kulingana naye, jamii ya Kalenjin ilikuwa imempigia kura kwa wingi kwa sababu ilikuwa inampenda kinyume na vile watu 'wengine' walivyofikiria. Mwanasiasa huyo alidai kuwa mambo hayangekuwa tofauti katika uchaguzi wa 2013. Kutokana na kulimbikiziwa lawama na viongozi wa jamii hiyo Raila aliiomba jamii hiyo msamaha kama njia moja ya kuyarejesha matumaini yake kwao, itakumbukwa kuwa jamii hiyo ilikuwa imempa mwanasiasa huyo lakabu ya 'arap Mibei', iliyokuwa inamaanisha 'yule atokaye ziwani'. William Ruto kwa upande wake alimsawiri Raila kama mwanasiasa mnafiki aliyekuwa ameisaliti jamii hiyo na japo walikuwa wamemsamehe hawangempigia kura tena; aidha alisema kuwa mtu akikudanganya mara ya kwanza angekuwa mwongo, lakini angetokea kukuhadaa kwa mara ya pili wewe ndiye ungekuwa nongwe.

Ili kuihitimisha mada ya ukabila katika kampeni za urais kwenye uchaguzi wa mwaka wa 2007 na 2013, ni bayana kukiri kuwa ukabila umekuwa suala sugu sana ambalo huegemewa na wanasiasa kama njia moja ya kuisawiri picha ya kabila moja au makabila fulani kutengwa na makabila mengine. Japo suala hilo halikutokea kuwa na nukuu nyingi kwenye magazeti yote mawili katika mwaka wa 2007, madai yake Onyango (2008), yanatokea kufumbatwa na utafiti huu, kwani msomi huyo alisema kuwa jumbe nyingi za kuusawiri ukabila wa kundi moja dhidi ya kundi jingine ziliitekelezwa sirini kwa njia ya simu za rukono (Onyango 2008). Katika mwaka wa 2013 siasa za ukabila zilishuhudiwa pale ambapo matukio ya Ruto kumtema Raila na kuungana naye Uhuru kulimpelekea Raila kujaribu kuirai jamii ya Kalenjin kwa kuiomba msamaha kutokana na lawama chungu mbovu alizozipata kutoka kwake Ruto. Japo usemi wa kikabila ulikuwa mwingi katika mwaka wa 2012 – 2013; mapigano ya kikabila hayakushuhudiwa; Cheeseman katika gazeti la *Sunday Nation 16th February 2014,* alinukuliwa akisema kuwa sababu ambazo zilichangia kutozuka kwa machafuko ya baada ya uchaguzi zilikuwa kama vile Katiba Mpya, Usemi wa Amani miongoni mwa masuala mengine (Tazama 5. 6.2).



Grafu 1.1 Mada ya Ukabila katika mwaka wa 2007 na 2013

Uchanganuzi wa mtafiti (2015). **Ufunguo:** RA N – Raila *Nation*

RA S – Raila *Standard*

UH N – Uhuru *Nation*

UH S – Uhuru *Standard*

RU N – Ruto *Nation*

RU S – Ruto *Standard*

Kwa kuirejelea grafu ya mada ya ukabila 1.1, picha amabayo ilisawiriwa ilidhihirisha bayana kuwa mwaka wa 2013 mada ya ukabila iliwavutia wanasiasa hao kwenye kampeni za uchaguzi kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na mwaka wa 2007. Katika mwaka wa 2007 Raila ndiye alikuwa mwanasiasa aliyekuwa na nukuu nyingi ikilinganishwa na Uhuru na Ruto; tukio lililojikariri katika kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2013. Picha inayosawiriwa na grafu kuwahusu Uhuru na Ruto inachangia kuonyesha kuwa nukuu za wanasiasa hao wawili zilikuwa zinakaribiana sana. Tukio hilo lote lilionyesha kuwa; huku muungano mmoja au chama kimoja kilipotokea kujitukuza, upande mwingine ulikuwa ukidhalilishwa. Chilton na Schaffner (1997) walisema kuwa ahadi huwa kinyume cha tishio (ambapo huwa kama onyo), na katika usemi wa kisiasa mpaka huwa telezi kwa kuwa tukio la baadaye ambalo hurejelewa katika hali zote huwa kirihishi kwa wengine na kwa wengine huwa la kutia moyo. Matumizi ya usemi wa kikabila yalienziwa hasa na mwanasiasa yule aliyekuwa akidhamiria kuonyesha kuwa ukabila ulikuwa unaenziwa na kundi pinzani.

### 4. 3. 2 Mada ya Ardhi

Mada kuhusu ardhi ilizungumziwa na Raila Odinga na kuashiria kwamba mwanasiasa huyo alikuwa akiutoa ushauri kuhusu vile chama chake kingelishughulikia suala hilo. Alidokeza kuwa suala la ardhi lingeshughulikiwa kikamilifu kwani serikali za hapo awali zilikuwa hazijalipa suala hilo umuhimu uliokuwa unastahiki. Alikumbusha kuwa tatizo hilo lilikuwa la kihistoria na ilikuwa si sawa kwa serikali za hapo awali kulipuuza. Alikuwa akisema hivyo kwa kuwarejelea Wanubi waliokuwa wamekaa katika eneo la Kibera kwa muda mrefu bila kuwa na hati miliki ya ardhi.

*Daily Nation 19$^{th}$ August 2007, (16)*

*Demarcation of land has not been done in Kibera and most residents don't have title deeds so no one can claim ownership of this land.*

Ugawaji wa ardhi haujafanywa kibera na wakaazi wengi hawana hati miliki, hivyo basi hakuna yeyote anayeweza kudai umiliki wake.

Akilirejelea tatizo sugu la ardhi, mwanasiasa huyo aliwaambia Wamaasai kuwa serikali zote zilikuwa hazijawaajibika katika kulisuruhisha suala hilo; akikumbusha kuwa lilikuwa suala moja ambalo lilikuwa linaikumba jamii hiyo tangu wakati wa Mkoloni na kuwa yeye angelishughulikia iwapo angeutwaa uongozi wa taifa hili la Kenya. Kulingana na mtazamo wa mwanasiasa huyo, ilikuwa wazi alikuwa akizilimbikizia lawama serikali za awali kwa kile alichokiona kama kulizembea jambo hilo.

*The Standard 8th December 2007, (17)*

*A comprehensive land reform programme is what is lacking. You cannot solve the problem started in 1923. Successful governments have not found a solution for you.*

Kumekosekana mpango mkamilifu kuhusu suala la ardhi katika nchi ya Kenya; huwezi ukaisuluhisha shida iliyoanza mwaka 1923. Serikali zote zilizotangulia hazijawapa suluhisho

Japo mada ya ardhi ilikuwa kaa la moja katika nchi ya Kenya; suala hilo halikuzungumziwa sana katika mwaka wa 2007 na William Ruto, ambaye aliligusia tu alipoitaja Ripoti ya Tume ya Ndu'ngu kama iliyokuwa imejukumishwa na serikali ili itoe maelezo kuhusu hali ya ardhi ilivyokuwa nchini. Mwanasiasa huyo alitokea kuahidi kuwa hawangeweza kuyatekeleza mapendekezo kulingana na Ripoti hiyo kwani kulingana naye ilikuwa imependekezwa na maadui zao waliokuwa wakimlenga yeye pamwe na Raila.

*Daily Nation 20th October 2007, (18)*

*My name and that of Raila are in the Report. How can we implement it? We are not foolish to implement a report that was engineered by our enemies.*

Jina langu na la Raila liko kwenye Ripoti hiyo, sisi si wajinga tuitekeleze ripoti hiyo iliyoshinikizwa na maadui zetu.

Kampeni za mwaka 2012 na 2013 za Raila Odinga kabla ya uchaguzi mkuu zilivutiwa na mada ya ardhi kwa mshindo mkubwa ambao ulidhihirisha kuwa ardhi ilikuwa donda ndugu katika nchi yetu kutokana na historia yake ndefu tangu siku za ukoloni. Mada ya usemi kuhusu ardhi ilichipuzwa ili kuisawiri picha kuwa baadhi ya kero zilizokuwa zimeikumba nchi ya Kenya kama ambazo zilikuwa na mizizi yake katika uongozi wa 'Jubilee'. Waliokuwa wakilengwa na mwanasiasa huyo walikuwa viongozi wa muungano wa Jubilee waliotuhumiwa kuwa walikuwa wanamiliki maeneo makubwa ya ardhi yaliyokuwa na ukubwa takriban mkoa mzima. Aliwashawishi wananchi kumpigia kura ili uwezekano wao wa kufika Kanani uweze kuafikiwa.

*The Standard 15th February 2013, (19)*

> *You cannot expect someone who has blemishes related to land to solve the land crisis in coast province; Kenyans must cross over from slavery into the Promised Land Canaan.*
>
> Huwezi ukatarajia mtu aliye na mawaa yanayohusu ardhi kuwa ndiye atasuluhisha suala la ardhi katika Mkoa wa Pwani, ni lazima Wakenya wavuke kutoka nchi ya utumwa na kuingia Nchi ya Ahadi ya Kanani.

Kulingana na Raila muungano wa Jubilee haungeweza kujukumishwa suala la kusaidia kutatuliwa kwa msukosuko wa suala la ardhi kwani aliwaona viongozi wa muungano wa jubilee kama wanafiki ambao wangefanya yote ili kulemaza au kutinga hatua zozote za kuitafuta suluhu kuhusu ardhi nchini Kenya.

*Daily Nation 29th January 2013, (20)*

> *This is unequal society where someone kills the other over an acre piece of land yet someone owns land the size of a province. This country would be changed by Kenyans patriots not hypocrites.*
>
> Hii ni jamii isiyo na usawa kwani mtu mmoja humuua mwingine kwa ajili ya kipande cha ardhi cha ekari moja, ilhali kuna mtu anayemiliki ardhi karibu mkoa mmoja. Nchi hii itabadilishwa na Wakenya wazalendo na siyo wanafiki.

Kwa upande wa Jubilee, mada kuhusu ardhi katika kampeni kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2013 zilizua mhemko uliolizaa joto; joto lililosikika katika kila sehemu ya taifa la Kenya. Familia ya rais wa kwanza hayati Mzee Jomo Kenyatta ilielekezewa dole la

lawama kuwa walikuwa wamechangia katika kusambaratisha jitihada za kusuluhisha suala hilo nyeti la kihistoria. Uhuru Kenyatta alilizungumzia jambo hilo na kusema kuwa suala hilo lilikuwa si suala la kufanyiwa mzaha kama vile wapinzani wake kutoka muungano wa CORD walivyokuwa wakilifanyia na kuwa huo haukuwa mchezo wa soka kwani asili ya vita vya uhuru ilichochewa na ardhi.

*Daily Nation 4th February 2013, (21)*

> *I have taken time to give this matter the consideration it deserves. I don't want to score cheap political points ... land was the basis on which the war of independence was waged – it is too serious a matter to become a political football; too much blood has been shed in this country for that.*
>
> Mimi nimelipatia jambo hili muda ili kulitolea msimamo unaohitajika. Sitaki kupata alama chapwa kisiasa… Suala la ardhi ndilo lilikuwa msingi wa mapigano ya uhuru kutekelezwa – ni suala nyeti mno lisilohitajika kufanywa siasa za soka; damu nyingi imemwagika katika taifa hili kwa ajili yake.

Akilizungumzia suala la ardhi, William Ruto aliangazia kuwa wapinzani wao walikuwa wakilitumia suala hilo wakilenga kuzitenganisha jamii. Alitaja kuwa wao kama Jubilee walikuwa na suluhisho kuhusu suala hilo kwani walikuwa wakiazimia kuwapa wamiliki wa ardhi hati miliki. Aliwataja wapinzani wao kama kundi lililokuwa likipiga mdomo tu lakini wao (Jubilee) walikuwa na suluhu ya suala hilo nyeti la ardhi.


*Daily Nation 24th February 2013, (22)*

> *Our opponents are talking about land problems, while we are speaking about finding solutions. We want to tell them we are focused on giving everyone a title deed to improve the economy.*
>
> Wapinzani wetu wanazungumza tu kuhusu shida za ardhi, wakati sisi tunazungumzia njia ya kutafuta suluhisho katika kutatua shida hizo. Tuanataka kuwaambia kuwa, tunalenga kummpa kila mmoja hati miliki ili kusaidia katika kuimarisha uchumi.

Suala la ardhi nchini Kenya limekuwa na historia ndefu tangu maajilio ya Makoloni ambapo kuja kwao kulichangia kwa kiasi kikubwa kuzalika kwa ubepari kutokana na kuhamishwa kwa makabila fulani kutoka maeneo yao na kuzitenga sehemu hizo kwa ajili

ya Wakoloni. Tukio hilo la Wakoloni limekuwa likipelekea suala la ardhi kuibua mhemko miongoni mwa wananchi wa Kenya hasa nyakati za uchaguzi mkuu. Chaguzi za mwanzo mwanzo baada ya kubatilishwa kwa kifungu cha 2B ziliibusha uhasama huo wa kihistoria kuota mizizi na kupelekea kutokea kwa mapigano ya mwaka wa 1992. Japo suala hilo halikuzungumziwa sana hadharani katika uchaguzi wa mwaka 2007, lilichangia kwa kiasi kikubwa kutokea kwa mapigano. Kunao uwezekano kuwa Raila hangeweza kulizungumzia sana suala hilo kama alivyofanya katika mwaka wa 2012-13 kwa kuwa Ruto alikuwa mshiriki wake wa karibu. Kuzungumziwa sana kwa suala hilo katika kampeni za uchaguzi wa 2013 kulitokana na kujitosa ulingoni kwa Uhuru Kenyatta, na hivyo basi kufufua suala hilo la kihistoria ambalo lilikuwa likioanishwa na uongozi wa hapo awali.

Grafu 1.2 Mada ya Ardhi Mwaka wa 2007 na 2013




Uchanganuzi wa mtafiti (2015)

**Ufunguo:**
RA N – Raila *Nation*
RA S – Raila *Standard*
UH N – Uhuru *Nation*
UH S –Uhuru *Standard*
RU N – Ruto *Nation*

Chilton na Schaffner (1997:222) wakizirejelea sitiari za uuzaji katika kuuchanganua usemi wa John Major (Aliyekuwa Waziri Mkuu wa Uingereza) walisema kuwa ikiwa sera huuzwa, basi sera ni bidhaa zilizo na uwezo wa kuuzwa. Kutokana na vile grafu inaonyesha ni bayana kusema kuwa kampeni kuhusiana na ardhi haikuchukua nafasi kubwa katika kampeni za 2007 kama vile ilivyodhihirika katika mwaka wa 2013, bila shaka tukio hilo huenda halikuwa miongoni mwa itikadi zilizokuwa zinashikiliwa kwa nguvu na vyama husika. Aidha, kuna uwezekano kuwa waliokuwa kwenye kinyanganyiro hicho pamwe na miungano yao kihistoria hawangeweza kufanikisha kampeni ikiwa mada hiyo ingetumiwa. Katika kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2013 ardhi ilikuwa ni bidhaa iliyowavutia wanasiasa, upande mmoja ukiitumia kama njia ya kuudhalilisha muungano mmoja dhidi ya mwingine nao waliopakwa tope wakijibiidisha kulifuta doa walilotiwa na wapinzani wao.

**4. 3. 3 Mada ya Uchumi wa Nchi**

Mada kuhusu uchumi wa nchi ya Kenya ilitokea kuzungumziwa sana kutokana na ukweli kuwa maisha ya mwananchi wa kawaida huweza kuimarika ikiwa uchumi wa nchi husika utamjali. Mada hii ilijenga usemi mzito uliotumiwa kudhihirisha kuwa uchumi ulikuwa uti wa mgongo wa kuistawisha nchi ya Kenya kwa jumla. Katika kazi yao kuhusu Siasa ya Vyombo vya Habari; kampeni zinazostahili, Lyenger na Mcgrady (2007:237-239) waliangazia kuwa jumbe za uchumi zilikuwa na uhusiano mkubwa katika mwaka 1992 kule Marekani, lakini katika mwaka wa 2004 halikuwa na msukumo huo hata kama kushamiri kwa uchumi kulitegemea nchi za nje. Mtazamo wao uliasikika bayana katika kampeni za uchaguzi wa urais nchini Kenya. Katika kampeni za urais nchini Kenya Raila Odinga aliijenga kampeni yake katika msingi aliouona dhaifu wa uchumi uliokuwa umekita mizizi katika nchi ya Kenya akizilenga serikali zote; ile ya wakati huo na za hapo awali, hivyo kudhihirisha kuwa hilo lilikuwa suala la kihistoria. Umaratokezi wa kuzungumziwa kwa mada ya uchumi ulidhihirika waziwazi katika kampeni za urais nchini Kenya ikiwa nukuu za wanasiasa hao zingezingatiwa.

*Standard 8th December 2007, (23)*

*This is an area with rich potential but you have been forgotten and I would like to assure you that I understand your problems ranging from roads, unexploited minerals and poverty.*

Hii ni sehemu yenye uwezo mkubwa kiuchumi; lakini, mmesahauliwa na ningetaka kuwaahidi kuwa naelewa shida zenu kuanzia barabara, madini ambazo hazijachimbuliwa na kukithiri kwa umasikini.

Mada ya uchumi iliegemezewa mahitaji ya eneo pamwe na watu waliohusika; hivyo basi kampeni ililenga eneo na hadhira lengwa kwani kila eneo nchini Kenya lilikuwa na mahitaji yake ya kimsingi. Mwanasiasa huyo alidai kuwa alikuwa amezifanya ziara nyingi sana nchini na kubaini kuwa Wakenya walikuwa wameamua kupiga kura ili kubadilisha maisha yao kwa sababu ya mizigo mikubwa ya ukosefu wa kazi, umaskini, ughali wa bidhaa za kimsingi na kupanda kwa kodi ya nyumba.

*Daily Nation 13th December 2007, (24)*

*My visits around the country show that Kenyans are determined to vote for change as they are tired of heavy burden for unemployment, poverty, high prices of basic commodities and rising house rent.*

Ziara zangu kote nchini zinaonyesha kuwa Wakenya wameamua kupiga kura ili kubadilisha maisha yao kwa sababu ya mizigo mikubwa ya ukosefu wa kazi, umaskini, ughali wa bidhaa za kimsingi na kupanda kwa kodi ya nyumba.

Mada ya Uchumi iliegemewa na Ruto aliyeonyesha kuwa mambo hayakuwa mazuri na yalihitaji kutengenezwa. Masuala kama hayo yagusiayo kudhoofika kwa uchumi na hali ya kutamausha ya wananchi hujenga msingi wa kuvutia uungwaji mkono. Lyenger na Mcgrady (2007: 238), wamegusia suala kama hilo katika kazi yao kuhusu Miktadha ya Kisiasa dhidi ya Athari ya Kampeni; wamesema kuwa miktadha ya wakati huo huwa si hoja, suala muhimu ni rekodi ya mwanasiasa au hali ya chama wakati huo. Ruto alisema kuwa walitaka kukarabati vitu vingi ambavyo havikuwa vikifanya kazi vyema kama kuzorota kwa usalama na umasikini.

*The Standard 2nd October 2007, (25)*

*We want to fix it, we want to fix so many things that are not working. Insecurity, poverty, we must fix it.*

> Tunataka kukarabati, tunataka kuvikarabati vitu vingi ambavyo havifanyi kazi vyema; Kuzorota kwa usalama, umasikini, lazima tuukarabati.

Uchumi wa nchi huwa uti wa mgongo ikiwa matamanio ya kuyaimarisha maisha ya mwananchi yataafikiwa. Wanasiasa wengi katika Kampeni nyingi za urais huangazia suala la uchumi kwa kuonyesha kuwa uchumi wao utaimarika zaidi ikilinganishwa na kundi pinzani. Raila Odinga aliiegemeza mada ya uchumi katika kampeni zake akionyesha kuwa alikuwa na uwezo wa kuyaimarisha maisha ya raia wa nchi ya Kenya.

*The Standard 15th January 2013, (26)*

> *Pan Paper mills that closed down would be revived the first month of CORD government.*
>
> Kiwanda cha *Pan Paper* kilichofungwa kitafunguliwa mwezi wa kwanza wa serikali ya CORD.

Mwanasiasa huyo alikuwa amekashifiwa kuwa ikiwa angeutwaa uongozi wa nchi kama rais, angezisambaratisha biashara za Wakikuyu. Tukio hilo lilimfanya azipuuzilie mbali tetesi hizo akisema kuwa yeye alikuwa mwanabiashara. Raila alisema kuwa madai kuwa angeziharibu biashara za Wakikuyu ilikuwa ni upuuzi mtupu akidai kuwa alielewa fika gharama iliyokuwapo katika kuimarisha na hata kuithibiti biashara. Ni vizuri kutaja kuwa, huo ulikuwa vilevile usemi wa kikabila.

*Daily Nation 11th January 2013, (27)*

> *Claims that Raila will destroy businesses owned by the Kikuyu is rubbish. I am a businessman and I understand what it means to build a business.*
>
> Madai kuwa Raila ataziharibu biashara za Wakikuyu ni upuuzi mtupu, mimi ni mwanabiashara na ninaelewa fika gharama iliyopo ya kuifanya biashara isimame imara.

Uhuru Kenyatta alilihusisha suala hilo kama njia mojawapo ya kuwavutia wapigaji kura wengi kwake; kama vile vijana na wanawake. Kutokana na imani kuwa wapigaji kura wengi huegemea zaidi upande ambao huweza kuwanufaisha zaidi ikiwa masuala kama ya uchumi wa nchi yatatokea kuzingatiwa. Uhuru alidai kuwa lengo lao lilikuwa ni kuwapa vijana na wanawake uwezo wa kujikuza kiuchumi na sio kuongea maneno matupu kila wakati kama walivyofanya wapinzani wao.

*The Standard 28th January 2013, (28)*


> *Our focus is economic empowerment for the youth and women and not mere rhetoric our competitors have dwelt on.*
>
> Lengo letu ni kuwapa vijana na wanawake uwezo wa kujikuza kiuchumi na sio kuongea maneno matupu kila wakati kama wanavyofanya wapinzani wetu.

William Ruto alilizungumzia kwa kina suala la umaskini na ukosefu wa kazi miongoni mwa wananchi wa Kenya. Alisema kuwa walikuwa wanaazimia kupunguza umaskini kwa kiwango kikubwa katika nchi ya Kenya kwani kulikuwa na mamilioni ya watu nchini Kenya ambao walikuwa wanaishi maisha ya uchochole na kuwa kulikuwa kuna haja ya kushirikiana katika vita dhidi ya umaskini. Alisema kuwa alitaka watembee pamoja na wananchi katika vita dhidi ya umasikini na ukosefu wa kazi katika nchi ya Kenya.

*Daily Nation 9th February 2013, (29)*

> *We have to move this country forward and we do not want a scenario where we have million of Kenyans who are poor and few millionaires. We want to walk together in the war against poverty and unemployment.*
>
> Itatuhitaji kuiendeleza nchi hii mbele na hatutaki kuona hali ambapo mamilioni ya Wakenya ni masikini na kuna mamilionea wachache. Tunataka tutembee pamoja katika vita dhidi ya umaskini na ukosefu wa kazi.

Grafu 1. 3 Mada ya Uchumi wa Nchi Mwaka wa 2007 na 2013




Uchanganuzi wa Mtafiti (2015)

**Ufunguo:**
RA N – Raila *Nation*
RA S – Raila *Standard*
UH N – Uhuru *Nation*
UH S– Uhuru *Standard*
RU N – Ruto *Nation*
RU S – Ruto *Standard*

Kuzungumziwa kwa uchumi nchini Kenya katika chaguzi hizo mbili kulidhihirisha kuwa, hilo lilikuwa jambo mojawapo lililowavutia wanasiasa hao wote kwa viwango vilivyokuwa tofauti baina ya chaguzi hizo za miaka hiyo. Raila Odinga ndiye mwanasiasa aliyetokea kulizungumzia suala hilo kwa viwango vilivyokuwa vinakurubiana ikilinganishwa na wanasiasa hao wengine. Viwango vyake William Ruto vilivipiku viwango vyake Uhuru Kenyatta ambaye katika mwaka wa 2007 alidhihirika kutolizungumzia suala hilo kama vile alivyotokea kulizungumzia katika mwaka wa 2013. Kutokana na vile grafu inadhihirisha, ni mtazamo ulio wazi kuwa uchumi ni suala ambalo daima litasalia kuibuka katika siasa kutokana na uwezo wake wa kuhisika katika kila aila

na jamii nzima kwa jumla. Kwa yakini, uchumi thabiti huchangia kuwapo kwa serikali yenye uwezo wa kuziendeleza ajenda zake vyema.

**4. 3. 4 Mada ya Uwajibikaji**

Mada ya usemi kuhusiana na uwajibikaji ilishamiri katika kampeni za urais kwani Raila Odinga alilizungumzia suala hilo nyeti kwa ari kutokana na mtazamo wake kuwa lilikuwa mwiba ambao ulikuwa umezitinga jitihada zote za kuimarisha uchumi. Kulingana naye Raila Odinga, kihistoria; alidai kuwa rais wa Kenya wakati huo alikuwa haongozwi na falsafa ya kuufumbata ukweli kuwa uwajibikaji ulikuwa umezikwepa serikali zote za awali. Mwanasiasa huyo aliangazia kuwa wale watu waliokuwa wamechangia katika kuisambaratisha nchi ya Kenya kiuchumi walikuwa wameungana ili kuziendeleza ajenda zao. Kihistoria, kudorora kwa uwajibikaji kulikuwa kumesababishwa na kujukumishwa uongozini kwa viongozi ambao azma yao ilikuwa kujifaidi. Nukuu ya mwanasiasa huyo katika gazeti la *Standard 13^th^ December 2007* ilikuwa dhahiri.

> *(30)*
>
> *What will change tomorrow if his current cabinet today has individuals who were linked to the Anglo-leasing and Goldenberg scandal?*
>
> Ni jambo gani litakalobadirisha kesho ikiwa baraza lake la mawaziri linajumuisha watu waliotuhumiwa kuhusika na sakata ya *Anglo-leasing* na *Goldenberg*?

Vilevile gazeti la *Daily Nation 9^th^ October 2007* mwaka uo huo lilikuwa na nukuu iliyoshadidia mitazamo ya hapo awali kulihusu jambo hilo.

> *(31)*
>
> *The very same men who turned Kenya into one of the most corrupt nations on the planet have united in the attempt to hold on to power once again so that they can continue enriching themselves and their friends.*
>
> Watu wale wale walioigeuza nchi ya Kenya na kuifanya iwe miongoni mwa nchi zilizo fisadi zaidi duniani wameungana ili kuhakikisha kuwa wamesalia katika mamlaka tena ili waendelee kujitajirisha pamwe na marafiki zao.

Mada ya uwajibikaji iliibuka katika kampeni za urais katika mwaka wa 2013 huku Raila akitokea kuwasuta viongozi wa Jubilee kutokana na madai ya kuhusika kwao katika

kutekeleza ufisadi; mwanasiasa huyo alihoji kuwa viongozi wa Jubilee hawangeweza kujukumishwa jukumu la kuhakikisha kuwa uwadilifu ungezingatiwa nchini Kenya. Mwanasiasa huyo alihoji kuwa; ingewezekana vipi watu waliokuwa na kesi kotini wawe viongozi?

*Daily Nation 6$^{th}$ February 2013, (32)*

> *Those with cases in court cannot be charged with the country's leadership, it is simply impossible.*
>
> Watu walio na kesi kotini hawawezi wakajukumishwa uongozi wa nchi; haiwezekani katu.

Mwanasiasa huyo aliirejelea bibilia na kuwazomea viongozi wa Jubilee akilenga kuwakosoa juu ya mtazamo wao kuhusu Jubilee kibibilia. Aliwauliza viongozi hao warejeshe mali waliyoiba kwani hiyo ndiyo ilikuwa *kauli mbiu* ya Jubilee kwenye bibilia.

*The Standard 15$^{th}$ December 2012, (33)*

> *In the bible, Jubilee means 50 years and during this time, prisoners and thieves were freed while those who had stolen were asked to return, so we are asking our colleagues in the so called Jubilee Alliance are you ready to return property you have stolen?*
>
> Katika bibilia, Jubilee humaanisha miaka 50 ambapo katika kipindi hiki wafungwa hufunguliwa na wezi huachiliwa huru nao wale ambao wameiba huulizwa warudishe, kwa hivyo ninawauliza marafiki zangu katika muungano wa Jubilee, je mko tayari kurejesha mali mliyoiba?

Mada ya uwajibikaji na wizi wa mali ya umma ilizua tumbo joto hasa katika muungano wa Jubilee kutokana na muungano wa CORD kuitumia mada ya uwajibikaji kuisawiri picha hasi kuwa, wapinzani wao walikuwa si watu wa kujukumishwa uongozi wa taifa . Uhuru Kenyatta alitokea kujaribu kuyafutilia mbali madai hayo kwa kuwajibu wapinzani wake na kuwaambia kuwa hayo madai yalihitajika kuthibitishwa; na kuwa, yeyote yule aliyekuwa na ushahidi kuhusu kuhusika kwake katika wizi wa mali ya umma alikuwa huru kuthibitisha. Mwanasiasa huyo alinukuliwa akimsuta mpizani wake Raila akimuuliza kuacha kuongea juu ya wengine lakini aziuze sera zake kwa Wakenya.

*The Standard 24$^{th}$ February 2013, (34)*

*If you have any evidence that I have stolen anything table it. My plan is to win the presidency and serve Kenyans equally. My dear brother Raila, sell your policies and stop talking about others.*

Kama unao ushahidi wowote kuhusu kuhusika kwangu katika wizi wa kitu chochote cha umma, sema. Mpango wangu ni kushinda kiti cha urais na kuwatumikia Wakenya wote sawa. Ndugu yangu Raila, ziuze sera zako na uache kuongea juu ya wengine.

Kukashifiwa kwa muungano wa Jubilee na muungano wa CORD kuwa Jubilee ilikuwa na viongozi waliokuwa wakiwagawanya watu kwa misingi ya kikabila kulimfanya Uhuru Kenyatta kulizungumzia suala hilo na kusema kuwa muungano huo ulidhamiria kuwaunganisha Wakenya wote ili waishi kwa amani kinyume cha vile wapinzani wao walivyokuwa wakitarajia.

*The Standard 3rd December 2012, (35)*

*Our alliance is to unite all Kenyans so that we live in peace. It is an alliance that unites all.*

Muungano wetu ni wa kuwaunganisha Wakenya wote ili tuishi na amani. Ni muungano ambao unawaunganisha wote.

Wakati mmoja Mwanasiasa huyo alieleza kuwa ushirikiano wao na Ruto ulikuwa ukidhamiria kuhubiri amani na kuahidi kuwa Wakanya hawangepigana tena kama ilivyokuwa kila kulipokuwa kuna uchaguzi mkuu nchini Kenya.

*Daily Nation 3rd December 2013, (36)*

*We want to promise you that our unity with Ruto… we shall preach peace and ensure that no other time shall Kenyans shed blood.*

Tunataka kuwaahidi kuwa ushirikiano wetu na Ruto… tutahubiri amani na tutahakikisha kuwa hakuna wakati mwingine ambapo Wakenya watamwaga damu.


Kutokana na kuzungumziwa kwa suala la uwajibikaji na muungano wa upinzani Ruto alitokea kuliangazia suala hilo kwa kuupuuzilia mbali mtazamo wao ambao ulikuwa unalenga kuwatia kiwewe wapigaji kura. Alisema kuwa wapinzani wao walikuwa wamelifadhili kundi jingine litie doa uwajibikaji wao katika masuala ya kijamii.

Mwanasiasa huyo alidai kuwa huo ulikuwa ni uvumi tu kwani Jamii ya Kizungu ilikuwa imejitenga na propaganda hizo.

*Daily Nation 24th February 2013, (37)*

> *They even sent some people to file other cases of integrity against us and spread rumors and fear to the electorate that if we are elected there will be sanctions, but the European Community has distanced itself from spreading propaganda.*
>
> Waliwatuma watu wengine kutushtaki na kesi zingine za ufisadi dhidi yetu na kueneza uvumi na woga kwa wapigaji kura kuwa ikiwa tutachaguliwa tutawekewa vikwazo, lakini Jamii ya Kimataifa imejitenga na uenezwaji wa propaganda hiyo.

Grafu 1.4 Mada ya Uwajibikaji Mwaka wa 2007 na 2013




Uchanganuzi wa Mtafiti (2015)

**Ufunguo:**
RA N – Raila *Nation*
RA S – Raila *Standard*
UH N – Uhuru *Nation*
UHS– Uhuru *Standard*
RU N – Ruto *Nation*

RU S – Ruto *Standard*

Mada kuhusiana na uwajibikaji wa wanasiasa aghalabu ilikuwa ikichipuza katika kampeni zote ziwe za ubunge au hata za urais kutokana na uwezo wake wa kuivutia jamii na kuishawishi. Katika chaguzi zote mbili suala hilo lilizungumziwa kwa viwango ambavyo vilikaribiana sana lakini kati ya wanasiasa hao, Raila Odinga ndiye aliyelizungumzia zaidi ya wote. Kutokana na kuchipuza kwa suala la Hague, mwanasiasa huyo aliidhalilisha misimamo ya Uhuru Kenyatta na mwenza wake William Ruto ya kuamua kukiwania kiti hicho cha urais akidai kuwa wale waliokuwa na kesi mahakamani hawakuwa watu ambao wangewajibika katika kuhakikisha kuwa Kenya imelipogoa zimwi la ufisadi na utowajibikaji kwa manufaa ya wananchi wote. Picha iliyosawiriwa na grafu kuhusiana na uwajibikaji bila shaka inachangia kuonyesha kuwa Raila alilizungumzia sana suala hilo kutokana na uwezo wake wa kuushawishi umma. Viwango vyake vilikuwa juu na mshiriki wake katika kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2007. Katika kampeni za uchaguzi wa mwaka 2013 viwango vya Raila vilikuwa zaidi ya vile vya awali. Raila alikuwa akilenga kujisawiri kama mtu aliyekuwa na utu; na hivyo kuwavunja moyo wafuasi wa kundi pinzani. Davis *et al;* (2004) walisema kuwa ufisadi huwafanya wapigaji kura kutojitokeza vyema, kuwatenga na kuwafundua wananchi kutojihusisha na masuala ya siasa.

### 4. 3. 5 Mada ya Wizi wa Kura

Kila baada ya uchaguzi mkuu nchini Kenya, uchaguzi wa kiti cha urais ulitajwa kuwa ulikuwa ukifanywa kwa njia iliyokuwa si ya haki, tetesi hizi kwa hivyo zilipelekea kuibuka kwa mada ya usemi wa wizi wa kura katika kampeni za urais. Hili lilionekana kuwa suala lililomfanya Raila kulizungumzia akionyesha kutamaushwa na jambo hilo lililokuwa limehanikiza hewa. Ilidaiwa kuwa mwaka wa 2007 muungano wa PNU ulikuwa umetanabahi kuwa ungeshindwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka huo, na kwa ajili hiyo walisawiriwa kama kundi lililokuwa likichapisha kura ghushi ili kufanikisha juhudi zao za kurejea uongozini. Itakumbukwa kuwa wizi wa kura ulikuwa mojawapo wa masuala nyeti ya kihistoria yaliyozungukia uchaguzi mkuu nchini Kenya tangu maajilio ya mfumo wa vyama vingi katika mwaka wa 1991. Kwenye gazeti la *Standard 7th December 2007* mwanasiasa huyo alinukuliwa akisema:

*(38)*

*I know PNU has sensed defeat and they are now indulged on a campaign to print fake ballot papers, which they will use to rig the elections, but we will stop them no matter what it takes.*

Ninajua kuwa muuungano wa PNU unahofia kushindwa na ndio maana wanajihusisha na harakati za kuchapisha karatasi ghushi za kupigia kura zitakazotumiwa katika wizi wa kura, lakini tutawazuia kwa vyovyote vile.

Mada ya wizi wa kura ilitokea kuzungumziwa zaidi hata baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 wakati mapigano ya kikabila yalipokuwa yamezidi viwango vya hapo awali. Ilidaiwa kuwa matokeo ya uchaguzi yalibatilishwa na kupelekea kutangazwa kwa rais mstafuu Mwai Kibaki kuwa mshindi. Suala hili la wizi wa kura lilikuwa likijikariri karibu katika kila mkutano wa kampeni za urais kabla ya upigaji wa kura kutekelezwa ikiwa umaratokezi wa nukuu zake Raila Odinga ni jambo la kuzingatiwa.

*Daily Nation 2nd November 2007, (39)*

*They are operating under a strong room located on the 13th or 14th floor of Anniversary Towers, the ECK headquarters. They are replacing names of voters in some constituencies with new names and even using those of the deceased.*

Wanafanya kazi wakiwa wamejifungia katika jumba katika orofa ya 13 au 14 katika jengo la *Anniversary Tower*, makao makuu ya Tume ya Uchaguzi ya Kenya; ili wabadilishe majina ya wapigaji kura katika maeneo ya bunge na majina mapya hata ya wale walioaga.

Mada kuhusu wizi wa kura huenda ilienziwa kutokana na uwezekano wake kuuvutia umma, hilo lilikuwa suala tata na telezi na kulingana na picha iliyokuwa ikisawiriwa na jambo hilo ni kuwa, uchaguzi na matokeo ya urais yalitekelezwa wizini.

Kuzungumziwa kwa wizi wa kura za urais katika kila uchaguzi na wanasiasa kulidhamiriwa kuibusha hisia kuwa kila wakati uchaguzi haukuwa wa huru na haki, ikizingatiwa kuwa katiba ya Kenya ilikuwa ikiwalinda wote wanaong'ang'ania viti mbalimbali cha urais kikiwa kimojawapo. Katika kampeni za urais mwaka wa 2013, Raila alishikilia kuwa yeye alikuwa ameshinda katika uchaguzi wa mwaka 2007 lakini kura zake zikaibwa.

*The Standard 22nd February 2013, (40)*

Si mnajua ng'ombe yetu ilizaa na ndama ikaliwa na mbwa?

Raila alinukuliwa akisema kuwa alikuwa mwingi wa matumaini kuwa katika uchaguzi wa mwaka wa 2013 angeibuka mshindi kwani tume ya awali ya uchaguzi nchini Kenya ilikuwa imevunjiliwa mbali, na hivyo basi ndoto yao ingeafikiwa hatimaye pale ambapo angeutwaa uongozi wa nchi ya Kenya.

*The Standard 22nd February 2013, (41)*

> *I am confident that unlike in 2007 botched presidential elections where my votes were stolen by the defunct ECK, Kenya will at long last have their dreams fulfilled when I ascend to power next year.*
>
> Nina uhakika kuwa kinyume na vile kulivyokuwa mwaka wa 2007 wakati uchaguzi wa urais ulivyoharibiwa na Tume ya Uchaguzi ya Kenya iliyovunjiliwa mbali, nchi ya Kenya hatimaye itaiafikia ndoto yake wakati nitakapounyakua uongozi wa taifa hili mwaka ujao.

Katika uchaguzi wa mwaka 2013 tetesi nyingi zilizozungukia suala nyeti la kihistoria la wizi wa kura zilijikuta kwenye jukwaa la Uhuru pamwe na wakereketwa wao walipolizungumzia suala hilo kwa kulipuuzilia mbali. Uhuru Kenyatta alimsuta mpizani wake kwa madai kuwa serikali ilikuwa imepanga kuiba kura kwa kuwatumia wakuu wa taarafa na machifu, akikumbusha kuwa Raila Odinga alikuwa akilenga kuwarejesha watu katika hali iliyokuwapo katika mwaka wa 2007.

*The Standard 25th February 2013, (42)*

> *He (Odinga) has claimed recentry that the provincial administration was being used to rig the elections among other outrageous claim. He is showing signs of wanting to pull us towards the 2007 troubles.*
>
> Yeye (Odinga) alisema hivi karibuni kuwa wakuu wa taarafa na machifu wanatumiwa ili kusaidia katika wizi wa kura na kufanya mambo mengine mabaya. Anaonyesha ishara za kutaka kuturejesha katika machafuko ya mwaka wa 2007.


Ruto alilizungumzia suala la wizi wa kura kwa kuomba muungano wa CORD kuyakubali matokeo ya uchaguzi baada ya kupigwa kwa kura tarehe 4 Machi 2013; na kuwa haikuwa na haja kwao kukengeushwa na matokeo ya kura ya maoni kuhusu katiba mpya iliyokuwa

imezinduliwa katika mwaka wa 2010. Ruto alidokeza kuwa walishang'aa kuona kuwa bado wakati huo kulikuwa kuna mtu ambaye alikuwa amesalia katika siasa za kura ya maoni kuhusu katiba, ilhali Wakenya walikuwa wanaendelea na shughuli zao za kulijenga taifa.

*Daily Nation 13th January 13, (43)*

> *On March 4 we are asking them that if they lose elections – that if Kenyans decide that it is Jubilee – they should be ready to accept defeat. We are sorry that there is someone on the other side who is still stuck in the referendum politics while Kenyans have moved on.*
>
> Tunawaomba wakubali matokeo ya uchaguzi tarehe 4 Machi – yaani ikiwa Wakenya wataamua kuwa ni Jubilee – ni lazima wawe tayari kukubali matokeo. Tunashang'aa kuona kuwa kungali kuna mtu ambaye amesalia katika siasa za kura ya maoni kuhusu katiba ilhali Wakenya wanaendelea na shughuli zao.

Grafu 1.5 Mada ya Wizi wa Kura 2007 na 2013




Uchanganuzi wa Mtafiti (2015) **Ufunguo:** RA N – Raila *Nation*

RA S – Raila *Standard*

UH N – Uhuru *Nation*
UHS– Uhuru *Standard*
RU N – Ruto *Nation*
RU S – Ruto *Standard*

Mada ya wizi wa kura kwenye kampeni za urais nchini Kenya ilikuwa ikizua mjadala mkali kutokana na wanasiasa kutokubaliana na matokeo ya chaguzi tangulizi. Wanasiasa hao walilizungumzia suala hilo wakiongozwa na itikadi ya vyama na miungano yao. Kila wakati kundi moja lililimbikizia kashfa kundi jingine kwa kuliona kama ambalo lilihusika katika kukitekeleza kitendo hicho. Raila alinukuliwa mara nyingi kwenye magazeti hayo akidai kuwa alikuwa amefanyiwa makuruhu kwa ushindi wake kuibwa na serikali iliyokuwa ikiongoza katika vipindi vyote alivyokuwa akikiwania kiti hicho cha urais. Katika uchaguzi wa mwaka wa 2007, William Ruto alilizungumzia suala hilo akiwa anamuunga Raila mkono. Akiwa katika muungano wa Jubilee alisawiriwa akilikosoa wazo lake Raila la kutaja kuwa alilaghaiwa ushindi wake. Uhuru kwa upande wake alikuwa amenukuliwa akilidosarisha wazo lake Raila akisema kuwa yeye Raila alikuwa akiazimia kuwarejesha watu katika siku za giza. Kwa kuirejelea grafu 1.4, ni dhahiri kuwa mada ya wizi wa kura ilijikuta kwenye ulingo wa kampeni za urais kwa kiwango kikubwa katika kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2013.

### 4. 3. 6 Mada ya Katiba

Kuhitajiwa kwa katiba mpya ni jambo jingine lililowavutia wanasiasa katika kampeni za urais za mwaka wa 2007. William Ruto kama wanasiasa wengine wa chama cha ODM kwenye kampeni za uchaguzi wa 2007 alishikilia kuwa ikiwa nchi ya Kenya ilikuwa ikiazimia kupiga hatua safi kimaendeleo, basi haikuwa na budi kuona ya kwamba Kenya inaipata katiba mpya ili kufanikisha hali bora ya mwananchi kimaisha. Alidokeza kuwa hilo lingewezekana kwa kuwa walikuwa naye Raila aliyekuwa kiongozi wao.

*The Standard 2nd September 2007, (44)*

> *We want a new constitution, we want a growing economy. It is for us now to achieve that with Raila as our captain.*
>
> Sisi tunaitaka katiba mpya, pia tunataka uchumi unaokua. Ni jukumu letu kuafikia hayo kwani tunaye Raila kama kapteni wetu.

Tukio la Umri lililinganishwa na uhitaji wa kuyafumbata mabadiliko kwa wagombeaji wa kiti cha urais pamwe na wafuasi wao ambao walishikilia misimamo yao ya awali ya kutoyafumbata mabadiliko. Mwanasiasa huyo alilitazama kundi la rais mstaafu Kibaki kama kundi lililokuwa linawaenzi wale viongozi waliokuwa wamepitwa na wakati na hivyo basi ikawa ni kama king'ang'anyiro baina ya kundi lililokuwa limechoka na lile lililokuwa na damu moto, zee likitokea kutoyaafiki mabadiliko; nalo changa likionekana kana kwamba ndilo lililoliafiki wazo la mageuzi.

*The Standard 2nd September 2007, (45)*

> *This will be a contest between those who represent the status quo, yesterday, and the past against those who represent today, tomorrow and future.*
>
> Hiki kitakuwa king'ang'anyiro baina ya wale wanaowakilisha hali ilivyo, jana, na siku zilizopita dhidi ya wale wanaowakilisha leo, kesho, na siku za baadaye.

Katiba iliyokuwa imezinduliwa tarehe 27 Aprili 2010 ilizua mjadala katika kampeni za urais za uchaguzi wa 2013, ambapo Raila Odinga aliwasuta wapinzani wake akiwauliza kama wangeweza kuwajibika katika kuitekeleza katiba hiyo. Mwanasiasa huyo alidai kuwa wapinzani wake walikuwa wameipinga katiba hiyo na kuwa ingekuwa kinaya kwao kuyatekeleza mapendekezo yaliyokuwa kwenye katiba hiyo. Itakumbukwa kuwa Uhuru Kenyatta alikuwa ameiunga mkono katiba husika huku mshiriki wake akiwa ndiye aliyeipinga katiba hiyo. Raila alisema kuwa haingewezekana watu waliokuwa wamezinyanyua 'kadi nyekundu' kuyatekeleza matarajio ya katiba hiyo; aliwakumbusha wapigaji kura kuwa watu hao ndio walioipinga katiba yenyewe kabla ya kupitishwa kwake katika mwaka 2010.

*The Standard 10th December 2012, (46)*

> *Some leaders who were at the forefront flashing red cards to oppose the new constitution are campaining on a platform of reform… you should reject them because they are not honest.*
>
> Viongozi wengine waliokuwa mstari wa mbele wakizionyesha kadi nyekundu ili kuipinga katiba mpya wanafanya kampeni kwa misingi ya mabadiliko… Ni lazima mwakatae kwa sababu hao si watu wakuaminiwa.

Raila aliuliza kuwa ingewezekanaje wananchi wa Kenya kuwaruhusu watu ambao hawangeweza kuyatekeleza matarajio ya katiba kikamilifu kuitekeleza, ilhali waliipinga? Alisema kuwa ingekuwa ni kama kumweka fisi kati ya kondoo ukitarajia asiwashambulie. Katika gazeti la *Daily Nation 5th February 2013* nukuu yake ilikuwa bayana:


> *(47)*
>
> *How can you expect non-reformers to implement a constitution full of reforms and which they rejected? It is like placing a hyena among sheep and expects it not to attack them.*
>
> Nyinyi mnawezaje kuwatarajia watu ambao hawawezi kutekeleza matarajio ya katiba kikamilifu kuitekeleza, ilhali waliipinga? Itakuwa ni kama kumweka fisi kati ya kondoo ukitarajia asiwashambulie.

William Ruto alilizungumzia suala la katiba mpya iliyokuwa imezinduliwa nchini Kenya katika mwaka 2010 ambapo yeye alikuwa akiipinga katiba hiyo; alisema kuwa haikuwa na haja ya mtu kuendelea kulizungumzia suala hilo kwani Wakenya walikuwa wanaendelea na maisha yao chini ya katiba mpya na kuwa kubadilika kwa mfumo wa analogi kuelekea dijitali ulikuwa wa upole mno. Tukio hilo lilidhamiriwa kumfanyia Raila Kinaya, kama mtu ambaye hakuwa tayari kukubali kuwa mabadiliko yalikuwa tayari yameingia, japo wazee walikuwa na ugumu wa kubadilika ikilinganishwa na 'dijitali', yaani vijana.

*The Standard 13th January 2013, (48)*

> *While I appreciate the fact that upgrading from analogue to digital is a slow process I want to tell him that a new constitution is now in place and all Kenyans have since moved on.*
>
> Wakati huu ninauafiki ukweli kuwa mabadiliko kutoka analogi kuelekea digitali ni hatua ya polepole mno ninataka kumwambia kuwa katiba ilizinduliwa nchini na kuwa Wakenya wanaendelea mbele.

Grafu1.6 Mada ya Katiba 2007 na 2013




Uchanganuzi wa Mtafiti (2015)

**Ufunguo:**
RA N – Raila *Nation*
RA S – Raila *Standard*
UH N – Uhuru *Nation*
UHS– Uhuru *Standard*
RU N – Ruto *Nation*
RU S – Ruto *Standard*

Mada kuihusu katiba ilichipuza katika kampeni za chaguzi zote mbili, katika mwaka wa 2007 suala hilo lilitumiwa na chama cha ODM kama mkakati mmojawapo wa kuudhalilishia uongozi wa rais mstaafu Kibaki ambaye hakuwa amemudu kuipa nchi ya Kenya katiba. Itakumbukwa kuwa Raila na Ruto walikuwa pamoja katika kampeni hizo za mwaka wa 2007; na wote pamwe na Uhuru walihusika katika kuipinga katiba hiyo ya mwaka wa 2006. Katika kampeni za katiba ya mwaka wa 2010, William Ruto aliipinga katiba iliyozinduliwa mwaka wa 2010, huku Uhuru na Raila wakiiunga mkono katiba hiyo. Uchaguzi wa mada hiyo ya usemi ilitumiwa kama nyenzo ya kuumbuliana kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine kama njia ya kujitukuzia. Kulingana na grafu ya kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2013, Raila Odinga alilizungumzia suala hilo zaidi

akifuatiwa na Ruto huku Uhuru akilizungumzia kwa wastani. Katika kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2013, mada hiyo ilizungumziwa zaidi ya vile ilivyokuwa mwaka wa 2007.

### 4. 3. 7 Mada ya Miungano ya Vyama

Mijadala kuhusu miungano ya vyama vya kisiasa katika kampeni za urais iliibuka kwa kiwango kikubwa kwani tukio la kuungwa mkono chini ya miungano ya kisiasa ilikuwa kiashiria cha kuelekezea kule ushindi ungekwenda. Kulikuwa na kushutumiana kwingi, kuvunjika kwa mikataba na kuibuka kwa unafiki miongoni mwa wanasiasa. Katika kampeni zake; Raila alisema kuwa Wakenya na Wakereketwa wa chama cha Chungwa walikuwa na huzuni nyusoni mwao alipodai kuwa mtu mmoja alikuwa amekiweka chama katika hali isiyoeleweka, lakini Mkenya mmoja alidhihirisha uzalendo na kukifungia chama kwenye friji.

*The Standard 2nd September 2007, (49)*

> *Just a month ago there was a gloom all over the faces of Kenyans and ODM supporters after one person held the party to ransom. But one Kenyan stood patriotic and locked the Orange safely in a fridge. That man is none other but Mr Mugambi Imanyara.*
>
> Mwezi mmoja uliopita Wakenya na Wakereketwa wa chama cha Chungwa walikuwa na huzuni nyusoni mwao pale mtu mmoja alipokuwa amekiweka chama katika hali isiyoeleweka. Lakini Mkenya mmoja akadhihirisha uzalendo na kukifungia chama kwenye friji. Mtu huyo si mwingine bali ni Bwana Mugambi Imanyara.

Usemi wa wanasiasa, akiwemo Raila ulisheheni malumbano baina ya wanasiasa waliokuwa ndio mwanzo walikuwa wakiiaka miungano iliyokuwa haijaimarika na iliyokuwa inakumbwa na ushindani mkali kutoka ndani na nje ya vyama. Siasa zilisalia kuwa nzito hasa baina ya serikali na chama cha upinzani. Itakumbukwa kuwa wakati mmoja Raila alimsuta Kalonzo akiirejelea miondoko yake kama ile iliyokuwa ikiwakilisha 'kivuli cha serikali', waasisi wa miondoko hiyo wakiwa marais wastaafu Kibaki na Moi.

*Daily Nation 4th August 2007, (50)*

> *Mr Musyoka and Maanzo's of this world are agents of Kibaki and Moi. We will not deal with the decoys in this matter but their principals.*

> Bwana Musyoka na Maanzo wa dunia hii ni mawakala wa Kibaki na Moi. Hatutashughulika na wao katika jambo hili lakini tutakabiliana na wakuu wao.

Matukio ya miungano ya vyama hasa muungano wao KANU na PNU, yalikuwa matukio yaliyotazamwa kwa njia tofauti chamani na nje ya chama. Ili kuhakikisha msimamo wao kama chama (chini ya uwenyekiti wake Uhuru Kenyatta) haungetokea kukisambaratisha chama hicho, mikakati ya kuimarisha umoja huo na kuupa msimamo wake mashiko ulikuwa dawa mjarabu wakati huo. Mwanasiasa huyo (Uhuru) aliisawiri picha ya chama ambacho kilikuwa na maono ya kuutwaa uongozi siku za baadaye. Uhuru, akiutetea msimamo wake wa kutogombea kiti hicho katika mwaka wa 2007, alisema kuwa yeye hakuwa mtu wa kugombea kiti hicho bila malengo ya kuutwaa uongozi kwani alikuwa anatarajia kukiongoza chama kunyakua ushindi baada ya Kibaki kutamatisha zamu yake.
*Sunday Standard 14th October 2007, (51)*

> *We are not people who just run. We run when we are sure we can win. I am leading the party to the next government.*
>
> Sisi si watu ambao hugombea tu kwa ajili ya kugombea; sisi hugombea viti wakati tunajua kuwa tunaweza kuibuka washindi. Ninakiongoza chama kuingia serikali ijayo.

Kihistoria Uhuru Kenyatta alijaribu kudhihirisha sababu zake za kuuafiki muungano wake na PNU kwani, itakumbukwa wakati rais mstaafu Moi alipompendekeza Uhuru Kenyatta kuwa mrithi wake katika uchaguzi wa 2002; Uhuru Kenyatta alitemwa na hao waliokirihishwa na muungano wake na PNU. Jambo hilo la kukashifiwa kwake na wanasiasa kutoka chama cha ODM kulimpelekea mwanasiasa huyo kuwasuta akiwarejelea kama wanafiki. Gazeti la *Sunday Standard 7th October 2007* lilibeba nukuu yake mwanasiasa huyo iliyokuwa;

> *(52)*
>
> *They are power hungry and hypocritical by criticizing my move yet they abandoned me and supported Kibaki in 2002.*
>
> Hawa ni watu walio na tamaa ya uongozi na unafiki kwa kuikashifu hatua yangu, ilhali walinitenga na kumuunga Kibaki mkono mwaka 2002.

Migongano ya vyama ilikuwa dhahiri wakati wa kampeni za mwaka wa 2007; itakumbukwa kuwa William Ruto alikuwa mwanachama wa Kanu lakini mwaka wa 2007 alikigura chama hicho na kuelekea ODM. Kutoka kwake kulitokana na mivutano ya uongozi iliyokuwa chamani. Mwanasiasa huyo alinukuliwa akidai kwamba yeye alikuwa rafiki yake Uhuru, lakini uamuzi wake (Uhuru) wa kuunga muungano wa PNU mkono ulikuwa dhihirisho la kibinafsi.

*The standard 18th October 2007, (53)*

> *Uhuru is my friend, but the decision he made was not in the interest of the party and its members.*
>
> Uhuru ni rafiki yangu, lakini hatua aliyoichukua haikuwa kwa faida ya chama na wanachama wake.

William Ruto akiwa kama Katibu Mkuu wa chama cha Kanu walikuwa wameshirikiana na ODM katika kuipinga katiba katika mwaka wa 2006 na hivyo msimamo wake ulikuwa chama cha Kanu kilikuwa na jukumu la kukiunga chama cha ODM mkono, la sivyo yeye alikuwa ametishia kukihama chama ikiwa Kanu ingetokea kuitema ODM.

*The standard 7th October 2007, (54)*

> *I promised Kenyans that if KANU ditches ODM then I will resign. I want to announce now that I have officially decamped from KANU and resigned my position as Secretary General.*
>
> Niliwaahidi Wakenya kuwa nitaihama KANU ikiwa KANU ingeitema ODM. Ninataka kutangaza kuwa nimeihama KANU rasmi na kujiuzuru kama Katibu Mkuu.

Mambo katika Kanu yalionekana kutokuwa mazuri kwani William Ruto alikuwa ameonyesha kuwa chama hicho kilikuwa na wenyewe ambao walikuwa wamesharejea, hivyo basi yeye alibidiwa kukitema chama hicho na kuwaachia wenyewe.

*Daily Nation 1st October 2007, (55)*

> *We have decided that since the original owners of the party have come back, then it's prudent for us to quit. We shall be making an announcement this week as to our next course of action.*

> Tumeamua kuwa, kwa sababu wamiliki asili wa chama hiki wamerudi; ni vizuri sisi tukihame. Kwa hivyo; tutayafanya matangazo yetu kuhusu uamuzi wetu Juma lijalo.

Kuhama kwake kuliashiria kuwa, yeye kama msemaji wa chama alikuwa amekihama chama na wafuasi wote; hili lilikuwa kama hakikisho kuwa KANU ilikuwa imeingia kwenye muungano na chama cha ODM. Ruto alidai kuwa watu na wafuasi wa chama cha KANU walikuwa naye katika ODM kwa sababu hicho ndicho kilikuwa chama kilichounga mkono suala la mabadiliko.

*The standard 7th October 2007, (56)*

> *The people and Kanu Party membership is with me in ODM because it is the party that supports real change for this country.*
>
> Watu na wafuasi wa chama cha Kanu wako nami katika ODM kwa sababu hiki ndicho chama kinachounga mkono suala la mabadiliko.

Katika kampeni za 2012 – 2013 Raila aliusuta muungano wa Jubilee kwa kutokuwa na msimamo kinyume na vile muungano wa CORD ulivyokuwa. Alidai ya kwamba muungano wao ulikuwa muungano ulioongozwa na Mungu lakini wao Jubilee uliongozwa na shetani. Hili liliibuka pale viongozi wa Jubilee walituhumiwa kuwa waliubatilisha mkataba waliokuwa wameafikiana na kiongozi wa chama cha UDF Musalia Mudavadi. Raila aliuona muungano wa Ruto, Uhuru na Mudavadi kama ambao ulikuwa unaongozwa na mawakala wa shetani'. Nukuu yake Raila katika *Daily Nation 21th January 2013* ilikuwa:

> *(57)*
>
> *Unlike guys who allowed the devil to mediate in their dealing with UDF presidential aspirant Musalia Mudavadi ours was guided by God and true principles that cannot be bent.*
>
> Kinyume na watu walioruhusu shetani kuwapatanisha katika mkataba wao na mgombeaji kiti cha urais kwa tikiti ya UDF Musalia Mudavadi, mkataba wetu uliongozwa na Mungu, hivyo basi mapatano yetu hayatavunjwa.

Masuala mengine yaliyoibuka katika kampeni za Uhuru Kenyatta yalihusiana na kutengwa kwake na wapinzani wake alipokuwa amependekezwa na rais mstaafu Moi kuwa yeye ndiye aliyekuwa na uwezo wa kikiongoza chama cha KANU katika uchaguzi

wa mwaka wa 2002. Waliomtema walidai kuwa walikuwa wamesalitiwa na rais huyo mstaafu. Mwanasiasa huyo alionyesha kukerwa na tukio la kutengwa lakini akakiri kuwa ushindi ulikuwa wao kutokana na ishara zilizokuwa wazi. Uhuru Kenyatta alisema kuwa katika mwaka wa 2002 bahati haikuwa nao baada ya watu wenye tamaa ya uongozi kuwatema na kuamua kumuunga mgombeaji mwingine mkono, lakini wao walikubali hayo na kulingana naye baada ya miaka kumi tangu wakati huo ishara zote ziliashiria kwamba wao ndio wangekuwa wamiliki wa Ikulu kipindi kilichokuwa kinakuja. Gazeti la *The Standard 11th January 2012* lilimnukuu hivi:

> *(58)*
>
> *In 2002, lack was not with us after people with selfish interests deserted us and declared another candidate, but we accepted that. It is now ten years and all indications are that we will be the next occupants of state house.*
>
> Katika mwaka wa 2002 bahati haikuwa na sisi baada ya watu wenye tamaa ya uongozi kututema na kuamua kumuunga mgombeaji mwingine mkono, lakini tulikubali hayo. Sasa ni miaka kumi tangu wakati huo na ishara zote zinaashiria kwamba sisi ndio tutakuwa wamiliki wa Ikulu kipindi kijacho.


Mjadala kuhusu kushirikiana kwa chama cha KANU na jamii ya Wakelenjin na muungano wa AMANI ulichipuza katika kampeni za Ruto aliyesema kuwa chama hicho hakingeweza kuutwaa uongozi wa taifa hili tena, na hivyo hawakuwa na budi kukitema chama hicho na kuiunga Jubilee mkono. Mwanasiasa huyo alisema kuwa muungano wa amani ukiongozwa naye Musalia Mudavadi haungeweza kuutwaa uongozi wa nchi ya Kenya na kuwaomba wapigaji kura kutozigawanya kura za Mkoa wa Bonde la Ufa. Alimrai Gideon Moi, aliyemtaja kama rafiki yake akisema kuwa anapigana vita ambavyo angeshindwa. Alisema hata kama wangeyaangalia matokeo ya Kura ya Maoni yaliyokuwa si sahihi; chama cha Amani hakikuwa na uwezo wa kuutwaa ushindi; hata kwa muujiza ambao haingekuwa rahisi kutokea.

*Daily Nation 21st February 2013, (59)*

> *My friend Gideon is fighting a losing war. Even with the inaccurate opinion polls, Amani has been getting less than two percent rating. Are they expecting a miracle to happen on March 4th? Please don't let the Baringo County votes split the Rift Valley votes.*

Rafiki yangu Gideon anapigana vita ambavyo atashindwa. Hata tukiyaangalia matokeo yasiyosahihi ya Kura ya Maoni; chama cha Amani kimekuwa kikipata chini ya asilimia mbili katika kuorodheshwa kwenye matokeo ya kura za maoni. Kwani wanatarajia muujiza kufanyika Machi 4? Tafadhali usiruhusu kura za Kaunti ya Baringo zigawanye kura za Mkoa wa Bonde la Ufa.

Grafu 1.7 Mada ya Miungano ya Vyama 2007 na 2013




Uchanganuzi wa Mtafiti (2015)

**Ufunguo:**

RA N – Raila *Nation*
RA S – Raila *Standard*
UH N – Uhuru *Nation*
UHS– Uhuru *Standard*
RU N – Ruto *Nation*
RU S – Ruto *Standard*

Mada kuhusu miungano ya vyama kulingana na utafiti huu ilidhihirika kutokea zaidi miezi miwili kabla ya kipindi rasmi cha kampeni kutangazwa. Miungano ya vyama ilitokea kuzumgumziwa na kila mwanasiasa akilenga kulishawishi kundi lake la kijamii kuuafiki msimamo wake wa kuunga muungano fulani mkono akidai kuwa hiyo ndiyo iliyokuwa njia ya kipekee kuhakikisha kuwa wameukaribia uongozi. Katika mwaka wa 2007, Raila

na Ruto walijumuika katika chama kimoja ambacho kilikuwa ODM ambapo William Ruto alidai kuwa jamii ya KAMATUSA ilikuwa katika ODM kikamilifu. Uhuru Kenyatta aliamua kumuunga Kibaki mkono baada ya kuamua kutokigombea kiti hicho cha urais katika mwaka wa 2007. Katika mwaka wa 2013 Raila alitemwa naye Ruto ambaye aliungana na Uhuru katika muungano wa Jubilee; hili lilipelekea jamii za wanasiasa hao kufuatana nao katika muungano huo. Usemi mwingi kuvihusu vyama ulikuwa wa kusiribiana tope, lengo likiwa kuwavutia wapigaji kura kwa misingi ya maeneo na jamii. Kulingana na grafu, ni wazi kusema kuwa kulikuwa na nukuu nyingi za wanasiasa hao kuhusiana na miungano katika kampeni uchaguzi za mwaka wa 2013 kuliko vile mambo yalivyokuwa katika mwaka wa 2007.

### 4. 3. 8 Mada ya Viongozi wa Awali

Katika kampeni za chaguzi zote mbili, katika mwaka wa 2007 na 2013, mijadala kuwahusu viongozi wa awali ilichipuza. Mijadala hiyo iliwahusu hayati Mzee Jomo Kenyatta, Hayati Oginga Odinga, rais mstaafu Moi aliyeondoka mamlakani katika mwaka 2002 na rais mstaafu Kibaki. Katika kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2002, rais mstaafu Moi alikuwa anakipungia mkono kiti cha urais, tukio lililomfanya amtafute mrithi wake; tukio hilo lilionekana kuibusha joto la kisiasa na kumpelekea Raila Odinga kuisuta miondoko yake iliyoonekana kama kurejea kwa "Mradi wa Moi" kama ilivyotajwa alipochukua hatua ya kumpendekeza Uhuru Kenyatta kuwa mrithi wake pindi tu pale kipindi cha uongozi wake kingetokea kutamatika.

Miondoko hiyo ilipelekea kutokea kwa usemi uliomwelekezea Moi kidole cha lawama; hivyo basi, tukio la rais mstaafu Moi kumpendelea Kibaki katika uchaguzi wa 2007 kulifufua masuala chungu mbovu ya kihistoria kama vile ufisadi, marejeo ya udikteta, kuzorota kwa uchumi miongoni mwa masuala mengine mengi. Mwanasiasa huyo alisema kuwa Mzee Moi alikuwa mfungwa wa rais mstaafu Kibaki kwa sababu alikuwa na kashfa ya ufisadi ambayo angetaka aondolewe na serikali yake rais mstaafu Kabaki.

*Nation 27$^{th}$ September 2007, (60)*

> *Mzee Moi is a prisoner of president Kibaki because he sought the president's support in order not to act on a corruption report implicating him.*

Mzee Moi ni mfungwa wa rais Kibaki kwa sababu anayo kashfa ya ufisadi na angetaka aondolewe lawama hiyo.

Itakumbukwa kuwa Mkoa wa Bonde la Ufa ulikuwa na viongozi wawili waliokuwa katika ushindani wa kiukoo upande mmoja ukiwa wa rais mstaafu Moi na upande mwingine ukiwa wa William Ruto aliyekuwa kwenye pilkapilka za kuutwaa uongozi wa jamii ya Kalenjin na kuwa msemaji wao. Miaka ya uongozi wa KANU chini yake Moi lilikuwa tukio lililoakisi marejeo ya nyakati za kutamausha, na kulingana naye Raila Odinga, wananchi wa Kenya walikuwa hawana budi kuibeza na kutoiafiki miondoko yoyote ambayo ingependekezwa na Moi.

*Daily Nation 27th November 2007, (61)*

> *They (The Moi's) are now Kibaki's friends. This shows where he wants to take the country when he says* kazi iendelee.
>
> Sasa (akina Moi) ni marafiki wa Kibaki. Hili linadhihirisha kule wanakodhamiria kuipeleka nchi pale anaposema kazi iendelee.

Raila Odinga aliisawiri picha ya mtu aliyefurushwa kutoka ikulu akirejea; marejeo yaliyokuwa yametokana na kurejea kwa washiriki wake wa zamani waliotuhumiwa kuwa walikuwa wameushiriki na kuufaidi utawala wa rais mstaafu huyo aliyekuwa na historia ndefu na ya kutamausha katika uongozi wa Kenya kulingana naye Raila.

*Daily Nation 23rd September 2007, (62)*

> *Today Daniel Moi who was evicted from state house 5 years ago has effectively returned and the man who served as his vice president is in the same state house. And recently he has sadly been joined there by the official opposition leader Mr Uhuru Kenyatta.*
>
> Sasa Daniel Moi aliyefurushwa kutoka ikulu ya rais miaka 5 iliyopita amerejea na mtu aliyemtumikia kama naibu wake katika ikulu iyo hiyo yumo katika ikulu hiyo; na hivi karibuni ameungana na kiongozi wa upinzani Uhuru Kenyatta.

Ni bayana kusema kuwa mada ya usemi iliyomhusu mheshimiwa Moi ilienziwa na wanasiasa walioliona jambo hilo kama, "baada ya donda msumari moto".

Mjadala kuhusu Kibaki na Moi kulingana na upinzani, uliashiria kuwa kulikuwa kuna njama ya kumrithisha Uhuru Kenyatta uongozi pindi tu pale zamu ya Kibaki ingetokea

kutamatika; itakumbukwa kuwa Uhuru Kenyatta alikuwa ameshaafikia uamuzi kuwa angemuunga mkono rais mstaafu Mwai Kibaki. Uhuru Kenyatta alitokea kuwasuta mawakala wa hoja hiyo kwani ilikuwa imechukua nafasi kubwa katika kampeni za urais za mwaka wa 2007.

*The Standard 3rd December 2007, (63)*

> *Kenya is not anyone's firm and the presidency is not a clan affair. It is Kenyans to decide.*
>
> Nchi ya Kenya si shirika la mtu binafsi; pia, urais si jambo la mbari fulani.
>
> Ni Wakenya watakaoamua.

Kwa upande mwingine, njama hiyo iliyokuwa ikionekana kuwa ya Uhuru Kenyatta na Mwai Kibaki ilipanuliwa na kumuingiza rais mstaafu Moi kwenye suala la Kibaki na kustaafu kwake; ilidaiwa kuwa Uhuru alikuwa ameingia kwenye mkataba naye Kibaki, ikisemekana kuwa angemrithi Kibaki baada ya Kibaki kutamatisha kipindi chake.

*The Standard 11th December 2007, (64)*

> *I have not entered into any agreement with president Kibaki and former president Moi.*
>
> Sijaingia kwenye mkataba wowote na rais Kibaki na rais Mstaafu Moi.

Wakati mwingine Uhuru Kenyatta alitokea kuutetea msimamo wake Moi akidai kuwa yeye Moi alikuwa na haki ya kikatiba kuuchukua msimamo aliodhamiria kwani katiba ilikuwa inamruhusu kumuunga mgombeaji yeyote aliyependelea.

*The Standard 29th August 2007, (65)*

> *The former president is a citizen of Kenya and entitled to his opinion and support of whichever candidate he wants.*
>
> Rais Mstaafu ni mwananchi wa Kenya na ana haki ya kutoa maoni yake kuhusu mgombeaji wa kiti cha urais anayemuunga mkono.

Suala la rais Mstaafu Moi lilikuwa kama kitendawili kilichohitaji kuteguliwa na mtu mwenye msimamo thabiti aliyekuwa tayari kujinasua kutoka kwenye utandu uliokuwa umedinda kuvunjika wa chama cha KANU. Ruto alimsuta mstaafu rais Moi akimwambia kwamba alihitajiwa kuiafiki misimamo yao kama jamii ya Kalenjin; kwa mujibu wake mheshimiwa Ruto, jamii hiyo ilikuwa imeafikia kumuunga Raila Odinga mkono na hivyo basi yeyote aliyekuwa akionekana kuwa kizingiti alisutwa; Itakumbukwa kuwa wakati

hilo lilikuwa likifanyika mheshimiwa Moi alikuwa akimuunga mkono rais mstaafu Mwai Kibaki.

*Daily Nation 21st December 2007, (66)*

> *We respect Moi as one of our own, and it is imperative that he also respects our decision; after all, respect is two – way traffic.*
>
> Tunamheshimu Moi kama mmoja wetu, vile vile ni muhimu aheshimu maamuzi yetu; kwani heshima ni ya pande mbili.

Mwanasiasa huyo alisema kuwa hapo zamani walikuwa wakimpigia Moi kura kwa sababu alikuwa mmoja wao, na kuwa katika mwaka wa 2002 walimpigia Uhuru kura kwa sababu Moi aliwaomba wamsaidie, lakini wakati huo walikuwa wameamua kumpigia Raila kura".

*Saturday Standard 11th November 2007, (67)*

> *In the past we voted for Moi because he was our own. In 2002 we voted for Uhuru Because Moi asked us to support him. But this time we have decided to vote for Raila.*
>
> Zamani tulimpigia Moi kura kwa sababu alikuwa mmoja wetu, katika mwaka wa 2002 tulimpigia Uhuru kura kwa sababu alituomba tumsaidie, lakini wakati huu tumeamua kumpigia Raila kura.

Msimamo wake Moi kuwa Mkoa wa Bonde la Ufa ulifaa kuyapuuzilia mbali mawazo na misimamo yake Ruto na kutokubali kukifanya chama cha Kanu kufifia ilitokea kusutwa vikali naye Ruto ambaye alisalia kuwa jeta ambaye hakukubali kauli yake kubanduliwa na mstaafu rais Moi aliyeonekana kuwa mwenye msimamo thabiti kukihusu chama cha KANU. Mwanasiasa huyo alisema hakukuwa na sababu ya kubishana naye Moi kutokana na uzee wake; kile ambacho hangekubali ni kuyaafiki mawazo ya Moi.

*The Standard 27th August 2007, (68)*

> *Do not make the mistake of thinking about Moi. When you fight an old man, people will blame you. Listen but go ahead with your plans as the elders have decided Rift Valley is ODM.*
>
> Usiyafanye makosa ya kumfikiria Moi; Unapobishana na mzee, watu watakulaumu. Sikiliza tu, lakini uendelee na mipango yako kwa kuwa wazee wameamua kuwa Mkoa wa Bonde la Ufa ni himaya ya ODM.

Masuala ya kihistoria kuwahusu viongozi wa awali yalirejelewa na miungano yote miwili katika kampeni za uchaguzi wa urais katika mwaka wa 2013, kwa kuzirejelea faimilia za viongozi wa zamani. Mojawapo wa masuala hayo lilikuwa suala lililokuwa likifungamanishwa na uongozi wa hayati Mzee Jomo Kenyatta aliyekuwa ameliongoza taifa la Kenya tangu Kenya ilipopata uhuru hadi mwaka wa 1978 wakati alipoiaga dunia. Kutokana na Raila Odinga kulirejelea suala hilo kama njia ya kuusuta muungano wa Jubilee, Uhuru Kenyatta alimjibu akikumbusha kuwa hata baba yake alikuwa naibu wa Rais katika serikali hiyo, hili likidhamiriwa kuonyesha kuwa yeye Raila alikuwa hasemi ukweli kama alivyokuwa akifikiriwa. Yumkini Uhuru alighadhabishwa na yale Raila alikuwa akiyasema kuhusiana na familia yake hayati rais Mzee Jomo Kenyatta, ikikumbukwa kuwa hayati Jaramogi Odinga alikuwa kwenye utawala uliokuwa ukidosarishwa naye Raila. Gazeti la *Daily Nation 27th January 2013* lilikuwa na nukuu ifuatayo:


*(69)*

*… Raila keeps blaming me over my father Jomo Kenyatta's administration. Wasn't his father a vice president in that government?*

… Raila amekuwa akinikashifu kuuhusu uongozi wa baba yangu Jomo Kenyatta. Kwani baba yake hakuwa Naibu wa Rais katika serikali hiyo?

Suala kumhusu hayati Mzee Jomo Kenyatta lilichipuza katika kampeni za urais za mwaka wa 2012-13 kutokana na Uhuru Kenyatta kujitoma uwanjani dhidi ya hasimu wake wa kisiasa Raila Odinga aliyekuwa mwana wa naibu wa rais wa kwanza katika nchi ya Kenya baada ya Kenya kujinyakulia uhuru kutoka kwa Wakoloni. Baada ya kiongozi huyo (Uhuru) kuelekezewa dole la lawama naye Raila kwa muda mrefu kumhusu babake (Hayati Mzee Kenyatta), Uhuru Kenyatta aliamua kumjibu kwa kumwambia kuwa yeye Raila alikuwa akimkashifu hayati Mzee Jomo Kenyatta na kusahau kuwa babake (Raila Odinga) alikuwa naibu wa rais katika serikali hiyo. Uhuru Kenyatta aliazimia kumsawiri Raila kama mnafiki aliyekuwa hasemi ukweli kama ulivyokuwa kwa wapigaji kura nchini Kenya.

Grafu 1.8 Mada ya Viongozi wa Awali 2007 na 2013




Uchanganuzi wa Mtafiti (2015)

**Ufunguo:**
RA N – Raila *Nation*
RA S – Raila *Standard*
UH N – Uhuru *Nation*
UH S–Uhuru *Standard*
RU N – Ruto *Nation*
RU S – Ruto *Standard*

Kurejea kwa mijadala kuwahusu viongozi wa awali katika nchi ya Kenya katika kampeni kabla ya chaguzi kuu mbili katika mwaka wa 2007 na 2013; ama kwa hakika ilikuwa ithibati tosha kuwa viongozi hao walisawiriwa kama ambao walikuwa asili ya kero zilizokuwa zinaikumba nchi ya Kenya, ikiwa itikadi za viongozi wa vyama vya upinzani zilikuwa za kuzingatiwa. Rais mstaafu Moi alisutwa naye Raila katika kampeni za uchaguzi wa 2002 (utafiti huu ulijikita katika chaguzi za mwaka wa 2007 na 2013) na pia kwa kiwango cha juu katika kampeni za uchaguzi wa 2007. William Ruto uliuzomea msimamo wake rais huyo na kumwona kama kiongozi aliyekuwa amepitwa na wakati na kumuuliza kuwaacha Wakalenjin kuuchukua msimamo badalia katika uchaguzi huo wa mwaka wa 2007. Uhuru Kenyatta aliutetea msimamo wake Moi na kusema kuwa alikuwa

ana haki ya kikatiba kuafikia maamuzi aliyoona kuwa bora. Kuingia kwake Uhuru Kenyatta ulingoni katika uchaguzi wa mwaka wa 2013 kulilifufua suala la hayati Mzee Jomo Kenyatta aliyekuwa akituhumiwa naye Raila kuwa kiongozi aliyekuwa asili ya kero za nchi ya Kenya. Kulingana na grafu, suala hilo kuwahusu viongozi wa awali lilizungumziwa zaidi katika kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2007; huenda ikawa ni kwa sababu ya rais mstaafu Moi kuungana nao Kibaki na Uhuru.

### 4. 3. 9 Mada ya Ghasia za Uchaguzi

Mada kuhusu ghasia za uchaguzi wakati wa uchaguzi haikuzungumziwa sana katika kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2007, japo kulikuwa na ghasia chache kabla ya uchaguzi kufanywa. Kuzungumziwa huko kuliangazia ghasia katika mikutano ambapo Raila Odinga alikikashifu kitendo cha akina Ruto kushambuliwa katika mkutano wake Nyachae na kusema kuwa wahusika walitakiwa kutiwa mbaroni (Tukio hilo lilikuwa limetokea huko Kisii).

*Daily Nation 3rd November 2007, (70)*

> *The government has failed to arrest perpetrators of political violence who have now become immune to prosecution. This is completely unacceptable.*
>
> Serikali imeshindwa kuwatia mbaroni wanaozua machafuko ya kisiasa na ambao sasa hawawezi wakashtakiwa. Hili halikubaliki kabisa.

Suala hilo kuhusu ghasia za kisiasa lilipenya kwenye kampeni za urais kwa njia tofauti, ikikumbukwa kuwa ghasia za siku za awali zilikuwa hazihusu kushambuliwa kwa viongozi wa vyama. Baada ya Ruto kushambulliwa huko Kisii ilikuwa bayana kuwa nchi ya Kenya ilikuwa inayatumbulia macho ghasia za kiwango tofauti kwani itakumbukwa kuwa Ruto alikuwa ameshambuliwa na wafuasi wa kundi pinzani kwa kutuhumiwa kuwa alikuwa hajapata mwaliko kuhudhuria mkutano wa kuchangisha pesa katika Wilaya ya Kisii.

*Daily Nation 4th October 2007, (71)*

> *I have called all of you to prove that I am stable and to end your worries because I have received so many calls, SMSs and emails. ODM believes in competition in agenda setting, policies and views, not the use of crude weapons as being advocated by some leaders.*

> Nimewaita nyinyi nyote hapa ili kudhihirisha kuwa niko imara kwa sababu nimepigiwa simu, na kupokea arafa nyingi na barua pepe; ODM inaamini katika ushindani wa ajenda, kujiegemeza katika maono na sera, na sio kutumia siraha butu kama vile viongozi wengine wanavyohimiza.

Ghasia za baada ya uchaguzi yalizungumziwa na Uhuru Kenyatta aliyesema kuwa ikiwa mgombeaji wa kiti cha urais kwa tikiti ya muungano wa CORD alikuwa mpenda amani angezuia vita hivyo vya kikabila katika mwaka wa 2007. Alisema kuwa hakuwa akimpinga kutokana na suala la kabila lake, lakini kutokana naye kutosaidia kusitisha ghasia hizo hadi pale alipokabidhiwa uongozi wake wa Serikali ya Muungano (nusu mkate).

*Daily Nation 19th February 2013, (72)*

> *I don't oppose him because of his ethnicity. In 2007 he was a key leader in the conflict but there is no single day he opened his mouth castigating the violence until when he was granted his half bread government.*
>
> Simpingi kwa sababu ya kabila lake. Katika mwaka wa 2007 alikuwa kiongozi mkuu wa ODM wakati wa machafuko lakini hakuna hata siku moja alikifungua kinywa chake akiyakashifu machafuko hayo hadi pale alipopokezwa serikali yake ya nusu mkate.

Matukio ya kuhofisha kuhusu ghasia za kisiasa baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 baada ya kura za urais kutangazwa yalimfanya Ruto kuyazungumzia na kusema kuwa waliamua kushirikiana na Uhuru Kenyatta ili kuhakikisha kuwa ghasia za kikabila katika Mkoa wa Bonde la Ufa hayangetokea tena. Alisema kuwa hakuna siku nyingine ambapo Wakenya wangeimwaga damu kwa sababu ya ushindani wa kisiasa.


*The Standard 2nd January 2013, (73)*

> *Never again should citizens shed blood on the account of political competition like it happened in 2007.*
>
> Wananchi hawataimwaga damu kwa misingi ya ushindani wa kisiasa kama ilivyofanyika katika mwaka wa 2007.

Mjadala kuhusu ghasia za kisiasa ulizungumziwa na wanasiasa wote hao niliowateua ili kuipata data ya kuchanganuliwa. Mjadala huo uliyahusisha machafuko yaliyoshuhudiwa huko Kisii miezi miwili kabla ya uchaguzi wa mwaka wa 2007, ambapo William Ruto

alishambuliwa. Katika uchaguzi wa mwaka wa 2013, suala hilo lilirejelewa na kuwafanya wanasiasa kama vile Ruto kukiri kuwa jambo hilo halingeweza kushuhudiwa tena katika nchi ya Kenya kutokana na kuungana kwa makabila mawili ambayo yalisemwa kuwa yalikuwa yakipigana nyakati za uchaguzi. Uhuru Kenyatta alimsimanga mpinzani wake Raila akisema kuwa yeye Raila hakujihusisha na juhudi za kuhubiri amani na kuwa, alifanya hivyo baada ya kuipata 'serikali yake ya nusu mkate'.

Grafu 1.9 Mada ya Machafuko 2007 na 2013




Uchanganuzi wa Mtafiti (2015)

**Ufunguo:**

RA N – Raila *Nation*
RA S – Raila *Standard*
UH N – Uhuru *Nation*
UH S–Uhuru *Standard*
RU N – Ruto *Nation*
RU S – Ruto *Standard*

Usemi wa wanasiasa huilenga hadhira katika miktadha mbalimbali ya jamii kwani usemi wao hauwezi ukatekelezwa katika ombwe tupu. Kutokana na mtazamo huo, picha inayosawiriwa na grafu inaonyesha kuwa mpando na mshuko wa kuzungumziwa kwa

mada hiyo katika miktadha ya kisiasa wakati wa kampeni za urais nyakati zote hizo mbili ilichangiwa na miktadha na matukio ya kihistoria. Akilizungumzia suala la usemi na siasa kwa kuchanganua matini na mazungumzo ya kisiasa, Chilton na Schaffner (1997:215) waliuliza ni kwa njia gani ambayo uchaguzi wa lugha ya mzungumzaji inaweza kufasiriwa kama inayofanya kazi kwa mkakati wa kisiasa, kwa kuangazia mawanda mapana ya siasa kiutamaduni na ufinyu wa miktadha ya kisiasa? Kwa mujibu wa grafu, katika kampeni za mwaka wa 2013 mengi yalisemwa kuhusu ghasia za baada ya uchaguzi.

### 4. 3. 10 Mada ya Umri wa Wagombeaji

Mada ya umri wa wagombeaji ilijitokeleza katika kampeni za urais kama njia moja ya kuonyesha kuwa, yeye Uhuru Kenyatta alikuwa anautengeneza mstakabali wake wa siku za usoni na si kwamba kulikuwa na njama yoyote. Uhuru alitokea kulileta suala la umri kwenye kampeni mwaka wa 2007 akidhamiria kuwashawishi wafuasi wa chama cha KANU kuuafiki msimamo wake na si kwamba alikuwa akikisaliti chama hicho. Gazeti la *The Standard 21st December 2007* lilikuwa na nukuu hii:

> *(73)*
>
> *Iam still young and time is on my side to contest the presidency in the future.*
>
> Ningali na umri mdogo na pia ningali na muda wa kung'ang'ania kiti hicho cha urais katika siku za usoni.

Wakati wa kampeni za urais za mwaka wa 2007 rais mstaafu Mwai Kibaki alisutwa huku uongozi wake ukitiwa dosari na wapinzani wake mmoja wao akiwa ni Ruto. Ruto aliliona kundi la rais mstaafu Mwai Kibaki kama kundi la viongozi waliokongoka na ambalo lilikuwa limepitwa na wakati. Ruto alilitaja kundi zima la wandani wake Kibaki kama kundi lililokuwa linajumuisha wazee ambao hawangeweza kuiendesha Kenya baada ya uchaguzi huo wa 2007; kulingana naye kundi lake Kibaki lilikuwa la kikabila.

*Daily Nation 18th September 2007, (74)*

> *The paraded supporters of Kibaki represented face of the past although Uhuru Kenyatta was youthful he succumbed to tribal politics and destroyed the oldest party in Kenya.*
>
> Kundi la wafuasi wa Kibaki lililoonyeshwa kuwa linamuunga mkono linawakilisha nyuso za zamani japo Uhuru Kenyatta alikuwa mwenye umri

mdogo aliemewa na siasa za ukabila na kukivunja chama chenye historia ndefu nchini Kenya.

Mwanasiasa huyo aliongezea kusema kinga'nga'nyiro cha mwaka huo kiliwahusisha viongozi wazee; yaani waliokuwa wa siku za nyuma na wale waliokuwa wanalenga siku za usoni. Kibaki na kundi lake walisawiriwa kama viongozi waliokuwa wamepitwa na wakati.

*The Standard 2nd September 2007, (75)*

> *This will be a contest between those who represent the status quo, yesterday, and the past against those who represent today, tomorrow and future.*
>
> Hiki kitakuwa king'ang'anyiro baina ya wale wanaowakilisha hali ilivyo, jana, na siku zilizopita dhidi ya wale wanaowakilisha leo, kesho, na siku za baadaye.

Katika kampeni za uchaguzi wa mwaka 2013, suala kuhusu umri wa viongozi wa muungano wa CORD lilijikuta katika jukwaa wakati wa kampeni. Akiyapuuzilia mbali madai ya umri Raila alisema kuwa umri haukuwa hoja muhimu katika kuelezea yule ambaye angeiongoza nchi ya Kenya; kazi ambayo ingefanywa na huyo rais ndiyo iliyokuwa na umuhimu kwani uongozi ulikuwa ni maono; na kuwa mtu angeweza kuwa na umri mdogo lakini atokee kuwa na maono hafifu na yule mzee akawe na maono mazito"

*Daily Nation 29th January 2013, (76)*

> *Age is just but a number, leadership is in ideas, so you can be very young but very old in ideas and you can be old but young in ideas.*
>
> Umri si kitu bali ni nambari, uongozi ni maono, kwa hivyo unaweza kuwa na umri mdogo lakini uwe na maono hafifu na huenda ukawa mzee lakini mwenye maono mazito.

Suala la umri na kustaafu lilizungumziwa na Uhuru Kenyatta aliyemuuliza Raila kustaafu na kuwaachia watoto ambao yeye Raila alikuwa amewapata katika ndoa kujihusisha na siasa. Mwanasiasa huyo alisema kuwa alimpenda Raila lakini hakuwa na budi kulifanya jambo aula la kustaafu kwa kuwa walikuwa wamezipiga siasa kwa zaidi ya miaka 30.

*The Standard 21st February 2013, (77)*

*We have respect for Raila not hatred that's why we want him to retire so that we can compete with the children he has sired.*

Sisi tunamheshimu Raila na si kumchukia, na hiyo ndio maana tunataka yeye astaafu ili tushindane na watoto aliowazaa yeye.

Wakati mmoja mwanasiasa huyo aliwauliza Raila Odinga na Kalonzo Musyoka kustaafu pamwe naye rais mstaafu Mwai Kibaki aliyekuwa anakaribia kukitamatisha kipindi chake katika uongozi wa taifa na kuwaachia vijana uongozi kwani hao ndio waliokuwa na nguvu ya kuwafanyia wananchi kazi. Nukuuu yake kwenye *Daily Nation 6$^{th}$ January 2013* ilikuwa:

*(78)*

*These two gentlemen should retire honorably with President Mwai Kibaki to leave the reign of power for the youthful and energetic leaders to move this country forward.*

Hawa wazee wawili lazima wastaafu kwa heshima pamwe na rais Mwai Kibaki ili kuuacha uongozi kwenye mikono ya vijana walio na nguvu na watakaoiendeleza nchi hii mbele.


Ruto alizungumzia umri na uongozi wa taifa la Kenya na kudai kuwa wakati wa vijana kuiongoza nchi ulikuwa umepiga hodi na kuwa ilikuwa ufisadi wa kisiasa kutoka kwa wapinzani wao kudai kuwa mtu angekuwa mzee ki umri lakini awe na mawazo mapevu ya uongozi. Aliliona suala la vijana kuiongoza nchi kama ambalo lilikuwa limepiga hodi na kuwa wazee walikuwa wanaulizwa kuachana na uongozi kama njia moja ya kuipa nchi nafasi ya kupiga hatua kimaendeleo.

*Daily Nation 6$^{th}$ January 13, (79)*

*The time for the youth to lead is now... their tomorrow has come. I hear some of our rivals saying that one can be old but young in terms of ideas; this is political fraud.*

Wakati wa vijana kutwaa uongozi ni sasa… kesho yao imeshafika. Ninawasikia wapinzani wetu wakisema kuwa mtu anaweza kuwa mzee lakini awe mchanga ki mawazo; huu ni ulaghai wa kisiasa.

Grafu 1.10 Mada ya Umri wa Wagombeaji 2007 na 2013




Uchanganuzi wa Mtafiti (2015)

**Ufunguo:**
RA N – Raila *Nation*
RA S – Raila *Standard*
UH N – Uhuru *Nation*
UH S–Uhuru *Standard*
RU N – Ruto *Nation*
RU S – Ruto *Standard*

Ili kutamatisha sehemu hii, ni msimamo wangu kutaja kuwa mada ya umri kwa wagombeaji wa kiti cha urais katika chaguzi zote mbili ilichipuza katika kampeni za mwaka wa 2007 ambapo Raila na Ruto walikuwa wakiichezea ngoma yao katika chama cha ODM. Wanasiasa hao walisema kuwa ikiwa Kenya ilikuwa inatarajia kujitanzua kutoka kwenye kinamasi cha ukoloni, basi wananchi waliwajibika kumpigia kura Raila ambaye aliliona kundi la Kibaki kama ambalo halingeweza kuyatekeleza majukumu muhimu ya kuimarisha taifa la Kenya. William Ruto aliuona muungano wa PNU kama ambao ulikuwa unaongozwa na 'mazee' yaliyokuwa yamechoka kweli, na ambayo kesho ya taifa la Kenya chini yao ingekumbwa na shida nyingi. Uhuru Kenyatta alishikilia kwamba yeye hakuwa na wasiwasi kwani umri wake ulikuwa mdogo na kuwa kumuunga Mwai Kibaki mkono ndiyo iliyokuwa njia rahisi ya chama cha KANU kurejea uongozini.

Katika mwaka wa 2012-13, Uhuru na Ruto walimsuta Raila na kumuuliza astaafu kwani wakati wa 'madijitali' kuiongoza nchi ya Kenya ulikuwa umefika. Raila alinukuliwa akisema kuwa lililokuwa muhimu ni busara; na kuwa mtu angekuwa na umri mdogo lakini akatokea kukosa busara, hivyo basi, kulingana naye alikuwa rai kukigombea kiti cha urais. Grafu inaonyesha kuwa umaratokezi wa kuzungumziwa kwa mada kuhusiana na umri wa wagombeaji viti vya urais ilienziwa na wanasiasa katika chaguzi hizo zote mbili, japo katika mwaka wa 2013 kiwango kilikuwa zaidi ya kile cha 2007.

**4. 3. 11 Mada ya Nchi za Kigeni**

Suala la mataifa ya nje kujiingiza katika siasa za nchi ya Kenya liliangaziwa na Raila Odinga, ambaye kulingana naye alisema kuwa; Kenya na mataifa ya nchi za nje ingetokea kutokubali kushirikiana ikiwa viongozi wa Jubilee wangechaguliwa kwani walikuwa wanakumbwa na makosa ya jinai. Aliangazia kuwa Uhuru Kenyatta angetafutwa kama rais wa Sudan Bashir aliyekuwa amewekewa ilani ya kukamatwa kama angezuru nchi zilizokuwa wanachama wa mahakama hiyo ya Hague huko Uholanzi. Mwanasiasa huyo alihoji kuwa Kenya ingeongozwaje kupitia mtandao; kulingana naye hilo lilikuwa jambo zito mno.

*The Standard 9th December 2012, (80)*

> *How will you lead Kenya when you are wanted like Bashir, he cannot travel alot because if he lands in countries which are ICC signatories he will be arrested.*
>
> Utaiongozaje Kenya ikiwa unasakwa kama Bashir, hawezi akazuru nchi nyingi kwa sababu akiwasiri katika nchi ambazo ni wanachama wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai ya Hague atatiwa mbaroni.

Raila Odinga alizidi kusema kuwa hakuna wawekezaji ambao wangedhubutu kuwekeza katika nchi ya Kenya ikiwa hao waliokuwa wametuhumiwa kwa makosa ya jinai wangechaguliwa, kwani picha waliyokuwa wakiisawiri kulihusu taifa la Kenya ilikuwa mbaya.

*The Standard 14th January 2013, (81)*

> *No investors would come to Kenya if you elect a president with a bad image internationally.*

> Hakuna wawekezaji ambao watakuja Kenya ikiwa mtamchagua rais aliye na dosari kimataifa.

Mijadala kuhusu mataifa ya kigeni kuyaingilia masuala ya kisiasa ya nchi ya Kenya yalizungumziwa na Ruto ambaye aliyauliza mataifa hayo kuutangaza msimamo wao kuhusiana na suala la kumuunga mkono Raila Odinga. William Ruto aliliona suala hilo la kujiingiza kwa mataifa hayo kama njia mojawapo ya kuzua ghasia na kuwatisha wapigaji kura. Alisema kuwa ikiwa mataifa hayo yalikuwa yakimuunga Raila mkono katika uchaguzi, wao hawakuwa na shida; walilohitaji kujua ni kuambiwa bayana kuuhusu msimamo wao juu ya madai hayo.

*Daily Nation 11th February 2013, (82)*


> *These nations should stop playing about issues; they should come out openly and tell Kenyans that they are supporting Raila Odinga. We will not have a problem with that.*
>
> Mataifa haya yanatakiwa yasitishe kuchezea masuala mengine, hawana budi kusema waziwazi na kuwaelezea Wakenya kuwa wao wanamuunga mkono Raila Odinga. Hatutakuwa na shida na jambo hilo.

William Ruto alishadidia kauli yake kwa kuangazia suala la Kofi Annan ambaye alitajwa naye mwanasiasa huyo kama mtu aliyekuwa hana mamlaka ya kuingilia siasa za nchi ya Kenya. Itakumbukwa kuwa Kofi Annan alishiriki katika kuyapatanisha makundi mawili kinzani (PNU na ODM) baada ya machafuko ya uchaguzi nchini Kenya yaliyotokea baada ya kutangazwa kwa kura za urais katika Uchaguzi Mkuu wa 2007 na kupelekea kuundwa kwa serikali ya muungano.

*The Standard 14th October 2012, (83)*

> *It is in bad taste for a person like Annan to travel all the way from Ghana to dictate voters on who to elect in the coming General Election and I am telling him to keep off from interfering with Kenyan politics.*
>
> Ni tabia mbaya kwa mtu kama Annan kusafiri kutoka nchi ya Ghana kuja kulazimisha wapigaji kura juu ya yule wanayehitajika kumchagua katika Uchaguzi Mkuu ujao; ninamwambia kuwa aache kujiingiza katika siasa za nchi ya Kenya.

Grafu 1.11 Mada ya Nchi za Kigeni 2007 na 2013




Uchanganuzi wa Mtafiti (2015)

**Ufunguo:**
RA N – Raila *Nation*
RA S – Raila *Standard*
UH N – Uhuru *Nation*
UH S–Uhuru *Standard*
RU N – Ruto *Nation*
RU S – Ruto *Standard*

Kwa mujibu wa picha iliyosawiriwa na grafu, mada hii ilijitokeza waziwazi kwa mara ya kwanza katika kampeni za urais za mwaka wa 2012-13 kutokana na Uhuru Kenyatta na William Ruto kushtakiwa katika Mahakama ya Kimataifa ya Jinai ya Hague kwa tuhuma za mauaji na kuyafadhili makundi ya kijangili ili kuyatekeleza mauaji dhidi ya wananchi wa jamii fulani nchini Kenya na kuhamishwa kwa wananchi kutoka kwenye makao yao. Kutokana na kushtakiwa kwao, Raila alionelea kuwa haikuwa murua kwa viongozi hao wa muungano wa Jubilee kujitosa uwanjani na kukigombea kiti hicho cha urais kutokana na tetesi kuwa Kenya kama taifa ingetokea kutengwa na mataifa mengine na kuwa viongozi hao wa muungano wa Jubilee wangewindwa kama rais wa Sudan Bashir aliyekuwa akisakwa. Viongozi hao wa muungano huo wa Jubilee walidai kuwa walikuwa na haki ya kikatiba nchini Kenya ya kuugombea urais, na kuwa mataifa hayo ya nje

yalikuwa yakikiuka mpaka kwa kuwapendelea viongozi wa muungano wa CORD. Suala hili lilikuwa mojawapo wa masuala nyeti yaliyotumiwa na muungano wa CORD; kwa upande wao muungano wa Jubilee uliyasimanga mataifa hayo ya kigeni pamwe na mawakala wao (Kofi Anaan) waliokuwa wakiisawiri picha ya kuwapo kwa uwezekano wa Kenya kutengwa na mataifa yenye uwezo mkubwa duniani.

### 4. 3. 12 Mada ya Mahakama ya Hague

Suala jingine lililochipuza kwa mara ya kwanza katika kampeni za uchaguzi wa 2013 lilihusiana na Mahakama ya Kimataifa ya Hague kufuatia kushtakiwa kwa Uhuru Kenyatta na mwenzake William Ruto kwenye mahakama hiyo kwa makosa ya jinai baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 walipotuhumiwa kuwa walihusika katika mauaji ya watu miongoni mwa mashtaka mengine. Raila hakuliafiki suala la washukiwa hao kulitawala taifa kwa kutumia mtandao kama walivyokuwa wamenukuliwa wakisema. Nukuu yake ya tarehe *12th February 2013* kwenye gazeti la *Daily Nation* ilikuwa:

> *(84)*
>
> *I do not want to eliminate my competitor, but I know that it will pose a serious challenge to run a government through skype from the Hague.*
>
> Mimi sitaki kumuondoa mpinzani wangu; lakini ninajua itakuwa changamoto kuitawala serikali kutoka huko Hague kupitia mtandao.

Mwanasiasa huyo alitokea kukanusha kuwa yeye hakuhusika kwa lolote katika kupelekwa kwa wapinzani wake huko Hague kama ilivyokuwa ikidaiwa na wapinzani hao. Raila alikuwa akituhumiwa kuwa kwa kiwango kikubwa ndiye aliyechochea kupelekwa kwa wanasiasa hao wakuu wa muungano huo wa Jubilee katika mahakama ya Hague.

*Daily Nation 3rd November 2012, (85)*

> *I have no hand in the problems facing (URP leader) William Ruto, (DPM) Uhuru Kenyatta, Francis Muthaura and Joshua Sang.*
>
> Mimi sikuhusika katika mambo yanayowakumba kiongozi wa *URP* William Ruto, *DPM* Uhuru Kenyatta, Francis Muthaura na Joshua Sang.

Mjadala kuhusu Mahakama ya Kimataifa ya Jinai ya Hague ulimvutia mwanasiasa huyo (Ruto) ambaye pamwe na mgombeaji kiti mwenza walikuwa wameshtakiwa katika mahakama hiyo kwa tuhuma za kuwa walikuwa wameshiriki katika mapigano ya baada ya uchaguzi mkuu katika mwaka wa 2007. Mwanasiasa huyo aliwasuta wapinzani wao kuwa

walikuwa wanaupoteza muda wao kwa kuzungumza juu yake na mgombeaji kiti mwenza (Uhuru Kenyatta) na kuwashauri kuzungumzia ajenda zao. Alitahadharisha kuwa ikiwa Wakenya wangetokea kuwachagua; basi mtu yeyote mwenye akili razini angetokea kuuhoji uamuzi wa kuwapeleka Hague uliafikiwa vipi.

*The Standard 1st February 2013, (86)*


> *If the people of Kenya elect two gentlemen who are alleged to have committed serious crimes against it citizens and actually participated in killing their own citizens, I am sure any reasonable person will want to ask themselves what is going on.*
>
> Ikiwa wananchi wa Kenya watawachagua wanaume wawili ambao walituhumiwa kuwa waliyafanya makosa mabaya sana ya kushiriki katika mauaji ya watu wake, nina hakika kuwa mtu yeyote mwenye akili razini atajiuliza kwani ni nini kinaendelea.

Kuna wakati mwingine ambapo mwanasiasa huyo alilitaja suala kuhusu kuwajibika kwake Waziri Mkuu wakati huo kuwa angehakikisha kuwa mashtaka hayo ya Kesi za Jinai yaliyokuwa yakiwakabili mwanasiasa huyo na mgombeaji kiti mwenza kuwa ingeletwa nchini kama dhihirisho la ulaghai wa kisiasa uliokuwa unafanywa na mpinzani wao; akimkumbusha kuwa hakuwa na budi kujua kuwa nchini Kenya kulikuwa na upungufu wa watu wajinga.

*The Standard 7th November 2012, (87)*

> *The prime minister should know that there is a shortage of foolish people in Kenya whom he can lie to that he would support local trial of ICC cases, at the very least, the PM should be honest on this what he is now engaging in is Political Conmanship (sic) Kenyans cannot buy.*
>
> Waziri mkuu anahitaji kujua kuwa kunao upungufu wa wajinga nchini Kenya ambao anaweza kuwahadaa kuwa yeye ataunga mkono msimamo wa kuzileta kesi za Mahakama ya Kimataifa ya Jinai nchini Kenya. Lazima Waziri Mkuu awe mwaminifu katika jambo hilo, kwani anachojihusisha kwacho ni Ulaghai wa Kisiasa (japo kwa makosa) Wakenya hawawezi kuliafiki jambo hilo.

Grafu 1.12Mada ya Mahakama ya Hague 2007 na 2013




Uchanganuzi wa Mtafiti (2015)

**Ufunguo:**
RA N – Raila *Nation*
RA S – Raila *Standard*
UH N – Uhuru *Nation*
UH S–Uhuru *Standard*
RU N – Ruto *Nation*
RU S – Ruto *Standard*

Kulingana na grafu ni dhahiri kusema kuwa, maajilio ya Mahakama ya Hague kwenye ulingo wa siasa yalikuwa kati ya masuala ya kihistoria yaliyokuwa na uchanga katika kipindi hicho cha uchaguzi mkuu nchini Kenya; suala hilo lilikuwa kiazi moto kwa upande wa muungano wa Jubilee kutokana na kushtakiwa kwa viongozi wa muungano huo kwenye mahakama hiyo. Raila Odinga aliliona wazo la washukiwa hao wawili la kukigombea kiti hicho cha urais wakiwa washtakiwa kama jambo lililokuwa likienda kinyume na uwajibikaji, na kulingana naye, wanasiasa hao hawangeruhusiwa kuwa wagombeaji wa kiti cha urais hadi pale mahakama hiyo ingetokea kuwanasua kutoka kwa 'utandu' huo ikiwa wangepatikana kuwa hawangekuwa na mashtaka ya kujibu. Kwa upande wao, Uhuru na Ruto waliliona wazo hilo la kupelekwa kwao kwenye mahakama hiyo kama njia iliyokuwa imetekelezwa na muungano mzima wa CORD ili kuhakikisha

kuwa Raila ameutwaa uongozi wa nchi ya Kenya. Kwingineko, wanasiasa hao walidai kuwa kulikuwa na uwezekano wao kuendelea na kesi hiyo na wakati huo huo kuiongoza nchi ya Kenya hata kama ingekuwa kwa njia ya mtandao.

### 4. 3. 13 Mada ya Kura ya Maoni

Uhuru Kenyatta alilizungumzia suala la kura ya maoni akimtahadharisha Raila Odinga kuwa kura ya maoni haikuwa na nafasi katika kutoa fununu za matokeo katika uchaguzi uliokuwa unangojewa. Alimwambia kuwa kilichokuwa na umuhimu ni idadi ya wapigaji kura na hivyo ikiwa angeshindwa hakuwa na budi kukubali ushinde wake. Uhuru aliiona kura ya maoni kama jitihada zilizokuwa hazina nafasi ikiwa idadi ya wapigaji kura ki maeneo ingezingatiwa. Alimuuliza Raila akubali kushindwa kwa amani ikiwa hilo lingetokea.

*The Standard 24th February 2013, (88)*


> *We have the numbers, I appeal to Raila to concede defeat once the Jubilee coalition wins. We want to peacefully send them home and give the PM his benefits with love.*
>
> Tunayo idadi kubwa ya wapigaji kura, ninamsihi Raila kuyakubali matokeo pindi tu Jubilee itakapotangazwa kuwa mshindi. Tunataka kuwatuma nyumbani kwa amani na tumpe Waziri Mkuu masrufu yake kwa upendo.

Suala kuhusu idadi ya wapigaji kura iliyokuwa imetolewa na Tume ya Uchaguzi na Mipaka ya Kenya ikiangazia idadi ya watu iliyokuwa imejiandikisha kupiga kura kutoka kila eneo nchini Kenya ilichipuka katika kampeni za Ruto aliyesema kuwa, ilikuwa dhahiri kuwa kulingana na matokeo yaliyokuwa yanaonyesha idadi ya wapiga kura nchini; ushindi ulikuwa unaegemea kwao – ushindi mkubwa. Gazeti la *Daily Nation 6th January 2013* lilikuwa na nukuu ya mwanasiasa huyo iliyokuwa:

> *(89)*
>
> *Going by figures released by IBEC we have the requisite numbers and we shall win by a landslide.*
>
> Kufuatia idadi ya wapigaji kura iliyotangazwa na Tume ya Uchaguzi na Mipaka ya Kenya, tutakuwa na ushindi mkubwa kwani tunayo nambari inayohitajika.

Wakati wa kampeni, kila mrengo uliibua njia mbadala ya kuwashawishi wapigaji kura ili wawapigie kura zao; muungano wa CORD uliegemea matokeo ya kura ya maoni iliyokuwa ikimweka Raila mbele ya mpinzani wake wa karibu Uhuru Kenyatta. Kwa upande wa muungano wa Jubilee, wao walisema kuwa kura ya maoni haikuwa njia ambayo ilikuwa kiashiria kizuri cha kuelezea ni muungano upi ungeutwaa uongozi wa taifa hili. Uhuru Kenyatta alinukuliwa wakati mmoja akisema kuwa walikuwa na nambari kubwa ya wapigaji kura, na kuwa Raila Odinga alikuwa hana budi kukubali kushindwa baada ya kura za rais kutangazwa. Kulingana na mwanasiasa huyo, aliiona Jubilee ikiutwaa ushindi kwa kiwango kikubwa cha kura.

Grafu 1.13 Mada ya Kura ya Maoni 2007 na 2013




Uchanganuzi wa Mtafiti (2015)

**Ufunguo:**
RA N – Raila *Nation*
RA S – Raila *Standard*
UH N – Uhuru *Nation*
UH S–Uhuru *Standard*
RU N – Ruto *Nation*
RU S – Ruto *Standard*

Matokeo ambayo yalidokezwa na grafu yalidhihirisha kuwa usemi kuhusiana na kura za maoni ulikuwa mwingi na kuwa viwango vya kuzunguziwa kwa suala hilo na wanasiasa kulidhihirika katika kampeni za wanasiasa hao. Usemi kuhusiana na tukio hilo la kura ya maoni ulikuwa na ncha mbili zilizokuwa zinakinzana, ncha moja ikiafiki matokeo hayo, nayo ncha nyingine ikijibidiisha kuyapuuzilia mbali matokeo hayo. Grafu ilionyesha kuwa viwango vilikuwa vina ukaribu wa kuwa sawa, hasa katika kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2013.

**4. 3. 14 Mada ya Mitafaruku katika Vyama**

Mijadala kuhusu mitafaruku katika vyama iliingia katika jukwaa wakati wa kampeni za urais katika mwaka wa 2007 kutokana na misimamo iliyokinzana ya viongozi vyamani. Mjadala mkali kukihusu Chama cha KANU ulishuhudiwa kutoka kwa wakereketwa wa chama hicho waliomkashifu Uhuru Kenyatta kutokana na msimamo wake wa kuwaongoza wanachama wa chama hicho kumuunga rais Kibaki mkono bila ya makubaliano safi kutoka kwa wajumbe wa chama hicho mashinani. Kwa upande wake Uhuru alishikilia kuwa wanachama wote waliafikiana katika uamuzi huo na hivyo basi haikuwa murua kwa chama cha ODM kutumia suala hilo kuitenga jamii ya Wakikuyu.

*The Standard 11th December 2007, (90)*

> *My support for president was a collective decision by Kanu's top organs and ODM should not capitalize on it to isolate the Kikuyu from other communities.*
>
> Uamuzi wangu wa kumuunga rais mkono ulikuwa wa viongozi wa juu wa chama cha Kanu na kwa hivyo ODM isilitumie jambo hilo kuitenga jamii ya Wakikuyu kutoka kwa jamii zingine.

Uhuru Kenyatta aliyekuwa anatuhumiwa kuwa alikuwa amekisambaratisha chama cha KANU alijaribu kuutetea msimamo wake kama njia mbadala ya kuhakikisha kuwa chama hicho kingerejea kwa kishindo uongozini, hili lilifuatia mtafaruku uliokuwa umekita mizizi katika chama hicho. Alitabiri kuwa rais Kibaki angekuwa akitawala kipindi chake cha mwisho nayo Kanu ingekuwa ikijitayarisha tena kurudi katika utawala mwaka wa 2012. Gazeti la *Daily Nation 20th September 2007* lilikuwa na nukuu yake:

> *(91)*

*President Kibaki will be making his final lap during which time Kanu will have re-organised itself to recapture power in 2012.*

Rais Kibaki atakuwa akitawala kipindi chake cha mwisho nayo Kanu itakuwa ikijitayarisha tena kurudi katika utawala mwaka wa 2012.

Migongano ya vyama ilikuwa dhahiri wakati wa kampeni mwaka wa 2007; itakumbukwa kuwa William Ruto alikuwa mwanachama wa Kanu lakini mwaka wa 2007 alikigura chama hicho na kuelekea ODM. Kutoka kwake kulitokana na mivutano ya uongozi iliyokuwa chamani. Alimkashifu Uhuru akisema kuwa Uhuru alikuwa ni rafiki yake lakini hatua aliyoichukua haikuwa kwa faida ya chama na wanachama wake lakini kwa faida yake mwenyewe.

*The standard 18th October 2007, (92)*

*Uhuru is my friend, but the decision he made was not in the interest of the party and its members.*

Uhuru ni rafiki yangu, lakini hatua aliyoichukua haikuwa kwa faida ya chama na wanachama wake.

William Ruto akiwa kama Katibu Mkuu wa chama cha Kanu alikuwa ameshirikiana na Raila katika harakati za kupinga kuzinduliwa kwa katiba mpya mwaka wa 2005, na hivyo msimamo wake ulikuwa, chama cha Kanu kilikuwa na jukumu la kukiunga chama cha ODM mkono, la sivyo yeye alikuwa ametishia kukihama chama ikiwa Kanu ingetokea kuitema ODM.

*The standard 7th October 2007, (93)*

*I promised Kenyans that if KANU ditches ODM then I will resign. I want to announce now that I have officially decamped from KANU and resigned my position as Secretary General.*

Niliwaahidi Wakenya kuwa nitaihama KANU ikiwa KANU ingeitema ODM. Ninataka kutangaza kuwa nimeihama KANU rasmi na kujiuzuru kama Katibu Mkuu.

Mambo katika Kanu yalionekana kutokuwa mazuri kwani William Ruto alikuwa ameonyesha kuwa chama hicho kilikuwa na wenyewe ambao walikuwa wamesharejea, hivyo basi ilimlazimu kukitema chama hicho kama hatua ya kuwaachia wenyewe chama chao. Kwenye gazeti la *Daily Nation 1st October 2007* alikuwa amenukuliwa akisema:

*(94)*

*We have decided that since the original owners of the party have come back, then it's prudent for us to quit. We shall be making an announcement this week as to our next course of action.*

Tumeamua kuwa, kwa sababu wamiliki asili wa chama hiki wamerudi; ni vizuri sisi tukihame. Kwa hivyo; tutayafanya matangazo yetu kuhusu uamuzi wetu Juma lijalo.


Kuhama kwake kuliashiria kuwa, yeye kama msemaji wa chama alikuwa amekihama chama na wafuasi wote (Wakalenjin); hili lilikuwa kama hakikisho kuwa KANU ilikuwa imeingia kwenye muungano na chama cha ODM chini ya uongozi wake Raila. Mwanasiasa huyo aliyekuwa na ushawishi mkubwa alikuwa ametabiri kuwa ODM ilikuwa ndicho chama ambacho kingeweza kuyaleta mabadiliko yaliyokuwa yanatarajiwa nchini Kenya.

*The standard 7th October 2007, (95)*

*The people and Kanu Party membership is with me in ODM because it is the party that supports real change for this country.*

Watu na wafuasi wa chama cha Kanu wako nami katika ODM kwa sababu hiki ndicho chama kinachounga mkono suala la mabadiliko.

Grafu 1.14 Mada ya Mitafaruku katika Vyama 2007 na 2013




Uchanganuzi wa Mtafiti (2015) **Ufunguo:** RA N – Raila *Nation*

RA S – Raila *Standard*

UH N – Uhuru *Nation*

UH S–Uhuru *Standard*

RU N – Ruto *Nation*

RU S – Ruto *Standard*

Suala la KANU liliibuka kwa kiwango kikubwa katika kampeni za urais za mwaka wa 2007 kutokana na viongozi wawili wa chama hicho kuzipiga siasa wakiwa katika vyama tofauti. William Ruto aliyekuwa katibu wa chama hicho alikuwa amehamia ODM yake Raila naye mwenyekiti wa chama cha KANU alikuwa akimuunga mkono Kibaki wa chama cha PNU. Tukio hilo lilipelekea kuibuka kwa malumbano makali dhidi ya Uhuru na wakereketwa sugu wa chama hicho akiwamo rais mstaafu Moi ambao walimtaja Uhuru kuwa msaliti. William Ruto alimtazama Uhuru kama kiongozi aliyekuwa amekidunisha chama hicho na kwa sababu ya tukio hilo yeye Ruto aliamua kukihama chama hicho na kuwaachia wenyewe. Kuhamia kwa Ruto ODM kulipelekea wafuasi wengi wa chama hicho kwenda naye katika ODM. Kulingana na maono yake Uhuru; Kibaki alikuwa akitarajia kukitawala kipindi chake cha mwisho na hivyo basi njia iliyokuwa rahisi ya chama cha KANU kurejea uongozini ilikuwa kwa kumuunga Kibaki mkono. Kutokana na

grafu jambo linalojitokeza waziwazi ni kudhihirika kuwa kulikuwapo na mitafaruku mingi vyamani katika kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2007 ikilinganishwa na vile mambo yalivyokuwa katika kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2013.

### 4. 3. 15 Hitimisho

Sehemu hii ilijikita katika kuangazia sehemu ya mada zilizoibuka katika kampeni za wanasiasa niliowateua ili kuufanikisha utafiti huu. Umuhimu wa kuzingatia mada katika usemi wa wanasiasa ulidhihirisha kuwa matukio yazungukiayo jamii huwa muhimu katika kubainisha usemi wa kisiasa kutoka kwa wanasiasa katika kipindi fulani. Lililobainika pia ni kuwa, mada zilizozungumziwa katika uchaguzi wa mwaka wa 2007 zilipata nafasi katika uchaguzi wa mwaka wa 2013. Kwa mujibu wa matumizi ya grafu, utafiti huu ulidhihirisha kuwa kulikuwa na kupunguka au kuongezeka kwa umaratokezi wa vile wanasiasa hao walivyoyazungumzia masuala ya mada hizo katika kampeni za chaguzi hizo mbili. Jambo jingine lililodhihirika ni kuwa, kulikuwa na mada zingine zilizoibuka, ikizingatiwa kuwa kulikuwapo na masuala mengine ya kihistoria yaliyozihusu jamii kwenye uchaguzi huo wa mwaka wa 2013. Kwa jumla, masuala yote yaliyozungumziwa na wanasiasa yalikuwa ya kihistoria na yalilengwa kulidhalilisha kundi moja dhidi ya kundi jingine na kulitukuza kundi moja zaidi ya jingine. Kulingana nao Lyenger na Magrady (2007) kwa mujibu wa kazi yao kuhusu kampeni zenye mashiko, wasomi hawa walisema kuwa haikujalisha hali ya wakati huo ya miktadha ya siasa ilikuwa vipi, elementi za kila wakati za kampeni huchangiwa na rekodi iachwayo na wagombeaji au vyama ambavyo huwa kwenye uongozi. Wasomi hao walizidi kusema kuwa wapigaji kura aghalabu hupendelea kuufanya uteuzi wao wa viongozi kwa kuegemea utendakazi wa awali wa viongozi hao dhidi ya wale wengine. Kwa mtazamo wao waliafiki kuwa hali ya maisha katika nchi huakisi sifa ya uzuri au ubaya kufungamana na uongozi wa awali katika nchi husika. Kurejelewa kwa mada za usemi na kutumiwa kwa grafu katika kuelezea uchanganuzi wa data ya utafiti kuliazimiwa kuisawiri picha ya chaguzi mbili kuwa mkabala lakini tofauti ikijidhihirisha kwa viwango vya kuzungumziwa kwa mada hiyo kutokana na rekodi ambayo huwa imeachwa na viongozi tangulizi serikalini. Matumizi ya grafu yalikuwa na mchango mwingine muhimu sana katika uchanganuzi wa data katika utafiti huu kwani grafu mseto zilidhihirisha kuwa, kihistoria matukio ya siasa huwa si tuli.

# SURA YA TANO

# UFASIRI, MJADALA NA MAELEZO

## 5. 1 Utangulizi

Sehemu hii ya uchanganuzi wa usemi wa kisiasa katika kampeni za urais nchini Kenya ilijikita katika kuibainisha mikakati ya usemi iliyotumiwa na wanasiasa niliokuwa nimewateua ili kuufanikisha utafiti huu. Mikakati iliyotumiwa na wanasiasa ilichunguzwa kama njia moja ya kuafiki ukweli kuwa wanasiasa huitumia mikakati ambayo kwa kiwango kikubwa huchochewa na mada mbalimabli. Baada ya kuijadili mikakati iliyotumiwa na wanasiasa hao kwenye kampeni, mtafiti aliweza kuzitathmini athari za usemi wa kisiasa ikizingatiwa kuwa kwa kawaida usemi wa kisiasa huwa na athari kwa njia moja au nyingine.

## 5. 2 Mikakati ya Usemi katika Mwaka wa 2007 na 2013

Mikakati ya usemi katika kampeni za urais katika vipindi vyote viwili ambayo mtafiti aliweza kulinganisha ilibainika kuwa wanasiasa hao watatu; yaani Raila Odinga, Uhuru Kenyatta na William Ruto waliitumia mikakati ya usemi kwa mujibu wa nadharia ya Usemi – Mkabala wa Kihistoria; Wodak (2001) huku wakiikita kwenye mada za usemi kama ilivyobainika (Rejelea 4.1 – 4.13). Mikakati hiyo ilikuwa Unominishaji/Urejelezi, Uarifishaji, Ubishi, Mkabala/Uhusishaji na Uongezaji na Upunguzaji wa Uzito (Rejelea 2.5 – 2.5.5). Utafiti huu ulibainisha kuwa wanasiasa hao waliitumia miondoko mingi halisi ya kisemantiki iliyodhihirisha kuwapo kwa ukinzani baina ya uwasilishwaji chanya wa kundi 'Letu' na uwasilishwaji hasi wa kundi 'Lao'. Mfano mzuri wa kielelezo hiki cha ukanusho ulikuwa Katao Dhahiri, 'Sina lolote dhidi ya..., lakini...' Hii ilikuwa miondoko muhimu sana iliyofanikisha mitazamo waliokuwa nayo wasikilizaji kuwahusu wazungumzaji (Wodak na van Dijk 2008). Wasomi hao walisema vile vile kuwa matumizi kama hayo ya lugha hutumiwa sana katika mazungumzo yazungukiayo masuala ya kikabila pamwe na mwingiliano wa makundi; mtazamo wao uliakisika katika utafiti huu. Mikakati iliyorejelewa katika uchanganuzi wa data ilikuwa:

1. Mkakati wa Unominishaji / Urejelezi
2. Mkakati wa Uarifishaji

3. Mkakati wa Uhusishaji/Mkabala

4. Mkakati wa Ubishi

5. Mikakati ya Uzidishaji na Upunguzaji wa Uzito

**5. 3 Mkakati wa Urejelezi/ Unominishaji katika Kampeni**

Mkakati wa Urejelezi ni mkakati ambao huhusika na namna mtu anavyotajwa na kurejelewa kilugha. Mkakati huu wa kwanza hulenga kujenga na kuwakilisha wahusika wa kundi fulani la kijamii. Ili kuyafanya maelezo ya mkakati huu kuwa bayana ni aula kusema kuwa mkakati wenyewe huwa kama picha ambayo hudokeza namna mhusika anavyotajwa ambapo tukio lenyewe huwakilisha usemaji na nafasi ya kundi husishwa na pia kundi lisohusishwa. Katika kampeni za urais miezi mitano kabla ya uchaguzi wa mwaka 2007 na miezi mitano kabla ya uchaguzi wa mwaka wa 2013, ilibainika bayana kuwa wanasiasa hao watatu waliitumia mikakati ya usemi ilyokuwa imekurubiana katika kampeni zao za urais. Vile vile, mada za usemi katika kampeni zao ziliingiliana sana ikawa kuwa, katika kila mada; kila mwanasiasa alikuwa anaivutia ngozi kwake kutegemea itikadi ya muungano wake na msimamo ulioegemewa kuhusu suala walilokuwa wakilizungumzia.

Mkakati wa urejelezi ulitokea kutumiwa sana na wanasiasa hao (Raila, Uhuru na Ruto) katika vipindi vyote viwili. Katika kampeni za 2007, miuungano ya ODM na ule wa PNU ulilitaja kundi lile jingine kama kundi lililokuwa limejengwa kwenye msingi wa kikabila na hivyo basi kuzua njia tofauti za kulirejelea kundi moja kuwa la kikabila. Katika gazeti la *Standard 15th December 2007* Raila Odinga aliurejelea ukabila akisema kuwa siasa za ukabila zilikuwa hazina budi kuzikwa; kulingana naye, kihistoria ukabila ulikuwa umekita mizizi katika uchaguzi wa kiti cha urais na hivyo basi njia ya kuuzika ukabila katika kaburi la sahau ilikuwa tu kuruhusu kiongozi mwingine kutoka katika kabila tofauti (Letu) kuwa rais wa Kenya. Mwananasiasa huyo alihoji ni kwa nini uongozi wa taifa hili uwe wa familia fulani tu (Hao), ilhali Kenya ilikuwa na makabila mengine. Itakumbukwa kuwa, Kenya ilikuwa imeunyakua uhuru wake kutoka kwa Serikali ya Mkoloni katika mwaka wa 1964 rais wake wa kwanza akiwa hayati Mzee Jomo Kenyatta ambaye aliaga dunia katika mwaka wa 1978 akiuacha uongozi wa taifa hili mikononi mwa rais mstaafu Daniel Moi ambaye alistaafu katika mwaka wa 2002 na kurithiwa na rais mstaafu Mwai Kibaki.

Kwa mtazamo wa wa kihistoria, Raila Odinga aliutumia mkakati wa urejelezi kama njia moja ya kuyahusisha makabila mengine ambayo yalikuwa yameambaaliwa na nafasi ya kuiongoza Kenya kuuafiki ukweli kuwa kihistoria walikuwa wametengwa na makabila ambayo tayari yalikuwa yamekwisha tawala, yaani – 'sisi' na 'hao'. Kama ilivyokwisha semwa mikakati hii hudhihirisha uongezaji wa uzito kwa upande mmoja na upunguzaji wa uzito kwa upande mwingine. Mikakati hii hufanikisha ufahamu wa nafasi ya kauli katika usemi kwa kuongezea au kupunguza uzito wa ilokusheni katika ubaguzi wa kiukoo, wanaopinga utaifa wa kisemitiki au usemi wa kikabila. Itakumbukwa kuwa mwanasiasa huyo alifahamu fika kuwa William Ruto alikuwa katika muungano wake na hivyo alipotokea kudai kuwa kila kabila lilikuwa lazima lipewe nafasi sawa katika harakati za kuwa rais alikuwa anautumia mkakati wa kuongeza nguvu na wakati huo huo kupunguza uzito anapotaja kuwa urais haukutengewa 'aila fulani' pekee; hapa mwanasiasa huyo alikwepa kitendo cha kuudhuru uso wa mshiriki wake na jamii nzima ya Kalenjin ilyokuwa inamuunga mkono na kuzielekezea lawama famila mbili, ile ya hayati Mzee Jomo Kenyatta na rais mstaafu Moi.

(96)

*We want to bury tribal politics and give every community equal chance to have a stub at the presidency. It should not be a reserve of certain families.*

Tunataka tuzike siasa za ukabila na kuipa kila jamii nafasi sawa ya kuwa rais; haiwezi kuwa urais umetengewa familia fulani tu.

Katika gazeti la *Nation 23rd August 2007* mwanasiasa huyo aliutumia mkakati huo zaidi kwa kuwarejelea mashujaa wa Kikuyu ambao kulingana naye; kihistoria, mashujaa hao hawakuingiwa na taasubi ya ukabila, na hivyo aliomba roho za mashujaa hao ziwashukie wale ambao hawakuwa wamewekwa huru kutokana na mitazamo yao hasi ya kikabila na kuingiwa na roho ya utaifa. Kurejelewa kwa mashujaa hao wa Kikuyu kulidhamiriwa kuisawiri picha pana kuwa viongozi hao mbali na kuwa walitoka Mkoa wa Kati walikuwa hawana chembechembe za ukabila kama vizalia waliokuwa ni tofauti na mashujaa hao. Kulikuwa na mashujaa kutoka katika makabila mengine kihistoria, lakini kulilenga kabila la Kikuyu kulitekelezwa kimakusudi ikiwa njia mwafaka kwa mwanasiasa huyo kuitenga jamii ya Kikuyu na jamii zingine.

*(97)*

*May the spirit of Waiyaki wa Hinga, Harry Thuku, Dedan Kimathi and J.M. Kariuki descend upon ethnic chauvinists who have not yet seen the light, and liberate them from their negative ethnicity, and imbue them with a new spirit of nationhood.*

Ni ombi langu kuwa walio na taasubi za ukabila washukiwe na roho za Waiyaki wa Hinga, Harry Thuku, Dedan Kimathi na J.M. Kariuki kwani hawajaona mwangaza, ili wanasuliwe kutoka kwa misimamo hasi ya kikabila na kujazwa na roho mpya wa uzalendo.

Mwanasiasa huyo aliyarejelea masuala ya kihistoria kuhusu kuondolewa kwa kabila la Kalenjin kutoka msitu wa Mau akidhihirisha kuwa yeye alikuwa akituhumiwa kimakosa kwani kihistoria aliyetenda hayo kwanza alikuwa rais mstaafu Moi akifuatiwa naye rais mstaafu Mwai Kibaki wakiwa naye hayati Waziri Michuki. Katika gazeti la *Daily Nation 1st October 2012,* suala hilo la kufurushwa kwa jamii ya Kalenjin kutoka Msitu wa Mau ni dhahiri. Mkakati huo ulitumiwa kama njia ya kuliweka wazi suala hilo la kihistoria. Kutajwa kwa jina 'Nyayo' ilikuwa njia ya kuwakumbusha kuwa aliyehusika kwanza alikuwa mmoja wao, yaani kiongozi kutoka kwa jamii yao. Kurejelewa kwa 'Rais Kibaki' na 'Hayati Waziri Michuki' ilidhamiriwa kuyafufua matumizi ya kiwakilishi 'sisi' na 'hao' na kudhihirisha kuwa aliyekuwa mzushi wa kero zao hakuwa yeye, bali mmoja wao na viongozi wengine kutoka kabila jingine.

*(98)*

*First it was Nyayo (retired president Moi) who first moved the people out of the forest, then president Kibaki together with the late minister John Michuki. Why should someone therefore think that I sent people to the camps?*

Aliyekuwa wa kwanza kuwaondoa watu kutoka kwenye msitu alikuwa Nyayo (rais mstaafu Moi) baadaye rais Kibaki wakiwa naye marehemu waziri John Michuki. Ni kwa nini basi mtu afikirie kuwa mimi niliwapeleka watu kwenye makampi?

Yumkini Raila alilitumia katao dhahiri kwa kuchochea kumbukumbu zao (Kalenjin) kwa njia ya 'upole' akionyesha kuwa 'nyayo' alikuwa ameziacha nyayo za kufuatwa na viongozi wa baadaye; hivyo, wa kulaumiwa kwanza alikuwa mmoja wao (Rais mstafuu).

Siku za mwanzo mwanzo wakati wa kuijenga miungano ilidhihirisha kuungana kwa vyama vingi, vingine vikitokea kutoiafiki miungano fulani fulani kwa sababu zilizotofautiana kifalsafa. Mwanasiasa huyo kwa upande wake alikuwa ameshakwisha amua chama alichokuwa ananuia kukitumia katika harakati zake za kukitafuta kiti cha urais nchini Kenya ambacho kilikuwa ni kile cha ODM katika mwaka wa 2007. Mkakati mmoja wa usemi alioutumia katika kukirejelea chama chake ni 'farasi' akitazamia kuibusha hisia za ushindani wa mnyama huyo anayejulikana kutokana na kasi yake katika mashindano ya kutimua mbio. Baada ya rais mstaafu Mwai Kibaki kukitangaza chama cha kisiasa ambacho angetumia katika pilkapilka zake za kuutafuta uongozi wa nchi ya Kenya kwa mara ya pili, mwanasiasa huyo alikidunisha chama hicho kwa kukirejelea kwa njia tofauti; katika gazeti la *Daily Nation 23rd September 2007* mwanasiasa huyo alinukuliwa akisema.

*(99)*

*President Kibaki has come with a mule instead of the horse they were promising.*

Rais Kibaki amekuja na punda badala ya farasi waliyekuwa wameahidi.

Nyumbu ni neno lililotumika kisitiari kwa kumrejelea mnyama ambaye kuzaliwa kwake hutokana na matokeo ya punda na farasi kujamiiana. Mwanasiasa huyo alikuwa akiuona muungano rejelewa kuwa kama 'nyumbu' ambaye hakuwa na uwezo wa kushindana vyema, hivyo basi akauona muungano wao kama muungano wa pekee uliokuwa na uwezo wa kushindana kikamilifu. Mwanasiasa huyo alitokea kuubadilisha mtazamo wake wa hapo awali wa kuurejelea muungano ambao mpinzani wake wa karibu rais mstaafu mheshimiwa Mwai Kibaki angeutumia kutoka kwa mnyama Nyumbu na kuuita 'kinyonga', yumkini alilenga kuirejelea tabia ya mnyama huyo ya kuibadilisha rangi yake pindi mazingira yake yalipomlazimisha; mtazamo wake uliashiria kuwa, chama cha PNU kilijumuisha vyama vingi. Vile vile itakumbukwa kuwa mnyama huyo alikuwa na mwendo ambao haukuwa wa kasi katika mazingira yoyote yale; hata yale yaliyohitaji kuepukwa kwa haraka kwa ajili ya hatari ambayo ingekuwapo.

*Sunday Standard 23rd September 2007, (100)*

*I told you the race will be between two horses. We gave you a horse named ODM but Kibaki has given us a chameleon…*

Niliwaambia shindano litakuwa baina ya farasi wawili. Tuliwaletea farasi ajulikanaye kama ODM lakini kibaki ametuletea kinyonga.

Suala la kuwa ushindani ulikuwa baina ya farasi wawili lilichipuka katika mwaka wa 2012; hili likifufua mtazamo aliokuwa nao katika mwaka wa 2007, alipourejelea muungano wa ODM kuwa ndio uliokuwa na uwezo wa kushindana. Katika mwaka wa 2012 mwanasiasa huyo alikuwa amebashiri kuwa ushindani ungewahusu farasi wawili; 'farasi – CORD' na 'farasi – Jubilee', wale wengine wangekuwa 'punda' tu. Urejelezi wa miungano kama 'farasi' ilikuwa istiari iliyodhamiriwa kuisawiri picha kuhusu miungano iliyokuwa inawavutia wafuasi wengi, ufuasi ambao ulikuwa ishara tosha ya kuelekeza kule ushindi ungeelekea. Katika gazeti la *The Standard 10th December 2012* maelezo yake ya urejelezi ni dhahiri.

*(101)*

*The battle would be between CORD and Jubilee. The rest are donkeys.*

Kinyang'anyiro kitakuwa baina ya *CORD* na Jubilee. Wale wengine wote ni punda.

Jedwali 4.1 lilitumiwa na mtafiti katika uchanganuzi wa usemi wa Raila kama kiashiria cha kuchangia kuisawiri misimamo yake Raila dhidi ya wapinzani wake katika vipindi hivyo viwili wakati wa kampeni. Raila odinga aliitukuza misimamo yake kwa njia chanya, huku akiidhalilisha misimamo ya wapinzani wake kwa njia hasi. Bila shaka uwasilishwaji chanya wa kundi 'LETU' ulidhamiriwa kuzitukuza itikadi za muungano wake Raila.

Jedwali 4.1 Baadhi ya Mitazamo Chanya na Hasi katika Usemi wake Raila 2007 na 2013

| **SISI** | **WAO** |
|---|---|
| Tunataka tuzike siasa za ukabila | walio na taasubi za ukabila |
| Uchaguzi wa mwaka wa 2013 utamaliza enzi ya uongozi mbaya | Makabila fulani ndiyo huteuliwa |
| Ni mimi tu ndiye ninayeweza kuliunganisha taifa | Wakiwagawanya watu katika misingi ya kikabila… |

| | |
|---|---|
| Nchi hii ni yetu sote | Viongozi wa Jubille wanafanya bidii kusambaza kuendeleza ukabila |
| Ni lazima Wakenya wavuke kutoka nchi ya utumwa | Serikali zote zilizotangulia hazijawapa suluhisho” |
| Mtu mmoja humuua mwingine kwa ajili ya kipande cha ardhi | Kuna mtu anayemiliki ardhi karibu mkoa mmoja |
| Madai kuwa Raila ataziharibu biashara za Wakikuyu | Baraza lake la mawaziri linajumuisha watu waliotuhumiwa kuhusika na sakata ya *Anglo-leasing* |
| Kati ya kondoo ukitarajia asiwashambulie | Ni kama kumweka fisi… |
| Mkataba wetu uliongozwa na Mungu | Kinyume na watu walioruhusu shetani kuwapatanisha |
| Umri si kitu bali ni nambari, uongozi ni maono | Unaweza kuwa na umri mdogo lakini uwe na maono hafifu |
| Ng’ombe yetu ilizaa… | Watu walio na kesi kotini hawawezi wakajukumishwa uongozi |
| **Sisi** hatujaifanya nchi hii kuwa fisadi | Watu wale wale walioigeuza nchi ya Kenya na kuifanya iwe miongoni mwa nchi zilizo fisadi zaidi duniani wameungana |
| Walikubali kuniunga mkono kwa sababu jamii hiyo ilinipenda | Wengine wanafikiria kuwa siwezi kwenda kwa jamii ya Kalenjin… |

Asili: Uchanganuzi wa Mtafiti (2015)

Kutuhumiwa kwake Uhuru Kenyatta na muungano wa ODM aliposema kuwa angemuunga mkono rais mstaafu Mwai Kibaki kulimfanya mwanasiasa huyo kuutumia

mkakati wa urejelezi kama njia moja ya kuzipuuzilia mbali tetesi kuwa kulikuwa na njama ya rais mstaafu Mwai Kibaki kumteua Uhuru Kenyatta kuwa naibu wa urais. Mwanasiasa huyo aliutumia mkakati huo kama njia moja ya kuibusha ukweli wa kihistoria kuhusiana na uteuzi uliokuwa ukisemwa kuwa ungefanyika. Katika gazeti la *The Standard 19th December 2007* mwanasiasa huyo alisema kuwa haingewezekana rais na naibu wake wateuliwe kutoka kabila moja. Kihistoria jambo hilo lilikuwa halijawahi kufanyika nchini Kenya kwani rais mtangulizi alikuwa amemteua hayati Jaramogi Oginga Odinga kama naibu wake wa urais baada ya Kenya kupata uhuru. Matumizi ya *sisi,* ilikuwa ikiashiria kuwa Wakenya wote kutoka miungano yote hawangeweza kuyaafiki maamuzi hayo yaliyokuwa kinyume cha ukweli, na yaliyotinga jitihada za kudhihirishwa kwa 'utu' kwenye ngazi za kiutawala.

*(102)*

*There is no way we are going to have a president and his deputy from the same tribe. It can never happen.*

Haiwezekani rais na naibu wake wakatoka katika jamii moja. Haiwezekani kabisa.

Katika gazeti lilo hilo Mwanasiasa huyo alishadidia ukweli huo kwa kuurejelea msimamo tangulizi wa kiutawala uliokuwa kama kumbukumbu ya kuusuta mtazamo uliokuwa unaegemewa na kundi hilo pinzani. Mwanasiasa huyo alionyesha kuwa kama jambo hilo lingewezekana, basi babake angekuwa ameashiria hilo katika uongozi wake, pia rais mstaafu Moi angetekeleza vivyo hivyo baada ya kukitamatisha kipindi chake na kumtawaza mmoja wa jamii yake kama mrithi wake. Katika gazeti la *Standard 26th November 2007* mtazamo wake ni wazi kuhusu suala hilo.

*(103)*

*If the arrangement was workable in Kenya, my late father Jomo Kenyatta would have handed over power to a Kikuyu. And similarly, retired president Moi would have done so to a fellow Kalenjin.*

Kama mpango huo ungeweza kufanya kazi nchini Kenya hayati baba yangu Jomo Kenyatta angemwachia Mkikuyu uongozi; Naye rais mstaafu Moi angefanya hivyo kwa Mkalenjin mwenzake.

Mkakati wa urejelezi ulitumiwa na mwanasiasa huyo aliyelirejelea tukio la kutemwa na washiriki wake katika chama cha KANU katika mwaka wa 2002 alipopendekezwa naye rais mstaafu Daniel Moi kuwa mgombeaji wa kiti cha urais kwa tikiti ya chama hicho. Mwanasiasa huyo alikuwa akililirejelea tukio hilo kama njia ya kuusuta muungano wa ODM uliokuwa umeakwa na viongozi wale waliomtema na kumuunga mkono rais mstaafu Mwai Kibaki na kuuona kuwa muungano wa 'wanafiki' waliokuwa na 'tamaa ya uongozi', yaani 'sisi si wanafiki', lakini 'hao ndio wanafiki'. Katika gazeti la *Sunday Standard 7th October 2007* alidhihirisha wazi kuwa mkakati wa urejelezi huwa na nafasi yake muhimu katika kampeni za kisiasa kama njia moja ya kuisawiri picha ya matukio ya hapo awali.

*(104)*

*They are power hungry and hypocritical by criticizing my move yet they abandoned me and supported Kibaki in 2002.*

Hawa ni watu walio na tamaa ya uongozi na unafiki kwa kuikashifu hatua yangu ilhali walinitenga na kumuunga Kibaki mkono mwaka 2002.

Mkakati wa urejelezi ulijitokeza katika kampeni za Uhuru Kenyatta alipojitosa kwenye harakati za kukigombea kiti cha urais wa Jamuhuri ya Kenya katika mwaka wa 2012. Mwanasiasa huyo alikumbusha kuwa katika mapigano ya baada ya kutangazwa kwa kura za urais Raila Odinga alikuwa na uwezo wa kuzuia kumwagika kwingi kwa damu ikiwa madai yake kuwa yeye alikuwa mpenda amani yangeweza kufumbatwa na Wakenya. Mkakati wa urejelezi unaotumiwa hapa ni 'nusu mkate' uliokuwa ukiirejelea serikali ya muungano iliyoitawala nchi ya Kenya baina ya mwaka wa 2008 na 2013. Sitiari ya nusu mkate ilitumiwa kwa mara ya kwanza pale Raila Odinga alikiri kuwa hangeweza kuwajumuisha washiriki wake wote katika muungano wa CORD katika kupata nyadhifa kwenye serikali hiyo ya muungano kwani alikuwa ameupata mkate nusu. Kutokana na maelezo hayo Uhuru Kenyatta aliutumia mkakati wa urejelezi kama njia moja ya kutia dosari usemi wake Raila Odinga ulioonekana kwenda kinyume na madai yake katika usemi wake wa kampeni; kulingana naye Uhuru Kenyatta kihistoria, mpinzani wake alidhamini uongozi kuliko amani aliyokuwa akisema aliithamini. Katika gazeti la *The Standard 19th February 2013* mtazamo wake Uhuru Kenyatta ni bayana.

*(105)*

*If Raila was a peace loving leader he would have stopped the 2007 post – election violence but only chose to plead for calm after he had been given half a loaf meaning he was interested in acquiring power.*

Kama Raila alikuwa mpenda amani angezuia vita vya baada ya uchaguzi wa 2007, lakini aliizungumzia amani baada ya kupewa serikali ya nusu mkate hii ikimaanisha kuwa alikuwa tu na haja ya kupata uongozi.

Uhuru Kenyatta aliyarejelea mapigano ambayo yalikuwa yakishuhudiwa kila baada ya miaka mitano na kuonyesha kuwa katika mwaka wa 2002 mambo yalikuwa kinyume kwani alikubali kuwa alikuwa ameshindwa kwenye uchaguzi naye rais mstaafu Mwai Kibaki. Mwanasiasa huyo alikuwa akilenga kuonyesha kuwa matokeo ya wanasiasa kuwatumia wananchi ndio yaliyochangia kutokea kwa mapigano ya kikabila kila baada ya miaka mitano; kulingana naye mwanasiasa huyo, ubinafsi wa wanasiasa ndio uliopelekea machafuko hayo yatokee. Katika gazeti la *The Standard 4th December 2012* mtazamo wake umeangaziwa.

*(106)*

*Every five years, Kenyans fight because leaders use them to ascend to power; but it is only in 2002 that Kenyans didn't fight because I conceded defeat.*

Wakenya hupigana kila baada ya miaka mitano kwa sababu viongozi huwatumia kupata uongozi; lakini ni katika uchaguzi wa mwaka wa 2002 tu ambapo Wakenya hawakupigana kwa kuwa nilikubali kushindwa.

Jedwali 4.2 lilitumiwa na mtafiti kama njia moja ya kuibusha kuwapo kwa mitazamo chanya ya kundi LETU katika usemi wake Uhuru katika kampeni za uchaguzi ule wa 2007 na 2013. Lengo lilikuwa kuonyesha kuwa usemi wa wanasiasa katika kampeni za urais huwa za ncha mbili ambapo upande mmoja hulenga kujitukuza na ncha nyingine hunuiwa kulidhalilisha kundi pinzani.

Jedwali 4.2 Baadhi ya Mitazamo Chanya na Hasi katika Usemi wake Uhuru 2007 na 2013

| **SISI** | **WAO** |
|---|---|

| | |
|---|---|
| Walinitenga na kumuunga Kibaki mkono mwaka 2002” | Walio na tamaa ya uongozi na unafiki |
| Mwaka wa 2002 Wakenya hawakupigana kwa kuwa nilikubali kushindwa | Aliizungumzia amani baada ya kupewa serikali ya nusu mkate |
| “… Raila amekuwa akinikashifu kuuhusu uongozi wa baba yangu Jomo Kenyatta | Kwani baba yake hakuwa naibu wa Rais katika serikali hiyo? |
| Tunayo idadi kubwa ya wapigaji kura… | Raila ayakubali matokeo pindi tu Jubilee itakapotangazwa kuwa mshindi |
| Ningali na umri mdogo na pia ningali na muda wa kung’ang’ania kiti | Tunataka yeye astaafu ili tushindane na watoto aliowazaa yeye |
| Simpingi kwa sababu ya kabila lake | Hakuna hata siku moja aliufungua mdomo wake akikashifu machafuko |
| Sisi si watu ambao hugombea tu kwa ajili ya kugombea… | Anaonyesha ishara za kutaka kuturejesha katika machafuko ya mwaka wa 2007 |
| Mimi nimelipatia suala hili muda ili kulitolea msimamo unaohitajika | Suala la ardhi ni nyeti mno lisilohitajika kufanywa siasa za soka |
| Tazama nyuso za wale walioko hapa mbele yenu kutoka muungano huu na uone wanawaakilisha nani… | Kuna watu wengine wanaosema kuwa mgombeaji kiti kutoka jamii ya Wakikuyu hastahili kuwa rais |
| Taifa linahitaji amani na utangamano na haliwezi kuongozwa na mhemko wa kisiasa | Tunatakiwa kuzuia hali ambapo mihemko ya mazimwi wa kisiasa inapata fursa |

Asili: Uchanganuzi wa Mtafiti (2015)

William Ruto aliyekuwa katika muungano wa ODM katika mwaka wa 2007 aliutumia mkakati wa urejelezi katika kampeni za chama hicho alipokuwa anampigia Raila Odinga 'debe' akiwa mgombeaji wa kiti cha urais. Mwanasiasa huyo alidai kuwa kulikuwa na 'Makabila yaliyokuwa kamilifu machoni mwa viongozi wakuu' ambayo alidai kuwa ndiyo yangepata kuteuliwa katika serikali. Kutaja kwake kuwa 'sasa ni wazi' kulidhihirisha kuwa mwanasiasa huyo alikuwa analirejelea jambo fulani lililokuwa limekita mizizi nchini japo halikuibuliwa waziwazi. Ikumbukwe kuwa kurejelewa kwa usemi 'makabila fulani' kulidhamiriwa kuonyesha kuwa kihistoria ukabila ulithaminiwa sana wakati wa kutekeleza uteuzi wa viongozi kwenye nyadhifa serikalini. Kauli iliyokuwa inashadidiwa na mwanasiasa huyo ilikuwa 'sisi' tunabaguliwa na 'wao'; hao ni viongozi wenye kudhihirisha ukabila, 'sisi' hatuna ukabila. Mtazamo huo ulikuwa dhahiri ikiwa usemi kwenye gazeti la *The standard 19th October 2007* utaegemewa.

*(107)*

*It is now clear that under this government, unless you belong to certain communities that are politically correct, you cannot land an appointment.*

Sasa ni wazi kuwa mtu hawezi kuteuliwa katika wadhifa wowote serikalini mpaka awe anatoka katika makabila fulani yaliyo na ushawishi wa kisiasa.

Mwanasiasa huyo (William Ruto), alikuwa mwanachama wa Kanu kabla kuhamia chama cha ODM katika uchaguzi wa mwaka wa 2007. Akikumbusha maelezo ya hapo awali ya 'wamiliki wa chama cha Kanu', mwanasiasa huyo alidhamiria kuurejelea mtazamo wake rais mstaafu Daniel Moi ambaye wakati mmoja alinukuliwa akisema kuwa chama cha Kanu kilikuwa na wenyewe. Kutokana na maelezo hayo aliurejelea mtazamo huo ambao kihistoria ni kama ulikuwa umedhihirishwa na wanasiasa fulani katika chama hicho kilichokuwa na historia ndefu katika nchi ya Kenya; katika gazeti la *Daily Nation 1st October 2007,* mwanasiasa huyo aliurejelea mtazamo wake rais mstaafu Moi alipokuwa anatazamia kukihama chama hicho kwani kulingana naye wenye chama walikuwa wamerejea chamani. Matumizi ya 'wenye' yalilenga kuashiria 'hao', wamiliki wa chama, kinyume chake kikiashiria kuwa, 'sisi', kuwarejelea kama 'maskwota' chamani.

*(108)*

*We have decided that since the original owners of the party have come back, then it's prudent for us to quit. We shall be making an announcement this week as to our next course of action.*

Tumeamua kuwa kwa sababu wenye chama asilia wamerejea, ni bora kwetu kughura. Sisi tutayafanya matangazo yetu rasmi juma hili kuihusu mipango yetu mipya.

William Ruto alilizungumzia suala la Kura ya Maoni kuihusu katiba ya Kenya iliyozinduliwa mwaka wa 2010 akimrejelea Raila Odinga aliyemtaja kama mtu aliyekuwa bado angali katika kumbukizi ya matokeo ya kura hiyo ya maoni. Suala hilo lilikuwa la kihistoria kwani itakumbukwa kuwa yeye Raila alikuwa akiiunga mkono katiba hiyo, ilhali Ruto alikuwa akiipinga. Kutokana na kushinda kwa upande ambao yeye Raila alikuwa akiunga mkono, alidokeza kuwa hiyo ilikuwa ishara kuwa mambo yangekuwa vivyo hivyo katika uchaguzi wa mwaka wa 2013. Katika gazeti la *Daily Nation 13th February 2013,* William Ruto alinukuliwa akitaja kuwa kulikuwa na mtu ambaye alikuwa amekwama katika siasa za Kura ya Maoni. Kumrejelea 'mtu' kulidhamiriwa kumtaja Raila, kukimaanisha 'wao' na kukengeushwa kwao na matokeo ya kura hiyo. Kwa upande wa pili, Ruto alijisawiri kama 'sisi', na kuwa walikuwa wameyaweka matukio hayo ya kihistoria nyuma na kuendelea na maisha.

*(109)*

*We are sorry that there is someone on the other side who is still in the referendum politics while Kenyans have moved on.*

Sisi tunamwonea huruma mtu fulani aliye upande ule mwingine kwani anaendelea na siasa za kura ya maoni kuihusu katiba, ilhali Wakenya wamepiga hatua mbele.

Kutokana na siasa za Kenya kuingiliwa na mataifa ya nje na kuonekana kana kwamba yalikuwa yakimuunga mkono Raila Odinga, William Ruto alitokea kuonyesha kutoridhika kwake kutokana na msimamo wa mataifa hayo alipoyasuta na kuyaambia yajitokeze kimasomaso na kusema kuwa yalikuwa yakimuunga mkono mwanasiasa huyo, kwani wao Jubilee hawakuwa na shida yoyote na msimamo huo. Katika gazeti la *Daily Nation 11th February 2013*, mtazamo wake mwanasiasa huyo ulikuwa dhahiri.

*(110)*

*These nations should stop playing about issues; they should come out openly and tell Kenyans that they are supporting Raila Odinga. We will not have a problem with that.*

Mataifa haya yanatakiwa yasitishe kuyachezea masuala mengine; hawana budi kusema waziwazi na kuwaelezea Wakenya kuwa wao wanamuunga mkono Raila Odinga, hatutakuwa na shida na jambo hilo.

Jedwali 4.3 lilitumiwa na mtafiti shabaha ikiwa kuchangia uwelewa wa kuwapo kwa mitazamo chanya na hasi katika misimamo ya Ruto katika kampeni za uchaguzi wa urais, itakumbukwa kuwa Ruto ndiye alikuwa mwanasiasa wa pekee kuzipiga kampeni zake akiwa katika miungano miwili tofauti na hivyo basi kuidhalilisha na kuitukuza miungano kwa kuongozwa na itikadi za chama alichokuwa anakienzi wakati huo.

Jedwali 4.3 Baadhi ya Mitazamo Chanya na Hasi katika Usemi wake Ruto 2007 na 2013

| **SISI** | **HAO** |
|---|---|
| Jina langu na la Raila liko kwenye Ripoti hiyo; Tunawezaje kuitekeleza… | Ripoti hiyo ilishinikizwa na maadui zetu |
| Sisi tulimuunga mtu huyo mkono katika uchaguzi uliopita | Mtu akikudanganya mara moja yeye ni mdanganyifu |
| Tunataka kuliunganisha taifa hili; tunataka kuwaleta Wakenya wote pamoja ili tuishi kwa amani | Wapinzani wetu wamekuwa wakieneza uvumi kuwa jamii hizi mbili haziwezi kupiga kura kwa ushirikiano |
| Sisi tunalenga kumpa kila mmoja hati miliki ili kusaidia katika kuimarisha uchumi | Wapinzani wetu wanazungumza tu kuhusu shida za ardhi |
| Hatutaki kuona hali ambapo mamilioni ya Wakenya ni masikini | Kuna mamilionea wachache. Tunataka tutembee pamoja… |

| | |
|---|---|
| Jamii ya Kimataifa imejitenga na uenezwaji wa propaganda hiyo". | Waliwatuma watu wengine kutushtaki na kesi zingine za ufisadi dhidi yetu |
| Katiba ilizinduliwa nchini na kuwa Wakenya wanaendelea mbele | Mabadiliko kutoka analogi kuelekea dijitali ni hatua ya polepole |
| Tumeamua kuwa…ni vizuri sisi tukihame chama hicho | Wamiliki asili wa chama hiki wamerudi |
| Tafadhali usiruhusu kura za Kaunti ya Baringo zizigawanye kura za Mkoa wa Bonde la Ufa | Chama cha Amani kimekuwa kikipata chini ya asilimia mbili |
| ODM inaamini katika ushindani wa ajenda | Sio kutumia silaha butu kama vile viongozi wengine wanavyohimiza |
| Wazee wameamua kuwa Mkoa wa Bonde la Ufa ni himaya ya ODM | Unapobishana na mzee, watu watakulaumu |

Asili: Uchanganuzi wa Mtafiti (2015)

Kama njia moja ya kudhihirisha kuwapo kwa matumizi ya masizitizo 'yetu' chanya na 'yao' hasi kwenye mkakati wa urejelezi, mtafiti aliyatumia majedwali matatu ya kila mwanasiasa (Rejelea majedwali 4.1, 4.2 na 4.3) ili kuwakilisha kauli kuwa matumizi ya nafsi tofauti tofauti kwenye usemi wa wanasiasa hao uliazimiwa na kundi moja kujitukuzia na kulishushia hadhi kundi lile jingine.

### 5. 4 Mikakati ya Uarifishaji

Kama ilivyodhihirika, mikakati hii hudhamiria aidha kutambulisha wahusika wa kijamii kwa njia ambayo huenda ikawa inazidisha au kupunguza namna wanavyosawiriwa kiunafiki au kwa kuthaminiwa kwa njia chanya au hasi, Reisigl na Wodak (2001). Mikakati hii haiwezi ikatenganishwa na mikakati ya unominishaji kwa urahisi. Kwa yakini, mikakati mingine ya urejelezi inaweza kuchukuliwa kwa njia mahususi kuwa mikakati ya uarifishaji, kwa kuwa utambuaji wa mikakati ya urejelezi huhusisha umaanishaji dhahiri na pia udokezaji wa maana kwa kuelezea wahusika wa kijamii kwa

njia ya kiunafiki au kwa kuwathamini. Barasa (2014), alimnukuu Chilton (2004) aliyekuwa amesema kuwa, mtazamo huo wote ungeweza kulinganishwa na kile Chilton alikiona kama hali ya uhalalishaji na uharamishaji. Katika utafiti huu mikakati hiyo ilitumiwa kuhalalishia au kukanushia mitazamo yao kama vyama au miungano katika vipindi hivyo vya kampeni.

Aswani na wenzake (2014:65) wamesema kuwa UHU huchukulia kuwa usemi huwa na maana katika kipindi maalum cha kihistoria na katika muktadha mahsusi, na kwamba mfumo wa kiuwezo huhalalishwa na itikadi za kundi mahususi katika jamii lenye kuhodhi uwezo na mamlaka. Wakimnukuu Wodak (2000), wanasema kuwa uchanganuzi kihistoria hutumiwa kwani ni mtazamo ambao hushirikisha maarifa mapana na ya kina kuhusu asili na usuli wa hali mbalimbali za kijamii katika misingi ya kidaikroniki, hususan mabadiliko mbalimbali yanayodokezwa katika tanzu mbalimbali za usemi kuhusu matukio na hali mbalimbali za maisha katika jamii husika. Mwelekeo ambao hulengwa kuelezewa na nadharia ya UHU ni bayana ambapo maelezo yote ambayo hulihusu kundi 'Letu' huwa chanya, ilhali maelezo kulihusu kundi 'Lao' huwa hasi. Uteuzi wa msamiati hulengwa kuisawiri picha chanya pale kundi 'Letu' hurejelewa na kuisawiri picha hasi pale kundi 'Lao' huwa linarejelewa.

Kulingana na mkakati huu wa Uarifishaji; mikakati ya unenaji au usemaji huweza kuwa katika kategoria kadhaa; baadhi yazo ni:-

1) Ujumuishaji.
2) Utatanishaji.
3) Uwekevishaji.
4) Ujenzi wa Siasa

Katika kampeni za chaguzi zote, wahusika wa kijamii walikuwa Uhuru Kenyatta, William Ruto na Raila Odinga. Matumizi ya mkakati huo wakati wa kampeni yalikuwa bayana kutokana na wanasiasa hao kutumia viwakilishi vya nomino kama njia moja ya kuashiria kuwapo kwa umoja katika kundi 'Letu' ambapo dhamira ikiwa kulisuta kundi 'Lao' aidha, dhamira ilikuwa kulisawiri kundi hilo kama ambalo lilikuwa haliendani na matarajio ya

wengi. Kwa jumla, matumizi ya mkakati huo yalidhamiriwa kutolea tathmini chanya ya kundi moja na kwa upande wa pili kutolea tathmini hasi ya kundi hilo jingine.

### 5. 4. 1 Ujumuishaji

Mkakati huu wa Uarifishaji husawirika bayana pale matumizi ya viwakilishi vya watu binafsi kama vile 'yetu', 'yao', 'mimi', 'sisi' na kadhalika kwenye matini hujitokeza. Kutumiwa kwa viwakilishi kama hivi huashiria umoja na utekelezwaji wa majukumu kwa kuzingatia ujumuishaji. Mkakati huo uliazimiwa kuwajumuisha wapigaji kura na Wakenya wote kwa jumla ambao kwa kiwango kikubwa waliwapelekea wanasiasa hao kuziegemea jamii zao na zile zilizodhaniwa ziliafiki itikadi zilizokuwa zinashikiliwa na miungano au vyama vya kila mwanasiasa aliyekuwa asili ya data katika utafiti huu.

Brummett (2008:1) akizungumzia masuala fiche ya kijamii; alisema kuwa maneno ambayo sisi husikia na kusema, ishara ambazo sisi hufanya au kuona, kwa kawaida hushesheni maana chungu mbovu, miingiliano, udokezaji, na hata mwangwi, lakini binadamu hukwepwa na kile ambacho huwa kinamaanishwa. Alizidi kusema kuwa masuala kama vile ya kisiasa hubeba jumbe fiche, mielekeo, au hata masuala ya kisiasa yaliyothibitishwa. Ili kufanikisha usemi wa kisiasa, jambo moja ambalo wanasiasa hufanya, hutumia mbinu mbadala za usemaji ili kulipa dai fulani la kijamii mashiko; kwa mfano wakati rais wa zamani wa Marekani George W. Bush alipoyataja mataifa ya Korea Kaskazini, Irani, na Iraqi kama "muungano wa uovu" (*axis of evil*) katika mwaka wa 2002 akiuhutubia Muungano wa Mataifa aliitumia sitiari iliyokuwa ya kihistoria na kuzua kumbukumbu ya Vita vya Pili vya Dunia wakati Ujerumani, Italia na Japani zilipojulikana kama "Muungano" (Brummett 2008:5). Nchini Kenya wanasiasa niliowarejelea walizitumia mbinu mbalimbali za usemaji kama vile, sitiari, balagha, tasifida, kinaya na kadhalika, kama ilivyobainishwa na utafiti huu.

Uhuru Kenyatta katika kampeni zake za kuwania kiti cha urais katika mwaka wa 2013 alitumia sitiari kama njia moja ya kumsuta mpizani wake Raila Odinga aliyekuwa amenukuliwa mara kadhaa akisema haikuwa sawa kwa mtu aliyekuwa anakabiliwa na mashtaka katika Mahakama ya Kimataifa ya Jinai huko Hague kuugombea urais; kwa sababu Kenya kama nchi ingewekewa vikwazo na nchi zingine na kuipelekea kutengwa

kiuchumi. Katika gazeti la *Daily Nation 24th January 2013* Uhuru Kenyatta akiutetea msimamo wake wa kukiwania kiti hicho aliwarejelea wananchi wa Kenya kama watu waliokuwa na akili razini kwani wangeweza kutofautisha bichi na bivu; kwa kusema kuwa nchi ya Kenya ilikuwa na upungufu wa watu wenye 'akili taahira', kwani ingetokea kuwa wangechaguliwa (Jubilee) basi Wakenya wenyewe wangekuwa wametia doa hatua yao ya kupelekwa huko Hague.

*(111)*

*…Kenya is not a banana republic.*

…Kenya si nchi ya watu wenye akili taahira.

Uhuru Kenyatta alilijumuisha taifa zima katika harakati zake za kuurejelea muungano wao (Jubilee) na Wakenya wote kwa jumla kama ambao walikuwa na akili tambuzi kinyume na vile walivyotazamwa 'nao', yaani, Raila na Wana CORD kwa jumla.

Mwanasiasa huyo alitia doa miondoko ya muungano wa CORD wa kwenda kinyume na hatua ya serikali ya kutafuta uwezekano wa kusukumwa mbele kwa kesi hiyo, pale Serikali ya Kenya ilipotekeleza Ushirikiano wa Kidiplomasia kupitia kwake naibu wa rais wakati huo Kalonzo Musyoka. Uhuru Kenyatta aliibuka na swali la balagha lililosheheni sitiari ya kibibilia akiuliza, 'ni wakati gani walishika njia kuelekea Damaski?'. Kibibilia, jina Damaski linapotajwa taswira ambayo huibuka ni ile ya Sauli akiwa njiani kuelekea mji huo ili kuwaadhibu Wakristo, tukio lililopekea Sauli kushukiwa na roho wa Mungu na kubadilishwa na kuwa mfuasi sugu wa imani aliyokuwa haiafiki. Hivyo basi, Uhuru Kenyatta aliuliza swali hilo kwa njia ya kijembe, akidhamiria kuwaonyesha wafuasi wake na nchi nzima kwa jumla kuwa muungano huo wa CORD ulikuwa ukifurahia hatua ya kiongozi huyo na mwenza wake kupelekwa Hague.

*(112)*

*When the government went out to convince the UN council over deferral, ODM wrote to say it wasn't party. When did they get on the road to Damascus?*

Wakati serikali ilipoamua kwenda kwa halmashauri ya Muungano wa Madola ili kuwarai waziunge mkono harakati za kuihairisha kesi, ODM

iliiandikia halmashauri hiyo wakisema kuwa hawangeliafiki wazo hilo. Ni wakati gani waliishika njia kwenda Damiski?

Matumizi ya 'serikali ilipoamua', ni kiwakilishi kilichokuwa kinatumiwa na mwanasiasa huyo kuisawiri picha ya harakati zilizokuwa zinatekelezwa na kundi fulani lililokuwa linawajali wananchi wake ambao walikuwa wanatuhumiwa kimakosa; lakini kukawa na kundi jingine lililokuwa na ajenda tofauti – ajenda iliyokuwa ikilenga kulizamisha kundi 'Lao'. Mwanasiasa huyo (Uhuru) aliwajumuisha wote waliokuwa kwenye muungano wa CORD kwa kuwaona kama watu waliokuwa wanafiki na ambao dhamira yao ilikuwa kuyaumbisha matarajio ya wanasiasa hao kwenye muungano wa Jubilee.

Sitiari hiyo ya kibibilia ilitumika vilevile kama njia ya kuukejeli msimamo wa mwanasiasa huyo pamwe na muungano wake wa CORD kuwa walikuwa wakidhamiria kuhakikisha kuwa kesi za viongozi hao wa muungano wa Jubilee zingerejeshwa nchini; katika gazeti la *The Standard 7th November 2012*, mwanasiasa huyo aliuliza, '…tangu lini Sauli akawa Paulo?', hiyo ilikuwa kejeli iliyodhamiriwa kusisitiza kuwa Raila Odinga hakuwa ameubadilisha msimamo wake hasi kuwahusu wawili hao.

William Ruto katika kampeni za mwaka 2007 alipokuwa katika chama cha ODM aliutumia mkakati huo wa Ujumuishaji, alipowajumuisha wale wote waliokuwa wakiwaunga mkono katika harakati zao za kukitwaa kiti cha urais, Raila akiwa mgombeaji wao wa kiti hicho. Kiwakilishi cha nomino ambacho mwanasiasa huyo alikitumia kilikuwa 'sisi', kilichowakilishwa na kiambishi 'tu' kwenye kitenzi '**tu**nataka' kukarabati mambo mengi. Mwanasiasa huyo alikuwa akiwahusisha wote waliokuwa wanakiunga mkono chama hicho na kuwatenga wale ambao kulingana na itikadi ya chama hicho walikuwa wamelemewa kufanya hivyo. Kwa upande mwingine, mkakati huo ulitumiwa na mwanasiasa huyo kama njia ya kudhihirisha umoja miongoni mwa viongozi katika chama hicho kilichokuwa na wafuasi wengi katika mkoa wa Bonde la Ufa na eneo la mashariki mwa nchi ya Kenya.

Akiiegemea Mada ya Uchumi, Ruto alionyesha kuwa mambo hayakuwa mazuri na yalihitaji kutengenezwa. Masuala kama hayo yagusiayo kudhoofika kwa uchumi na hali

ya kuwatamausha wananchi hujenga msingi wa kuvutia uungwaji mkono. Lyenger na Mcgrady (2007: 238), wamegusia suala kama hilo katika kazi yao kuhusu Miktadha ya Kisiasa dhidi ya Athari ya Kampeni; wamesema kuwa miktadha ya wakati huo huwa si hoja, suala muhimu ni rekodi ya mwanasiasa au hali ya chama wakati huo. Ruto alisema kuwa walitaka kukarabati vitu vingi ambavyo havikuwa vikifanya kazi vyema kama Kuzorota kwa usalama na umasikini.

*The Standard 2nd October 2007*

*(113)*

*We want to fix it, we want to fix so many things that are not working. Insecurity, poverty, we must fix it.*

Tunataka kukarabati, tunataka kuvikarabati vitu vingi ambavyo havifanyi kazi vyema; Kuzorota kwa usalama, umasikini, lazima tuukarabati

Matumizi ya kiwakilishi cha nomino '**tu**nataka' ilikuwa njia bora ya kuisawiri picha kuwa, waliokuwa na uwezo wa kuyafanya hayo walikuwa ODM, yaani kundi 'Letu', tukio hilo likisalia kuwa kama kejeli kwa kundi 'Lao', yaani PNU.

Raila Odinga pia aliutumia mkakati huo wa Ujumuishaji kwa kuurejelea muungano wa PNU kama muungano uliokuwa hauna uwezo wa kuyabatilisha mabadiliko yoyote ikizingatiwa kuwa viongozi wake walikuwa wale wale waliokuwa na historia ya kuipuja nchi ya Kenya. Katika kampeni za uchaguzi wa 2007, mwanasiasa huyo alinukuliwa akivitumia viwakilishi kadha vya nomino kama njia moja ya kuurejelea muungano huo wa PNU.

Mada ya usemi kuhusiana na uwajibikaji ilishamiri katika kampeni za urais ambapo Raila Odinga alilizungumzia suala hilo nyeti kwa ari kutokana na ukweli kuwa (kulingana naye) lilikuwa mwiba ambao ulikuwa umezitinga jitihada zozote za kuimarisha uchumi. Kulingana naye Raila Odinga, kihistoria; alidai kuwa rais wa Kenya wakati huo alikuwa haongozwi na falsafa ya kuufumbata ukweli kuwa uwajibikaji ulikuwa umezikwepa serikali zote za awali. Mwanasiasa huyo aliangazia kuwa wale watu waliokuwa wamechangia katika kuisambaratisha nchi ya Kenya kiuchumi walikuwa wameungana ili kuziendeleza ajenda zao. Kihistoria, kudorora kwa uwajibikaji kulikuwa kumesababishwa na kujukumishwa uongozini kwa viongozi ambao azma yao ilikuwa kujifaidi.

*Daily Nation 9th October 2007, (114)*

> *The very same men who turned Kenya into one of the most corrupt nations on the planet have united in the attempt to hold on to power once again so that they can continue enriching themselves and their friends.*
>
> Watu wale wale walioigeuza nchi ya Kenya na kuifanya iwe miongoni mwa nchi zilizo fisadi zaidi duniani wameungana ili kuhakikisha kuwa wamesalia katika mamlaka tena ili waendelee kujitajirisha pamwe na marafiki zao.

Matumizi ya viwakilishi 'watu wale wale' ilikuwa njia moja ya kulisuta kundi lake rais mstaafu Mwai Kibaki kama kundi lililokuwa na ajenda moja – ile ya kujifaidi. Mtazamo wao ulikuwa ukiazimia kuonyesha kuwa, 'kero' walizokuwa wakizipitia zilikuwa zinafufuliwa na kundi hilo 'Lao', lililokuwa halina budi kudondolewa kutoka kwenye uongozi wa nchi ya Kenya. Kiwakilishi '**wa**endelee' kilitumiwa kikiwa na lengo moja; kuonyesha kuwa ikiwa uchaguzi huo haungeliondolea mbali kundi hilo, basi matukio ya 'awali' yangeendelezwa na kundi hilo.

Tukio la Uhuru Kenyatta na William Ruto kushtakiwa katika mahakama ya Hague kulimpelekea Raila Odinga kuwajumuisha viongozi wa muungano wa Jubilee na kuwataja kama ambao hawangeweza kupewa mamlaka ya kuiongoza nchi ya Kenya. Raila Odinga alilisawiri kundi hilo kama ambalo lilikuwa 'mzigo', na kuwa 'Hao' wenye kesi walikuwa viongozi waliokuwa hawana maadili. Kwenye gazeti la *Daily Nation 6th February 2013*, mwanasiasa huyo alitumia kiwakilishi 'hao', sababu ikiwa moja – kuwatambulisha viongozi hao wa Jubilee kama ambao walikuwa na walakini.

### 5. 4. 2 Utatanishaji

Katika kampeni za urais katika chaguzi zote mbili, mkakati wa Uarifishaji ulitumiwa na wanasiasa kutoka katika makundi yote mawili kila kundi likilenga kulisawiri kundi moja kama ambalo lilikuwa likizua utata katika kutekelezekeka kwa masuala yote ambayo yangelifaidi taifa la nchi ya Kenya. Kundi moja lilitokea kujitukuza kama kundi lililokuwa na uwezo wa kuwaletea wananchi wa Kenya maendeleo chanya na kulisawiri kundi hilo jingine kama kundi lililokuwa halina uwezo wa kuyaafiki marekebisho chanya. Kila kundi lilikuwa likililaumu kundi lile jingine kwa kutokuwa na maono safi ya kuwafaa wananchi

kwa jumla. Wanasiasa hao walikuwa wakinukuliwa kwenye magazeti ya *'Daily Nation'* na *'The Standard'* wakiwa wanalimbikiziana lawama kwa kulionyesha kundi moja kama kundi lililokuwa linasababisha kutokea kwa shida katika nchi ya Kenya.

Katika kampeni za uchaguzi wa 2013 Raila Odinga aliirejelea bibilia na kuwazomea viongozi wa Jubilee akilenga kuwakosoa juu ya mtazamo wao kuhusu Jubilee kibibilia. Aliwauliza viongozi hao warejeshe mali waliyoiba kwani hiyo ndiyo iliyokuwa *kauli mbiu* ya Jubilee kwenye bibilia.

*The Standard 15$^{th}$ December 2012, (115)*

> *In the bible, Jubilee means 50 years and during this time, prisoners and thieves were freed while those who had stolen were asked to return, so we are asking our colleagues in the so called Jubilee Alliance are you ready to return property you have stolen?*
>
> Katika bibilia, Jubilee humaanisha miaka 50 ambapo katika kipindi hiki wafungwa hufunguliwa na wezi huachiliwa huru nao wale ambao wameiba huulizwa warudishe, kwa hivyo ninawauliza marafiki zetu katika muungano wa Jubilee, je mko tayari kurejesha mali mliyoiba?

Mwanasiasa huyo alikuwa amelenga kuisawiri picha ya 'wizi', wizi uliokuwa umetekelezwa na viongozi hao wa Jubilee. Mwanasiasa huyo alikuwa na ajenda moja – ile ya kuudhihirishia umma kuwa asili ya shida zao ilikuwa viongozi hao ambao walikuwa wameiba; tukio hilo liliwasawiri viongozi wakuu katika muungano wa Jubilee kwa mtazamo hasi – yaani, 'hao' walikuwa wezi, na kuwa ikiwa wangewachagua, wajue kuwa hao walikuwa wezi; na hilo halikuwa jambo zuri kwa taifa lililokuwa linalenga kuzika masuala ya utowajibikaji katika kaburi la sahau.

Mwanasiasa huyo alilisawiri kundi lao kama kundi lililokuwa tayari kuwatumikia wananchi wakiongozwa na maadili ambayo yangepatikana kutoka kwa muungano wa CORD ambao lengo lao lingekuwa kuyafanya mambo kwa usawa. Raila aliusawiri muungano wao kama ambao ulikuwa unaongozwa na maadili; na hivyo basi kuufanya kuonekana kuyaafiki mabadiliko chanya kwa jamii zote nchini Kenya. Katika gazeti la *The Standard 11$^{th}$ December 2012*, mwanasiasa huyo alinukuliwa akisema:

> *(116)*

> *In the bible, Joshua divided Cannans resources according to the 12 tribes of Israel and similary when we cross to Canaan next year, we will share this cake equitably among the 42 tribes.*
>
> Katika bibilia, Joshua aliigawanya mali ya Kanani kulingana na makabila 12 ya Israili na kwa njia hiyo hiyo tukiingia Kanani mwaka ujao, tutaigawanya keki hii sawa kulingana na makabila 42.

Matumizi ya mkakati huo wa Uarifishaji kwa kuonyesha kuwa shida zilizokuwapo zingetatuliwa nao, ilikuwa mbinu moja ya kuuvutia umma kwake kwa kuwafanya wapigaji kura kuona kuwa shida zilizokuwa zimeletwa na viongozi hao tangulizi zilikuwa zimepata wa kuzisuluhisha. Mwanasiasa huyo alikitumia kiwakilishi cha nomino '**tu**kiingia' akiazimia kuwajumuisha wote waliokuwa katika muungano huo wa CORD.

Kutokana na mataifa ya nchi za kigeni kuonekana kana kwamba hayakuwa yakiuafiki msimamo wa viongozi wa Jubilee kukipigania kiti cha urais nchini Kenya; Raila Odinga alitokea kumsawiri Uhuru Kenyatta kama mwanasiasa ambaye hangeweza kuliongoza taifa la Kenya kwa njia nzuri kutokana na kuwindwa kwake kama rais wa Sudan – Bashir (wakati wa kampeni za uchaguzi wa 2013). Katika gazeti la *The Standard 9th December 2012*, Raila Odinga alinukuliwa akihoji kuwa ingewezekana vipi kutawaliwa na watu waliokuwa wanawindwa kama alivyokuwa akiwindwa rais Bashir wa sudan?

*The Standard 9th December 2012, (117)*

> *How will you lead Kenya when you are wanted like Bashir, he cannot travel alot because if he lands in countries which are ICC signatories he will be arrested.*
>
> Utaiongozaje Kenya ikiwa unasakwa kama Bashir, hawezi akazuru nchi nyingi kwa sababu akiwasiri katika nchi ambazo ni wanachama wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai ya Hague atatiwa mbaroni.

Nukuu hiyo ilikuwa inaingiliana vyema na matukio ya kihistoria yaliyotokana na machafuko ya baada ya kutangazwa kwa kura za urais katika uchaguzi wa 2007. Tukio la usemi huo liliazimiwa kumsawiri Uhuru Kenyatta kama mhalifu na hivyo basi kuchaguliwa kwake kungefungamanishwa na tukio la Kenya kutawaliwa na rais 'mhalifu', na hivyo basi kuusawiri muungano wote wa Jubille kwa jumla kama ambao ulikuwa hauwezi kuitawala nchi ya Kenya kwa kutozingatia suala la uwajibikaji.

Uhuru Kenyatta kwa upande wake aliutumia mkakati huo wa utatanishaji kama njia moja ya kuonyesha kuwa mpinzani wake (Raila) alikuwa chanzo cha mtafaruku ambao ulishuhudiwa baada ya kura za urais kutangazwa katika uchaguzi wa 2007. Mwanasiasa huyo alikuwa akimsawiri Raila kama mnafiki ambaye alichangia kuzuka kwa mapigano ya mwaka wa 2008 kutokana na kutojihusisha kwake katika kuhubiri amani wakati wa machafuko hayo. Katika gazeti la *The Standard 19th February 2013;* nukuu yake Uhuru Kenyatta kuhusiana na tukio hilo ilikuwa bayana.

(118)

*If Raila was a peace loving leader he would have stopped the 2007 post – election violence but only chose to plead for calm after he had been given half a loaf meaning he was interested in acquiring power.*

Kama Raila alikuwa mpenda amani angezuia vita vya baada ya uchaguzi wa 2007, lakini aliizungumzia amani baada ya kupewa serikali ya nusu mkate hii ikimaanisha kuwa alikuwa tu na haja ya kupata uongozi.

Mwanasiasa huyo alikuwa akiisawiri picha ya Raila kama mtu ambaye alikuwa na azma moja, ile ya kukitwaa kiti cha urais nchini Kenya, na kuwa hakuwa mpenda amani kama alivyokuwa akijaribu kujisingizia. Uhuru Kenyatta aliendelea kuonyesha kuwa, viongozi nchini Kenya walikuwa wanawatumia wananchi ili kuyaafikia malengo yao, kinyume na vile walivyokuwa wakijionyesha. Katika gazeti la *The Standard 4th December 2012,* mtazamo wake uliashiria yale aliyokuwa akiyasema. Mwanasiasa huyo aliyarejelea mapigano ambayo yalikuwa yakishuhudiwa kila baada ya miaka mitano na kuonyesha kuwa katika mwaka wa 2002, mambo yalikuwa kinyume kwani (Yeye Uhuru) alikubali kuwa alikuwa ameshindwa kwenye uchaguzi naye rais mstaafu Mwai Kibaki. Mwanasiasa huyo alikuwa akilenga kuonyesha kuwa matokeo ya wanasiasa kuwatumia wananchi ndiyo yaliyochangia katika kutokea kwa mapigano ya kikabila kila baada ya miaka mitano; kulingana naye mwanasiasa huyo ubinafsi wa wanasiasa ndio uliopelekea machafuko hayo yatokee.

*(119)*

*Every five years, Kenyans fight because leaders use them to ascend to power; but is only in 2002 that Kenyans didn't fight because I conceded defeat.*

Wakenya hupigana kila baada ya miaka mitano kwa sababu viongozi huwatumia kupata uongozi; lakini ni katika uchaguzi wa mwaka wa 2002 ambapo Wakenya hawakupigana kwa kuwa nilikubali kushindwa.

William Ruto aliutumia mkakati huo wa utatanishaji kama njia moja ya kuyasawiri matukio katika kampeni za urais akiongozwa na itikadi na matarajio ya vyama na miungano kwenye kampeni za urais. Mwanasiasa huyo alikuwa amejumuika katika miungano miwili tofauti wakati wa kampeni za chaguzi za 2007 na 2013. Katika kila uchaguzi, aliusawiri utata uliofungamanishwa na kundi moja dhidi ya kundi jingine. Katika gazeti la *The Standard 5th November 2012,* Ruto alinukuliwa akiishikilia kataa yake ya kutoungana tena na Raila ambaye alituhumiwa kuwa alikuwa ameikosea sana jamii ya Kalenjin. Nukuu yake Ruto iliingiliana sana na tukio la kihistoria ambapo Raila alituhumiwa na jamii ya Kalenjin kutokana na kero chungu mbovu walizokuwa wamezipitia hata baada ya kumuunga mkono katika uchaguzi wa 2007. William Ruto alinukuliwa akisema kuwa walikuwa wamemsamehe lakini hangeweza kujiingiza katika muungano mwingine na mwanasiasa huyo kwani alikuwa ameuvunjilia mbali ushirikiano wake na mwanasiasa huyo.

*(120)*

*I am done with the PM. We would not go into a coalition with ODM. We can forgive him for the wrongs he has commited against us, but we would not vote for him again.*

Nimeukata uhusiano wangu na WM. Hatutaingia kwenye muungano na ODM. Tunaweza kumsamehe kwa mabaya aliyotufanyia, lakini hatuwezi kumpigia kura tena.

William Ruto alikuwa akiikumbusha jamii ya Kalenjin kuwa mtu huyo alikuwa amewazushia shida baada ya kuungana kwao katika uchaguzi wa mwaka wa 2007. Kulingana na mtazamo wa mwanasiasa huyo, asili ya shida nyingi za jamii hiyo zilichangiwa na kuingia kwenye ndoa kwa jamii ya Kalenjin na ile ya Wajaluo.

Katika mwaka wa 2007 William Ruto aliurejelea ukabila na kuusawiri kama utata au shida iliyokuwa inawakumba wananchi wa Kenya kutokana na kuendelezwa kwake na viongozi kwenye serikali iliyokuwa ikitawala kipindi hicho. Mwanasiasa huyo alilisawiri tukio hilo kama shida iliyokuwa siyo tu kwa jamii yake pekee, lakini pia kwa jamii zingine ambazo

zilikuwa hazijumuishwi kwenye uongozi wa taifa hilo. Mwanasiasa huyo aliuirejelea ukabila kuhusiana na uteuzi kwenye nyadhifa mbalimbali na nafasi za kazi katika mashirika ya Kiserikali alipoangazia kuwa kuteuliwa kwa mtu serikalini kulitegemea alikuwa ni wa kabila gani. Kwa mujibu wa mwanasiasa huyo, uteuzi serikalini uliegemezwa kwenye suala nyeti la ukabila.

*The standard 19th October 2007, (121)*

> *It is now clear that under this government, unless you belong to certain communities that are politically correct, you cannot land an appointment.*
>
> Sasa ni wazi kuwa mtu hawezi kuteuliwa katika wadhifa wowote serikalini kama yeye hajatoka katika kabila fulani.

Utafiti huu ulibainisha kuwa mkakati wa uarifishaji kufungamana na mitazamo miwili, ule wa ujumuishaji na utatanishaji uliegemewa na wanasiasa hao watatu dhamira ikiwa ni moja; kuhalalishia mitazamo iliyoshikiliwa na wanasiasa hao watatu ikiwa nukuu za usemi wao zitarejelewa. Utafiti huu uliafiki mtazamo kuwa, wanasiasa hao waliitumia mikakati hiyo kama njia moja ya kuuridhisha umma kuwa kila mmoja alikuwa na uwezo wa kuyatekeleza mambo ambayo yalikuwa na uwezo wa kuchangia kuendelea kwa hali za maisha za jamii husika. Kwa yakini dhamira kuu ilikuwa kulitukuza kundi moja na kulidhalilisha kundi hilo jingine.

### 5. 4. 3 Ujenzi wa Siasa

Reisigl na Wodak (2001:49-50), wameurejelea mkakati wa Uarifishaji kwa kuangazia mtazamo ambao waliuita ujenzi wa siasa, chini ya mitazamo kadhaa ambapo baadhi ya mitazamo hiyo na ambayo utafiti huu uliirejelea ilikuwa utaifa, utabaka, uundaji wa vyama, zahama, kuridhia au kunyimana haki ya kisiasa, kukawiza matukio ya kisiasa na kadhalika. Tukio la kufumbata utaifa katika kampeni za urais katika chaguzi zote mbili lilionekana kuegemewa na makundi yaliyokuwa yakiwakilishwa na wanasiasa ambao utafiti huu uliwaegemea ili kuipata data ya uchanganuzi. Raila Odinga alinukuliwa akilirai taifa la Kenya kuafiki ukweli kuwa kila kabila lilihitajiwa kuliongoza taifa la Kenya, na kuacha kuongozwa na siasa za ukabila. Katika gazeti la *Daily Nation 24th February 2013,* mwanasiasa huyo alinukuliwa akisema kuwa yeye alikuwa tofauti na wapinzani wake kwani alikuwa hawagawanyi Wakenya kwa kuzingatia misingi ya kikabila kama wapinzani wake kutoka muungano wa Jubilee. Mwanasiasa huyo alisema kuwa yeye

pekee ndiye aliyekuwa na uwezo wa kuwaunganisha Wakenya ikiwa msimamo wake wa kusema 'Kibaki Tosha' ungeweza kuzingatiwa.

> *(122)*
>
> *Compared to my rivals in Jubilee who have been dividing Kenyans along tribal lines, I am the only one who can unite the country. I have sacrificed a lot politically for the sake of this country. In 2002, I said Kibaki Tosha; not because he was a Kikuyu but because he is a Kenyan.*
>
> Ikilinganishwa na wapinzani wangu wa Jubilee ambao wamekuwa wakiwagawanya watu katika misingi ya kikabila, ni mimi tu ninayeweza kuliunganisha taifa. Nimejitolea sana kisiasa kwa ajili ya taifa hili. Katika mwaka wa 2002 nilisema Kibaki Tosha; si kwa sababu alikuwa Mkikuyu lakini kwa sababu alikuwa Mkenya.

Raila Odinga aliangazia umuhimu wa utaifa akitaja kuwa yeye pekee ndiye alikuwa ameonyesha utaifa huku wapinzani wake wakiyatumia makabila yao ili kuwawezesha kuutwaa ushindi. Wakati mmoja mwanasiasa huyo alikumbusha kuwa Kenya ilikuwa ya watu wote hivyo basi mawakala wa ukabila hawakuwa na lao kwani siku za kupiga kura kwa misingi ya *mtu wetu* zilikuwa zimepitwa na wakati.

Ujenzi wa siasa wakati wa kampeni uliegemezewa vyamani ambapo kila muungano ulijaribu kuusawiri muungano au chama chao kama kimojawapo kilichokuwa na uwezo wa kuwaunganisha wananchi wote katika nchi ya Kenya. Katika kampeni za 2012 – 2013 Raila aliusuta muungano wa Jubilee kwa kutokuwa na msimamo kinyume na vile muungano wa CORD ulivyokuwa. Alidai ya kwamba muungano wao ulikuwa muungano ulioongozwa na Mungu lakini ule wa Jubilee uliongozwa na shetani. Hili liliibuka pale viongozi wa Jubilee walituhumiwa kuwa waliubatilisha mkataba waliokuwa wameafikiana na kiongozi wa chama cha UDF Musalia Mudavadi. Raila aliuona muungano wa Ruto, Uhuru na Mudavadi kama ambao ulikuwa unaongozwa na mawakala wa shetani'

*Daily Nation 21$^{th}$ January 2013, (123)*

*Unlike guys who allowed the devil to mediate in their dealing with UDF presidential aspirant Musalia Mudavadi ours was guided by God and true principles that cannot be bent.*

Kinyume na watu walioruhusu shetani kuwapatanisha katika mkataba wao na mgombeaji kiti cha urais kwa tikiti ya UDF Musalia Mudavadi, mkataba wetu uliongozwa na Mungu, hivyo basi mapatano yetu hayatavunjwa.

Siku za mwanzo mwanzo wakati wa kuijenga miungano ilidhihirisha kuungana kwa vyama vingi, vingine vikitokea kutoiafiki miungano kwa ajili ya itikadi ya chama kimoja dhidi ya kingine. Raila Odinga katika harakati zake za kukitafuta kiti cha urais nchini Kenya; alikuwa anakitumia chama cha ODM katika mwaka wa 2007. Mkakati mmoja wa usemi alioutumia katika kukirejelea chama chake ni 'farasi' akitazamia kuibusha hisia za ushindani wa mnyama huyo anayejulikana kutokana na kasi yake dharura inapohitajika. Baada ya rais mstaafu Mwai Kibaki kukitangaza chama cha kisiasa ambacho angetumia katika pilkapilka zake za kuutafuta uongozi wa nchi ya Kenya kwa mara ya pili, mwanasiasa huyo (Raila) alikidunisha chama hicho kwa kukirejelea kwa njia tofauti; katika gazeti la *Daily Nation 23rd September 2007* mwanasiasa huyo alinukuliwa akisema.

*(124)*

*President Kibaki has come with a mule instead of the horse they were promising*

Rais Kibaki amekuja na punda badala ya farasi waliyekuwa wameahidi.

Nyumbu ni neno lililotumika kisitiari kwa kumrejelea mnyama ambaye kuzaliwa kwake hutokana na matokeo ya punda na farasi kujamiiana. Mwanasiasa huyo alikuwa akiuona muungano rejelewa kuwa kama 'nyumbu' ambaye hakuwa na uwezo wa kushindana vyema hivyo basi akauona muungano wao kama muungano wa pekee uliokuwa na uwezo wa kushindana kikamilifu.

William Ruto katika kampeni za uchaguzi wa 2007, alinukuliwa akikirejelea chama cha KANU kwa kudokeza azma yake ya kukigura chama hicho kutokana na kile alichokitaja kurejea kwa wenye chama hicho asili chamani; huo ulikuwa mtazamo ambao bila shaka uliashiria kujengwa kwa siasa vyamani, hali ambayo ilikuwa kudhihirika kwa kuwapo kwa mkakati wa uarifishaji. Katika gazeti la *Daily Nation 1st October 2007* mwanasiasa

huyo alinukuliwa akisema kuwa wenye chama walikuwa wamerejea… dhihirisho kuwa tabaka fulani ndilo lilikuwa linakimiliki chama hicho.

> *(125)*
>
> *We have decided that since the original owners of the party have come back, then it's prudent for us to quit. We shall be making an announcement this week as to our next course of action.*
>
> Tumeamua kuwa, kwa sababu wamiliki asili wa chama hiki wamerudi; ni vizuri sisi tukihame. Kwa hivyo; tutayafanya matangazo yetu kuhusu uamuzi wetu Juma lijalo.

Kulingana naye, kuhama kwake kuliashiria kuwa, yeye kama msemaji wa chama alikuwa amekihama chama na wafuasi wote (Wakalenjin); hiki kilikuwa kama kiashiria cha kuonyesha kuwa tabaka fulani katika KANU lilikuwa limeingia kwenye muungano na chama cha ODM chini ya uongozi wake Ruto. Tabaka hilo huenda lilikuwa la wafuasi waliokuwa wanyonge, ambao waliamua kuwaachia wafuasi waliokuwa na ushawishi mkubwa kusalia chamani.

### 5. 4. 4 Uwekevishaji

Mkakati wa uarifishaji kuhusiana na uwekevishaji uliibusha mambo kadha wakati wa kuichanganua data kuhusu usemi wa wanasiasa wakati wa kampeni za urais katika chaguzi hizo mbili. Wanasiasa hao walijisawiri kama wanasiasa waliokuwa wanaijali nchi ya Kenya na wananchi wote kwa jumla, kwa kuliweka suala la uchumi mbele na kuliegemezea kwenye matukio mengine ya kihistoria. Kutokana na yale yaliyoibuliwa na utafiti huu kama vile yalivyoangaziwa na makundi ya upinzani kwenye kampeni ni kuwa, serikali ilikuwa imezisahau jamii fulani fulani kwa kutoyashughulikia masuala fulani ambayo yalikuwa yamechangia katika kulemazwa kwa kuinuliwa kwa hali za 'jamii' hizo. Katika gazeti la *Standard 8th December 2007,* Raila Odinga aliyagusia masuala kadhaa yaliyohusiana na serikali yake rais mstaafu Kibaki kukosa kuyajali maisha ya raia wake. Kulingana na mwanasiasa huyo; kihistoria wananchi hao walikuwa wamesahauliwa kwa muda mrefu. Madai ya mwanasiasa huyo ni bayana katika nukuu kwenye gazeti hilo la mwezi wa Desemba:

> *(126)*

*This is an area with rich potential but you have been forgotten and I would like to assure you that I understand your problems ranging from roads, unexploited minerals and poverty*

Hii ni sehemu yenye uwezo mkubwa kiuchumi; lakini, mmesahauliwa na ningetaka kuwaahidi kuwa naelewa shida zenu kuanzia barabara, madini ambazo hazijachimbuliwa na kukithiri kwa umaskini.

Mada ya uchumi iliegemezewa mahitaji ya eneo pamwe na watu waliohusika; hivyo basi kampeni ililenga eneo na hadhira, kwani kila eneo nchini Kenya lilikuwa na mahitaji yake ya kimsingi. Mwanasiasa huyo alidai kuwa alikuwa amezifanya ziara nyingi sana nchini na kubaini kuwa Wakenya walikuwa wameamua kupiga kura ili kubadilisha maisha yao kwa sababu ya mizigo mikubwa ya ukosefu wa kazi, umaskini, ughali wa bidhaa za kimsingi na kupanda kwa kodi ya nyumba.

*Daily Nation 13th December 2007, (127)*

*My visits around the country show that Kenyans are determined to vote for change as they are tired of heavy burden for unemployment, poverty, high prices of basic commodities and rising house rent.*

Ziara zangu kote nchini zinaonyesha kuwa Wakenya wameamua kupiga kura ili kubadilisha maisha yao kwa sababu ya mizigo mikubwa ya ukosefu wa kazi, umasikini, ughali wa bidhaa za kimsingi na kupanda kwa kodi ya nyumba.

Mwanasiasa huyo alikuwa akijaribu kuyahalalisha madai yake kufungamana na itikadi za chama cha ODM kwa kuzirai jamii ambazo kulingana na vile maeneo yao yalivyokuwa yamesahauliwa kihistoria; hakukuwa na uwezekano wa hali zao kuimarika ikiwa serikali iliyokuwa ikiongoza haingebanduliwa na serikali nyingine kuutwaa uongozi wa taifa la Kenya. Mwanasiasa huyo alinukuliwa katika gazeti la *Daily Nation 11th January 2013* akiudhalilisha mwelekeo ambao ulikuwa umechukuliwa na wanasiasa fulani katika muungano wa Jubilee kwenye kampeni za mwaka wa 2013, ilipodaiwa kuwa endapo mwanasiasa huyo angeutwaa uongozi wa nchi ya Kenya, ilihofiwa kuwa angehakikisha kuwa biashara za Wakikuyu zingeharibiwa.

*(128)*

*Claims that Raila will destroy businesses owned by the Kikuyu is rubbish. I am a businessman and I understand what it means to build a business.*

Madai kuwa Raila ataziharibu biashara za Wakikuyu ni upuuzi mtupu, mimi ni mwanabiashara na ninaelewa fika gharama iliyopo ya kuifanya biashara isimame imara.

Katika kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2013, Uhuru Kenyatta alilirejelea suala la uchumi akilenga kuwavutia wapigaji kura kutoka kwa makundi yote, yale ya vijana na wanawake lengo likiwa moja, kudhihirisha kuwa kuimarishwa kwa maisha ya makundi hayo ilikuwa ishara nzuri ya kuimarika kwa maisha ya Wakenya kwa jumla. Katika gazeti la *The Standard 28th January 2013*, mtazamo wake mwanasiasa huyo ulikuwa dhahiri kuhusiana na yale wangefanya kama muungano wa Jubilee ikiwa muungano huo ungeutwaa uongozi wa nchi ya Kenya.

*(129)*

*Our focus is economic empowerment for the youth and women and not mere rhetoric our competitors have dwelt on.*

Lengo letu ni kuwapa vijana na wanawake uwezo wa kujikuza kiuchumi na sio kuongea maneno matupu kila wakati kama wanavyofanya wapinzani wetu.

Kila chama na miungano katika kampeni za urais katika chaguzi zote mbili ziliyarejelea masuala ya uchumi lengo likiwa kuyahalalisha maono na matamanio ya vyama vyao. Katika kampeni za mwaka wa 2007 kulikuwa na chama cha ODM na muungano wa PNU; na katika kampeni za uchaguzi wa kiti cha urais katika mwaka wa 2012 – 2013, miungano miwili mikubwa ilikuwa Jubilee na CORD. Kila kundi lilikuwa likiyahalalisha matarajio yake kufungamana na suala la uchumi na kuimarishwa kwa maisha ya wananchi kwa jumla.

### 5. 5 Mikakati ya Ubishi kwenye Usemi katika Kampeni za Urais

#### 5. 5. 1 Utangulizi

Akimnukuu Kienpointner (2005), Onyango (2007) anasema kuwa topoi au loki (kituo) ni kipengele cha uneni ambacho huweza kuelezwa kama sehemu ya mjadala iliyo wazi au yenye kauli inayoweza kuhitimishika. Msomi huyo akimnukuu Kienpointner (2005),

aliyekuwa amemnukuu Wodak (2001: 75) alisema kuwa, hayo ni maudhui yaliyo na ukuruba na yenye mahitimisho yenye utaratibu yanayoingiliana na mjadala au mijadala na madai katika mahitimisho; Kwa mfano, nchini Kenya kuna topoi za kutolea maana au fasiri ya jina kwa kitambulisho cha ukabila - "wageni". Kitambulisho hiki humaanisha kuwa kwa sababu hao ni "wageni tu" itabidi au ni lazima warudi sehemu zao za asili. Reisigl na Wodak (2001:70), walisema kuwa, mkakati huo wa ubishi vilevile hufumbata dhana ya upotoshaji, isiyosheheni ukweli. Katika sehemu hii ya ubishi, kanuni hubanangwa kwa kutazama mazungumzo kimantiki na kwa umakinifu wa kina. Ili kuufanikisha uchanganuzi wa data ya utafiti huu nadharia ya UMK na ubainishaji wa topoi ilitumiwa.

### 5. 5. 2 Matumizi ya Topoi katika Mkakati wa Ubishi

Kampeni za urais katika chaguzi za mwaka wa 2007 na za mwaka wa 2013 ziliyaweka makundi mawili kinzani katika hali iliyochangia kuibuka kwa matumizi ya topoi kwa kiwango kikubwa katika usemi wa wanasiasa ambao waliteuliwa na mtafiti. Wanasiasa hao walikuwa Uhuru Kenyatta, William Ruto na Raila Odinga, ambapo Uhuru na Raila walikinzana katika chaguzi zote mbili huku Ruto akijikuta katika pande mbili tofauti kwenye kampeni hizo za urais. Wanasiasa hao katika harakati za kuzifanikisha kampeni za miungano yao katika vipindi hivyo viwili walitumia topoi tofauti tofauti kama nyenzo za kuwanatia wapigaji kura na kuuboresha usemi wao wakati wa kampeni zao. Topoi zilizoteuliwa na wanasiasa hao zililenga kusisitiza uzuri wa kundi 'Letu' na kusisitiza ubaya wa kundi 'Lao'. Kutokana na kuwapo kwa nukuu nyingi za wanasiasa hao kwenye magazeti yaliyotumiwa; topoi zilizoteuliwa zilikuwa chache na tena hakukuwa na kanuni mahususi iliyoegemewa katika uteuzi huo (Rejelea 2.7.4).

### 5. 5. 3 Topoi za Ubaguzi

Onyango (2008:7) alisema kuwa, ili kuifanikisha Mikakati ya Ubishi uteuzi wa topoi huwa unatekelezwa kwa kuwa hiki huwa kipengele cha uneni ambacho huweza kuelezwa kama sehemu ya mjadala ambayo huwa wazi na inayoweza kuhitimishika. Nukuu yake anapomrejelea Kienpointner kwenye Wodak (2001:75) aliangazia kuwa kunazo topoi nchini Kenya zinazotumiwa kutolea maana kama kitambulisho cha ukabila; mfano mzuri ukiwa ule wa neno 'Wageni'. Maelezo haya yanatokea kuupata msukumo kutokana na

matumizi ya topoi katika kampeni za wanasiasa nchini Kenya katika mwaka 2007. Kwa mujibu wa Ripoti ya Waki ya mwaka wa 2008 matumizi ya topoi kama kiashiria cha Ugeni na Ukabila yalikuwa bayana kwani makabila yaliyoishi katika sehemu zilizoonekana kama za wenyeji katika Mkoa wa Bonde la Ufa zilitambuliwa kwa topoi zilizokuwa zinachora picha ya ugeni – ugeni wenye kusheheni uhasama uliokuwa umekolea.

Kulingana na matokeo ya Ripoti ya Waki topoi tofauti tofauti zilitumiwa na jamii ya Kalenjin katika Mkoa wa Bonde la Ufa kuirejelea jamii ya Kikuyu baadhi ya majina hayo yalikuwa, *Madoadoa, maharagwe, bunyot* (adui), *sangara (aina fulani ya nyasi)* kauli mbiu ya kipindi hicho ilikuwa sharti jamii hiyo ing'olewe. Topoi ya madoadoa ilitumiwa kama njia ya kuonyesha kuwa jamii ya Kikuyu ilikuwa imejipenyeza ndani kwa ndani na kuwa wamiliki wa mashamba ya jamii ya Kalenjin jambo ambalo kulingana nao halikuwa murua. Kuwapo kwa madoadao hayo kulionekana kama njama ya jamii ya Kikuyu ya kutaka kuufutilia mbali uwezo wa kiutawala wa jamii hiyo. Matumizi mengine ya majina yalikusudiwa kudhihirisha kuwa kuwapo kwa jamii hiyo baina yao ilikuwa si jambo zuri, ndio maana wakaibusha visawe vya kuisawiri jamii hiyo kama adui ambaye kuondolewa kwake ilikuwa dawa mjarabu.

Katika kampeni za Raila Odinga kwenye kampeni za chaguzi zote mbili, ilidhihirika bayana kuwa topoi za 'ubaguzi' zilijitokeza kwenye kampeni zake, kwani Mwanasiasa huyo alikuwa akiisawiri picha pana ya kubaguliwa kwa jamii zingine katika harakati za jamii hizo kuutwaa uongozi wa taifa la Kenya. Kama ilivyosemwa na Doane (2006), (Rejelea 4. 3.1)… ushindani wa kisiasa hutekelezwa kwa njia ya usemi wa ubaguzi wa rangi ambao alikuwa ameuelezea kama mkusanyiko wa matini na usemi wa kijamii kwa kuzingatia matukio ya ubaguzi wa rangi. Raila Odinga aliliangazia suala la ubaguzi kwa kulioanisha na kuchaguliwa kwa jamii nyingine kama rais ili kuchangia nafasi ya kuuzika ukabila. Nukuu yake katika gazeti la *The Standard 15th December 2007* ilihodhi usemi wa mwanasiasa huyo uliokuwa ukionyesha kuwa ubaguzi ulikuwa hai kulingana naye Raila.

(130)

*We want to bury tribal politics and give every community equal chance to have a stub at the presidency. It should not be a reserve of certain families.*

Tunataka tuzike siasa za ukabila na kuipa kila jamii nafasi sawa ya kuwa rais; haiwezi kuwa urais umetengewa familia fulani tu.

Katika kazi yake Onyango (2008) tukio la kuwapo na ubaguzi wa kikabila nchini Kenya baina ya makabila mawili ilidhihirika kwani msomi huyo alikiri kwamba jumbe nyingi za kubaguana baina ya jamii kadhaa nchini Kenya zilitekelezwa sirini kwa njia ya rununu. Katika kampeni za mwaka huo wa 2007, Raila Odinga aliwarejelea mashujaa wa jamii ya Kikuyu akiomba kuwa roho za mashujaa hao ziwashukie wale bado walikuwa wanaongozwa na roho ya ukabila nchini Kenya. Sababu za mwanasiasa huyo kuwarejelea viongozi wa jamii ya Kikuyu ilikuwa dhahiri; alikusudia kuisuta jamii hiyo ambayo aliiona kama iliyokuwa inaendeleza ukabila. Mtazamo huo unao mashiko ikizingatiwa kuwa nchini Kenya kulikuwa na mashujaa wengine kutoka katika jamii zingine nchini Kenya; hivyo basi uteuzi wake wa kabila la Kikuyu lilikuwa tukio la kimakusudi. Katika gazeti la *Nation 23rd August 2007* nukuu yake ni dhahiri. Picha ambayo mwanasiasa huyo alikuwa akiisawiri ni kuwa; kihistoria kulingana na mtazamo wake, mashujaa hao hawakuwa na ukabila kama vizalia vyao.

*(131)*

*May the spirit of Waiyaki wa Hinga, Harry Thuku, Dedan Kimathi and J.M. Kariuki descend upon ethnic chauvinists who have not yet seen the light, and liberate them from their negative ethnicity, and imbue them with a new spirit of nationhood.*

Ni ombi langu kuwa walio na taasubi za ukabila washukiwe na roho za Waiyaki wa Hinga, Harry Thuku, Dedan Kimathi na J.M. Kariuki kwani hawajaona mwangaza, ili wanasuliwe kutoka kwa misimamo hasi ya kikabila na kujazwa na roho mpya wa uzalendo.

Katika kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2013 Raila Odinga alinukuliwa akiusuta Muungano wa Jubilee kutokana na kile alichokiona kama hatua ya wapinzani wake kuwagawanya Wakenya kwa misingi ya kikabila. Alikumbusha kuwa yeye alikuwa amedhihirisha kuwa hakuwa mkabila kwani alitokea kumuunga rais mstaafu Mwai Kibaki mkono hapo awali katika uchaguzi wa mwaka wa 2002. Katika gazeti la *Daily Nation 24th February 2013,* mwanasiasa huyo alinukuliwa akisema kuwa yeye alikuwa tofauti na wapinzani wake kwani alikuwa hawagawanyi Wakenya kwa kuzingatia misingi ya

kikabila kama wapinzani wake kutoka muungano wa Jubilee. Mwanasiasa huyo alisema kuwa yeye pekee ndiye aliyekuwa na uwezo wa kuwaunganisha Wakenya ikiwa msimamo wake wa kusema 'Kibaki Tosha' ungeweza kuzingatiwa (Rejelea 4.3.1).

Uhuru Kenyatta ambaye alikuwa akikiwania kiti cha urais kwa mara ya pili nchini Kenya katika uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2013 alilizungumzia suala la ubaguzi akiuchukua msimamo wa kulihalalisha tukio lake la kuwania kiti cha urais kama uamuzi uliokuwa unazingatia sheria kwenye katiba ya nchi. Maelezo yake yalikuwa yakilenga kuyapuuzilia mbali madai yaliyokuwa yanasambazwa na wapinzani wake. Katika gazeti la *The Standard 16th November 2012* mwanasiasa huyo akiwakemea wale waliokuwa wakisema kuwa haikuwa sawa kwa Mkikuyu kukigombea kiti cha urais; alitaka kujua ikiwa katiba ya Kenya ilikuwa na kipengele kama hicho. Uhuru Kenyatta aliirejelea Katiba na kusema kuwa kila mtu nchini Kenya alikuwa na haki zake za kikatiba kuuwania uongozi wa urais na kuwa hakuna yeyote ambaye angezuiwa kutekeleza haki yake hiyo ya kikatiba.

> *(132)*
>
> *There are people who say that someone from the Kikuyu community should not become the president. Where is that written in the constitution? Everybody has a right to vie as well as elect whoever he likes.*
>
> Kuna watu wengine wanaosema kuwa mgombeaji wa kiti kutoka jamii ya Wakikuyu hastahili kuwa rais. Jambo hilo limeandikwa wapi kwenye katiba? Kila mtu ana haki ya kugombea na vilevile anaweza kumchagua yeyote ampendaye.

Wakati mmoja Uhuru Kenyatta aliyapuuzilia mbali maelezo kuwa muungano wa Jubilee ulikuwa wa kikabila kwa kuhoji kuwa waliokuwa wamesimama naye katika hafla moja ya kampeni walikuwa wanasiasa kutoka makabila mengine ikiwa wale waliokuwa na mawazo hayo wangeweza kuwatupia macho na kuona walikuwa wakiwawakilisha nani.

*Daily Nation 6th January 2013, (133)*

> *Look at the faces at the forefront of the alliance and see who they represent.*
>
> Tazama nyuso za wale walioko hapa mbele yenu kutoka muungano huu na uone wanawaakilisha nani.

William Ruto aliuzungumzia ukabila akisema kuwa waliodhania kuwa makabila mawili; yaani, Wakikuyu na Wakalenjin hawangeweza kuungana na kupiga kura kwa kushirikiana walikuwa hawajui walilokuwa wakilisema kwani kulingana naye ajenda yao muhimu ilikuwa ni kuwaunganisha wananchi wa Kenya. Mwanasiasa huyo alikuwa akilenga kuyapuuzilia mbali madai ya kuwapo kwa ubaguzi wa kikabila katika muungano wa Jubilee.

*The Standard 3rd December 2012, (134)*

> *Our opponents have been peddling lies that the two communities will never vote together. We are set to disapprove that this time around. We want to reconcile this country; we want to bring all Kenyans together so that we live in peace.*
>
> Wapinzani wetu wamekuwa wakieneza uvumi kuwa jamii hizi mbili haziwezi kupiga kura kwa ushirikiano; lakini, tutadhihirisha kuwa uvumi huo hauna nafasi wakati huu. Tunataka kuliunganisha taifa hili; tunataka kuwaleta Wakenya wote pamoja ili tuishi kwa amani.

Akimsuta Raila; Ruto aliikumbusha jamii yake kuwa kutokana na kumuunga mwanasiasa huyo mkono katika uchaguzi wa 2002, wao walikuwa wamesalia kuwa nje ya serikali kwa jumla ya miaka kumi; hili aliliona kama jambo ambalo lilisababishwa naye Raila Odinga ambaye walikuwa wameuunga ugombeaji wake wa urais mkono.

*The Standard 6th November 2012, (135)*

> *We supported that man in the last elections but we are now telling him bye. We have been in the opposition for 10 years because of his Kibaki Tosha slogan. If someone cheats you once, he is a liar, but when you are cheated for the second time, you become a fool yourself.*
>
> Sisi ndio tuliomuunga mtu huyo mkono katika uchaguzi uliopita, lakini sasa tunamwambia kwaheri. Tumekuwa nje ya serikali kwa jumla ya miaka 10 kwa sababu ya kauli mbiu yake ya Kibaki Tosha. Mtu akikudanganya mara moja yeye ni mdanganyifu, lakini akikudanganya mara ya pili, wewe utakuwa mpumbavu.

Mwanasiasa huyo wakati mmoja aliwasuta wale waliokuwa wakidhania kuwa jamii moja haingefanya kazi na jamii nyingine kuyasahau hayo kwani uchaguzi haungeegemezwa

kwenye misingi ya ukabila bali ungeegemezwa kwenye misingi ya shida zilizokuwa zikiwakumba Wakenya na namna shida hizo zingetatuliwa. Usemi wake ulikuwa ukiazimia kuusisitiza ubaya uliokuwa ukitekelezwa na muungano wa CORD kutokana na uwezekano wa kukoleza mielekeo ya ubaguzi.

*The Standard 25th December 2012, (136)*

> *If our competitors think this election will be defined by ethnicity, they are damn wrong. This poll will be defined by problems facing 40 million Kenyans and solutions for these problems.*
>
> Ikiwa wapinzani wetu wanafikiria kuwa uchaguzi huu utaamuliwa kwa misingi ya ukabila, wamekosea sana. Uchaguzi huu utaamuliwa kwa misingi ya shida zinazowakumba Wakenya milioni 40 na namna shida hizo zitakavyotatuliwa.

**5. 5. 4 Topoi za Hila/Wizi katika Upigaji Kura**

Raila Odinga aliuzungumzia wizi wa kura wakati wa uchaguzi mkuu akiurejelea mkakati wa Ubishi akiushirikisha na tukio la matumizi ya hila katika upigaji kura kutokana na hatua ya serikali kuwabadilisha wahudumu katika Tume ya Uchaguzi ya Kenya iliyofutiliwa mbali. Katika gazeti la *Sunday Standard 14th November 2007,* mwanasiasa huyo alimwelekezea rais mstaafu Mwai Kibaki kidole cha lawama akimwambia kuwa asisubutu kufanya hila katika uchaguzi mkuu wa mwaka huo kwani angekumbana na upinzani mkali ambao kihistoria haukuwa umeshuhudiwa nchini Kenya.

> *(137)*
>
> *If Kibaki tries rigging this poll, he will see the kind of opposition he has never seen in his life. But even if he does that we will still beat him.*
>
> Ikiwa Kibaki atajaribu kufanya hila katika uchaguzi huu, atakabiliwa na upinzani ambao hajapata kuona katika maisha yake. Lakini, hata kama atafanya hivyo bado tutamshinda.

Kutokana na nukuu hii, ni dhahiri kuwa lililosawiriwa na topoi, 'kufanya hila katika uchaguzi' ni kuwa 'Wizi' ulikuwa utekelezwe na 'Kibaki' kwani hangeweza kuibuka kuwa mshindi bila ya wizi wa kura kufanywa. Kuwapo kwa mitazamo ganda katika hali kama hizo ni wazi, ikikumbukwa kuwa kila pale neno wizi linapotajwa nchini Kenya

jamii ya Kikuyu huhusishwa na jambo hilo. Usemi huo bila shaka ulitokana na mawazo ya awali kihistoria ambapo rais wa awali Moi alikuwa ametuhumiwa kuwa alikuwa akiiba kura. Topoi ya 'uasi' ni dhahiri kutokana na nukuu hiyo, ikizingatiwa kuwa mwanasiasa huyo alivitumia viangaza mbele kuashiria kuwa vitendo vya kifidhuli kama ishara ya kutoyaafiki matokeo yangeshuhudiwa, hata hivyo mwanasiasa huyo anaupunguza ukali katika usemi wake na kudai kuwa hata kama hila katika upigaji wa kura ungeshuhudiwa, ushindi ulikuwa tayari ni wao.

Topoi kufungamana na wizi ilijitokeza tena katika kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2013 ambapo mwanasiasa huyo alikirejelea kipindi chote cha kampeni na hatimaye upigaji wa kura kama 'ng'ombe' aliyekuwa amezaa na ndama wake kuibwa na mbwa. Topoi ya 'ndama' iliusimamia ushindi – urais wa nchi ya Kenya. Kwa kawaida ng'ombe akijifungua ndama na ikatokea kuwa kuna mbwa karibu, basi yule ndama huenda asifanikiwe kuishi. Topoi ya 'mbwa' imetumika kumrejelea Kibaki na washiriki wake ambao wanasawiriwa kama mbwa kwa kuwa; kwa mujibu wa mwanasiasa huyo alikuwa ametendewa kitendo kibaya cha ng'ombe kuibiwa ndama wake. Mtazamo wa mwanasiasa huyo ni wazi katika nukuu kwenye gazeti la *The Standard 22nd February 2013* ambapo nukuu yake iliangazia tukio la awali.

(138)

Si mnajua ng'ombe yetu ilizaa na ndama ikaliwa na mbwa.

Ruto alilizungumzia suala la wizi wa kura kwa kuuomba muungano wa CORD kuyakubali matokeo ya uchaguzi baada ya kupigwa kwa kura tarehe 4 Machi 2013; na kuwa haikuwa na haja kwao kukengeushwa na matokeo ya kura ya maoni kuhusu katiba mpya iliyokuwa imezinduliwa katika mwaka wa 2010. Ruto alidokeza kuwa walishang'aa kuona kuwa bado kulikuwa na mtu ambaye alikuwa amesalia katika siasa za kura ya maoni kuihusu katiba, ilhali Wakenya walikuwa wanaendelea na shughuli zao.

*Daily Nation 13th January 13, (139)*

> *On March 4 we are asking them that if they lose elections – that if Kenyans decide that it is Jubilee – they should be ready to accept defeat. We are sorry that there is someone on the other side who is still stuck in the referendum politics while Kenyans have moved on.*

> Tunawaomba wakubali matokeo ya uchaguzi tarehe 4 Machi – yaani ikiwa Wakenya wataamua kuwa ni Jubilee – ni lazima wawe tayari kukubali matokeo. Tunashang'aa kuona kuwa kungali kuna mtu ambaye amesalia katika siasa za kura ya maoni kuhusu katiba ilhali Wakenya wanaendelea na shughuli zao.

Katika uchaguzi wa mwaka 2013 tetesi nyingi zilizozungukia suala nyeti la kihistoria kuhusu udanganyifu wakati wa upigaji wa kura lilijikuta kwenye jukwaa la Uhuru pamwe na wakereketwa wao na kumchochea kulizungumzia suala hilo na kulipuuzilia mbali. Uhuru Kenyatta alimsuta mpinzani wake kwa madai kuwa serikali ilikuwa imepanga kuiba kura kwa kuwatumia wakuu wa taarafa na machifu, akikumbusha kuwa Raila Odinga alikuwa akilenga kuwarejesha watu katika hali iliyokuwapo katika mwaka wa 2007.

*The Standard 25$^{th}$ February 2013, (140)*

> *He (Odinga) has claimed recentry that the provincial administration was being used to rig the elections among other outrageous claim. He is showing signs of wanting to pull us towards the 2007 troubles.*
>
> Yeye (Odinga) alisema hivi karibuni kuwa wakuu wa taarafa na machifu wanatumiwa ili kusaidia katika wizi wa kura na kufanya mambo mengine mabaya. Anaonyesha ishara za kutaka kuturejesha katika machafuko ya mwaka wa 2007.

Katika chaguzi zote mbili topoi kuhusiana na wizi na hila katika uchaguzi ilikuwa kama mwangwi wa usemi kutokana na kujikariri kwa suala hilo kila baada ya miaka mitano nchini Kenya. Kutokana na tukio hilo la kujikaririkariri kwa usemi wa wizi wa kura; uwezekano mkubwa upo wa topoi kuhusiana na wizi wa kura kusalia katika masikio ya wananchi nchini Kenya kwa miaka mingi. Kwa ufupi, mada ya usemi kuhusu wizi wa kura huenda isife siku za hivi karibuni.

### 5. 5. 5 Topoi za kutahadharisha

Usemi mwingi uliotumiwa na wanasiasa hao watatu ulizibeba chembechembe za kuwatahadharisha wapigaji kura na Wakenya kwa jumla. Katika kampeni za urais za mwaka wa 2007 na 2013, usemi wa wanasiasa hao ulikuwa ukilenga kusisitiza uzuri wa kundi moja na kusisitiza ubaya wa kundi hilo jingine. Kusisitizwa huko kama kulikuwa

chanya au hasi kuliegemezewa itikadi ya makundi hayo. Topoi za kutahadharisha zilitumiwa na Raila akiyarejelea matukio mengi kihistoria; mbinu hiyo ilidhamiriwa kulisisitiza jambo fulani na hata kumhusisha msikilizaji katika jambo lililojadiliwa. Usemi katika kampeni za urais nchini Kenya ulisheheni maswali chungu mbovu ya balagha yaliyotumika kimakusudi kama chambo cha kumvutia na kumhusisha mpigaji kura na mwananchi wa Kenya kwa jumla ili aweze kuhisi maono ya mwanasiasa huyo (Ugeuzi – nafsi).

Katika kampeni zake nyingi Raila Odinga alitumia topoi kwa mapana na marefu akidhamiria kwanza, kuwashirikisha wafuasi wake katika maono aliyokuwa nayo, pili, kama njia ya kutahadharisha na tatu kama vijembe vilivyodhamiriwa kuwadhalilisha wapinzani wake. Katika gazeti la *Saturday Standard 20th October* 2007; Raila alisema kuwa haingewezekana awe alishiriki katika kuipindua serikali ya rais mstaafu Moi, ilhali alikuwa raia. Itakumbukwa kuwa katika mwaka wa 1982 serikali yake Moi ilitikiswa kwa saa kadhaa na upepo wa mageuzi yaliyovunjwa baadaye na kuurejesha utawala mikononi mwake rais mstaafu Moi.

*(141)*

*How could I participate in a coup while I was a civilian?*

Ingewezekanaje nishiriki katika kuipindua serikali ilhali nilikuwa raia?

Swali hili la balagha lilidhamiriwa kuwahusisha wafuasi wake katika kero ambazo mwanasiasa huyo alikuwa akidai alipitia mikononi mwa rais mstaafu Moi na hivyo kulifanya chambo cha kuwanatia wapigaji kura kwa ajili ya huruma zao. Mwanasiasa huyo alikuwa akilitahadharisha taifa kuwa, uongozi wake Kibaki ulikuwa si tofauti na ule wa Moi. Mwanasiasa huyo, pia alitumia stihizai, hili likiwa kama shambulio lililosheheni nia mbaya ambayo ilikusudiwa kuwa kama kijembe kuuhusu muungano wa Jubilee. Stihizai yenyewe ilisheheni chembechembe za tashtiti, iliyoisawiri picha ya kinaya na dhihaka ikidhamiriwa kuufichua uovu fulani uliokuwapo katika muungano wa Jubilee. Kimsingi lengo kuu la mwanasiasa huyo katika gazeti la *The Standard 1st December 2012* lilikuwa kudhihirisha na kubeza maovu aliyodai yalikuwa yametekelezwa na viongozi wa muungano huo wa Jubilee kwa njia ambayo ingewafanya wananchi wa Kenya wachukizwe na kukerwa na hali iliyodaiwa. Dai lake mwanasiasa huyo kuwahusu viongozi wa Jubilee lilikuwa tahadharishi.

*(142)*

*In the bible, Jubilee means 50 years and during this time, prisoners and thieves were freed while those who have stolen were asked to return, so we are asking our colleagues in the so – called Jubilee Alliance are you ready to return property you have stolen?*

Katika bibilia Jubilee humaanisha miaka 50 na wakati huo, wafungwa na wezi waliachiliwa huru nao wale waliokuwa wameiba waliulizwa kurejesha, sasa tunawauliza ndugu zetu katika muungano wa Jubilee, mko tayari kurejesha mali mlioiba?

William Ruto aliukejeli uongozi wa rais mstaafu Kibaki alipokuwa katika chama cha ODM kutokana na utendakazi wake ambao kulingana na mwanasiasa huyo, kihistoria utendakazi wa rais huyo ulikuwa wa kutiliwa shaka, na hivyo hakuwa na sababu ya kuongezewa kipindi kingine kwani hangeufanya muujiza wowote. Nukuu katika gazeti la *The Standard 11$^{th}$ November 2007* ni kejeli iliyourejelea utendakazi wa mwanasiasa huyo mkongwe. Kejeli yenyewe iliazimiwa kuwarai wananchi wa Kenya na kuwatahadharisha kuwa Kibaki alikuwa ametingwa na uzee na hangeweza kubadilisha hali yao ya maisha kwa njia yoyote.

*(143)*

*If Kibaki has not performed miracles for 35 years, 20 years of which he was minister, 11 as vice president and the rest as president, which miracles can he perform in the five years he is asking for?*

Ikiwa Kibaki hajaifanya miujiza kwa miaka 35, miaka 20 akiwa waziri, miaka 11 akiwa kama Naibu wa rais na hiyo mingine akiwa kama Rais, ni miujiza gani atafanya katika kipindi cha miaka mitano anayouliza aongezewe?

Mwanasiasa huyo akiwa katika muungano wa Jubilee aliukejeli msimamo wa Raila Odinga kuutetea ugombeaji wake wa urais kama ambao ulikuwa na matumaini makubwa kuliko vile mambo yalivyokuwa katika mwaka wa 2007 alipokuwa anaungwa mkono na wanasiasa wengine waliokuwa na ushawishi mkubwa kuliko wale aliokuwa nao katika mwaka wa 2013. Kukejeliwa huko kuliingia daraja tofauti na kuisawiri picha ya kijembe;

alipoulizwa katika nukuu kwenye gazeti la *The Standard 21st February 2013,* angeshinda vipi ilhali wanajeshi wake wakuu sita hawakuwa naye.

> *(144)*
>
> *How on earth can Raila win this race when six of his strongest soldiers left?*
>
> Inawezekanaje katika dunia hii Raila ashinde ilhali wanajeshi wake sita wakuu walimwacha?

Dhamira yake Ruto ilikuwa inalenga kuuvua ubabe ambao Raila alikuwa akidai alikuwa angali nao hata baada ya kutemwa na washiriki wake wa karibu. Ruto alikuwa analenga kuwatahadharisha wafuasi wake na umma mpana kwa jumla kuuona ukweli huo uliokuwa ukiisawiri picha ya mwanasiasa huyo kushindwa.

Uhuru Kenyatta aliutumia usemi uliosheheni topoi za kutahadharisha wapigaji kura kumpigia Raila jicho la ndani na kumwona kama mnafiki. Akiyazungumzia machafuko ya kikabila, Uhuru Kenyatta alisema kuwa ikiwa mgombeaji wa kiti cha urais kwa tikiti ya chama cha CORD alikuwa mpenda amani angevizuia vita hivyo vya kikabila katika mwaka wa 2007. Alisema kuwa hakuwa akimpinga kutokana na mwelekeo kuihusu jamii yake, lakini kutokana naye kutosaidia kusitisha mapigano hayo hadi pale alipokabidhiwa uongozi wake wa 'nusu mkate'. Katika gazeti la *Daily Nation 19th February 2013* nukuu yake ni dhahiri.

> *(145)*
>
> *I don't oppose him because of his ethnicity. In 2007 he was a key leader in the conflict but there is no single day he opened his mouth castigating the violence until when he was granted his half bread government.*
>
> Simpingi kwa sababu ya kabila lake. Katika mwaka wa 2007 alikuwa kiongozi mkuu wa ODM wakati wa machafuko lakini hakuna hata siku moja aliufungua mdomo wake akikashifu machafuko hayo hadi pale alipopokezwa serikali yake ya nusu mkate.

Kutokana na maelezo ya nukuu yake Uhuru Kenyatta, ujumbe unaosimbuliwa ni; huenda ukaashiria kuwa mwanasiasa huyo alikuwa akilenga kuwashawishi Wakenya na kwa njia ya kipekee wapigaji kura ili waweze kumwona Raila Odinga kama kiongozi ambaye

alikuwa anauficha unafiki na kuongozwa na tamaa ya uongozi aliokuwa anauficha kwenye kivuli cha uzalendo.

### 5. 5. 6 Topoi za Ufisadi

Matumizi ya topoi za ufisadi yalifungamanishwa na matumizi ya chuku au udamisi; udamisi huwa mbinu ya kuikuza sifa ya kitu fulani kuliko kawaida. Mbinu hii hudhamiriwa kusisitiza sifa hiyo ya ukubwa au udogo na kwa kiasi kikubwa huchangia katika kuyachimuza masuala fulani katika usemi. Raila Odinga alikuwa mgombeaji kiti mmoja wa kiti cha urais aliyekuwa akizipiga kampeni zake kwa kuutumia usemi uliokuwa umesheheni chuku, akiwa na nia ya kuwafanya wananchi na wapigaji kura kuuona uzito uliokuwa katika suala lililokuwa katika shajara ya kampeni zake. Suala kuhusu ardhi katika uchaguzi wa mwaka wa 2013 lilichukuliwa kwa uzito ambao hakuna uchaguzi mwingine nchini Kenya ambao ulikuwa umekoleza kampeni za urais jinsi hiyo. Uhuru Kenyatta alikuwa akituhumiwa kuwa alikuwa amenyakua ardhi ya umma bila kuzingatia sheria zilizohusu ardhi nchini Kenya; ambapo alisimangwa na wapinzani wake waliomuuliza arejeshe ardhi hiyo ili maskwota wapate kugawiwa. Katika gazeti la *Daily Nation 29$^{th}$ January 2013,* Raila Odinga alitumia usemi uliolenga kuisawiri picha ya ukubwa wa ardhi ambayo Uhuru Kenyatta alituhumiwa kuimiliki katika Mkoa wa Pwani. Mwanasiasa huyo alidai kuwa Uhuru Kenyatta alikuwa anamiliki ardhi iliyokuwa kubwa kama mkoa mzima katika nchi ya Kenya. Hii ilikuwa chuku iliyokusudiwa kumsawiri Uhuru Kenyatta kama bepari aliyekosa chembe dogo ya utu; na hivyo basi hangestahili kuutwaa uongozi wa nchi ya Kenya. Usemi wa mwanasiasa huyo ulibeba topoi za ufisadi ambazo zilikuwa na uwezo wa kutahadharisha na tukio lake kuweza kuushawishi umma.

> *(146)*
>
> *This is unequal society where someone kills the other over an acre piece of land yet someone owns land the size of a province…*
>
> Hii ni jamii isiyo na usawa ambapo mtu anamuua mwenzake kwa ajili ya ekari moja ya ardhi ilhali mtu mwingine anamiliki ardhi yenye ukubwa wa mkoa mzima…

Akilishadidia suala la ufisadi ambao ulikuwa umekithiri katika nchi ya Kenya mwanasiasa huyo aliijenga sifa ya ufisadi ambayo ilitoa picha ya mazimwi, na kuonyesha kuwa hali nchini Kenya ilikuwa mbaya sana kiasi kwamba mafisadi walikuwa wanauliza kupewa

kila kitu; jambo aliloliona kama kikwazo kwa wawekezaji. Katika gazeti la *The Standard 28th October 2007* mwanasiasa huyo aliahidi kuwa serikali yake ingefutilia mbali tabia hiyo kama njia moja ya kuwavutia wawekezaji.

*(147)*

*My government will not subject investors to the shameful culture of TKK* (Toa Kitu Kidogo) *culture which has of late become* Toa Kitu Kikubwa *or* Toa Kila Kitu…

Serikali yangu haitawahusisha wawekezaji katika mazoea ya kitendo cha aibu cha TKK (Toa Kitu Kidogo) mazoea ambayo sasa yamebadilika na kuwa Toa Kitu Kikubwa au Toa Kila Kitu…

Udamisi ulioakika hapa ulisawiri picha ya jamii ambayo ilikuwa imechengwa na maadili na kuwa, ufisadi huo ulimithirishwa na ile hali ambayo mtu huvamiwa na wezi na kupokonywa kila kitu; yaani ulikuwa ufisadi wa mabavu. Nukuu yake mwanasiasa huyo ilikuwa na lengo moja kubwa; kuutahadharisha umma kukaa ange na kutoafiki rairai za wagombeaji kiti cha urais kutoka kwa muungano wa Jubilee.

William Ruto katika kuonyesha kuwa mabadiliko yalikuwa jambo la lazima katika uchaguzi mkuu wa 2007, alitumia chuku alipoimithilisha hali ya majilio ya mabadiliko katika kipindi hicho kama jambo lililokuwa la lazima na kuwa hakuna jambo lolote lile ambalo lingeweza kubatilisha upepo wa mabadiliko uliokuwa unavuma nchini Kenya. Alidokeza kuwa hata jeshi halingeweza kubatilisha; huo ulikuwa ni udamisi kwani wanajeshi ni kitengo kimoja cha usalama kinachojulikana kuchukua hatua ambazo huwaponza watu kutokana na hatua zao za uhayawani. Hivyo basi, nukuu katika gazeti la *The Standard 4th October 2007* lilifumbata usemi uliodhamiriwa kuisuta misimamo ya viongozi ambayo ilikuwa haijazindukana kutokana na mtazamo uliokuwa katika chama cha ODM; mwanasiasa huyo alikusudia kuwatahadharisha wale ambao walikuwa bado hawajaamua kukubali kuwa mabadiliko yalikuwa halali ya wakati huo.

*(148)*

*Not even an army can stop the wind of change.*

Hata jeshi haliwezi kuuzuia upepo wa mabadiliko.

### 5. 5. 7 Topoi za Kudhihaki

Kampeni za urais nchini Kenya hupigwa huku dhamira ikiwa kulidhalilisha kundi moja dhidi ya kundi lile jingine; kama njia moja ya kuusisitiza uzuri fulani katika kundi moja, wanasiasa hutumia kinaya wakilenga kuwashawishi wapigaji kura. Kinaya hutokea pale ambapo maneno yanayotumiwa yanaelekea kukinzana na fahiwa au maana inayohitajika katika muktadha maalum na inayokusudiwa na msemaji au mtumiaji. Maneno yanapoishia kumlenga mtu maalum aghalabu huishia kuwa 'dhihaka' ambayo ni shutuma fulani ambayo haisemwi waziwazi. Katika usemi wao wanasiasa katika kampeni za uchaguzi wa urais, kinaya hutumiwa kwa ajili ya sababu kadhaa, ile ya kimsingi ikiwa kama dhihaka. Kinaya cha kidhihaka hukusudiwa kukera, kuudhi au kumletea mlengwa hisia fulani ya kubezwa au kudharauliwa. Kinaya hiki hutokea pale ambapo maneno yanayosemwa hayamaanishi tu kinyume bali pia yanakusudiwa kukera, kukosoa au kumuudhi anayezungumziwa.

Aina ya kinaya kilichohusishwa na kampeni za urais nchini Kenya kilisheheni 'Dhihaka', wanasiasa wakikusudia kuwasuta na kuwakera wenzao kama njia ya kuzipaka sera zao tope, dhamira ikiongozwa na mtazamo wa kusisitiza uzuri **wetu** lakini kusisitiza ubaya **wao** (Rejelea 2. 2. 3). Katika gazeti la *Daily Nation 27th January* 2013, Uhuru Kenyatta alitumia kinaya cha kidhihaka akilenga kuitia doa mitazamo yake Raila Odinga kuwa hakuwa akiwaambia Wakenya ukweli, kwani kihistoria babake Raila alikuwa katika serikali hiyo aliyokuwa akiikashifu na kuitia mawaa.

*(149)*

*…Raila keeps on blaming me over my father Jomo Kenyatta's administration. Wasn't his father a vice president in that government?*

…Raila amekuwa akinikashifu kwa ajili ya serikali ya hayati babangu Jomo Kenyatta. Kwani babake hakuwa Naibu wa Rais katika serikali hiyo?

Mwanasiasa huyo aliuona usemi wa Raila kuwa kinaya; Kinaya cha Usemi kama hicho huwa kinaya cha kimsingi sana na hupatikana katika usemi na hutokea pale ambapo pana mkinzano fulani baina ya kisemwacho na uhalali wenyewe – kusema kitu fulani ukiwa na maana nyingine na hadhira nayo itambue hilo. Matumizi ya vitendawili kulingana naye Uhuru Kenyatta ilikuwa jambo lililokuwa haliingiliani na ukweli kama vile hali halisi ilivyokuwa ikitazamika. Katika gazeti la *Daily Nation 9th February* 2013, anayatolea

maelezo hali hiyo alipolenga kuonyesha kuwa usemi wake Raila ulisadifu 'kinaya cha usemi'

*(150)*

Siasa yake ya vitendawili haiwezi kuweka ugali katika meza ya mwananchi wa kawaida"

Kulingana na Kenyatta wale watu ambao wangevifaidi vitendawili walikuwa wananchi wa tabaka la juu, kinyume na vile hali halisi ilivyokuwa ikionekana kwa wananchi wa kawaida waliokuwa wakiiwakilisha asilimia kubwa ya wananchi katika nchi ya Kenya.

William Ruto alitumia kinaya cha kijaala ambacho hutokea katika muktadha mpana wa kihistoria na hasa pale ambapo historia hiyo inaangaliwa katika mtazamo wa sasa na hasa kurejelea watu ambao walikuwa na maoni fulani kuhusu wakati ujao (wa sasa) na kwamba hali iliyotokea ni kinyume cha matarajio hayo. Kimsingi, kwenye nukuu yake kulikuwa na kinaya cha kijaala kwa mtazamo mpana wa kihistoria. Katika gazeti la *The Standard 4$^{th}$ February* 2013, Ruto alikumbusha kuwa, kihistoria Raila Odinga aliibananga nafasi yake ya kuutwaa uongozi wa nchi ya Kenya kama rais, na hivyo hakuwa na mtu wa kulaumu, bali alihitaji kujilaumu yeye mwenyewe.

*(151)*

*Those who have squandered their chance to lead only have themselves to blame. If you have made a mistake retrace your steps, the only way to repent is to support other.*

Wale walioiharibu nafasi yao ya kuongoza wanastahili kujilaumu wenyewe. Kama ulifanya makosa, tazama nyuma na utafakari, kwa kuwa njia ya pekee ya kuomba msamaha ni kuwaunga wengine mkono.

Raila Odinga alikitumia kinaya kama njia moja ya kutahadharisha wapiga kura dhidi ya viongozi katika mrengo wa Jubilee akiusuta usemi wa William Ruto aliyekuwa amenukuliwa akisema muungano huo wa Jubilee ulikuwa ukiongozwa na kauli mbiu ya 'kusema na kutenda'. Akilirejelea suala la ardhi lililokuwa limepandisha mhemko katika kampeni za urais, mwanasiasa huyo aliutumia usemi wa kuwakejeli wapinzani wake 'kidhihaka' alipouliza swali lililokusudiwa kuwasawiri wapinzani wake kama 'Wezi' waliokuwa hawana punje ya utu. Katika gazeti la *Daily Nation 21$^{st}$ January* 2013

aliirejelea kauli mbiu ya William Ruto ya 'kusema na kutenda' kama ile iliyokuwa ikitumiwa kurejelea hali ya kuwapokonya wananchi mali yao.

> *(152)*
>
> *How can you say* kusema na kutenda *and then you go to your neighbour and snatch his property?*
>
> Utasemaje kusema na kutenda, halafu uende kwa jirani yako na kuchukua mali yake?

Utafiti huu ulibainisha kuwa wanasiasa wote waliutumia usemi uliokuwa amesheheni topoi za kuwatahadharisha wapigaji kura, lengo lao lilikuwa likilenga kuwashawishi wapigaji kura baada ya kuchorewa picha tahadharishi na kila mwanasiasa.

### 5. 5. 8 Topoi za Nambari/idadi ya Wapigaji Kura

Usemi kuhusiana na idadi ya wapigaji kura katika kampeni za urais nchini Kenya ilijipata katika ulingo wa kisiasa, ambapo wanasiasa walitokea na usemi uliozungukia idadi ya wapigaji kura kwa misingi ya vile jamii tofauti zilikuwa zimejiandikisha kama wapigaji kura; hasa katika uchaguzi wa 2013. Uhuru Kenyatta alilizungumzia suala la kura ya maoni akimtahadharisha Raila Odinga kuwa, kura ya maoni haikuwa na nafasi katika kutoa fununu za matokeo katika uchaguzi uliokuwa unangojewa. Alimwambia kuwa kilichokuwa na umuhimu ni idadi ya wapigaji kura na hivyo ikiwa angeshindwa hakuwa na budi kukubali ushinde wake. Uhuru aliiona kura ya maoni kama jitihada zilizokuwa hazina nafasi ikiwa idadi ya wapigaji kura ki maeneo ingezingatiwa. Katika gazeti la *The Standard 24th February 2013* nukuu yake mwanasiasa huyo ilikuwa ikilenga kuusuta mtazamo wake mheshimiwa Raila.

> *(153)*
>
> *We have the numbers, I appeal to Raila to concede defeat once the Jubilee coalition wins. We want to peacefully send them home and give the PM his benefits with love.*
>
> Tunayo idadi kubwa ya wapigaji kura, ninamsihi Raila kuyakubali matokeo pindi tu Jubilee itakapotangazwa kuwa mshindi. Tunataka kuwatuma nyumbani kwa amani na tumpe Waziri Mkuu masrufu yake kwa upendo.

Suala kuhusu idadi ya wapigaji kura iliyokuwa imetolewa na Tume ya Uchaguzi na Mipaka ya Kenya, ikiangazia idadi ya watu iliyokuwa imejiandikisha kupiga kura kutoka

kila eneo na kuangazia idadi ya kila jamii nchini Kenya ilichipuka katika kampeni za Ruto aliyesema kuwa ilikuwa dhahiri kuwa kulingana na matokeo yaliyokuwa yanaonyesha idadi ya wapigaji kura nchini, ushindi ulikuwa unaegemea kwao; ushindi mkubwa.

*Daily Nation 6th January 13, (154)*

> *Going by figures released by IBEC we have the requisite numbers and we shall win by a landslide.*
>
> Kufuatia idadi ya wapigaji kura iliyotangazwa na Tume ya Uchaguzi na Mipaka ya Kenya, tutakuwa na ushindi mkubwa kwani tunayo nambari inayohitajika.

Bila shaka topoi za idadi zilikuwapo katika usemi wa wanasiasa wakati wa kampeni, lengo la wanasiasa hao lilikuwa ni kuwashawishi wapigaji kura ambao hawakuwa na uwelewa huo na ambao huenda hawakuwa wameamua yule ambaye wangempigia kura kama rais. Topoi ya 'nambari' ilirejelea idadi ya wapigaji kura ambayo ingeweza kuuhakikishia muungano wa Jubilee ushindi.

### 5. 5. 9 Topoi za Mzigo/Uhalifu

Kulingana naye Raila, viongozi wa hapo awali katika nchi ya Kenya walionekana kama ambao walikuwa wameamua kuibebesha nchi ya Kenya mzigo uliokuwa umetuliwa chini baada ya rais mstaafu Moi kutamatisha kipindi chake cha uongozi wa taifa na kumpendekeza Uhuru Kenyatta kuwa mrithi wake. Miondoko hii ilipelekea kutokea kwa mada ya usemi iliyodhihirika kama Suala la Moi; hivyo basi, tukio la rais mstaafu Moi kumpendelea Kibaki lilifufua masuala chungu mbovu ya kihistoria kama vile ufisadi, marejeo ya udikteta, kuzorota kwa uchumi miongoni mwa masuala mengine mengi. Mwanasiasa huyo alisema kuwa Mzee Moi alikuwa mfungwa wa rais mstaafu Kibaki kwa sababu alikuwa na kashfa ya ufisadi ambayo angetaka aondolewe na serikali yake mstaafu Kibaki. Nukuu yake mwanasiasa huyo ilionyesha kuwa kurejea kwa rais huyo kungeonekana kama 'mzigo'; katika gazeti la *Nation 27th September 2007*, mwanasiasa huyo alinukuliwa akionyesha hofu yake.

> *(155)*
>
> *Mzee Moi is a prisoner of president Kibaki because he sought the president's support in order not to act on a corruption report implicating him.*

Mzee Moi ni mfungwa wa rais Kibaki kwa sababu anayo kashfa ya ufisadi na angetaka aondolewe lawama hiyo.

Kutokana na kushtakiwa kwa Uhuru na Ruto katika mahakama ya Hague, Raila Odinga aliliangazia tukio hilo kama ambalo lilikuwa kama mzigo kwa wananchi wa Kenya kutokana na ukweli kuwa, nchi ya Kenya haingeweza kuyaafikia matazamio yake. Raila hakuliafiki tukio la washukiwa hao kulitawala taifa kwa kutumia mtandao kama walivyokuwa wamenukuliwa wakisema. Gazeti la *Daily Nation 12th February 2013* lilikuwa na nukuu ambayo ingeweza kutazamika kuwa kama mzigo.

*(156)*

*I do not want to eliminate my competitor, but I know that it will pose a serious challenge to run a government through skype from the Hague.*

Mimi sitaki kumuondoa mpinzani wangu; lakini ninajua itakuwa changamoto kuitawala serikali kutoka huko Hague kupitia mtandao.

Mwanasiasa huyo alitokea kukanusha kuwa yeye hakuhusika kwa lolote kuwapeleka wapinzani wake huko Hague kama ilivyokuwa imedaiwa na wapinzani hao. Raila alikuwa akituhumiwa kuwa kwa kiwango kikubwa ndiye aliyechochea kupelekwa kwa wanasiasa hao wakuu wa muungano huo wa Jubilee katika mahakama ya Hague. Raila Odinga alishadidia mtazamo wake akiwaona Ruto na Uhuru kwenye usemi wake kama 'wahalifu' ambao wangepelekea nchi yake kutengwa na mataifa mengine ya kigeni. Raila aliangazia kuwa Uhuru Kenyatta angetafutwa kama rais wa Sudan Bashir aliyekuwa amewekewa ilani ya kukamatwa kama angezuru nchi zilizokuwa wanachama wa mahakama hiyo ya Hague huko Uholanzi. Mwanasiasa huyo alihoji kuwa Kenya ingeongozwaje kupitia tovuti; kulingana naye hilo lilikuwa jambo zito mno.

*The Standard 9th December 2012, (157)*

*How will you lead Kenya when you are wanted like Bashir, he cannot travel alot because if he lands in countries which are ICC signatories he will be arrested.*

Utaiongozaje Kenya ikiwa unasakwa kama Bashir, hawezi akazuru nchi nyingi kwa sababu akiwasiri katika nchi ambazo ni wanachama wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai ya Hague atatiwa mbaroni.

Raila Odinga alizidi kusema kuwa hakuna wawekezaji ambao wangedhubutu kuwekeza katika nchi ya Kenya ikiwa hao waliokuwa wametuhumiwa kwa makosa ya jinai wangechaguliwa kwani picha waliyokuwa wakiisawiri kulihusu taifa la Kenya ilikuwa mbaya.

*The Standard 14th January 2013, (158)*

> *No investors would come to Kenya if you elect a president with a bad image internationally.*
>
> Hakuna wawekezaji ambao watakuja Kenya ikiwa mtamchagua rais aliye na dosari kimataifa.

Topoi zilizokuwa zinabainishwa na mwanasiasa huyo zilifungamana na 'uhalifu'; uhalifu uliokuwa kama 'mzigo' kwa taifa lote la Kenya. Topoi hiyo ilidhamiriwa kuisawiri picha ya taifa lililokuwa linalikondolea macho tukio la taifa hilo kutengwa na mataifa mengine na kulipelekea taifa hilo kuwa – taifa pweke. Topoi hiyo ilikuwa inatumiwa na mwanasiasa huyo ili kuwa nyenzo ya kuwashawishia wapigaji kura.

### 5. 5. 10 Hitimisho

Katika kampeni za urais nchini Kenya baina ya vipindi vilivyoteuliwa, ufanisi wa mkakati wa ubishi ulichangiwa na uteuzi na utumiaji wa topoi kwani tukio hilo lilielezwa kama sehemu ya mjadala. Usemi wa wanasiasa uliibusha topoi za ubaguzi, nambari, wizi, ufisadi, uonevu, dhihaka, tahadharishi miongoni mwa topoi zingine nyingi (Topoi chache ndizo zilizorejelewa, Rejelea 2.7. 4). Wanasiasa niliowateua ama kwa hakika waliuchagua usemi wao kwa ufundi wakiwa na azma moja – kulidhalilisha kundi jingine. Topoi moja iliyoibuka ni kama ile ya kulisawiri kundi moja kama jizi wakati wa kura za mwaka wa 2007, hapa Raila alinukuliwa akimtahadharisha rais mstaafu Mwai Kibaki asidhubutu kuiba kura; na kama angefanya hivyo angekiona cha mtema kuni. Katika usemi wa mwanasiasa huyo (Raila) kulizalika topoi 'tahadharishaji' na vilevile 'wizi', yaani rais mstaafu Mwai Kibaki angeweza kushinda tu kwa kuiba kura. Topoi kama hizi zilitumiwa katika vipindi vyote viwili na hivyo kudhihirisha kuwapo kwa mwangwi wa topoi za kisiasa katika kampeni za urais.

### 5. 6 Mkakati wa Mkabala

Wodak (2001) alisema kuwa mkakati wa mkabala kwa yakini huelezea kuhusika kwa uhusiano wa mtazamo wa mzungumzaji. Kama ilivyoelezewa, mkakati huu huirejelea mikakati ya urejelezi na uarifishaji ili kuyapa madai yake mashiko. Kutokana na yale yaliyobainishwa na matokeo ya utafiti ni bayana kusema kuwa wanasiasa walioteuliwa kuwa asili ya data walisimama kidete na misimamo na itikadi za vyama na miungano waliyokuwa wakiiwakilisha katika kampeni zao. Wanasiasa hao watatu; yaani Uhuru Kenyatta, William Ruto na Raila Odinga waliishikilia misimamo yao bila kutokea kuyumbayumba katika kampeni za chaguzi zote mbili, ule wa mwaka wa 2007 na 2013. Itakumbukwa kuwa William Ruto alikuwa mwanasiasa mmoja ambaye alikuwa amemuunga mkono Raila Odinga katika mwaka wa 2007 na kutokea kumpinga miaka mitano baadaye. Uamuzi wa mwanasiasa huyo kuchukua mielekeo hiyo, ilibainisha kuwa huyo alikuwa mwanasiasa mwenye misimamo sugu na iliyokuwa haitetereshwi na lolote wala yeyote.

Uhuru Kenyatta alitokea kuutetea uamuzi wake wa kumuunga rais mstaafu Mwai Kibaki mkono katika uchaguzi wa mwaka wa 2007 aliposema kuwa uamuzi huo haukuwa wake peke yake bali wanachama wote wa chama hicho walikuwa wameafikiana kwa pamoja kufanya hivyo. Mwanasiasa huyo alikuwa akiyapuuzilia mbali madai ya wanachama wa ODM ambao kulingana naye Uhuru walikuwa na ajenda moja; ile ya kuitenga jamii ya Kikuyu. Kwenye gazeti la *The Standard 11$^{th}$ December 2007*, nukuu yake ilikuwa wazi:

> *(159)*
>
> *My support for president was a collective decision by Kanu's top organs and ODM should not capitalize on it to isolate the Kikuyu from other communities.*
>
> Uamuzi wangu wa kumuunga rais mkono ulikuwa wa viongozi wa juu wa chama cha Kanu na kwa hivyo ODM isilitumie jambo hilo kuitenga jamii ya Wakikuyu kutoka kwa jamii zingine.

Kama mwenyekiti wa chama cha KANU wakati huo, mwanasiasa huyo aliushikilia msimamo wake wa kumuunga Mwai Kibaki mkono hata baada ya kukemewa akiambiwa kuwa alikuwa amechangia katika kukisambaratisha chama hicho kutokana na msimamo wake huo ambao, kwa mtazamo wake alikuwa akitabiri kuwa njia iliyokuwa rahisi kwa

chama cha KANU kurejea uongozini ilikuwa kumuunga Kibaki mkono katika uchaguzi huo wa mwaka wa 2007. Gazeti la *Daily Nation 20th September 2007* lilisheheni mtazamo wake Uhuru (wakati huo) kuhusu uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2012.

> *(160)*
>
> *President Kibaki will be making his final lap during which time Kanu will have re-organised itself to recapture power in 2012.*
>
> Rais Kibaki atakuwa akitawala kipindi chake cha mwisho nayo Kanu itakuwa ikijitayarisha tena kurudi katika utawala mwaka wa 2012.

Kama mwenyekiti wa chama cha KANU wakati huo, Uhuru Kenyatta alikuwa akidhamiria kuitoa picha ya mambo na misimamo kama vile ilivyokuwa katika chama cha KANU, na kuwa uamuzi ambao ulikuwa ukiafikiwa katika kipindi hicho haukuwa wake bali ulikuwa wa chama chote kwa jumla. Kama mwenyekiti wa chama hicho cha KANU, Uhuru Kenyatta hakuwa na budi kuuonyesha ubabe wake chamani ikizingatiwa kuwa William Ruto alikuwa akidai kuwa wafuasi wote wa chama hicho walikuwa naye katika chama cha ODM. Msimamo wake William Ruto ulikusudiwa kudhihirisha kuwa hata yeye alikuwa na nafasi yake chamani kama katibu mkuu wa chama hicho; na kuwa wafuasi wote wa KANU walikuwa wamekihamia chama cha ODM pamoja na yeye.

*The standard 7th October 2007, (161)*

> *I promised Kenyans that if KANU ditches ODM then I will resign. I want to announce now that I have officially decamped from KANU and resigned my position as Secretary General.*
>
> Niliwaahidi Wakenya kuwa nitaihama KANU ikiwa KANU ingeitema ODM. Ninataka kutangaza kuwa nimeihama KANU rasmi na kujiuzuru kama Katibu Mkuu.

Matumizi ya kiwakilishi ‘ni’ kwenye vitenzi niliwaahidi na nitaihama ilikuwa njia moja ya kuonyesha kuwa mwanasiasa huyo alikuwa na misimamo sugu, kwanza kama mwanachama, na pili kama katibu mkuu. Tukio la kuwa KANU ilikuwa imedinda kukiunga chama cha ODM mkono; ililenga kumsuta Uhuru Kenyatta ambaye alikuwa mwenyekiti wa chama hicho cha KANU.

Raila Odinga ambaye walikuwa wametalikiana na William Ruto aliibeza miondoko ya mwanasiasa huyo (Ruto) akisema kuwa alikuwa ameteuliwa na jamii hiyo, kinyume cha vile watu wengine walivyokuwa wakidhania. Raila alimsuta Ruto akihoji kuwa watu wengine walikuwa wakidhania kuwa yeye Raila hangeweza kwenda kwa jamii hiyo ya Kalenjin bila kuongozwa na 'mtu huyo' akisema kuwa jamii hiyo ilimpenda na kuwa mambo hayangekuwa tofauti katika uchaguzi wa mwaka wa 2013. Katika gazeti la *The Standard 6$^{th}$ October 2012*; Raila alinukuliwa akiibeza miondoko ya William Ruto ya kujichukulia kuwa yeye ndiye alikuwa na nafasi ya kumpeleka kwa jamii hiyo ya Kalenjin.

> *(162)*
>
> *Others think I cannot go to the Kalenjin without them. Even in 2007, it is the community itself that drove them to support me because they loved me. This time round it is not going to be any different.*
>
> Wengine wanafikiria kuwa siwezi kwenda kwa jamii ya Kalenjin bila wao kunipeleka. Hata mwaka wa 2007, ni jamii yenyewe ndiyo iliyowafanya wakubali kuniunga mkono kwa sababu jamii hiyo ilinipenda. Hata sasa haitakuwa tofauti bado jamii hii itakuwa name.

Matumizi ya kiwakilishi 'si' katika kitenzi siwezi na kiwakilishi 'ni' katika kitenzi kuniunga mkono, ni viwakilishi vilivyokuwa vikiashiria ubabe wa mwanasiasa huyo katika jamii hiyo. Kushikilia kwake kuwa aliungwa mkono kwa sababu jamii hiyo ilikuwa inampenda ni tukio ambalo liliazimiwa na mwanasiasa huyo kuonyesha wapinzani wake kuwa alikuwa bado ana ushawishi mkubwa katika suala zima la siasa katika jamii hiyo.

## 5. 7 Uongezaji na Upunguzaji wa Uzito

Mikakati hii hudhihirisha uongezaji wa uzito katika usemi kwa upande mmoja na upunguzaji wa uzito katika usemi kwa upande mwingine. Mikakati hii hufanikisha ufahamu wa nafasi ya kauli katika usemi kwa kuongezea au kupunguza uzito wa ilokusheni katika masuala kama vile ya ubaguzi wa kiukoo, wanaopinga utaifa wa kisemitiki au usemi wa kikabila, haya ni kwa mujibu wa Onyango (2008), akiwanukuu Reisigl na Wodak (2001:45). Katika uongezaji wa uzito katika usemi, haya yanaweza kudhihirika kupitia maneno kama "hasa" na "bila shaka" na katika upunguzaji wa uzito

yanaweza kudhihirika kupitia usemi kama vile "ndio, lakini" Reisigl na Wodak (2007:383).

Reisigl na Wodak (2001) walisema kuwa mkakati wa uongezaji wa uzito katika usemi humaanisha kule kulisema jambo waziwazi bila kulificha wakati ambapo uzuiaji katika usemi humaanisha kulisema jambo kwa kulidokeza tu. Katika kampeni za urais jambo moja lililokuwa bayana ni kutokea kwa wingi kwa matumizi ya mkakati wa uongezaji wa uzito katika usemi wa kisiasa ikilinganishwa na mkakati wa upunguzaji wa uzito katika usemi wa kisiasa kwani umaratokezi wa upunguzaji wa uzito katika usemi wa kisiasa ulikuwa finyu.

Katika vipindi vyote viwili vya kampeni, Raila Odinga alinukulikwa akiwa ametumia mkakati wa uongezaji wa uzito katika usemi wa kisiasa kwa kina; dhamira yake ikidhihirika kuwa njia moja ya kumuumbua mpinzani wake. Katika gazeti la *The Standard* tarehe 4th *November 2007*, Raila Odinga alinukuliwa akimtahadharisha rais mstaafu Mwai Kibaki kuwa kama angedhubutu kutumia hila (kuiba kura), basi angetokea kukiona cha mtema kuni. Hapa kulikuwa na hali ambapo Raila aliongeza uzito katika usemi wake, kama njia moja ya kuwamotisha wafuasi wake na wakati huo huo akidhamiria kuisuta njama yoyote ambayo huenda ingefutikwa na serikali yake Mwai Kibaki (Tazama nukuu hizi 163 na 164 ukurasa ufuatao). Wakati huo huo mwanasiasa huyo alipunguza uzito katika usemi wake huo tangulizi, dhamira yake kuu ikiwa kupunguza hatua ya kuudhuru uso wa rais huyo mstaafu Mwai Kibaki. Hatua yake ya kupunguza uzito katika usemi wake ililenga kuwadhihirishia wananchi jambo moja, kuwa yeye alipenda amani na kuwa hakuna jambo lolote ambalo lingetinga azma yake ya kuingia Ikulu.

> *(163)*
>
> *If Kibaki tries rigging this poll, he will see the kind of opposition he has never seen in his life. But even if he does that we will still beat him.*
>
> Ikiwa Kibaki atajaribu kuiba kura katika uchaguzi huu, atauona upinzani ambao hajawahi kuuona maishani mwake mwote, lakini hata kama atajaribu hayo tutamshinda tu.

Mwanasiasa huyo alikuwa mwepesi wa kutumia upunguzaji wa uzito katika usemi wa kisiasa pale ambapo alionekana kuwa angewakera wafuasi wa mpinzani wake hasa kama

hatua hiyo ingetokea katika eneo la mpinzani wake; yaani alikuwa mwepesi wa kuzichezea hisia za jamii zilizokuwa zinadhihirisha kuwa zilikuwa zinamuunga mpinzani wake mkono.

Katika kampeni za mwaka wa 2007, mwanasiasa huyo alinukuliwa katika gazeti la *The Standard 8th September* 2007 akiwa anadai kuwa Mwai Kibaki alikuwa mtu mzuri lakini wale waliokuwa wamemzunguka ndio waliokuwa wakiuzuga uongozi wake kwa kumshinikiza afanye mambo kinyume na vile alivyokuwa ameahidi. Katika gazeti la *Standard* Tarehe *29th September* 2007, mwanasiasa huyo aliutumia mkakati wa kuongeza uzito katika usemi wake akimrejelea Mwai Kibaki kama mtu aliyekuwa amevunja au kukiuka sheria kutokana na kashfa ya mandugu wawili 'Waalmenia' (Arturs). Alidai kuwa rais huyo mstaafu alikuwa amezivunja sheria kama ilivyokuwa imedaiwa.

> *(164)*
>
> *Kibaki is a good man but he is held hostage by the 'Mount Kenya Mafia' who cannot allow him to effectively manage the affairs of Kenya.*
>
> Kibaki ni mtu mzuri lakini anashinikizwa na Mamafia wa Mkoa wa Kati ambao hawawezi kumruhusu azitekeleze shughuli za Kenya kikamilifu. Uongozi wa mtu mmoja utaisha pale tutakapoichukua serikali.

Maelezo kwenye nukuu ya mwanzo ilikuwa imepogolewa makali naye mwanasiasa huyo, lakini nukuu ya mwezi uo huo ilionyesha kuwa kupunguzwa kwa ukali kulikokuwa kumetangulia kulifuatiwa na usemi ambao ulisheheni uzito uliokuwa unakinzana na hali kama ilivyokuwa awali.

> *(165)*
>
> *Kibaki is 'guilty as charged'; the report mentions people who are close to him. If these people were in touch with the Arturs, it cannot be said Kibaki did not know what was going on.*
>
> Kibaki anayo makosa kama alivyotuhumiwa; ripoti inawataja watu ambao wana uhusiano wa karibu naye. Kama watu hao walishirikiana na ndugu hao wa Kiarmenia, haiwezekani ikawa Kibaki hakuyajua yaliyokuwa yakiendelea.

Kutokana na masuala hayo ya siasa; kihistoria, mwanasiasa huyo alikuwa akilenga kumshushia hadhi mpinzani wake kutokana na makosa hayo yaliyofanywa na viongozi

katika serikali yake na kujiweka juu kwa kujipambanua kama kiongozi aliyekuwa na suluhisho kwa matatizo yaliyokuwa yanawakumba Wakenya. Katika kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2013, mwanasiasa huyo aliwarejelea wapinzani wake kama 'fisi' waliokuwa hawana uwezo wa kuleta mabadiliko kwenye kizizi cha mbuzi; jambo aliloliona lingeweza kutokea tu kama mbuzi wote walikuwa wamekufa. Kufa kwa mbuzi ilikuwa si kufa kwa hali ya kawaida, bali kuliwa na viongozi hao; *The Standard 5th February* 2013. Mwanasiasa huyo alitumia mbinu ya kuzidisha uzito katika usemi wake lakini kwa njia ya kuzunguka.

Mwanasiasa huyo aliutumia mkakati wa kupunguza uzito katika usemi wake wakati wa kampeni zake hasa ikiwa alitokea kuona kuwa usemi wake katika siku za awali ungetokea kumharibia kuzitwaa kura za jamii ya yule aliyekuwa akimrejelea katika kampeni zake. Kihistoria, suala kuihusu jamii ya Kalenjin lilikuwa 'donda ndugu' katika kampeni zake kutokana na kutengana kwake na aliyekuwa mwenza wake katika kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2007 (William Ruto). Wakati mmoja mwanasiasa huyo alidokeza kuwa hakuna mtu ambaye angemzuia kwenda kwa jamii hiyo kwani jamii yenyewe ndiyo iliyokuwa inampenda na hivyo basi mambo hayangekuwa tofauti katika mwaka wa 2013. Nukuu katika gazeti la *The Standard 6th December* 2012 ilidhihirisha wazi matumizi ya mkakati wa kuzidisha uzito katika usemi.

> *(166)*
>
> *Others think I cannot go to the Kalenjin without them. Even in 2007, it is the community itself that drove them to support me because they loved me. This time round it is not going to be any different.*
>
> Wengine wanafikiria kuwa siwezi kwenda kwa jamii ya Kalenjin bila wao kunipeleka. Hata mwaka wa 2007, ni jamii yenyewe ndiyo iliwafanya wakubali kuniunga mkono kwa sababu jamii hiyo ilinipenda. Hata sasa haitakuwa tofauti bado jamii hii itakuwa nami.

Katika gazeti lilo hilo la tarehe *30th December* 2012, mwanasiasa huyo alionyesha kuwa mwingi wa toba, jambo ambalo lingeisawiri picha ya mtu aliyekuwa ameshapambaukiwa na uhalisia wa mambo katika Mkoa wa Bonde la Ufa kuwa, kiongozi huyo (Ruto) alikuwa anahusudiwa na jamii yake. Uombaji wake wa msamaha ni dhihirisho safi lililotambulisha

kuwa, mwanasiasa huyo aliitumia mbinu hiyo mbadala alipotanabahi kuwa angethurika kisiasa mikononi mwa jamii hiyo. Huo ulikuwa mkakati wa kupunguza uzito kutokana na usemi wake wa hapo awali.

*(167)*

*Forgive me, I am seeking forgiveness. If I erred, I am sorry I am a human being and appologize as we were in the same team last time.*

Nisameheni, ninawaomba msamaha. Kama nilikosea, poleni kwa kuwa mimi ni binadamu na ninaomba msamaha kwa kuwa tulikuwa katika timu moja wakati uliopita.

Uhuru Kenyatta katika kampeni zake aliitumia mikakati hiyo ya uongezaji wa uzito na upunguzaji wa uzito katika usemi wake, dhamira yake ikiwa ni pamwe na kutaka kuisawiri picha ya mtu aliyekuwa na roho ya utu na kuwa hangepandwa na jaziba ovyo. Uwezekano mwingine ni kuwa mashtaka dhidi yake huko Hague huenda yalichangia pakubwa katika kuufanya usemi wake kukosa makeke kama ya mpinzani wake aliyekuwa akimtia mwanasiasa huyo lawamani pindi tu alipoipata nafasi ya kufanya hivyo. Katika kampeni za mwanasiasa huyo kwenye nukuu katika gazeti la *The Standard 21st February* 2013, kulikuwa na matumizi ya mikakati yote miwili; ule wa kuongeza uzito katika usemi na ule wa kupunguza uzito katika usemi. Mwanasiasa huyo alihoji kuwa, kundi hilo la viongozi lilikuwa na miondoko ambayo ilikuwa ikisawiri picha kuwa, ingekuwa ni lazima watwae uongozi kwa vyovyote vile; alisema kuwa kila mtu alikuwa na haki ya kuutafuta uongozi, lakini muda wa mtu ukiisha basi alikuwa hana budi kuwapisha wengine. Huo ulikuwa mkakati wa kuongeza uzito katika usemi wake wakati huo wa kampeni zake kwani alikuwa akimshinikiza kung'atuka kutokana na ukweli kuwa yeye Raila Odinga alikuwa amechangia kuiongoza Kenya alipokuwa Waziri Mkuu katika kile; kihistoria kilikuja kujulikana kama 'Serikali ya Nusu Mkate' naye mwenza wake katika uchaguzi wa mwaka 2013 alikuwa Naibu wa Rais (Kalonzo Musyoka).

Katika nukuu ya tarehe iyo hiyo kwenye gazeti lilo hilo Uhuru Kenyatta aliutumia mkakati wa upunguzaji wa uzito katika usemi wake dhamira kuu ikiwa kudhihirishia wapigaji kura katika nchi ya Kenya kuwa yeye alikuwa hana chuki na mtu yeyote na kuwa aliwapenda wote hata na wale waliokuwa wakionekana kama adui zake. Mwanasiasa huyo

alisema kuwa walimheshimu Raila Odinga na kumwomba astaafu ili kuwaachia wao Uhuru Kenyatta na mwenza wake William Ruto kushindana na watoto wake. Neno 'kuheshimu' lilibeba chembechembe ya upunguzaji wa makali katika usemi wake mwanasiasa huyo; jambo ambalo kwangu nililiona kuwa 'madanganyo ya upole', kwani uhasama baina ya wanasiasa hao wawili ulikuwa wa wazi.

Katika harakati za kuwadhihirishia wananchi wa Kenya na ulimwengu kwa jumla kuwa yeye (Uhuru) alikuwa hana doa wala toa katika msururu mzima wa maisha yake, mwanasiasa huyo alimpa Raila Odinga changamoto kudhihirisha au kuyapa madai yake mashiko kuwa kama yeye Uhuru Kenyatta alikuwa ameiba chochote kile; alimuuliza auweke ushahidi wake wazi badala ya kuzua madai yaliyokuwa hayana mbele wala nyuma. Katika gazeti la *The Standard 14th February* 2013, nukuu ya usemi wa mwanasiasa huyo ni dhahiri.

> *(168)*
>
> *If you have any evidence that I have stolen anything table it.*
>
> Ikiwa mnao ushahidi wowote kuwa nimeiba chochote, wekeni wazi ushahidi huo.

Kati ya mikakati hiyo miwili, mkakati ambao ulitokea kutumiwa sana na mwanasiasa huyo ulikuwa ule mkakati wa kuongeza uzito kwenye usemi, lengo likiwa ni moja, lile la kumdhalilisha mpinzani wake; kwa yakini wanasiasa hao wote waliutumia mkakati huo zaidi ya ule mwingine.

William Ruto alitokea kuutumia mkakati wa kuongezea uzito kwenye usemi wake katika kampeni zake zaidi ya mkakati wa kupunguza uzito katika usemi; yumkini, hiyo ndiyo iliyokuwa njia mjarabu ya kusisitizia yale aliyokuwa akidhamiria kuutangazia umma. Mojawapo wa suala lililokuwa limezua utata ni kukosa kupitishwa kwa Katiba Mpya ambapo mwanasiasa huyo aliisuta serikali yake rais mstaafu Mwai Kibaki kwa kutowapa Wakenya katiba mpya na kumsawiri Kibaki kama kiongozi ambaye hangeweza kuyaafikia malengo hayo baada ya kushindwa kufanya hivyo. Kwenye gazeti la *Daily Nation 23rd October* 2007 mwanasiasa huyo alinukuliwa akiisuta serikali hiyo; kwa kuwa katika uchaguzi wa mwaka wa 2002 alikuwa ameahidi Wakenya kuwa wangeipata katiba mpya.

*(169)*

*He had a chance to deliver a new constitution but he failed. ODM will do so as a priority when it comes to power.*

Alikuwa na nafasi ya kuwapa Wakenya katiba mpya lakini hakuwapa. ODM watalishughulikia jambo hilo pindi watakapoutwaa uongozi.

Kutokana na matokeo ya mwanasiasa huyo kumuunga mkono Raila Odinga katika uchaguzi wa 2007; mambo yalikuwa yamechukua mkondo mwingine kwani katika uchaguzi wa mwaka wa 2013, Raila Odinga na William Ruto walijikuta wakizicheza ngoma tofauti kabisa zilizodhihirisha kuwa kulikuwa na uhasama uliokuwa umekolea na kuuacha ukame wa mioyo miwili kusawirika bayana. Nukuu ya tarehe *6th November* 2012 katika gazeti la *The Standard,* mwanasiasa huyo aliutumia mkakati wa kuongezea uzito katika usemi wake alipomkumbusha Raila Odinga kuwa, yeye Raila ndiye alikuwa ameifanya jamii ya Kalenjin kusalia nje ya serikali kwa miaka kumi kutokana na kauli mbiu yake ya mwaka wa 2002 ya ‘Kibaki Tosha’ na hivyo basi aliona haja ya kumuaga, kwani hangeweza kuhadaiwa tena.

*(170)*

*We supported that man in the last elections but we are now telling him bye. We have been in the opposition for 10 years because of his Kibaki* Tosha *Slogan*

Sisi tulimuunga mtu huyo mkono katika uchaguzi uliopita, lakini sasa tunamwambia kwaheri; tumekuwa nje ya serikali kwa jumla ya miaka 10 kwa sababu ya kauli mbiu yake ya “Kibaki Tosha”. Mtu akikudanganya mara moja yeye ni mdanganyifu, lakini akikudanganya mara ya pili, wewe utakuwa mpumbavu.

Mwanasiasa huyo alikuwa akilenga kuamsha kumbukumbu ya vile mambo yalivyokuwa kihistoria kwa sababu ya Raila Odinga; hivyo kumzidishia lawama ambazo zingemtenga na jamii hiyo ya Kalenjin.

Uongezaji na upunguzaji wa uzito ni mojawapo wa mkakati ambao wanasiasa katika kampeni za urais nchini Kenya waliitumia, lengo lilikuwa kulisawiri kundi moja au mgombeaji fulani wa kiti cha urais kama mtu aliyekuwa si mkamilifu. Ukamilifu wa

mgombeaji huyo ulidosarishwa kwa uzito fulani na wakati huo huo uzito huo ulipogolewa makali yake kwa ustadi fulani ambapo lengo lilikuwa kukwepa tendo la kuudhuru uso wa mgombeaji wa kiti hicho cha urais. Wakati wa kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2007 na 2013, wagombeaji wa kiti hicho cha urais waliitumia mikakati hiyo wakidhamiria uzuri uwarejelee 'wao' nao ubaya uwaendee 'hao'. Maneno ambayo yalidhihirika katika usemi wa wanasiasa yalilenga kuzidisha uzito na yalikuwa kama hasa, bila shaka na kadhalika, ilhali maneno ambayo yalitumiwa kama njia moja ya kuupunguzia uzito yalikuwa kama ndio, lakini na kadhalika (makatao). Kwa ufupi, hivyo vilikuwa vitendo kama vya kuuma na kuvuvia kama wafanyavyo panya – panya wa siasani. Ni vizuri kutaja kuwa mkakati ambao ulitumiwa zaidi kati ya hiyo miwili ulikuwa ule wa uongezaji wa uzito,

### 5. 8. Hitimisho

Kama vile ambavyo imebainika, kampeni za urais katika vipindi viwili vilivyokuwa vikilinganishwa na mtafiti; ilibainika kuwa usemi wa wanasiasa walioteuliwa na mtafiti kama msingi wa data ya utafiti, waliitumia mikakati tofauti tofauti wakati wa kuzipiga kampeni zao. Mikakati hiyo ya usemi ilikuwa urejelezi, uarifishaji, mkabala, ubishi na uongezaji na upunguzaji wa uzito. Mikakati hiyo ama kwa hakika ilidhihirisha kwamba wanasiasa walikuwa na lengo moja; lile la kuishawishi hadhira. Utafiti huu pia ulibainisha kuwa usemi ambao ulitumiwa na wanasiasa hao ulifungamanishwa na itikadi za vyama na miungano yao katika vipindi hivyo viwili ambavyo mtafiti alikuwa akivilinganisha. Mikakati hiyo ilitumiwa kama nyenzo ya kuumbuliana ambapo mwanasiasa mmoja alipokuwa akiutumia mkakati mmoja; picha iliyosawiriwa ilimdhihirisha mpinzani wake kama mnafiki ambaye ikiwa angejukumishwa hatamu za uongozi, basi huenda angelemaza maendeleo na shughuli zote kwa jumla za nchi ya Kenya. Kwa ufupi, mikakati ya usemi ilitumiwa na makundi yote mawili dhidi ya kundi jingine kama njia ya kuudhihirisha "udhaifu" uliojikita katika kundi pinzani.

### 5. 9 Athari za Usemi wa Kisiasa katika Kampeni za Urais

Mtazamo wao Lyenger na Mcgrady (2007) ulidai kuwa uchaguzi wa urais kwa kawaida hufuata sheria ya 'kuzawadi - kuadhibu', si jambo linaloweza kwenda kinyume na nafasi madhubuti inayotekelezwa na kampeni katika chaguzi kama hizo. Mojawapo wa umuhimu wa kampeni za urais ni kumweka mgombeaji wa urais katika nafasi aula ya kujinasibisha

na misimamo ya chama husika. Kimsingi wapigaji kura huenda wakampigia kura mgombeaji wa kiti cha urais kwa misingi kuwa, mgombeaji kiti huyo ni mwaminifu, au anasimamia sera zilizo na mwingiliano na matakwa yao wenyewe. Usemi wa wanasiasa huweza kuwa na athari kwa wapigaji kura kwa njia moja au nyingine, katika masuala ya siasa usemi huenda ukachangia katika kuwafanya wananchi kuzifumbata itikadi za chama kwa mujibu wa usemi wa mwanasiasa. Mtafiti alikuwa amelionyesha hili kwa kumrejelea Asher (1992) aliyekuwa amesema kuwa matamshi yanayotolewa na mtu huwa na tukio la ghafla au hasi ama chanya. Chukulio la mtazamo wake Asher (1992) na mtafiti ni kuwa, athari ya matamshi kutoka kwa wanasiasa huenda ikawa aidha kwa uzuri au kwa ubaya wa mtu, kabila au chama.

Kwa yakini; kwa moto huo huo, kampeni za urais huenda zikatinga matarajio ya wapinzani – dhaniwa kutoshiriki katika upigaji kura, ikumbukwe kuwa mojawapo wa malengo ya kampeni hasi kumhusu mgombeaji wa kiti cha urais ni kuwafanya wapigaji kura ambao huwa hawajauafikia uamuzi wa kupiga kura kubeua haja ya kupiga kura, hivyo basi kuyapogoa makali yao katika kupiga kura. Kampeni za urais nchini Kenya kama zilivyo kampeni zingine kwingineko huwa jukwaa la kuuwasilishia ujumbe kuhusu historia na misimamo ya wagombeaji wa kiti cha urais kuhusu matukio muhimu ya nchi. Kwa mujibu wa kampeni nchini Kenya, usemi wa wagombeaji wa kiti cha urais hupelekea wapigaji kura kuiaka mielekeo chanya au hasi kuwahusu wagombeaji wa viti hivyo vya urais.

Kampeni za urais nchini Kenya ama kwa hakika katika vipindi viwili nilivyochunguza, miezi mitano kabla ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 na miezi mitano kabla ya uchaguzi wa mwaka wa 2013, ni wazi kusema kuwa usemi wa wanasiasa husika, yaani Raila Odinga, Uhuru Kenyatta na William Ruto ulisheheni athari kadha wa kadha ikiwa nukuu zao kwenye magazeti ya vipindi hivyo *The Standard* na *Daily Nation* yataegemewa. Onyango (2008) amedhihirisha kuwa usemi wa kikabila wa kumuumbua mgombeaji ulikuwa wa siri katika maeneo ya umma, lakini dhahiri katika maeneo ya siri kabla ya uchaguzi wa mwaka wa 2007. Msomi huyo aliyarejelea matumizi ya jumbe kwenye rununu ili kuyapa madai yake mashiko. Ujumbe mmojawapo ulikuwa:

> *A Deadly Mountain Flu known as PNU, which affects the brain, has been reported in Central Kenya. The region is under quarantine. People in other parts of Kenya are advised to take ODM pills. One full orange for 3 months to avoid infection*
>
> Maradhi ya kutisha kutoka Mlimani yajulikanayo kama PNU, na ambayo yanaweza kuathiri ubongo yametokea Mkoa wa Kati. Eneo hilo limetengwa; watu wengine katika sehemu tofauti nchini Kenya wanashauriwa kumeza tembe 3 za ODM. Chungwa moja kwa muda wa miezi mitatu ili kuzuia kuambukiwa.

Ujumbe huo kulingana naye msomi huyo ulikuwa na majukumu kadhaa; kwanza ulidhamiriwa kuwahimiza wafuasi wa chama hicho kusalia chamani pasina kuighairi misimamo yao katika kipindi chote cha kampeni ambacho huwa miezi mitatu kulingana na katiba (Sheria za Uchaguzi, 2011). Pili, chungwa moja liliashiria alama ya chama hicho iliyokuwa chungwa zima kinyume na chama cha ODM-K ambacho kiliwakilishwa na chungwa moja unusu. Ujumbe huo vilevile ulitokea kuzalisha mkakati wa kuwashawishi wafuasi kusalia chamani. Kwa upande mwingine, wafuasi wa PNU walikuwa na ujumbe mfupi dhidi ya kabila la Waluo. Ujumbe huo ulikuwa:

> *Do you want to be ruled by Luo to take us back to joblessness? Safeguard the Kingdom. Let us ALL come out and give all the votes to Kibaki so that we are not ruled by an uncircumcised man who will make us wear shorts and plunder all our wealth. It's your vote that will prevent our country from going back to Egypt. May our God bless you.*
>
> Unataka kutawaliwa na Mjaluo aturejeshe nyuma kwa hali ya ukosefu wa ajira? Hifadhi Ufalme. SOTE tujitokeze na tumpe Kibaki kura zetu zote ili tusitawaliwe na mtu ambaye hajatahiriwa kwani atatufanya tuvae kaptura na vilevile atapora utajiri wetu. Ni kura yako itakayoizuia nchi yetu kurejeshwa Misri. Mungu na akubariki.

Huo ulikuwa usemi wa kikabila usio na uasili uliotengenezwa dhidi ya Mjaluo wakati wa utawala wa kikoloni. Msomi huyo akimnukuu Ochieng' (1975) alisema kulikuwa na vitambulisho kadhaa kuyahusu makabila fulani wakati wa utawala wa ukoloni; Mkikuyu alisemwa kuwa msafihi, Waluo wazembe nao Wamaasai wasioaminika. Ujumbe huo

ulisheheni topoi zilizosawiri picha ya kukosa ukomavu wa kuongoza kwani Mjaluo hakuwa ametiwa suna. Misri, kibibilia ni sehemu iliyoibusha picha ya Wana wa Israeli kuteswa na Firauni; hii ikiwa topoi ya mateso ambayo yangeshuhudiwa nchini, hivyo basi kuufanya kuwa mkakati shawishivu. Kulingana na mtazamo wa msomi huyo (Onyango 2008), jumbe nyingi za kudhalilisha kabila moja dhidi ya makabila mengine yalifanywa kwa kina sirini lakini jumbe zilizokuwa zinalengewa umma mpana zilisheheni usemi uliokuwa umepogolewa maneno kirihishi. Kutokana na mtazamo huo ilikuwa ni wazi kuwa magazeti ya *Daily Nation* na *The Standard* katika mwaka wa 2007 na mwaka wa 2013 miezi mitano kabla ya chaguzi kuu hizo zilibeba jumbe zilizokuwa zimechujwa; hata hivyo jumbe hizo zilikuwa na athari kwa wapigaji kura katika nchi ya Kenya.

### 5. 9. 1 Athari ya Usemi wa Raila

Nukuu ya Raila Odinga kwenye gazeti la *Standard 15th December 2007* iliibusha topoi za ukabila kushuhudiwa katika kampeni za urais katika uchaguzi wa mwaka wa 2007. Usemi wake uliashiria kuwa ukabila ulikuwa hai na kuwa ulihitajiwa kuzikwa (Tazama 4.1.3). Kulingana na mwanasiasa huyo, ukabila huo ulizungukia kiti cha urais kwani alitarajia kila jamii ingepata nafasi ya kuiongoza nchi yake. Matokeo ya usemi huo yalidhihirisha kuibuka kwa mkakati wa usemi bembelezi ikikumbukwa kuwa William Ruto alikuwa mshiriki wake wa karibu na kuwa rais mstaafu Moi kutoka kwa jamii ya Kalenjin alikuwa amekwisha kuiongoza nchi ya Kenya. Raila Odinga alikuwa akiinasihi jamii ya Kalenjin na jamii zingine nchini Kenya kuukubali msimamo huo na kuuchukua kama ‘mkataba’ wa kusaidisha kuuzika ukabila.

Nukuu hiyo kwa upande mwingine ilidhamiriwa kuisawiri picha pana kuwa uongozi wa nchi ya Kenya ulikuwa wa familia fulani kwani Uhuru Kenyatta na mstaafu rais Moi walikuwa wakimuunga mkono rais mstaafu Kibaki na kuwa kulingana na Raila, Uhuru Kenyatta angeteuliwa kuwa naibu wa rais. Nukuu katika gazeti la *Standard 15th December 2007* ilisheheni matini ifuatayo:

> *(171)*
> *We want to bury tribal politics and give every community equal chance to have a stub at the presidency. It should not be a reserve of certain families.*

> Tunataka tuzike siasa za ukabila na kuipa kila jamii nafasi sawa ya kuwa rais; haiwezi kuwa urais umetengewa familia fulani tu.

Gazeti la *Daily Nation 23rd September 2007* lilikuwa na nukuu ya Raila Odinga ikitaja kuwa rais mstaafu aliyefurushwa kutoka ikulu miaka mitano iliyokuwa imepita alikuwa amerejea na kuwa mtu aliyemtumikia kama naibu wake katika ikulu hiyo alikuwamo na kuwa alikuwa ameungana na kiongozi wa upinzani Uhuru Kenyatta.

Usemi wake Raila Odinga mbali na kuwa bembelezi ulisheheni usemi wa kikabila na mbari; kwa sababu hiyo, usemi huo ulilenga kuzishawishi jamii zingine nchini Kenya kuuambaa muungano wa PNU ambao kulingana naye kihistoria ulizitenga jamii na mbari zingine kutoka kwa uongozi wa Kenya. Katika gazeti la *Daily Nation 24th February 2013* nukuu yake ilikuwa:

> *(172)*
>
> *Compared to my rivals in Jubilee who have been dividing Kenyans along tribal lines, I am the only one who can unite the country. I have sacrificed alot politically for the sake of this country. In 2002, I said Kibaki Tosha; not because he was a Kikuyu but because he is a Kenyan.*
>
> Ikilinganishwa na wapinzani wangu wa Jubilee ambao wamekuwa wakiwagawanya watu kwa misingi ya kikabila, ni mimi tu ninayeweza kuliunganisha taifa. Nimejitolea sana kisiasa kwa ajili ya taifa hili. Katika mwaka wa 2002 nilisema Kibaki Tosha; si kwa sababu alikuwa Mkikuyu lakini kwa sababu alikuwa Mkenya.

Usemi huo wa Raila ulidhihirisha kuwa kulikuwapo na topoi za kudhihirisha ukabila ulikuwapo nchini Kenya. Mwanasiasa huyo alinukuliwa akisema kuwa wapinzani wake wa Jubilee walikuwa wakiwagawanya watu kwa misingi ya kikabila na kuwa ni yeye tu angeweza kuliunganisha taifa. Alidai kuwa alikuwa amejitolea sana kisiasa katika nchi ya Kenya. Alinukuliwa akikumbusha kuwa katika mwaka wa 2002 alisema 'Kibaki Tosha, si kwa sababu alikuwa Mkikuyu bali alikuwa Mkenya. Mkakati alioutumia Raila Odinga kwa yakini unatokea kuafikiana kikamilifu na mtazamo wao Carter na McCarthy (1994) wa upole hasi wa utafutaji wa fadhila ambapo hatua za utafutaji wa fadhila huwa:

1. Hatua ya matayarisho,

2. Hatua ya kulenga, na
3. Hatua ya mwisho.

Nukuu ya mwanasiasa huyo ilitokea kuzifuata hatua zote tatu kwa mujibu wa Carter na McCarthy (1994) kwani mwanasiasa huyo aliutayarisha usemi wake wa mwisho kwa kujilinganisha na wafuasi wake katika muungano wa Jubilee ambao aliwaona kuwa walikuwa wakiwagawanya Wakenya kwa misingi ya kikabila. Mwanasiasa huyo alitokea kulenga jambo alilodhamiria kuliwasilisha kwa wapigaji kura alipodai kuwa yeye alikuwa amejitolea kwa nchi ya Kenya kwa jumla kisiasa. Hatua yake ya mwisho ilitokea pale alipoisawiri picha ya mtu aliyekuwa mzalendo na ambaye aliidhamini nchi ya Kenya kiasi cha kumuunga rais mstaafu Kibaki mkono alipotokea na kauli mbiu yake ya 'Kibaki Tosha!', topoi ya 'unyenyekevu' ilizalika katika usemi wa mwanasiasa huyo ambayo ilimchora kama mzalendo aliyekuwa hana tamaa lakini aliudhamini umoja wa wananchi wa Kenya kwa jumla (Tazama 4. 8 1). Hayo yalikuwa marejeo ya usemi wa kikabila kwani kihistoria ukabila ulikuwa ukitumiwa katika makabiliano ya uongozi baina ya wagombeaji wa kiti hicho cha urais. Usemi wa mwanasiasa huyo ulidhamiriwa kuwafanya wapigaji kura nchini Kenya waingiwe na ugeuzi - nafsi kumhusu Raila, na kumfanya kuonekana kama mzalendo kindakindaki na kuzivutia kura za jamii zingine kwake.

Itakumbukwa kuwa katika mwaka 2007 William Ruto alikuwa mshiriki wake Raila lakini katika mwaka wa 2012-2013 kila mmoja wao aliivutia kamba kwake. Katika gazeti la *The Standard 6th October 2012* Raila Odinga alinukuliwa akisema kuwa wengine walikuwa wakifikiria kuwa hangeweza kwenda kwa jamii ya Kalenjin bila wao kumpeleka. Alidai kuwa ukweli ulikuwa kwamba katika mwaka 2007 jamii ya Kalenjin yenyewe ndiyo iliyowafanya (Ruto) wakubali kuwaunga mkono kwa sababu jamii hiyo ilimpenda na kuwa hata wakati huo haingekuwa tofauti kwani jamii hiyo ingekuwa naye. Usemi huo bila shaka ulibeba topoi za masuto au kejeli kwa William Ruto aliyekuwa amemtoka Raila Odinga kwa kishindo. Pia, usemi huo ulikuwa bembelezi na ulikusudiwa na mwanasiasa huyo kujinasibisha na jamii hiyo iliyokuwa imemuunga mkono kwa kina katika uchaguzi wa mwaka wa 2007; aidha, itakumbukwa kuwa mwanasiasa huyo alikuwa amepewa lakabu ya 'arap Mibei' iliyomaanisha 'yule atokaye kwenye ziwa'.

*(14)*

*Others think I cannot go to the Kalenjin without them. Even in 2007, it is the community itself that drove them to support me because they loved me. This time round it is not going to be any different.*

Wengine wanafikiria kuwa siwezi kwenda kwa jamii ya Kalenjin bila wao kunipeleka. Hata mwaka wa 2007, ni jamii yenyewe ndio iliyowafanya wakubali kuniunga mkono kwa sababu jamii hiyo ilinipenda. Hata sasa haitakuwa tofauti kwani jamii hii itakuwa name.

Masuala mengine ya kijamii yaliyoibusha usemi wa dhuluma za kihistoria yalizungukia suala la ardhi na katiba ya nchi ya Kenya na kumfanya mwanasiasa huyo kuangazia masuala hayo katika kampeni zake. Kwenye gazeti la *Daily Nation 3rd December 2007* Raila alinukuliwa akiirejelea dhuluma aliyodai kuwa Wamaasai walikuwa wameipitia tangu wakati wa utawala wa kikoloni kutokana na wao kunyang'anywa mashamba yao na kuhamishiwa katika wilaya za Kajiado na Narok. Kulingana naye, hii ilikuwa dhuluma ya kihistoria iliyoipuja haki ya Wamaasai kwani ardhi yao ilikuwa haijarejeshwa hata baada ya Wakoloni kuigura nchi ya Kenya.

*(173)*

*The historical injustice meted against them (Maasai), have not been addressed properly. Their land was reduced by 60% when the British evicted them to create room for settler ranches, confining them to present day Kajiado and Narok Districts.*

Dhuluma ya kihistoria dhidi yao (Maasai), haijasuluhishwa kikamilifu. Mashamba yao yalipunguzwa kwa asili mia sitini wakati Waingereza walipowafurusha ili kutenga nafasi ya mifugo yao na kuhamishiwa katika wilaya za Kajiado na Narok.

Usemi huo wa dhuluma za kihistoria kutoka kwa mwanasiasa huyo ulidhamiriwa kuishawishi jamii ya Maasai kwa kuisawiri picha pana ambayo ilikuwa ikizilenga serikali za hapo awali. Itakumbukwa kuwa suala hilo la dhuluma za kihistoria halikuikumba jamii hiyo peke yake kwani jamii kama vile ya Kikuyu ilikuwa imepokonywa ardhi yao katika Mkoa wa Kati na kuwafanya kuhamia maeneo ya mkoa wa Bonde la Ufa ambapo waliajiriwa kama wafanyakazi katika mashamba ya makoloni hao, na Kenya iliponyakua

uhuru, jamii ya Kikuyu pamwe na jamii zingine ziliunda mashirika ya kununua mashamba; na hivyo basi huo ukawa mwanzo wa dhuluma za kihistoria. Usemi huo wa dhuluma za kihistoria ulijenga mwangwi kwenye kampeni nyingi za wagombeaji wa kiti hicho cha urais, dhamira ikiwa ni kulidhalilisha au kulitweza kundi moja na kulilimbikizia kundi jingine sifa. Usemi huo vilevile ulikuwa na jukumu la kuhahishia hadhira iliyokuwa inatarajiwa kuona kuwa dhuluma hizo za kihistoria zilikuwa zinawakumba wao na kuwa waasisi wa dhuluma hizo walikuwa viongozi ambao kihistoria walitoka kwa jamii zilizokuwa zimeiongoza nchi ya Kenya.

Kampeni za mwanasiasa huyo za mwaka wa 2007 zilijikita zaidi kwenye harakati za kumdhalilisha rais mstaafu Mwai Kibaki kama kiongozi ambaye alikuwa hawezi kwa lolote kuufutilia mbali ufisadi ambao kwa mujibu wake Raila Odinga, ulikuwa unatiwa mbolea naye Mwai Kibaki. Mwanasiasa huyo alinukuliwa kwenye gazeti la *The Standard 13th December 2007* akihoji, "ni kitu gani kitakachobadilisha kesho ikiwa Baraza lake la Mawaziri sasa lina watu waliotuhumiwa kuhusika katika kashfa ya *Anglo-leasing* na *Goldenberg?"* Raila Odinga alikuwa akilenga kuutamausha umma na kuwafanya wapigaji kura kuingiwa na ari ya kupiga kura, lengo lao likiwa kuuondolea mbali uongozi wa wazee ambao itikadi yao ilikuwa inakwamiza kutekelezeka kwa mabadiliko mengine ambayo yangemfaidi mwananchi wa kawaida. Kutokana na kuibuka kwa masuala kama hayo, ni wazi kutaja kuwa usemi – tamaushi ulitokeza kwenye kampeni za mwaka wa 2007. Usemi kama huo ulitumiwa na mwanasiasa huyo kukolezea kampeni zake na kuwashawishi wapigaji kura kumwona kama mkombozi wa jamii zingine nchini Kenya.

> *(30)*
>
> *What will change tomorrow if his current cabinet today has individuals who were linked to the Anglo-leasing and Goldenberg scandal?*
>
> Ni jambo gani litakalobadirisha kesho ikiwa baraza lake la mawaziri linajumuisha watu waliotuhumiwa kuhusika na sakata ya *Anglo-leasing* na *Goldenberg*?

Usemi mwingine ambao ulijitokeza katika kampeni za mwanasiasa huyo ulizungukia harakati za kujenga imani katika matarajio ya wapigaji kura ambao kulingana na usemi wa mwanasiasa huyo matukio ambayo yalikuwa yamekwisha shuhudiwa nchini Kenya yalikuwa ya kuvunja moyo. Nukuu ya mwanasiasa huyo katika gazeti la *The Standard 16th*

*December 2007* ilionyesha kuwa mwanasiasa huyo alikuwa na suluhu ya kero za wananchi wa Kenya kuhusu karo kwa wana wao. Mwanasiasa huyo alinukuliwa akisema kuwa serikali yake ingepeana masomo ya sekondari bila malipo kabisa kinyume na ahadi yake rais mstaafu Mwai Kibaki aliyekuwa ameahidi ufadhili wa asili mia kumi na tano pekee ya masomo bila malipo. Mwanasiasa huyo alisema kuwa alijua kule hizo pesa zingetoka kwani jamii ya kimataifa ilikuwa imedokeza kuwa ilijua namna Kenya ilikuwa ikipoteza kima cha shilingi bilioni 50 za Kenya kwa njia ya ufisadi. Usemi wa aina hii ulikuwa mwingi ambapo kulingana na uchanganuzi wangu ulitokea kuibusha usemi – tumainishi ambao shabaha yake kuu ilikuwa kuishawishi jamii pana ya nchi ya Kenya ambayo ilikuwa na uwelewa wa kina kuhusu suala hilo la kijamii, na hivyo kushawishika kumuunga mkono.

*(190)*

*My government will provide absolute free secondary education unlike Kibaki pledge of 15% of cost of secondary education. I know where the money will come from, the international community has confirmed that in Kenya sh 50 billionis sieved through corruption loopholes every year which I will go and seal.*

Serikali yangu itapeana masomo ya bure kabisa kwa shule za upili kinyume na vile Kibaki alivyowaahidi asilimia kumi na tano ya malipo hayo. Ninajua pesa zitapatikana wapi kwa kuwa jamii ya kimataifa imetuhakikishia kuwa katika nchi ya Kenya shilingi bilioni 50 huporwa kupitia mianya ya ufisadi kila mwaka, nami nitaiziba mianya hiyo.

Katika kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2013 usemi wa kikabila ulirejea kwenye kinywa cha mwanasiasa huyo aliyekuwa amempoteza mmoja wa wanasiasa waliokuwa ngome katika kampeni zake za mwaka wa 2007; William Ruto ambaye katika kampeni za uchaguzi mkuu wa 2013 alikuwa mshiriki wa Uhuru Kenyatta. Usemi wa kikabila ambao Raila aliutumia ulikuwa usemi wa kushawishi uliojengwa kwenye msingi wa kukumbusha wananchi wa Kenya kuwa ingetokea kuwa wangelinganishwa na wapinzani wake wa muungano wa Jubilee, ingedhihirika wazi kuwa wao walikuwa wakiwagawanya Wakenye katika misingi ya kikabila na kuwa ni yeye tu ambaye angeweza kuliunganisha taifa. Aidha, alidai kuwa alikuwa amejitolea sana kisiasa kwa ajili ya taifa la Kenya kwani

kulingana na usemi wake katika mwaka wa 2002 hakusema Kibaki Tosha kwa sababu alikuwa Mkikuyu bali kwa kuwa alikuwa Mkenya. Usemi huo ulikuwa wa kihistoria kwani itakumbukwa kuwa katika mwaka wa 2002 walikuwa wameungana na Kibaki dhidi ya chama cha KANU na mgombeaji wa kiti cha urais Uhuru Kenyatta. Kulingana na madai yake, mwanasiasa huyo alikuwa akiisawiri picha ya kiongozi ambaye hakuwa na tamaa ya uongozi kwani historia ilikuwa wazi kwa wananchi wa Kenya kukumbuka tangazo lake la kihistoria na hivyo kuwarai wapigaji kura ili wamtazame kwa jicho la mzalendo.

*Daily Nation 24th February 2013, (7)*

> *Compared to my rivals in Jubilee who have been dividing Kenyans along tribal lines, I am the only one who can unite the country. I have sacrificed a lot politically for the sake of this country. In 2002, I said Kibaki Tosha; not because he was a Kikuyu but because he is a Kenyan.*
>
> Ikilinganishwa na wapinzani wangu wa Jubilee ambao wamekuwa wakiwagawanya watu katika misingi ya kikabila, ni mimi tu ninayeweza kuliunganisha taifa. Nimejitolea sana kisiasa kwa ajili ya taifa hili. Katika mwaka wa 2002 nilisema Kibaki Tosha; si kwa sababu alikuwa Mkikuyu lakini kwa sababu alikuwa Mkenya.

Usemi wa kuumbuana katika uchaguzi wa mwaka wa 2013 ulijikita kwa kiwango kikubwa katika suala la ardhi na ufisadi. Itakumbukwa kuwa katika mwaka wa 2007 mwanasiasa huyo hakulizungumzia suala hilo kama alivyofanya katika mwaka wa 2013, kwanza kulikuwa na uwezekano mkubwa kuwa katika mwaka wa 2007 William Ruto alikuwa mshiriki wake wa karibu na hangeweza kujiponza kwa suala la ardhi kwani jamii mbili ambazo zilikuwa zikituhumiwa kwa kutowajibika katika masuala ya ardhi ilikuwa jamii ya Kikuyu na ile ya Kalenjin. Nukuu katika gazeti la *Daily Nation* tarehe *1st December 2007* inaupa mtazamo wangu mashiko kwani mwanasiasa huyo alinukuliwa akikisifu chama cha ODM akiwa kule Likoni, Mombasa;

> *(174)*
>
> *The ODM government will implement comprehensive land reforms to ensure all residents enjoy both equity and fairness on the land question.*

> Serikali ya ODM itatekeleza kikamilifu marekebisho ya suala la ardhi kwa wakaazi wote ili wafurahie haki na usawa katika suala la ardhi.

Usemi wake katika mwaka wa 2013 unakinzana na msimamo wake katika mwaka wa 2007 kwani alinukuliwa akiwasimanga wapinzani wake kuwa ingewalazimu kwanza warejeshe ardhi waliyokuwa wameiba. Mwanasiasa huyo alinukuliwa akihoji kuwa iliwezekanaje watu wengine kuimiliki ardhi kubwa kama mkoa mmoja ilhali watu wengine walikuwa hawana ardhi. Pili, kulikuwa na uwezekano kuwa mpinzani wake wakati huo alikuwa hajakumbwa na ufisadi uliokuwa unazungukia suala la ardhi. Usemi wake mwanasiasa huyo katika kipindi hicho ulitokea kuwa usemi – kinyume uliodhamiriwa kumuumbua mpizani wake kwa kuirejelea historia ya nchi ya Kenya.

Matumizi ya usemi wa bibilia yaliibuka kwa kiwango cha juu  sana, jambo ambalo lilifanyika likiwa na dhamira mbili, kwanza kuushawishi umma kuona haja ya kumuunga mkono na kwa upande mwingine kuwaumbua wapinzani wake kwa kuisawiri picha akionyesha kuwa hao waliongozwa na nguvu za giza. Kama njia moja ya kuonyesha kuwa aliwajali watu wote, mwanasiasa huyo alinukuliwa katika gazeti la *The Standard* tarehe *11th December 2012* akiirejelea bibilia akisema kuwa Joshua aliigawanya mali ya Kanani kulingana na makabila kumi na mawili ya Israili na kwa njia hiyo kama wangevuka Kanani mwaka ambao ungefuata wangegawanya keki sawasawa kwa makabila yote 42 ya nchi ya Kenya.

Usemi huo wa bibilia ulikuwa shawishivu na ulirejelea Kanani kama njia ya kuonyesha kuwa Wakenya hawakuwa wamefika Kanani yao na kuwa kiongozi ambaye angeweza kuzifanya ndoto zao ziafikiwe alikuwa bado hajautwaa uongozi. Kimsingi Kanani kibibilia iliashiria utele na kuboreshwa kwa maisha ya wananchi ambao kulingana na Raila Odinga walikuwa wamegandamizwa kwa kipindi kirefu. Aidha usemi huo ulikuwa ukitumiwa kuyajenga matumaini ya wapigaji kura kuwa mwanasiasa huyo alikuwa akiongozwa na haki na utu ikilinganishwa na viongozi waliokuwa wametangulia kuwa wao waliongozwa na ubinafsi. Katika gazeti la *The Standard* tarehe *11th December 2012* mwanasiasa huyo alinukuliwa akisema kuwa:

> *(175)*

*In the bible, Joshua divided Cannans resources according to the 12 tribes of Israel and similary when we cross to Canaan next year, we will share this cake equitably among the 42 tribes.*

Katika bibilia, Joshua aliigawanya mali ya Kanani kulingana na makabila 12 ya Israili na kwa njia hiyo hiyo tukiingia Kanani mwaka ujao, tutaigawanya hii keki sawa kulingana na makabila 42.

Katika mwaka wa 2002 kwenye Muungano wa Madola, George Bush alitamka kuwa 'kuna nguvu, nguvu ya ajabu, katika uzuri na ukamilifu na imani ya watu wa Amerika' alipoiunga mkono imani yake ya msingi katika kuzinduliwa kwa Hati ya Huduma kwa Wananchi. Namna usemi huo ulivyosimbuliwa kulitofautiana, kulingana naye Albertson (2005) kirai 'kuna nguvu ya ajabu' kuliashiria maana mahususi kwa wale waliokuwa na fununu ya kiitikio cha wimbo. 'Kuna Nguvu kwenye Damu'. Kulingana na Albertson (2005) wanasiasa na wagombeaji wa viti vya kisiasa aghalabu hutumia usemi wa kidini kwa sababu usemi huo hubeba nguvu za kushawishi wananchi kuyaafiki masuala ya kisiasa kwa njia yenye uzito. Msomi huyo alidokeza kuwa, kimsingi athari ya matumizi ya usemi wa kidini ambao huwa wa kiistiari ni kuwa; huwezesha wanasiasa kuzungumza waziwazi kwa watu walio na mitazamo sawa nao na kubadilishana misimamo, ilhali wale wasiokuwa na mitazamo kama hiyo wasiweze kung'amua yanayolengwa.

*(191)*

*In the bible, Jubilee means 50 years and during this time, prisoners and thieves were freed while those who had stolen were asked to return, so we are asking our colleagues in the so called Jubilee Alliance are you ready to return property you have stolen?*

Katika bibilia, Jubilee humaanisha miaka 50 ambapo katika kipindi hiki wafungwa hufunguliwa na wezi huachiliwa huru nao wale ambao wameiba huulizwa warudishe, kwa hivyo ninawauliza marafiki zangu katika muungano wa Jubilee, je mko tayari kurejesha mali mliyoiba?

Matumizi ya usemi wa kidini yalikuwa mengi (Mfano nukuu nambari *175*) katika mwaka wa 2013 ambapo lengo la mwanasiasa huyo likilenga kuukejeli Muungano wa Jubilee akiazimia kuudosarisha kwa kutozingatia yale yaliyokuwa yakiendana na bibilia kuhusu Jubilee. Katika gazeti la *The Standard* tarehe *15$^{th}$ December 2012* aliirejelea kauli mbiu ya

neno Jubilee na kusema kuwa, katika bibilia, Jubilee ilimaanisha miaka 50 na wakati huo, wafungwa na wezi waliachiliwa huru, vilevile walioiba waliulizwa kurejesha waliyoiba, hivyo basi akawauliza wapinzani wao katika kile walichokiita Muungano wa Jubilee; kama walikuwa tayari kuirejesha mali ambayo walikuwa wameiba. Usemi huo ulitumiwa na mwanasiasa huyo akikusudia kuwasawiri wapinzani wake kama 'wezi' ambao walikuwa wakienda kinyume na maadili katika bibilia. Usemi huo kwa hivyo ulikuwa nyenzo ya kuushushia hadhi Muungano wa Jubilee kwa njia ya kuushawishi umma kuuona muungano huo kama ambao ulikuwa unaongozwa na mawakala wa nguvu za giza.

Usemi mwingine ambao mwanasiasa huyo aliutumia ulikuwa ukimsawiri kama kiongozi ambaye hakuwa na mate ya fisi kuhusu uongozi wa nchi ya Kenya kwani kulingana naye, sherehe za kuapishwa kwake zilikuwa zimeandaliwa lakini yeye hangeweza kuliafiki wazo hilo kwani kulingana naye alikumbushwa jinsi shetani alivyomjaribu Yesu wakati alipomwonyesha uzuri wa nchi; akimwahidi kuwa angempa yote hayo ikiwa Yesu angemwabudu. Kulingana naye alitafakari na kuona kuwa hatungekuwa na nchi kama Kenya. Kutokana na mwanasiasa huyo kuitumia lugha ya kidini, ni wazi kusema kuwa wanasiasa wengi hutumia usemi wa kidini kutokana na nguvu ndanimwe ya kushawishi wapigaji kura, kuhoji au kudadisi maadili ya wapinzani katika king'ang'anyiro cha uongozi na kama njia ya mgombeaji uchaguzi kujisawiri kama kiongozi ambaye huongozwa na maadili ya kiungu.

Suala la wizi wa kura katika nchi ya Kenya lilikuwa likijikuta kwenye ulingo wa kisiasa katika kampeni za urais kila wakati kampeni za uchaguzi mkuu zilipokuwa zikiendelezwa; tukio hilo lilidhihirisha kuwa kulikuwapo na mwangwi wa masuala ya awali katika chaguzi fuatilizi. Katika kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2013 Raila Odinga alinukuliwa akilizungumzia suala hilo la wizi wa kura katika uchaguzi wa 2007 kwenye gazeti la *The Standard 18^th^ February 2013* ambapo alisema kuwa alielewa fika kuwa jamii ya Kalenjin ilimpigia kura akiwa katika chama cha ODM mwaka wa 2007 lakini hangeweza kutekeleza yale aliyoahidi kwa kuwa kura zake ziliibwa. Kutokana na tukio hilo aliwaomba wamuunge mkono tena katika mwaka wa 2013; wakati mmoja, mwanasiasa huyo alinukuliwa akisema, 'Si mnajua ng'ombe *yetu* ilizaa na ndama *ikaliwa* na mbwa'.

*(192)*

*Iam aware that you threw your whole weight behind me and ODM in 2007, but we could not deliver the promise after we were rigged out. I appeal to you to give me one more chance and we will deliver.*

Ninajua vyema kuwa nyote mliniunga mkono pamoja na chama cha ODM katika mwaka 2007, lakini hatukuupata ushindi baada ya kura zetu kuibwa. Ninawaomba mniunge mkono mara nyingine moja na tutashinda.

Katika mwaka wa 2007 tarehe *4th November 2007* kwenye gazeti la *Sunday Standard,* mwanasiasa huyo alinukuliwa akimtahadharisha rais mstaafu Kibaki kuwa angedhubutu kuiba kura angeuona upinzani ambao hakuwa ameuona maishani mwake kutoka kwa upinzani. Kulingana na Raila hata kama (Kibaki) angefanya hivyo yeye Raila alikiri kuwa angeibuka kuwa mshindi.

*(176)*

*If Kibaki tries rigging this poll he will see the kind of opposition he has never seen in his life. But even if he does that, we will still beat him.*

Kibaki atauona upinzani ambao hajawahi kuuona maishani mwake akijaribu kuuiba uchaguzi huu; lakini hata akifanya hivyo, tutamshinda tu.

Usemi wa mwanasiasa huyo ulibeba topoi ya 'kuonya' au 'kutahadharisha' na 'imani'. Kwanza mwanasiasa huyo alikuwa akiuonya uongozi wa serikali ya rais mtaafu Kibaki kuwa wangejaribu kuiba kura wangejikuta upande mbaya wa upinzani; hiyo ilikuwa njia moja ya kuonyesha wafuasi wake kuwa alikuwa mkakamavu. Kama njia moja ya kudhihirisha kuwa alikuwa na imani na harakati zake za kukigombea kiti hicho cha urais, mwanasiasa huyo hakuwa na budi kuthibiti suala zima la uchaguzi kwa kuonyesha kuwa kwa vyovyote vile wangeibuka kuwa washindi.

### 5. 9. 2 Athari ya Usemi wa Uhuru

Katika mwaka wa 2007 Uhuru Kenyatta aliamua kutojitoma uwanjani ili kuking'ang'ania kiti cha urais nchini Kenya na badala yake aliamua kumuunga mkono rais mstaafu Mwai Kibaki. Tukio hilo lilizua tumbo joto katika uongozi wote wa chama cha KANU na kumpelekea mwanasiasa huyo kusutwa vikali na wanasiasa wa chama cha KANU na wengine kutoka katika miungano mingine.

Najib Balala alinukuliwa katika gazeti la *The Standard 17th September 2007* akimshutumu Uhuru Kenyatta na kusema kuwa ilikuwa aibu kubwa sana kuona kuwa mwenyekiti wa chama cha KANU alikuwa amekidunisha chama cha kitaifa na kukifanya kuwa chama cha kijijini ili kumwezesha kukihifadhi kiti chake cha eneo bunge la Gatundu.

*(193)*

*It is a big shame to see Kanu Chairman Uhuru Kenyatta reduce a national party to a village party for the sake of winning his Gatundu parliamentary seat*

Ni aibu kubwa kuona Mwenyekiti wa chama cha Kanu Uhuru Kenyatta akikifanya chama cha kitaifa kuwa chama cha kijijini kwa ajili ya kukishinda kiti cha ubunge cha Gatundu

Mwanasiasa mwingine kutoka mkoa wa Bonde la Ufa kwa jina Jonathan Kipchumba aliudhalilisha msimamo wake Uhuru Kenyatta wa kumuunga mkono rais mstaafu Mwai Kibaki akidai kuwa serikali ya Kibaki iliwafurusha kutoka kwenye ardhi yao, ikawafuta kazi wana wao kutoka utumishi wa umma na kuwafanya kuwa watu wa daraja la pili (*The Standard 20th September 2007*), *(194).*

*The Kibaki government evicted us from our land, sacked our sons and daughters from the civil service and treated us like second class citizen*

Serikali ya Kibaki ilitufukuza kutoka kwa mashamba yetu, ikawafuta wavulana na wasichana wetu kutoka kwa kazi zao serikalini na kutufanya kama wananchi wa daraja la pili

Kutokana na kusutwa kama huko, mwanasiasa huyo alijikuta katika mkono mbaya wa wakereketwa wa chama cha KANU ambao pamoja na mwanasiasa Raila walipata fursa ya kuzuka na tetesi kuwa kulikuwa na mpango wa Uhuru kumrithi Mwai Kibaki na hivyo kupelekea kuibuka kwa usemi wa kuyapuuzilia mbali madai ya mwanasiasa huyo (Raila). Kwenye gazeti la *Daily Nation* tarehe *3rd December 2007* mheshimiwa Uhuru Kenyatta alinukuliwa akisema:

*(177)*

*Kenya is not anyone's firm and the Presidency is not a clan affair. It is Kenyans to decide.*

Kenya si shirika la mtu yeyote na Urais si shughuli ya kimbari; ni jukumu la Wakenya kuamua.

Hapa usemi wa kuyapuuzilia mbali madai unaibuka katika usemi wa mwanasiasa huyo katika kampeni za urais ambapo wapigaji kura waliokuwa wakiisawiri picha hasi kuuhusu msimamo wake walikuwa wakishawishiwa kutokubali madai hayo.

Kama njia moja ya kuhakikisha kuwa mwanasiasa huyo (Uhuru) alikuwa anaungwa mkono na wakereketwa wa chama cha KANU; Uhuru Kenyatta aliutumia usemi wa kushawishi kwa kuonyesha ukweli (kulingana na madai yake) uliokuwa umefichika kwa wakereketwa wa chama cha KANU ambao waliubeza msimamo wake na kuuona kama njia ya kukisambaratisha chama hicho kilichokuwa na historia ndefu. Katika gazeti la *Sunday Standard 28$^{th}$ October 2007* mwanasiasa huyo aliwaeleza wafuasi wa chama cha KANU kuwa njia iliyokuwa fupi ya chama hicho kurejea mamlakani ilikuwa kukiunga chama cha PNU mkono kwani ikiwa Raila angeshinda kulikuwa na uwezekano wake kusalia mamlakani kwa miaka 10 na kuwa alikuwa na watu wake. Katika gazeti la *Daily Nation 20$^{th}$ September 2007* Uhuru Kenyatta alinukuliwa akiwashawishi wakereketwa wa chama cha KANU kuuona ukweli kuwa rais mstaafu Mwai Kibaki alikuwa amesalia na kipindi kimoja cha kuiongoza nchi ya Kenya; kipindi ambacho ingekuwa wakati mzuri wa KANU kujipanga upya na kukinyakua kiti hicho cha urais. Kauli hiyo inasawiri picha mufti ya upinzani uliokuwa umemsibu mwanasiasa huyo na hivyo kumfanya autumie muda mwingi kuwarai wakaazi wa Mkoa wa Bonde la Ufa katika kampeni za urais katika mwaka wa 2007. Usemi huo ulikuwa shawishivu na kutokana na nguvu iliyokuwa kwenye usemi wenyewe ingekuwa njia ya kuijenga imani kwa wafuasi wa chama hicho. Kwa mujibu wa usemi huo imani ingeweza kujengeka na kuibua kutumiwa kwa usemi tumainishi katika kampeni za mwanasiasa huyo.

*(195)*

*President Kibaki will be making his final lap during which time Kanu will have reorgnized itself to recapture power in 2012*

Rais Kibaki atakuwa akikiwania kiti cha urais kipindi chake cha mwisho ambapo wakati huo Kanu itakuwa imejiandaa kukitwaa tena kiti hicho mwaka wa 2012

Kuibuka kwa usemi wa kihistoria kuliweza kudhihirika katika kampeni za mwanasiasa huyo alipokosa kuuafiki mtazamo wa wapinzani wake alipoamua kumuunga mkono rais mstaafu Mwai Kibaki. Mwanasiasa huyo alikuwa ameambiwa na wapinzani wake kuwa uamuzi wake ulikuwa wa kibinafsi na kuwa alikuwa akidhamiria kuteuliwa kuwa naibu wa rais. Mwanasiasa huyo alidokeza kuwa jambo hilo halingeweza kutekelezeka nchini Kenya na kama lingewezekana, Hayati babake Jomo Kenyatta angemrithisha Mkikuyu urais, vilevile rais mstaafu Moi angeweza kufanya vivyo hivyo kwa Mkalenjin mwenzake. Hapa, ilitokea kudhihirika wazi kuwa usemi wa kihistoria ulitumiwa kuidhalilisha mitazamo iliyokuwa ikitumiwa na wanasiasa wa muungano wa ODM kuivutia ngozi kwao. Usemi huo wa kihistoria ulikuwa na umuhimu mkubwa katika kampeni zilizokuwa zinalenga kukiaka chama cha PNU kwani kihistoria ukweli ulikuwa bayana na matokeo yake kuyajenga matumaini; hivyo basi kuzalika kwa usemi tumainishi.

Usemi wa kikabila uliibuka katika kampeni za mwaka wa 2007 kwani katika harakati zake za kuhakikisha kuwa rais mstaafu Kibaki angeungwa mkono, mwanasiasa huyo alinukuliwa akiinasihi jamii ya Kikuyu kuwa hawakuwa na jingine ila kuhakikisha kuwa kura zao zote zingeingia katika kikapu kimoja wakati wa uchaguzi mkuu. Hayo aliyasema alipokuwa ameyahudhuria maziko huko Muranga katika Mkoa wa Kati. Huu ulikuwa usemi wa kikabila ambao dhamira yake ilikuwa kuishawishi jamii ya Mkoa wa Kati *(The Standard 8th September 2007), (196).*

*I appeal that we vote as a bloc and make sure that we turn out in large numbers during the election day*

Ninawasihi kuwa tupige kura kama jumuiya na tuhakikishe kuwa tumejitokeza kwa wingi siku ya uchaguzi

Aidha, usemi wa kihistoria ulizaa usemi wa kitabaka ambapo Mwanasiasa huyo alinukuliwa akihoji msimamo wa Raila Odinga kuwa ulikuwa na dosari kwa kutouona ukweli ambao ulikuwa ni bayana ikiwa uongozi wa nchi ya Kenya wa hapo awali ungerejelewa. Katika gazeti la *Daily Nation 27th January 2013* Uhuru Kenyatta alimsuta

Raila Odinga kwa kujitwika jukumu la kumlaumu kila wakati akiurejelea uongozi wa hayati Mzee Jomo Kenyatta na kuhoji kuwa katika uongozi huo babake Raila Odinga, hayati Jaramogi Oginga alikuwa makamu wa rais.

*(178)*

*...Raila keeps blaming me over my father Jomo Kenyatta's administration. Wasn't his father a Vice President in that government?*

... Raila anaendelea kunilaumu kutokana na uongozi wa babangu Jomo Kenyatta. Kwani babake hakuwa Naibu wa Rais katika serikali hiyo?

Katika nukuu hiyo kunaibuka topoi kadhaa, 'lawama' na 'familia za kifalme'; Topoi kuhusu lawama inaashiria kuwa ikiwa uongozi wa awali ulikuwa ukitumiwa na Raila kumchafua Uhuru Kenyatta, basi lawama hiyo ingetakikana kuwaangukia wote wawili kwani wote walikuwa wana wa viongozi wa hapo awali; wana wa familia za kifalme. Uhuru Kenyatta aliitumia topoi ya lawama kama njia moja ya kumtahadharisha Raila Odinga kukumbuka kuwa historia ya uongozi wa awali ilikuwa hai na kuwa, 'Mchezea mavi hayaachi kumrukia'. Kwa mujibu wa nukuu hii Uhuru alikuwa akiwatahadharisha wananchi wa nchi ya Kenya wamtazame Raila kwa jicho la upembuzi na wangetokea kumwona kama kiongozi aliyekuwa ameficha chembechembe za unafiki ndani yake.

Katika gazeti la *Sunday Nation* tarehe *16th February 2014* ukurasa wa 18, Cheeseman alizungumzia hali ya Taifa la Kenya baada ya uchaguzi mkuu tatanishi wa mwaka wa 2013 alipozirejelea harakati za kuipogoa taharuki ya kikabila iliyokuwapo; harakati aliyosema kuwa ilihusiana na Masimulizi ya Amani yaliyoharamisha shughuli zote za kisiasa zilizofikiriwa kuwa zingeibua mihemko na kuchangia kudorora kwa usalama. Msomi huyo aliangazia kuwa muungano wa Jubilee uliweza kuyatumia masimulizi hayo kama njia moja ya kujikidhia haja yake na kusema kuwa amani ilikuwa jambo la kimsingi na ambalo kila mtu alibidiwa ajitwike mzigo katika kuhakikisha kuwa amani ingezingatiwa kwa vyovyote vile. Muungano wa Jubilee ulizungumzia dhidi ya kuandaliwa maandamano, jambo ambalo lilichangia kufifisha tukio la mgombeaji wa kiti hicho cha urais kuandaa maandamano ikizingatiwa kuwa katika mwaka wa 2007 kulikuwa na usemi mwingi kwenye vinywa vya wanasiasa jambo lililosemekana kuchangia kuibuka kwa machafuko ya kikabila.

*(197)*

*…the resulting consensus around the importance of peace was both understandable and, to an extent, desirable. But the Jubilee alliance was also able to manipulate the peace narratives to serve its own interests. By arguing that peace should be prioratised at all costs, Jubilee leaders delegitimized public protests, which effectively made it harder for losing candidates to contest the results…*

…umuhimu wa matokeo ya makubaliano kuhusu amani kwa jumla yalieleweka, na kwa kiwango kikubwa yalihitajiwa. Lakini, Muungano wa Jubilee pia uliweza kutumia kwa werevu usemi wa amani kama nyenzo ya kufanikishia ajenda yao. Kwa kusema kuwa ilikuwa ni sharti amani ipewe nafasi ya mbele kwa vyovyote vile, viongozi wa jubilee walikuwa wameharamisha maandamano ya umma, kwani usemi huo wa amani ulifanikisha na kuifanya nafasi ya mgombeaji wa kiti katika uchaguzi kutokuwa na msukumo wa kupinga matokeo…

Katika mwaka wa 2013 kulizuka matumizi mengi ya usemi wa amani katika kampeni za urais ambapo Uhuru Kenyatta aliutumia usemi wa amani kama njia moja ya kujenga matumaini na kuushawishi umma kuwa kwenye mstari wa mbele kuyatinga mawazo yoyote ambayo yangeweza kukolezwa na wanasiasa na kupelekea kuzuka kwa uhasama baina ya jamii tofauti nchini Kenya. Katika gazeti la *The Standard* tarehe *28$^{th}$ January 2013* mwanasiasa huyo alinukuliwa akihubiri amani; usemi ambao lengo lake kwa mujibu wa mwanasiasa huyo uliazimiwa kuuashiria muungano wao kama njia mjarabu ya kuleta ushirikiano na utangamano katika jamii zote nchini Kenya.

*(179)*

*Jubilee is a year of reconciliation and we stand for that. CORD is looking at the rear view mirror and promoting tribalism and hatred. Tribalism will not bring ugali on the table.*

Jubilee ni mwaka wa kupatanisha watu na sisi tunasimamia hilo. CORD wanatumia kioo cha nyuma cha gari na kuzidisha chuki na ukabila. Ukabila hautaweka ugali kwenye meza.

Mwanasiasa huyo alikuwa na jumbe nyingi za maridhiano katika usemi wake uliolenga kuishawishi jamii kutokumbushwa vile jana yao ilivyokuwa na badala yake wajenge matumaini katika kesho yao ambayo ilikuwa ikitabiriwa kuwa safi na ambayo ingebeba ufanisi iwapo matukio ya miaka tangulizi hayangetazamwa kwa jicho la ukabila. Kwenye gazeti la *The Standard 3rd December 2012* mwanasiasa huyo alinukuliwa akikumbusha kuwa muungano wa Jubilee ulikuwa kiashiria aula cha kudhihirisha wakati wa jamii zote nchini Kenya kuishi kwa amani ulikuwa umefika kwani Muungano huo ulikuwa na ajenda moja; ile ya kuwaunganisha watu wote.

> *(180)*
>
> *Our Alliance is to unite all Kenyans so that we live in peace. It is an alliance that unites all.*
>
> Muungano wetu ni wa kuwaunganisha Wakenya wote ili tuishi kwa amani; ni muungano ambao unawaunganisha watu wote.

Kwa ufupi, usemi wa amani ulizitawala kampeni za muungano wa Jubilee ulioongozwa na mwanasiasa huyo. Usemi wa amani uliazimiwa kulisawiri kundi hilo kama kundi lililokuwa likiongozwa na utu na mbeko za utaifa ambapo dhamira yao ikiwa ilikuwa kuwapatanisha wananchi. Usemi huo wa amani ulichochewa na ukweli kuwa jamii mbili hasimu zilikuwa zimekutanishwa na majaaliwa kwani ndizo zilikuwa zikihusika katika uhasama kila baada ya miaka mitano kwenye uchaguzi nchini Kenya. Nukuu yake kiongozi wa mrengo wa Jubilee ilibeba topoi za amani, tukio lililodhihirisha kuwa usemi wa amani ulishuhudiwa katika kampeni zake.

Kulingana na Cheeseman kama ilivyodhihirika katika maelezo yake (*Sunday Nation 16th February 2014. Page 18-19*) ilikuwa kwamba; kuzinduliwa kwa katiba mpya kulichangia kwa kiwango kikubwa kufifiza uwezekano wa kutokea kwa mapigano ya kikabila kwani mabadiliko ya kidemokrasia yalitazamwa kuwa yangetokea kumpendelea Raila Odinga na muungano wa CORD kwa jumla.

> *(198)*
>
> *The third reason that the elections were peaceful despite being of poor quality relates to the passing of the new constitution in 2010. While the*

*peace narrative was widely understood to constrain Mr Odinga, many Kenyans believed that the new constitution would empower him.*

Sababu ya tatu iliyoufanya uchaguzi kuwa wa amani hata kama kusimamiwa kwake kulikuwa kwa kiwango duni ni kuzinduliwa kwa katiba mpya katika mwaka wa 2010. Huku usemi wa amani ukiwa ulieleweka kuwa ulimzuia Bwana Odinga, Wakenya wengi waliamini kuwa katiba mpya ingempa uwezo.

Uhuru Kenyatta aliirejelea katiba kwa kusema kuwa hilo lilikuwa jambo zuri lililokuwa limetokea nchini Kenya kwani kuzinduliwa kwa katiba hiyo ilikuwa njia moja ya kuhakikisha kuwa nguvu nyingi walizokuwa nazo maofisa wa serikali pamwe na rais wa nchi ya Kenya zilikuwa zimefifizwa. Kubadilishwa kwa katiba kulipelekea kuibuka kwa usemi tumainishi kutokana na kujikita kwake kwenye haja ya sheria kuzingatiwa. Mwanasiasa huyo aliangazia kuwa kiongozi wa kiimla hakuwa na nafasi katika uongozi wa nchi ya Kenya. Kwenye gazeti la *The Standard 19th November 2012* nukuu yake mwanasiasa huyo ilidhamiriwa kutumainisha na hivyo kutokea kuwa nyenzo bora ya kuwashawishi wananchi nchini Kenya.

*(181)*

*Today the President must listen to the people, the Judiciary and Parliament.*

Rais wa leo ni lazima awasikilize wananchi, Idara ya Mahakama na Bunge.

Kuibuka kwa mijadala kuhusu mahakama ya Hague na kushtakiwa kwa Uhuru Kenyatta na William Ruto kwa makosa ya Jinai kulipelekea kuchipuza kwa usemi wa 'kusingiziwa' kwa wanasiasa hao wawili kwa kutuhumiwa kuhusika katika machafuko ya kikabila baada ya uchaguzi wa 2007. Makabila mawili yaliyojulikana kuwa hasimu hasa kila kulipokuwa na uchaguzi yalitambuliwa kuwa Kikuyu na Kalenjin na hivyo basi kuungana kwao wanasiasa hao kulichangia kuibuka kwa usemi tangamanishi baina ya makabila hayo. Topoi kuhusiana na Mahakama ya Hague iliisawiri picha kuwa viongozi wa Jubilee walikuwa wakisingiziwa kuwa waliyachongea machafuko kuibuka. Nukuu nyingi za mwanasiasa huyo ziliibua na kuchochea hisia za imani kutoka kwa wananchi wa makabila ya Kikuyu na Kalenjin hivi kwamba usemi wake Uhuru Kenyatta kwenye gazeti la *Daily*

*Nation* tarehe *10th February 2013;* uliibua picha ya mtu mnyonge aliyesingiziwa jambo alilokuwa halijui kichwa wala mkia wake.

*(182)*

*They brought those charges against us and we are determined to prove that we are innocent and ready to lead this nation to prosperity.*

Walitusingizia makosa na tumeazimia kudhihirisha kuwa sisi hatuna makosa na tuko tayari kuliongoza taifa hili na kuufikia ufanisi.

Kwenye nukuu hiyo kuliibuka topoi ya 'uonevu', 'uajibikaji' na 'uhakika'. Kulingana na topoi uonevu picha inayojisawiri hapa ilikuwa wazi (kulingana na usemi wake Uhuru) kuwa mwanasiasa huyo alikuwa ametuhumiwa makosa ambayo yeye alikuwa hana habari nayo. Topoi ya 'uwajibikaji' ilijitokeza pale mwanasiasa huyo alipodokeza kuwa hata kama walikuwa wamesingiziwa wao walikuwa radhi kushirikiana na mahakama ya Hague hadi haki itendeke. Topoi ya 'uhakika' iliweza kuonekana kupitia matumaini aliyoonyesha kwa kutaja kuwa hata kama kulikuwa na mashtaka ya kusingiziwa wao walikuwa na uhakika kuwa wangeweza kushinda na kuiendesha nchi ya Kenya na kufikia kiwango cha juu cha ufanisi.

Kutokana na maelezo hayo ni dhahiri kutaja kuwa usemi wake mwanasiasa huyo kwa mujibu wa nukuu yake ulikuwa shawishivu kutokana na dai lake kuwa kulikuwa na uonevu na kuwa wao walikuwa tayari kuwajibika. Usemi wowote wa mwanasiasa huyo uliogusia suala la Hague ulikuwa unawashawishi wapigaji kura kutoka kwa jamii mbili zilizokuwa na historia ndefu ya kuhusika katika machafuko ya kikabila kwani waliokuwa wametuhumiwa walikuwa wana wao kindakindaki. Katika gazeti la *Daily Nation* tarehe *12th February 2013* mwanasiasa huyo alinukuliwa akisema kuwa ilikuwa ni haki yake ya kidemokrasia kujiwasilisha na kukigombea kiti cha urais nchini Kenya na ikiwa wananchi wangeamua kumchagua basi hilo lingekuwa dhihirisho kuwa wao walikuwa na imani naye na angeendelea na kazi yake ya urais na kwa upande mwingine aendelee kujishughulisha na kesi hiyo.

*(199)*

*It is my democratic right to present myself to the people of Kenya. If they so chose to elect me, it means they have confidence in me to continue doing my job as president while handling the cases*

Ni haki yangu ya kidemokrasia kujiwasilisha kwa Wakenya. Ikiwa watanichagua, itamaanisha kuwa wanayo imani kwangu kuwa nitaifanya kazi ya urais huku nikiendelea kuzishughulikia kesi

Kulingana naye Cheeseman kwenye gazeti la *Sunday Nation 16th February 2014* Uhuru Kenyatta na William Ruto waliutumia werevu mwingi kuwasawiria wafuasi wao kutoka jamii za Kikuyu na Kalenjin kuona kuwa wanasiasa hao walipelekwa Hague kutokana na njama za mataifa ya kigeni. Kwenye kampeni zao usemi wao kuhusu tukio hilo ulikaririwa na kutokea kupiga mwangwi kwenye masikio ya jamii hizo; hili lilichangia kuisawiri picha moja maridhawa ya kuwapo kwa 'adui mmoja' na hivyo basi kuwafanya wafuasi wao kukosa kutererka. Cheeseman alidokeza kuwa hata kama jamii hizo zilisalia kwenye muungano wa Jubilee kutoaminiana na kushukiana kulisalia kuwa suala nyeti. Kabla ya uchaguzi kulikuwa na maoni mengi yaliyokuwa yametolewa kuuhusu ushirikiano wa Uhuru na Ruto kutokana na jamii zao kuwa na mitafaruku mingi ya kisiasa kihistoria; swali lilikuwa, baada ya mwaka 2008 wangeizika tofauti yao na kuuwasilisha muungano mmoja imara?

*(200)*

*The elections proved that they could, but only after some very clever politicking by Mr Kenyatta and Mr Ruto, who manipulated the ICC proceedings against them to create a "siege mentality" among their communities. Every statement made by an official of the foreign government was seized upon as evidence that the two were victims of an international conspiracy by "the west".*

Uchaguzi ulidhihirisha kuwa wangeweza, lakini baada tu ya Bwana Kenyatta na Bwana Ruto kuzipiga siasa za werevu, ambao (Uhuru na Ruto) kwa werevu walitumia kuendelea kwa kesi zao za ICC kuijenga dhana ya "kutwaaliwa kwa mawazo" baina ya jamii zao. Waliyatumia maelezo yoyote yaliyotolewa na wakuu wa serikali za kigeni kama ushahidi kuwa

wawili hao walikuwa waadhiriwa wa njama za nchi za kimataifa "kutoka ulaya".

Kama njia moja ya kudhihirisha unyenyekevu, Uhuru Kenyatta kama vile Raila aliutumia mkakati wa utafutaji wa fadhila; Carter na McCarthy (1994) alipouhamisha usemi wake na kuwahutubia wapigaji kura kwa lugha ya jamii yake. Katika gazeti la *Standard* tarehe *1st February 2013* mwanasiasa huyo alinukuliwa baada ya kuwahutubia wakazi wa Gatuzi la Meru akiwaomba wasizigawanye kura zao na badala yake wampigie kura kwani kulingana naye walikuwa wametoka mbali pamoja.

*(183)*

*Oma ya Ngai mutikadige niundu nimui ati tumete haraya.*

Haki ya Mungu msiniache kwa sababu mnajua kuwa tumetoka mbali.

Matumizi ya maneno haki ya Mungu ilikuwa njia ya kutafuta fadhila, usemi uliolenga hatua ya matayarisho; maneno ambayo yalikuwa yakilenga hatua ya pili ambayo kwa mujibu wao Carter na McCarthy (1994) ni kutaja kile msemaji au mtafutaji wa fadhila hutaja ambacho kilikuwa kimefichwa kwenye maneno, *'nimui ati tumete haraya'*. Hatua ya mwisho ambayo ilikuwa ni kuwauliza wapigaji kura katika eneo hilo kufanya hivyo (kumpigia kura) iliachiwa wapigaji kura hao kujijazia na hivyo basi kukosa kuziafikia kanuni za Grice (1975) za ushirikiano.

Kutokana na kuingia ulingoni kwa mara nyingi kwa suala sugu la wizi wa kura mheshimiwa Uhuru Kenyatta kutoka katika muungano wa Jubilee aliamua kuisuta misimamo yake (Raila) alioiona kama iliyopitwa na wakati. Katika nukuu yake kwenye gazeti la *The Standard 18th February 2013* alimwambia Raila ache kusambaza fitina kuwa uchaguzi ungeibwa na badala yake ajitayarishe kukubali kuwa ameshindwa baada ya uchaguzi kwani Wakenya walikuwa na imani na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Kenya. Usemi wake Uhuru ulibeba topoi za 'imani' au 'matumaini' na 'maonyo'. Kwa wafuasi wa Jubilee, usemi wake Uhuru Kenyatta uliweza kuwatia moyo na kuwashawishi kuwa na matarajio chanya. Mwanasiasa huyo aliutumia usemi huo kama njia ya kuuduwaza muungano wa CORD ambao ulikuwa ukilizugumzia suala la wizi wa kura katika kampeni zao za urais kuwa kushindwa wangeshindwa na wangetakiwa kulifanya jambo moja; kukubali kushindwa. Tukio la kuzungumziwa kwa suala hilo katika chaguzi

mbili mtawalia lilidhihirisha kuwa kulikuwapo na kuingiliana kwa matini katika usemi wa kisiasa katika nchi ya Kenya.

*(201)*

*Iam telling Raila to stop spreading rumours that the elections will be rigged and instead prepare to concede defeat because Kenyans have faith in Independence Electoral and Boundaries Commission*

Ninamwambia Raila aache kueneza uvumi kuwa uchaguzi utaibwa na badala yake ajitayarishe kukubali kushindwa kwa kuwa Wakenya wanayo imani na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Kenya

### 5. 9. 3 Athari ya Usemi wa Ruto

Usemi wa William Ruto ulijikita katika mirengo miwili tofauti kutokana na kujihusisha na wagombeaji wawili tofauti katika vipindi hivyo viwili. Katika uchaguzi wa 2007 mwanasiasa huyo alikuwa katika muungano wa ODM na katika uchaguzi wa 2013 alikuwa katika muungano wa Jubilee. Nukuu za usemi wake zilikuwa na athari zilizoegemea itikadi za muungano aliokuwa amejiunga nao katika kila mojawapo wa chaguzi hizo mbili. Kwenye nukuu za mwanasiasa huyo katika mwaka wa 2007 ilikuwa wazi kuwa alikuwa na ajenda moja ya kuudhalilisha muungano wa PNU ambao ulikuwa unasawiriwa kama muungano wa eneo la Mkoa wa Kati na ambao kulingana naye ulikuwa unaongozwa na wazee waliokuwa wameudhamini ukabila. Kaika gazeti la *Daily Nation 18$^{th}$ September 2007* Ruto alisema kuwa wale waliokuwa wakimuunga Kibaki mkono waliwakilisha 'nyuso za zamani' japo Uhuru Kenyatta alikuwa kijana alikuwa ametekwa na mkono wa siasa za kikabila na kukiharibu chama kilichokuwa na historia ndefu nchini Kenya.

*(184)*

*… The paraded supporters of Kibaki represented 'face of the past' although Uhuru Kenyatta was youthful he succumbed to tribal politics and destroyed the oldest party in Kenya.*

Kundi linalomuunga mkono Kibaki linawakilisha "nyuso za zamani", isipokuwa Uhuru Kenyatta ambaye alikuwa kijanakijana lakini alizama katika siasa za ukabila na kukibananga chama cha zamani nchini Kenya.

Usemi huo ulikuwa tahadharishi na shawishivu kwani uliisawiri picha ya 'wazee' waliokuwa yamechoka tiki! Na ambayo hayangeweza kuongoza. Topoi ya 'uzee' ilikuwa inaonyesha kuwa uongozi haungekuwa tofauti na ule wa awali; yaani, wananchi wangeendelea kuumia. Kuwapo kwa Uhuru katika muungano wa PNU kulionekana kama jitihada ya 'wazee' kuendelea kuiongoza nchi ya Kenya kwa misingi ya ukabila. Topoi ya 'uzee' ilitumika kama njia ya kuonyesha wananchi kuwa mabadiliko katika hali zote zao za maisha zingesalia; ufisadi ungekithiri na uongozi kuendelezwa kwa hadaa na dhuluma. Nukuu hii ilikuwa inatumiwa kama mkakati mmoja maridhawa wa kutahadharisha wapigaji kura kuona hatari iliyokuwa kwenye 'upeo wa macho kisiasa' ikiwa 'wazee' hao wangechaguliwa. Usemi huo ulikuwa shawishivu ili kuwafanya wapigaji kura kuona 'giza' ambayo ingelikumba taifa la Kenya, ikiwa hawangeweza kujitokeza na kupiga kura.

Katika kampeni zake akimpigia Raila debe, mwanasiasa huyo aliyarejelea matukio ya hapo awali wakati wa rais mstaafu Moi kuukabidhi uongozi wa urais kwake rais mstaafu Kibaki na kuusababisha usemi wa kihistoria kuibuka ambapo Moi alizomewa na kushushiwa heshima na wafuasi wa muungano wa NARC katika uwanja wa Uhuru Park. Katika gazeti la *Saturday Standard 25$^{th}$ October 2007* nukuu hiyo ya mwanasiasa huyo ilikuwa dhahiri:

> *(185)*
>
> *We will handle Kibaki with dignity unlike the handing-over of power we experienced at Uhuru Park five years ago.*
>
> Tutampa Kibaki heshima wakati wa kukabidhiwa maamlaka kinyume cha vile tulivyoshuhudia katika uwanja wa Uhuru Park.

Usemi wake mwanasiasa huyo ulibeba kumbukizi za hapo awali ambapo topoi ya 'ukosefu wa utu' ilidhihirika; itakumbukwa kuwa hali haikuonyesha mbeko wakati wa kubadilishana uongozi nchini Kenya katika mwaka wa 2002 kwenye uwanja wa Uhuru Park. Ilidaiwa kuwa rais Moi alitupiwa tope na wakereketwa wa muungano wa NARC jambo lililokuwa dhalilishi. Topoi hiyo ilisawiri picha ya uadilifu kwa upande wa muungano wa ODM; yaani wao walikuwa wadhamini wa utu na mbeko katika masuala yote ya uchaguzi. Huo ulikuwa usemi tumainishi ambao ulikuwa unaendana kinyume na tukio la (Moi) kushindwa na muungano wa NARC.

Usemi wa kisiasa katika kampeni za mwanasiasa huyo ulivibeba vishazi tumainishi na shawishivu kwa kiwango kikubwa. Alipokuwa akiyazungumzia majimbo kama suala muhimu la kuhakikisha uchumi wa nchi ya Kenya ungestawi vyema alisema kuwa Majimbo ambayo ODM ilikuwa inayazungumzia yalilenga kuimarisha uchumi wa watu wote kutoka mashinani wala si majimbo ambayo yangewagawanya Wakenya kwa misingi ya ukabila. Alisema kuwa wale waliokuwa wameupuja uchumi wa Kenya ndio waliokuwa wakilipinga suala lote zima la majimbo *Saturday Standard 25th October 2007*.

*(202)*

*The majimbo ODM is talking about is for the economic betterment of people at the grassroot and not one to divide Kenyans along tribal lines. It is those who have imperverished Kenyans who are opposed to majimbo*

Yale majimbo ambayo ODM inayazungumzia ni ya kuinua uchumi wa wananchi mashinani lakini si yale ya kuwagawanya Wakenya kwa misingi ya ukabila. Wale ambayo wamewafilisi Wakenya ndio wanaopinga majimbo

Katika kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2013 usemi wa kihistoria ulichukua nafasi kubwa katika kampeni za mwanasiasa huyo. Usemi mwingi wa kihistoria ulitokea kuwa shawishivu kwa upande mmoja na tahadharishi kwa upande mwingine. Katika gazeti la *Standard 6th November 2012* mwanasiasa huyo alinukuliwa akisema kuwa walimuunga mtu huyo (Raila) mkono katika uchaguzi uliokuwa umepita (2007) lakini walikuwa wakimwambia kwaheri kwa kuwa walikuwa wamesalia katika upinzani kwa miaka kumi kwa sababu ya kauli mbiu yake ya 'Kibaki Tosha'. Alizidi kusema kuwa mtu angetokea kukulaghai mara ya kwanza, yeye angekuwa mwongo, lakini kama angekulaghai kwa mara ya pili, basi wewe ungekuwa nongwe.

Kauli mbiu ya 'Kibaki Tosha' ni topoi iliyouzaa upweke wao (Kalenjin) na kuwafanya kusalia katika upinzani kwa miaka kumi. Kulingana na usemi huo chanzo cha kero zao kama jamii zilifumwa na mtu huyo waliyemuunga mkono katika mwaka wa 2007. Topoi ya 'kulaghai' inasawiri picha ya washiriki katika mkataba fulani waliolaghaiwa na huyo waliyemwona kuwa mtu mwadilifu lakini akawa mwongo; hivyo kuusawiri mkataba kubadilika kuwa kama ule wa nyuki na nyengere ambapo baada ya nyuki kufanya kazi,

nyengere aliingia mzingani na kumfukuzilia mbali nyuki kwa ushuzi wake sugu. Topoi ya uongo inatokea kuisawiri picha kuwa huyo waliyemuunga mkono alikuwa mwongo na kuwa hangeweza kuaminiwa. Mwanasiasa huyo alikuwa ameuafiki ukweli kuwa mshiriki wake alikuwa amewadanganya na kuwa kama wangekubali kudanganywa tena basi wao wangekuwa nongwe au wajinga.

*(203)*

*We supported that man in the last elections but we are now telling him bye. We have been in the opposition for 10 years because of his Kibaki Tosha slogan. If someone cheats you once, he is a liar, but when you are cheated for the second time, you become a fool yourself.*

Sisi ndio tuliomuunga mtu huyo mkono katika uchaguzi uliopita, lakini sasa tunamwambia kwaheri. Tumekuwa nje ya serikali kwa jumla ya miaka 10 kwa sababu ya kauli mbiu yake ya Kibaki Tosha. Mtu akikudanganya mara moja yeye ni mdanganyifu, lakini akikudanganya mara ya pili, wewe utakuwa mpumbavu.

Usemi huo ulikuwa shawishivu kwa jamii nzima ya Kalenjin na Mkoa wote wa Bonde la Ufa kwa jumla. Ungeweza kushawishi wapigaji kura kuwa 'mtu huyo' waliyemuunga mkono alikuwa mwongo na hivyo hawakuwa na budi kumwambaa kama mgonjwa wa ukoma. Usemi huo kwa upande mwingine ulikuwa tahadharishi kwani yeyote yule ambaye alikuwa anadhamiria kusalia katika muungano huo (ODM) hangesema kuwa hakuambiwa, hivyo basi kuchukua mwelekeo wa kuwa usemi tahadharishi. Kwa jumla, usemi wake mwanasiasa huyo ulisheheni majuto – majuto ambayo kulingana naye hayangeweza kurejelewa tena na jamii yake.

Mbali na usemi wa mwanasiasa huyo kuwa shawishivu usemi wake mwingi ulichukua nafasi ya kuwa daraja ya kumuumbulia kiongozi huyo wa CORD katika uchaguzi wa mwaka wa 2013. Uumbuaji huo ungeweza kusimbuliwa na mtu yeyote aliyekuwa na historia ya uchaguzi wa 2007. Topoi ya uongo ilimsawiri mwanasiasa huyo (Raila) kama mtu laghai ambaye hangeweza kuwajibika endapo angejukumishwa urais wa nchi ya Kenya. Usemi wa mwanasiasa huyo kwa mapana na marefu yake ulitokea kutumiwa ukilenga kumuumbua Raila Odinga.

Katika gazeti la *The Standard 7th November 2012* Ruto alinukuliwa akisema kuwa aliyekuwa Waziri Mkuu wa nchi ya Kenya angetakiwa kujua kuwa nchini Kenya kulikuwa na upungufu wa wajinga ambao angewadanganya kuwa yeye (Raila) angeunga mkono mipango ya kubuniwa kwa mahakama ambayo yangezishughulikia kesi zilizokuwa zinawakabili katika Mahakama ya Kimataifa ya Jinai huko Hague. Nukuu yake Ruto ikimlenga Raila ilibeba topoi ya 'furaha kwa upande wa Raila', yaani, haingewezekana Raila kuiafiki mipango kama hiyo kwani kutokana na kesi hiyo kupelekwa Hague muungano wa Jubilee ulikuwa umeduwazwa. Maelezo yake Ruto yalipelekea kuonyesha kuwa msimamo wake Raila ulikolea madanganyo ya upole kwani kulingana na nukuu yake Raila hangeweza kuchangia katika jitihada zozote za kuirejesha kesi hiyo nchini Kenya. Matokeo hayo yangeweza kutumiwa kumuumbulia Raila na hivyo basi kuwa usemi wa kuumbua au kudhalilisha.

*(186)*

*The Prime Minister should know that there is a shortage of foolish people in Kenya whom he can lie to that he would support local trial of ICC cases.*

Lazima Waziri Mkuu ajue kuwa kunao upungufu wa watu wajinga nchini Kenya ambao anaweza kuwadanganya kuwa yeye ataunga mkono kurejeshwa kwa kesi zilizoko katika Mahakama ya Kimataifa ya Jinai nchini Kenya.

Katika kampeni za mwaka wa 2012-2013 mwanasiasa huyo aliwapa wapigaji kura matumaini kuwa wakati huo wangeweza kuibuka na ushindi ikizingatiwa kuwa katika uchaguzi wa mwaka wa 2007 jamii yake ilijikuta katika upinzani baada ya kushindwa na PNU. Usemi huo ulikuwa muhimu kwani kama hilo halingewezekana, basi jamii yake na wote waliokuwa wamekigura chama cha ODM hawangekuwa na msukumo wa kujitokeza na kumuunga mkono katika miondoko yake ya kujiunga na muungano wa Jubilee. Gazeti la *Daily Nation 22nd February 2013* lilimnukuu mwanasiasa huyo akikiri kuwa hawakuwa wakikisia kuhusu ni nani angenyakua uongozi wa nchi ya Kenya kwani ukweli ulikuwa bayana.

*(187)*

*This time Kenyans are not guessing who will succeed President Kibaki because the writing is on the wall.*

Wakati huu Wakenya hawakisiikisii ni nani ambaye atamrithi Rais Kibaki kwa kuwa atakayeutwaa uongozi ni dhahiri.

Mbali na kuwa shawishivu usemi huo ulikuwa tumainishi kwani ulibeba topoi ya 'uhakika'. Uhakika husika katika nukuu hiyo ulikuwa kipengele muhimu cha kuyarejesha matumaini kwa jamii iliyokuwa imekaa nje ya serikali kwa kipindi cha miaka kumi. Topoi husika ya uhakika ilikuwa kama sumaku ya kuzivutia nyoyo zilizokuwa na walakini kumfuata ikikumbukwa kuwa chama kilichokuwa kimezoewa katika Mkoa wa Bonde la Ufa kilikuwa kinajizoazoa ili kuurejesha ubabe wake wa awali chini ya uwenyekiti wa mwanawe rais mstaafu Moi – Gideon Moi.

Usemi mwingine wa kisiasa ulioshamiri katika kampeni za urais nchini Kenya, ulikuwa usemi uliojikita katika mahakama ya Hague, ambapo mwanasiasa huyo pamwe na mshirika wake walikuwa wametuhumiwa kuwa walihusika katika kuzua mapigano nchini Kenya ambapo wananchi wengi walipoteza maisha yao pamoja na mali yao. Usemi huo 'tuhumishi' ulijitokeza katika kampeni za mwanasiasa huyo ambapo aliusawiri kama kusingiziwa na kuzalisha topoi ya 'uonevu'. Kulingana na tetesi za mwanasiasa huyo kesi hiyo ya Hague ilinuiwa na wapinzani wake kuwatenga na umma mkubwa wa nchi ya Kenya na kuwafanya mashabiki katika harakati zote za uchaguzi wa mwaka wa 2013. Kwa yakini, usemi husika ulikuwa shawishivu na jumuishi kwani kushtakiwa kwake kuliisawiri picha ya kushtakiwa kwa jamii nzima ya Kalenjin. Katika gazeti la *The Standard 25th December 2012* nukuu yake ni wazi kulihusu suala la Mahakama ya Hague.

*(188)*

*We want to show the ICC that the allegation that I led the Kalenjin community to fight Kikuyu community and Uhuru did vice versa is not true, we have exhibited this unity.*

Tunataka kuionyesha Mahakama ya Kimataifa ya Jinai kuwa tuhuma kuwa mimi niliiongoza jamii ya Kalenjin kuipiga jamii ya Wakikuyu naye Uhuru akaiongoza jamii yake si ukweli, tumeuonyesha ushirikiano huu.

Topoi ya 'kupuuzilia mbali tuhuma' ni bayana, ambapo dhamira hiyo ilikuwa ikilenga kuonyesha kuwa makabila hayo mawili yalikuwa yamegonganishwa na nguvu kutoka nje na kuwa uhasama uliokuwa ukisemekana kuwa ulikuwapo, ulikuwa haupo kwani walikuwa wakishirikiana. Azma nyingine ya usemi huo ilikuwa kuonyesha ulimwengu

kuwa makabila hayo yalikuwa na umoja, hivyo basi kuizua topoi ya 'ushirikiano' hata kama 'makabila' hayo yalikuwa yamesingiziwa suala zito la makosa ya jinai.

Usemi wa kisiasa katika kampeni za urais mwaka wa 2013 ziliibusha kurejea kwa usemi wa kikabila katika kampeni za mwanasiasa huyo. Ukweli ni kuwa, huo ulikuwa mwangwi wa suala zima la siasa za kikabila ambalo azma yake ilikuwa ni kuhakikisha kura zote za jamii moja hazikuparaganywa visivyostahili. Katika gazeti la *The Standard 11th January 2013* Ruto alinukuliwa akisema kuwa ukweli ulikuwa dhahiri kuwa ushindi ulikuwa wao na kuwa watabiri wa kura za maoni hawakuwa na budi kuuafiki ukweli kuwa nambari ya wapigaji kura huwa haidanganyi. Kuibuka kwa topoi ya 'nambari' ni tukio lililokuwa wazi kwa mujibu wa usemi wa mwanasiasa huyo kwani tukio la vyama vya TNA na URP kuungana kulizua mhemko miongoni mwa vyama vingine vya kisiasa ikizingatiwa kuwa idadi ya wapigaji kura kutoka katika jamii husika ilikuwa kubwa. 'Nambari' kwa hivyo ilikuwa topoi ya kuzirejelea jamii husika katika mikoa yote miwili ule wa Kati na wa Bonde la Ufa; nambari kwa hivyo iliashiria topoi ya ushindi dhidi ya CORD.

> *(204)*
> *The writing is on the wall. The magicians of opinion polls should know that numbers don't lie. We have the numbers to form the next government this year. Our team is focused and we will win the March elections.*
> Maandishi ni wazi kwenye ukuta. Mchawi wa kura ya maoini lazima ajue kuwa nambari hazidanganyi. Tunayo nambari yakutuwezesha kuiunda serikali mwaka huu. Kundi letu linaomwelekeo na tutaushinda uchaguzi wa mwezi wa machi.

Maelezo ya mwanasiasa huyo yalipata msukumo pale aliponukuliwa katika gazeti lilo hilo tarehe *14th January 2013* akisema kuwa Mikoa ya Bonde la Ufa, Kati, Nairobi, Mashariki na Magharibi ilikuwa imeuafikia uamuzi kuwa muungano ulikuwa Jubilee. Aidha, suala lote zima la usemi wa mwanasiasa huyo bila shaka lilizungukia ukabila; jambo ambalo lilikuwa likiegemewa na wanasiasa wote katika kampeni za urais nchini Kenya. Mbali na kushawishi, usemi huo uliaka matumaini kwa wapigaji kura wote wa jamii husika katika mikoa hiyo na kuisawiri picha ya ubabe na kufifiza matumaini ya wapinzani wao. Mkakati

huo ulidhamiriwa kuwavutia wapigaji kura wale waliokuwa bado hawajaamua kuwa wangezipiga kura zao wapi.

> *(205)*
>
> *Rift Valley, Central, Nairobi, Eastern and Western have all decided that it is Jubilee.*
>
> Mikoa ya Bonde la Ufa, Kati, Nairobi, Mashariki na Magharibi wameamua ya kuwa ni Jubilee

Japo utafiti huu haukuwa wa kifasihi, Wamitila (2003:262-263) akiurejelea Uhakiki wa ki-Bakhtin alisema kuwa huu ni uhakiki ambapo mwingiliano wa ki-usemezano au kimazungumzo baina ya sauti mbalimbali hudhihirika. Kulingana na maelezo yake ni wazi kusema kuwa, huwa kuna uhusiano kati ya tamko moja na matamko mengine yaliyotangulia na kuwa matamko yaliyotangulia ndiyo yanayolichochea tamko au matamko ya baadaye. Usemi wake mwanasiasa huyo katika kampeni za mwaka wa 2012-2013 ulijikuta ukiingiliana au kusemezana na kampeni zake za mwaka wa 2007.

Katika kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2013 mwanasiasa huyo alinukuliwa akiwasuta wafuasi wa chama cha KANU kuwa hawangeweza kuutwaa uongozi wa nchi ya Kenya tena na kuwashauri kukiambaa chama hicho na kuunga muungano wa Jubilee mkono. KANU ilichukuliwa kama ‘baba na mama’ na jamii ya Kalenjin wakati rais mstaafu Moi alikuwa akiitawala Kenya na yeyote ambaye angetokea kuzipinga sera za chama hicho alichukuliwa kuwa kibaraka. Kulingana naye KANU iliisawiri picha ya ‘ushinde’- yaani topoi ya ‘unyonge’ ambayo ilikuwa haina matumaini ya kujizoazoa tena na kuiongoza nchi ya Kenya tena *The Standard 21st February 2013), (206)*

> *Let me inform you that Kanu will never take the leadership of this country again, we should abandon it and support Jubilee.*
>
> Acheni niwaambie kuwa Kanu haitaweza kutwaa uongozi wa nchi hii tena, hatuna budi kuachana na chama hicho na tuiunge Jubilee mkono.

Katika uchaguzi wa mwaka wa 2007 mwanasiasa huyo alikuwa mshiriki sugu wa Raila na hivyo basi ngozi aliivuta kuelekea upande huo. Katika kampeni za kipindi hicho Ruto alinukuliwa akiwatahadharisha wafuasi wa KANU kukigura chama hicho kwani kilikuwa

hakiwezi kurejea katika uongozi wa nchi ya Kenya na kuwa wenye chama walikuwa wamerejea *Daily Nation 1st October 2007*, *(55)*

> *We have decided that since the original owners of the party have come back, then it's prudent for us to quit. We shall be making an announcement this week as to our next course of action.*
>
> Tumeamua kuwa, kwa sababu wamiliki asili wa chama hiki wamerudi; ni vizuri sisi tukihame. Kwa hivyo; tutayafanya matangazo yetu kuhusu uamuzi wetu Juma lijalo.

### 5. 9. 4 Hitimisho

Ili kuhitimisha sehemu hii ni vyema kutaja kuwa sehemu hii ilijihusisha na kuangazia athari za usemi wa kisiasa katika kampeni za urais nchini Kenya kwani lengo la tatu la utafiti huu lilizungukia athari za usemi wa kisiasa katika usemi wa wanasiasa Uhuru Kenyatta, Raila Odinga na William Ruto. Mojawapo wa athari zilizoibuka ni kuibuka kwa usemi wa kihistoria uliolengwa na wanasiasa kuashiria kuwa kulikuwa na masuala mengi ya kihistoria ambayo huweza kuwavutia wanasiasa. Usemi wa kikabila ulitokea kukolezwa na wanasiasa kwa kudhalilishana kwa misingi ya jamii nchini Kenya. Mbali na kuibuka kwa usemi wa kuumbuana usemi mwingine ulioibuka ulikuwa na jukumu la kushawishi ambapo matukio tofauti tofauti ya matumizi ya lugha yalitokea kuibuka kwa topoi tofauti tofauti katika usemi wa wanasiasa husika. Sehemu inayofuatia inajishughulisha na muhtasari, hitimisho na mapendekezo ambapo matokeo ya utafiti huu yameelezewa pamwe na rai kuhusu utafiti wa baadaye.

# SURA YA SITA

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 6.1 Utangulizi

Sura hii ya mwisho inaangazia matokeo ya utafiti kuambatana na uchanganuzi wa data kufungamana na vile nadhariatete za utafiti zilivyoafikiwa na mtafiti. Muhtasari na kuhitimishwa kwa utafiti huu kulikitwa kwenye nadhariatete za utafiti kwa mujibu wa matokeo ya utafiti (Rejelea 1. 4). Kufuatia matokeo hayo rai na mapendekezo ya utafiti wa baadaye imetolewa.

## 6. 2. Mada za Usemi kwenye Kampeni za Urais

Itakumbukwa kuwa utafiti huu ulikusudiwa kuangazia usemi tofauti wa kisiasa kwenye kampeni za urais nchini Kenya miezi mitano kabla ya chaguzi za mwaka wa 2007 na 2013. Kutokana na mtazamo huo utafiti huu ulikuwa hauna budi kuangazia mada za usemi zilizoibuka katika kampeni za kiti cha urais kabla ya chaguzi hizo kuu; ule wa mwaka wa 2007 na 2013. Uteuzi wa mada ulitekelezwa na Uhuru Kenyatta, William Ruto na Raila Odinga kulingana na hali za jamii kwa kuegemezwa kwenye matukio ya kihistoria na vile yalivyoiathiri jamii husika na Wakenya kwa jumla. Mada zilizochaguliwa zilikuwa nyenzo muhimu sana katika kufanikishia kukuzwa kwa itikadi za kundi moja dhidi ya kundi jingine kwani mikakati ya kijumla iliyotumiwa kuukuzia usemi wao ilijengeka vizuri chini ya mraba wa itikadi:

- Kusisitiza uzuri wa mambo **Yetu**
- Kusisitiza ubaya wa mambo **Yao**
- Kutosisitiza ubaya wa mambo **Yetu**
- Kutosisitiza uzuri wa mambo **Yao**.

Kulingana na matokeo ya utafiti mikakati hii ya kijumla iliweza kutumiwa katika viwango vyote vya uteuzi wa mada za usemi katika kampeni kwenye mikutano ya kampeni za urais. Kwa hivyo, hotuba za kisiasa, mahojiano, mipango, au propaganda kwa yakini zililenga mada zilizotokea kuzikuza itikadi za muungano au chama 'chetu', kwa kuangazia mazuri ambayo walikuwa wameyafanya au yale wangeyafanya na kuwahusisha wapinzani wao na mada hasi kama vile vita, mapigano, mihadarati, ufisadi, kukosekana

kwa uhuru na mambo mengine mengi; yote hayo yakizungukia matukio (mada) za kihistoria.

Wakati wa kuichanganua data ilibainika kuwa wanasiasa hao waliyazungumzia masuala yaliyokuwa na uwezekano wa kuwashawishi wapigaji kura kwani kimsingi kampeni huwa njia moja ambayo wanasiasa huitumia kuushawishia umma wakiongozwa na mitazamo ya kuyaongea na kuyasisitiza mazuri 'yetu' na kutoyaongea na kuyasisitiza mabaya 'yao'. Kutokana na ithibati hii, utafiti huu ulibainisha kuwa mada ambazo zilikuwa na uwezekano wa kutumiwa kama zana ya kumuumbulia mpizani mmoja dhidi ya mwingine ilitumiwa maradufu, lengo likiwa kumdhalilisha mgombeaji wa kiti hicho cha urais pamwe na wafuasi wake na jamii yake kwa jumla.

Katika mwaka wa 2007 miezi mitano kabla ya uchaguzi mkuu mada zilizozungumziwa kwa kiwango kikubwa zilijumlisha ukabila, wizi wa kura, uwajibikaji, kuzorota kwa uchumi, masuala ya vyama na miungano, majimbo na katiba mpya miongoni mwa masuala mengine. Kimsingi, jambo lililoibuka wakati wa kuziteua mada kulichochewa na wahusika katika ushindani kwani mada zilimlenga mpinzani mmoja dhidi ya mwingine. Wagombeaji wa kiti cha urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2007 walikuwa rais mstaafu Kibaki na Raila, na hivyo basi usemi wa kudhalilishana ulizungukia utawala wa wakati huo; Raila akiulenga 'unyonge' wa Kibaki katika kuyatekeleza majukumu ya nchi ya Kenya na kuzungumzia 'uhodari wake' ikiwa angetunukiwa jukumu la kuwa rais wa Kenya baada ya uchaguzi wa mwaka huo – yaani mwaka wa 2007.

Mshiriki wake Raila (Ruto) katika uchaguzi wa mwaka wa 2007 ambaye nilimteua kama chemichemi ya data katika utafiti huu alikuwa ndio kwanza kakigura chama chake cha KANU na kuwaacha 'wenye' chama chamani kama vile alivyokuwa amenukuliwa; hivyo basi, Ruto aliyazungumzia masuala yayo hayo ambayo yalizungumziwa na Raila kwani ajenda yao ilikuwa moja – ile ya kuudhalilisha muungano wa PNU ambao Mwai Kibaki alikuwa akiutumia kurejea katika uongozi wa nchi ya Kenya na kuwashawishi wapigaji kura hasa wale waliotoka katika jamii zilizokuwa zimekiaka chama cha ODM.

Uhuru Kenyatta katika kampeni za urais za mwaka wa 2007 aliazimia kumuunga rais mustaafu Mwai Kibaki mkono katika jitihada zake za kurejea kwenye uongozi wa nchi ya Kenya. Msimamo wake wa kumuunga mkono Kibaki ulisutwa na washiriki wake Raila kutoka chama cha ODM ambapo Uhuru alisawiriwa kama mmoja wa mawakala wa kukuza ukabila kwani muungano wa PNU ulihusishwa na 'Wazee' kutoka eneo la Mlima Kenya. Kutokana na kusimangwa kwake Uhuru hakuingia siasani zaidi ikiwa data yetu itarejelewa lakini mwanasiasa huyo aliyazungumzia hasa masuala yaliyohusiana na chama cha KANU, rais mustaafu Moi, sababu zake za kumuunga Kibaki mkono, haja ya wapigaji kura katika eneo la mkoa wa Kati kumrejesha Kibaki mamlakani miongoni mwa masuala mengine madogo (Rejelea 4.3.8 na 4.3.9).

Kama vile data katika utafiti huu ilivyobainisha, kampeni za mwaka 2012-2013 kabla ya uchaguzi wa mwaka wa 2013 zilikuwa tofauti ikizingatiwa kuwa kulikuwa na miungano tofauti nchini kama vile, miungano ya CORD, Jubilee, Amani na pia kulikuwa na vyama vingi ambavyo ajenda yao ilikuwa kuutwaa uongozi wa urais wa nchi ya Kenya kama ingewezekana. Kutokana na mabadiliko hayo, mada za usemi zilizojadiliwa zilitofautiana kwa kiasi na zile za mwaka wa 2007 ikizingatiwa kuwa mabadiliko hayo kwa kiasi kikubwa yalikuwa yamesababishwa na matukio tofauti tofauti baada ya uchaguzi huo; pale ambapo suala lilipojikariri ilibainika kuwa suala hilo lilizungumiziwa kwa kiwango kikubwa. Masuala yaliyoingia katika ulingo wa siasa nchini Kenya katika uchaguzi wa mwaka wa 2013 yalikuwa ukabila, ardhi, uwajibikaji, mahakama ya Hague, katiba, suala la umri, wizi wa kura miongoni mwa masuala mengine mengi.

Kubadilika na kwenda kwa matao ya juu kwa masuala yaliyozungumziwa katika kampeni za urais nchini Kenya kulichochewa na kubadilika kwa wagombeaji, miungano, masuala ya kihistoria na masuala mengine ibuka. Masuala yaliyozua mhemko na joto kubwa la kisiasa kwenye kampeni yalikuwa ya ukabila, ardhi na lile suala la mahakama ya Hague. Japo suala la ardhi liligusiwa katika mwaka wa 2007 halikuingia kwenye kampeni kama vile lilivyoingia katika kampeni za mwaka wa 2012-2013. Utafiti huu ulibainisha kuwa huenda Raila Odinga alihofia kujiumbua kutokana na ukweli kuwa William Ruto alikuwa mshiriki wake wa karibu na ambaye alikuwa amelizungumzia suala hilo akiikashifu Tume

ya Ndungu iliyokuwa imepewa jukumu kuliangazia suala hilo la kihistoria na kulitolea mapendekezo (Rejelea 4.3.1).

Kutokana na mtazamo huo, ni bayana kuwa Raila hangeweza kulizungumzia suala hilo kama vile alivyolizungumzia katika kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2013 alipokuwa akinukuliwa karibu katika kila kampeni akilizungumzia (Rejelea 4.3.1). Suala jingine lililoibusha mhemko lilikuwa lile la Mahakama ya Hague lililotumiwa sana na muungano wa CORD na vyama vingine kama nyenzo ya kuzivutia kura kwao kwani wenza hao wawili katika muungano wa Jubilee walikuwa wameshtakiwa kwenye Mahakama ya Jinai ya Hague huko Uholanzi kwa kosa la jinai. Kwa ufupi, mada za usemi zilizoingizwa kwenye kampeni zote zilizungukia masuala nyeti ya kijamii; ambayo yalikuwa ya kihistoria kwa kiwango kikubwa au hata kwa kuibuka, jambo la kimsingi likiwa kuushawishi umma. Imebainika kuwa, ushawishi ni mbinu ya kimakusudi ya kumwathiri mtu ili mtu huyo aweze kuibadilisha misimamo yake, mielekeo na mitazamo yake ili silika yake iafiki kufanya kazi fulani kwa mwongozo wa ncha mbili; ambazo ni 'kujitukuza' na 'kuwadhalilisha' wapinzani kwa upande wa pili.

### 6. 2. 1 Aina ya Mikakati katika Kampeni za Urais

Kati ya malengo ya utafiti kwenye ripoti hii, mojawapo wa malengo hayo lilidhamiriwa kubainisha mikakati ambayo ilitumiwa na wanasiasa katika kampeni za chaguzi zote mbili, uchaguzi wa mwaka wa 2007 na ule wa mwaka wa 2013. Utafiti uliweza kubainisha kuwa wanasiasa waliitumia mikakati mbalimbali kama vile Urejelezi, Uarifishaji, Ubishi, Mkabala, na Uongezaji na Upunguzaji wa Uzito. Mikakati hiyo yote ililenga kuusawiri mtazamo maarufu wa Uwasilishaji Chanya wa 'kundi letu' dhidi ya, Uwasiliswaji Hasi wa 'kundi lao'. Mikakati ambayo ililenga mtazamo wa uwasilishaji chanya ilikuwa nyenzo ya kuisawiria picha chanya ya kundi hilo na mambo yote waliyokuwa wakitekeleza au walikuwa wakidhamiria kuyatekeleza ikiwa wangetokea kuchaguliwa katika uongozi wa Taifa la Kenya. Kwa upande mwingine uwasilishwaji hasi wa kundi lao ulidhamiriwa kutumika kama njia ya kuyapuuzilia mbali madai kutoka kwa kundi pinzani kwa kuyataja kuwa propaganda ya kukipuja chama au muungano wao. Mitazamo yote miwili ilikuwa njia safi ya kuhalalishia sera zao na kuyasawiri makundi hayo mengine kama makundi ambayo hayakuwa na ajenda kwa mwananchi wa kawaida.

Kwa mfano, kutumiwa kwa mkakati wa urejelezi ilikuwa njia safi iliyotumiwa na wanasiasa hao kama nyenzo ya kulidhalilishia kundi moja na kwa upande mwingine kama njia ya kujitukuzia; hivyo kushadidia kuwapo kwa mitazamo ya 'SISI' na 'HAO'.

Mbinu zote hizo kama zilivyotumiwa zilikuwa na lengo moja kuushawishi umma kuziafiki itikadi za muungano mmoja au chama kimoja dhidi ya kingine tofauti ya ushawishi huo ukikitwa dhidi ya mitazamo hiyo ya 'SISI' na 'HAO'. Mkakati kama vile wa ubishi ulizalisha topoi za uonevu, wizi, dhihaka, nambari, uhalifu/mzigo, ufisadi, kutahadharisha, hila, uzalendo, utu, uzee miongoni mwa topoi zingine; japo masuala yaliyokuwa yakiibusha topoi hizo yalikuwa yanalandana, masuala hayo yalisawiri topoi zilizokuwa zikikinzana; jukumu likiwa lile la kuivutia ngozi 'kwetu'. Matumizi ya mkakati huo wa ubishi yanapelekea kuibuka kwa topoi zilizofinyangwa kulifaidi kundi moja na kulifanya kundi lile jingine kubezwa na umma mpana.

### 6. 2. 2 Athari za Usemi wa Wanasiasa kwenye Kampeni

Kwa kuurejelea mtazamo mmoja katika suala la utafiti; mtafiti alisema kuwa haikuwa dhahiri ikiwa wanasiasa wangetokea kuyapunguza makali na uchochezi kwenye usemi wao ikilinganishwa na vile mambo yalivyodaiwa yalikuwa baada ya kutangazwa kwa kura za urais katika mwaka wa 2007. Kutokana na kauli hiyo' kulikuwa na umuhimu mkubwa wa utafiti huo kuangazia athari za usemi kwenye kampeni za urais nchini Kenya. Jambo moja ambalo lilibainika kutokana na utafiti huu ni kuwa uteuzi wa mada tofauti tofauti kwenye kampeni ulizalisha mambo kadhaa kama vile kufufuza usemi wa kihistoria ambao ulidhamiriwa na kundi moja kuimarisha harakati zake za kukitwaa kiti cha urais na kukitweza kikundi fulani kama njia moja ya kufifiza makali yao machoni mwa wapigaji kura. Mbali na kuibuka kwa usemi wa kihistoria, kuliibuka usemi wa kitabaka uliokuwa ukizilenga familia tatu ambazo zilikuwa zimehusika katika uongozi wa nchi ya Kenya. Usemi huo wa kitabaka ulizihusu familia za hayati Mzee Jomo Kenyatta, mstaafu rais Moi na hayati Jaramogi Oginga Odinga; usemi huo ulitumiwa kama njia moja ya kudhalilishana pale kundi moja lilituhumu kuwa Uso wake Hasi ulikuwa umeingiliwa na mwingine (Rejelea 4.3.1 na 5.6). Athari nyingine ya usemi wa kisiasa ilikuwa kuibuka kwa kiwango kikubwa cha matumizi ya usemi wa bibilia, hasa katika kampeni za uchaguzi wa 2013 lengo kuu la usemi huo likiwa kuishawishi jamii ambayo

ingeshawishika kutokea na misimamo mbadala kulihusu kundi moja dhidi ya kundi jingine. Raila Odinga alinukuliwa kwingi akiyarejelea maandiko ya bibilia kama njia moja ya kulidhalilisha kundi la Jubilee na kulisawiri machoni mwa wapigaji kura kama kundi lililoongozwa na viongozi wanafiki ambao walikuwa wakienda kinyume na matarajio ya Kiungu na vile msahafu ulivyohitaji. Kwa jumla, athari ya usemi wa kisiasa ilikuwapo kwani upigaji wa kura katika chaguzi zote mbili ulitendeka kwa misingi ya ukabila ikizingatiwa kuwa viongozi wa miungano yote iliegemea makabila yao. Kwingineko usemi wa kuumbuana ulizalika kwenye kampeni zote, kuumbuana huko kukilenga kuutenga muungano mmoja dhidi ya mwingine kutokana na falsafa ya viongozi katika miungano hiyo. Ni bora kusema kuwa kwenye kampeni za wanasiasa hao kulikuwa na usemi uliowanda kwingi kama vile, usemi tahadharishi, usemi tumainishi, usemi wa kiunafiki, usemi wa kihistoria, usemi wa kitabaka, usemi wa kimbari na kadhalika.

## 6. 3 Hitimisho

Kwa kuyarejelea makisio au tuhuma za utafiti huu; utafiti huu uliweza kubainisha kuwa matumizi ya lugha katika kampeni za urais nchini Kenya hufinyangwa kutokana na mada za usemi. Ilibainika kuwa mada za usemi katika kampeni huwa na umuhimu mkubwa mno kwani mada hizo hugusia matukio ya jamii na kutokana na kuwa jamii hiyo ndiyo hulengwa na wanasiasa, basi kampeni huendana na mada ambazo aghalabu huwa nyeti na ambazo utawala au tawala tangulizi huwa hazijazishughulikia ipasavyo. Uvumbuzi mwingine ulikuwa kwamba, mada za usemi katika kampeni za urais hubadilikabadilika kutokana na masuala kama vile wagombeaji wa kiti hicho kuwa ni akina nani, masuala ya kihistoria yazungukiayo wagombeaji wa kiti hicho ni yapi na masuala ibuka katika uchaguzi huo ni yapi. Kwa jumla ulinganuzi wa usemi wa uchaguzi wa mwaka wa 2007 na ule wa mwaka wa 2013 ulidhihirisha kuwa masuala yazungukiayo uchaguzi si tuli kwani hubadilika kutegemea wahusika, matukio ya kihistoria, masuala ibuka na hali zingine zote ambazo huenda zikawa nyenzo za kuushawishia umma, kwa kujitukuza na kulidhalilisha kundi jingine.

Kama ilivyobainika, wakati wa kampeni za urais wanasiasa walitumia mikakati mbalimbali; mikakati ambayo ilinuiwa kujenga matumaini kwa wapigaji kura ambapo mikakati hiyo ililenga kuwaumbua wapinzani kwa njia ya kuushawishi umma. Mikakati

kama vile Urejelezi, Uarifishaji, Ubishi na Uongezaji na Upunguzaji wa Uzito, ni mikakati ambayo ilitumiwa na wanasiasa kwa kiwango kikubwa mno katika kampeni za chaguzi zote mbili. Kimsingi mikakati hiyo ilifinyangwa na kuzalisha muwala baina ya mada za usemi na mikakati husika.

Tukio la wanasiasa kuziteua mada za usemi kufungamana na itikadi ya vyama na miungano, na kuitumia mikakati mbalimbali wakati wa kampeni za urais kabla ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 na ule wa 2013, kulichongea kuathirika kwa jamii nchini Kenya kwa njia moja au nyingine kutokana na kuwapo kwa mtazamo kuwa, vyama na miungano mbalimbali ya kisiasa iliumbika kwa misingi ya ukabila; hivyo basi, usemi wa wanasiasa ulipelekea kuzalisha usemi wa kikabila ambao ulichochewa na masuala ya kihistoria kuibuka katika kampeni hizo za kiti cha urais. Urais nchini Kenya huchukuliwa kama ishara ya uwezo, sio tu kwa rais achaguliwaye bali pia kwa jamii nzima atokayo rais huyo. Usemi wa kisiasa katika kampeni za urais ulidhihirisha kuwa kiwango cha kuumbuana, kudhalilishana na uchochezi wa kundi moja dhidi ya kundi jingine, huota, humea, hupaliliwa na hata huvunwa nyakati hizo za kampeni za urais nchini Kenya.

Ni vizuri kukumbusha kuwa utafiti huu ulichochewa na masuala yaliyoibuka baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 pale rais mstaafu Mwai Kibaki alipotawazwa kama rais wa nchi ya Kenya; mapigano ambayo yalishuhudiwa yalielekezewa uchaguzi huo na kupelekea kuundwa kwa serikali ya muungano au ya 'nusu mkate' (kama ilivyojulikana), rais akiwa Mwai Kibaki naye Raila Odinga akitengewa kiti cha Waziri Mkuu kilichoundwa baada ya maafikiano ya kuiunda serikali ya muungano. Katika mwaka wa 2008 mabadiliko mengi ya kisheria, kuundwa kwa tume kadhaa zilizochochewa na uchaguzi huo wa mwaka wa 2007, kuingia kwa Mahakama ya Hague nchini Kenya; miongoni mwa matukio mengine kulipelekea kuibua haja ya kuulinganua usemi wa kisiasa miezi mitano kabla ya chaguzi za 2007 na 2013 kwani ilikuwa si dhahiri kuwa wanasiasa wangeweza kuusetiri usemi wao wakati wa kampeni za urais.

Utafiti huu unauafiki mtazamo wake Cheeseman (Rejelea 5.6.1 – 5.6.3) alipoyagusia matokeo ya utafiti uliokuwa umefanywa na ripoti kutolewa kwenye Jarida la Usomi la Afrika Mashariki na kuhoji kama sababu zilizochangia kuifanya Kenya kujizoazoa na kusimama kama taifa baada ya uchaguzi telezi wa mwaka wa 2013 zingelifanya taifa la

Kenya kusimama katika chaguzi za baadaye. Msomi huyo alisema kuwa sababu zilizochangia kuwapo kwa amani nchini Kenya zilikuwa woga wa vita vya kikabila, kuzinduliwa kwa katiba mpya, usemi wa amani, Muungano wa Jubilee na ugatuzi. Kutokana na mtazamo wake Cheeseman ni rai yangu kuwa mabadiliko mengi yaliyoshuhudiwa nchini Kenya baada ya uchaguzi wa 2007 yalichangia mno kuyapogoa makali ya chuki yaliyokuwa yakikuzwa na kuenezwa na wanasiasa; itakumbukwa kuwa Onyango (2008) alikuwa ameufanya utafiti na kubainisha kuwa, jumbe nyingi za chuki na kuumbuana kwa misingi ya ukabila kabla ya uchaguzi wa 2007 zilifanywa sirini. Huenda ikawa kutokana na hofu ya wanasiasa kuchelea kushtakiwa baada ya mabadiliko mengi ya kisheria kutekelezwa nchini Kenya baada ya mapigano ya mwaka wa 2008, pindi tu kura za urais zilipotangazwa – tahadhari ilichukuliwa, lakini zaidi matumaini yaliakika kwenye katiba na matukio mengine kwani viwango vya usemi kwa mujibu wa mada kulitofautiana pakubwa; viwango vya 2007 vilikuwa chini ya vile vya 2013. (Rejelea 4.3 – 4.3-15).

**6. 4 Mapendekezo**

Azimio la utafiti huu lilikuwa kuulinganisha usemi wa kisiasa katika kampeni za urais baina ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 na ule wa 2013, jambo lililochochewa na hali ilivyokuwa katika uchaguzi wa mwaka wa 2008 baada ya kutangazwa kwa kura za urais za mwaka wa 2007. Data ya utafiti huu ilikusanywa kutoka kwa magazeti mawili ya humu nchini; lile la '*Daily Nation'* na '*The Standard'* ambayo mtafiti alitanabahi kuwa, kutokana na ujumbe mwingi ambao hubebwa na magazeti hayo usampulishaji wa data ungeweza kuafikiwa kikamilifu. Ni vizuri kukiri kuwa uenezwaji wa magazeti hayo kwa wasomi huwa wa kiwango cha juu sana tukio ambalo lingeweza kuwafanya wanahabari kuwa na ari ya kuripoti kwa uyakinifu matukio yaliyozihusu kampeni za urais. Kama njia moja ya kuchangia kuwaelewa wanasiasa wakati wa kampeni za urais katika nchi ya Kenya; kuna haja ya kuunasa usemi wao ukiwa hai kwani magazeti ya *'Daily Nation'* na '*The Standard'* huwa yameandikwa kwa lugha ya kiingereza na pia huenda wanahabari huyasafidi magazeti hayo. Ni vyema kutaja kuwa kampeni za kiti cha urais kwa kiwango kikubwa hufanywa kwa lugha ya Kiswahili na kwa kiasi kidogo ile ya kiingereza na ya jamii ya mgombeaji na mwenza wake pale haja inapotokea ya kuhamisha au kuchanganya ndimi.

Kutokana na tukio hilo, ninapendekeza kuwa; kuna haja ya tafiti zingine kufanywa ambapo njia ya kukusanya data itakuwa kwa kuzinasa hotuba za wanasiasa zikiwa hai. Hili huenda likawa tukio bora kwani usemi utakaochanganuliwa utakuwa umenenwa moja kwa moja na wanasiasa husika, na hivyo basi kudhihirisha uasilia. Tena; usemi huo hautakuwa umesafidiwa na waandishi wa magazeti ili kufifiza uchochezi miongoni mwa wananchi kwa jumla. Kwingineko ninapendekeza kuwa utafiti unaweza kulenga kuulinganisha usemi wa mwanasiasa mmoja ambapo upande mmoja utajikita katika usemi wake asilia nao upande wa pili ukijikita katika nukuu zake kwenye magazeti ya humu nchini.

## 6.5 MAREJELEO


Achieng', B. (2007) Interpretation and Implications of Political Discourse: A Kenyan Experience.Unpublished M.A Thesis: Egerton University.

Albertson, B. (2005) Dog-Whistle Politics, Coded Communication and Religious Appeals: *LSO Working Papers in Linguistics 5: Proceedings of WIGL 2005, 124-139.*

Apollos, M. (2001) "Ethnicity, Violence and Democracy," *Africa Development*, Vol. XXVI, no.1&2: 99-144

Asher, R. (1994) *Encyclopaedia of Language and Linguistics*. Vol.6. Oxford: Pergamon Press.

Austin, J.L. (1962) *How to do Things with Words.* Caredon: O.U.P

Bakhtin, M.M. (1986) *Speech Genres and Other Late Essays,* (eds) Emerson, C. and Holquist, M., Austin, University of Texas Press.

Barasa, N. (2014) Discursive Strategies in Kenya's 2008 Post-Election Consultation Discourse. Laikipia University. Nyahururu. Unpublished PhD Thesis.

Blommaert, J. (2005) *Discourse.* Cambridge: Cambridge University Press.

Brown, P. and Levinson, S. (1987) *Politeness*: Some Universals in Language Usage. Cambridge. Cambridge University Press.

Brummett, B. (2008) *Uncovering Hidden Rhetorics: Social Issues in Disguise*. Los Angeles: Sage Publications.

Carter, R. and McCarthy, M. (1994) *Language and Discourse – Perspective for Language Teaching*. New York: Longman Publishers.

Chilton, P. (2004) Analysing Political Discourse: Theory and Practice. London: Routledge.

*Daily Nation* 4th August 2007

*Daily Nation* 19th August 2007

*Daily Nation* 23rd August 2007

*Daily Nation* 17th September 2007

*Daily Nation* 18th September 2007

*Daily Nation* 20th September 2007

*Daily Nation* 23rd September 2007

*Daily Nation* 27rd September 2007

*Daily Nation* 1st October 2007

*Daily Nation* 4th October 2007

*Daily Nation* 9th October 2007

*Daily Nation* 11st October 2007

*Daily Nation* 20th October 2007

*Daily Nation* 23rd October 2007

*Daily Nation* 2nd November 2007

*Daily Nation* 27st November 2007

*Daily Nation* 1st December 2007

*Daily Nation* 3rd December 2007

*Daily Nation* 13rd December 2007

*Daily Nation* 21st December 2007

*Daily Nation* 27th March 2010

Daily Nation 1st October 2012

*Daily Nation* 3rd November 2012

*Daily Nation* 3rd December 2012

*Daily Nation* 1st January 2013

*Daily Nation* 6th January 2013

*Daily Nation* 13th January 2013

*Daily Nation* 27th January 2013

*Daily Nation* 9rd February 2013

*Daily Nation* 10th February 2013

*Daily Nation* 11th February 2013

*Daily Nation* 12th February 2013

*Daily Nation* 19th February 2013

*Daily Nation* 21nd January 2013

*Daily Nation* 24th January 2013

*Daily Nation* 27th January 2013

*Daily Nation* 29th January 2013

*Daily Nation* 31st January 2013

*Daily Nation* 4th February 2013

*Daily Nation* 5th February 2013

*Daily Nation* 6th February 2013

*Daily Nation* 11th February 2013

*Daily Nation* 12th February 2013

*Daily Nation* 13th February 2013

*Daily Nation* 21st February 2013

*Daily Nation* 22nd February 2013

*Daily Nation* 24th February 2013

Doane, A. (2006) *What is Racism? Racial Discourse and Racial Politics*: Critical Sociology, Volume 32, Issue 2 – 3. University of Harford.

Fairclough, N. (1989) *Language and Power*. London: Longman.

Fairclough, N. (1993) "Critical Discourse Analysis and the marketization of public discourse,"*Discourse and Analysis* 4(2): 133-168.

Fairclough, N. (1995) *Critical Discourse Analysis*. London: Longman.

Gal, D. M., Bog, R.W., Gal, P. G. (1996) Educational Research, An Introduction (6th Ed.), New York: Longman Publishers.

Gitonga, A. (1991) The Science of Election Campaigning: How to Win Elections. Nairobi: Cosmopolitan Publishers.

Girnth, H. (1996) "Texte im politischen Diskurs: Ein Vorschlag zur diskursorientierten Beschreibung von Textsorten", *Muttersprache* 106(1): 66-80

Glaser, B. na Strauss, A. L (1967) *The Discovery of Grounded Theory: Strategies for qualitative research*. Chicago: Weidenfeld and Nicolson.

Grice, H. P. (1975) "*Logic and Conversation," Syntax and Semantics 3: Speech Acts*, Cole, P & Morgan, J. L. (Eds), New York: Academic Press.

Gumperz, J. (1982) *Discourse Strategies*. Cambridge: Cambridge University Press.

Habwe, J. (1999). *Political Rally Speeches in Kenya*. Nairobi: University of Nairobi.

Haugerud, A and Njogu, S.K (1991) *State Voices in the Country Side: Politics and the Kenyan Baraza*. African Studies Center, Boston University.

Hordge, R. na Kress, G. (1993) *Language as Ideology* (2nd ed.). London: Routledge.
Irungu, K. (1999) *The Machiavellian Art of Political Manipulation: The Kenyan Experience*. Thika:The House of Hedges.
Johnstone, B. (2008) *Discourse Analysis* 2ed. Australia: Blackwell Publishers.

Jonyo, F. (2003). "The Centrality of Ethnicity in Kenyan Political Transition" Katika Oyugi, W. *The Politics of Transition in Kenya: From KANU to NARC*.NAIROBI: Heinrich Boll Foundation.
Kastellec, J., and Leoni, E. (2007). Using graphs instead of tables in political science. Perspectives on Politics 5, 755-771. https://www.google.com/?gws_rd=ssl#q=using+graphs+instead+of+tables+in+political+science. 27/10/2015. 9.58 pm
Kariithi, F. (2010) Mikakati ya Upole ya Lugha katika Matumizi ya Lugha ya Vijana. Shahada ya Uzamili ambayo Haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Nairobi.
Kienpointner, M. (1992) " Argumentation Illustrated", *International Society for the Study of Argumentation.* Amsterdam: Netherlands.
Kenya National Commission on Human Rights. *On the Brink of the Precipice: A Human Rights Account of Kenya's Post-Election Violence. 15th August 2008.* Nairobi: 2007.23-129
Kimenyi, M. S. (1997) *Ethnic Diversity, Liberty and the State: The African Dilemma*, Cheltenham, Eng: Edward Elgar:
King'ei, K. (2001) "Language, Political Communication and Development" Katika N.Shitemi, N. Mwanakombo na wengine (Whr) *Kiswahili: A tool for Development*. Eldoret: Moi University Press.
KNCHR, Kenya National Commission on Human Rights (2008) *On the Brink of the Precipice: A Human Rights Account of Kenya's Post-Election Violence*. Nairobi: KNCHR.
Kriegler Report (2008) The Independent Review Commission on the General Elections: Nairobi.

***https**://**rescuekenya**.**wordpress.com/2008**/.../kreigler-**report-report**-of-the-...Report* of the Independent Review *Commission* on the General Elections held in Kenya on 27 December 2007

Kristeva, J. (1981) *Desire in Language: A Semiotic Approach to Literature and Art*. Ed. Leon S. Roudiez, Trans. Thomas Gora and Alice Jardine. Oxford: Blackwell.

Leech, G. and Short, M. (1981) *Style in Fiction*. London: Longman.

Leech, G. (1983) *Principles of Pragmatics*. London: Longman.

Lutz, W. (1999) *Doublespeak Defined: Cut through the Bull and Get the Point!* New York: Harper Collins.

Lwaitama, A. F. (1988) *Variations in the Use of Personal Pronouns in the Political Oratory of J.K Nyerere and A.H Mwinyi.* Tanzania: University of Dar es Salaam.

Lwaitama, A. F. (1995) A Critical Language Study of Tanzanian Kiswahili Presidential Political Oratory PhD Thesis. Birminggham: Department of Modern Languages, Aston University in Birminggham U.K.

Lyenger. S & Mcgrady. J. (2007) *Media Politics: A Citizen Guide.* WW Norton & Company: London.

Muigai, G. (1995) "Ethnicity and the Renewal of Competitive Politics in Kenya," in Harvey Glickman, ed.*Ethnic Conflict and Democratization*, Atlanta, GA: The African Studies Association Press161-96.

Murungi, K. (2000) *In The Mud of Politics*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers.

Mutahi, P. (2005) Political violence in the Elections" Katika Maupeu, H na Wenzie. *The MoiSuccession: Elections 2002*. Nairobi: Transafica Press Kenwood House.

Nwadiuto, N. (1999) Educational Research For Modern Scholars. 4$^{th}$ Nigerian Dimension Publishers.

Oduori, R. (2009) "Lugha na Siasa Nchini Kenya: 2005." Tasnifu ya Uzamifu ambayo Haijachapishwa. Eldoret: Chuo Kikuu Moi.

Odhiambo, A. (2004) "ethnicity and the politics of democratization" Katika Berman, B na

Wenzie. *Ethnicity and Democracy in Africa*. Athens: James Currey Ltd.

Onyango, J.O. (2008) *Ethnic Discourse on Contentious Issues in the Kenyan Press after the 2007 General Elections*. Presented at 12th General Assembly, CODESRIA.

Onyango, J.O. (2007) *Ethnolinguistics Vitality and Democratic Practice in Kenya*. A a proposal presented at APISA, CODESRIA and CLACSO summer Institute in Kuala Lumper, Malaysia.

Orodho, A. J (2003) Essentials of Education and Social Science Research Methods. Nairobi: Masola Publishers.

Orvis, S. (2001) "Moral Ethnicity and Political Tribalism in Kenya's 'Virtual Democracy', *African Issues*, 29, No. 1/2: 8-13.

Oyugi, Walter O. "Ethnicity in the Electoral Process: The 1992 General Elections in Kenya," *African Journal of Political Science* 2, no 1 (1997): 41-69.

Patton, M. (1990) Qualitative evaluation and research methods (pp. 169-186). Beverly Hills, CA: Sage. http://legacy.oise.utoronto.ca/research/field-centres/ross/ctl1014/Patton1990.pdf 29/10/2015

Petofi, J. S. (1985) Language as a Written Medium: Text. In N.E. Collinge (ed) *An encyclopaedia of Language*. London: Routledge.

Popitz, H. (1992) *Phanomene der Macht*. Tubingen: Mohr.

Reisigl, M. and Wodak, R. (2001) The discourse- historical approach (DHA): history, agenda theory and methodology. In R. Wodak na M, Meyer (Eds). *Methods of Critical Discourse Analysis* (2ed). London: SAGE.

Reisigl, M. and Wodak, R. (2001) *Discourse and Discrimination; Rhetorics of racism and anti- Semitism*: Routledge. London.

Samuel Kumba. "Five Summoned Over Hate Speech As Peace Broker Starts Mission."

*Saturday Nation* 30th January 2010.

*Saturday Nation* 30th January 2010

*Saturday Standard* 25th October 2007

*Saturday Standard* 11th November 2007

Schiffrin, D. (1994) *Approaches to Discourse Analysis*. Cambridge: Blackwell Publishers.

Stubbs, M. (1983) *Discourse Analysis: The Socio-linguistic Analysis of Natural Language*. Oxford: Blackwell Publishers.

*Sunday Nation* 16th February 2014

*Sunday Standard* 2nd September 2007

*Sunday Standard* 23rd September 2007

*Sunday Standard* 7th October 2007

*Sunday Standard* 20th October 2007

*Sunday Standard* 4th November 2007

*Sunday Standard* 14th November 2007

*Sunday Standard* 11th December 2012

*The Standard* 27th August 2007

*The Standard* 2nd September 2007

*The Standard* 8th September 2007

*The Standard* 17th September 2007

*The Standard* 20th September 2007

*The Standard* 29th September 2007

*The Standard* 4th October 2007

*The Standard* 28th October 2007

*The standard* 7th October 2007

*The standard* 18th October 2007

*The standard* 19th October 2007

*The Standard* 4th November 2007

*The Standard* 11th November 2007

*The Standard* 26th November 2007

*The Standard* 2nd December 2007

*The Standard* 7th December 2007

*The Standard* 8th December 2007

*The Standard* 9th December 2007

*The Standard* 11th December 2007

*The Standard* 13th December 2007

*The Standard* 15th December 2007

*The Standard* 16th December 2007

*The Standard* 19th December 2007

*The Standard* 23rd December 2007

*The Standard* 6th October 2012

*The Standard* 14th October 2012

*The Standard* 30th October 2012

*The Standard* 5th November 2012

*The Standard* 6th November 2012

*The Standard* 7th November 2012

*The Standard* 16th November 2012

*The Standard* 19th November 2012

*The Standard* 1st December 2012

*The Standard* 3rd December 2012

*The Standard* 4th December 2012

*The Standard* 6th December 2012

*The Standard* 9rd December 2012

*The Standard* 10th December 2012

*The Standard* 11th December 2012

*The Standard* 14th December 2012

*The Standard* 15th December 2012

*The Standard* 25th December 2012

*The Standard* 30th December 2012

*The Standard* 2nd January 2013

*The Standard* 11th January 2013

*The Standard* 13th January 2013

*The Standard* 14th January 2013

*The Standard* 15th January 2013

*The Standard* 28th January 2013

*The Standard* 1st February 2013

*The Standard* 4th February 2013

*The Standard* 15th February 2013

*The Standard* 18th February 2013

*The Standard* 19th February 2013

*The Standard* 21st February 2013

*The Standard* 22nd February 2013

*The Standard* 24th February 2013

*The Standard* 25th February 2013

Thibault, P. J. (1994) *Intertextuality*. In R. E. Asher (Ed.), The Encyclopedia of Language and Linguistics, 4. Oxford: Pergamum Press.

Thomson, J. B. (1984) *Studies in The Theory of Ideology.* Cambridge: Polity Press.

van Dijk, T. A. (1987) *Communicating racism: Ethnic prejudice in thought and talk.* Newbury Park, CA: Sage.

van Dijk, T.A. (1997) 'Political discourse and racism: describing others in Western parliaments'. In S.H. Riggins (ed.), *The*

van Dijk, T. A (1997) *Discourse as Social Interaction. Discourse Studies: A Multidisciplinary Introduction* Vol 2. London: Sage.

van Dijk, T. A (1998) *Ideology. A Multidisciplinary Study.* London: Sage.

van Dijk, T. A. (2006) Discourse and Manipulation. *Discourse & Society* 17(3): 359-383

van Dijk, T. A. (2006). Politics, Ideology, and Discourse: Barcelona. Elsevier Ltd.

van Dijk, T. (2008) *Racism at the Top: Parliamentarians Debate on Ethnic Issues in Six*

*European States.* In R. Wodak & T. van Dijk. (Eds): Brava. Wien Town.

Waki Report (2007/2008) Commission of Inquiry into Post-Election Violence (CIPEV): Nairobi.

Wamitila, K (2003) *KAMUSI ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

_________ (2008). *KANZI YA FASIHI Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa.

Weber, M. (1980) *Wirtchaft und Gesellchaft*. 5th edn. Tubingen: Mohr.

Wilson, J. (1990) *Politically Speaking: The Pragmatic Analysis of Political Language.* Oxford: Blackwell Publishers.

Wodak,R. (1996) *Disorders of Discourse*. London: Longman.

Wodak, R. and Meyer, M. (2009) Critical Discourse Analysis: History, Agenda, Theory and Methodology. In R. Wodak and M, Meyer (Eds). *Methods of Critical Discourse Analysis* 2ed. London: SAGE.

Wodak, R. and Reisigl, M. (2008) *Discourse and Recism*: European Perspectives. Annual Review of Anthropology, Vol. 28, (1999), pp 175 – 199.

## CHETI CHA UTAFITI

THIS IS TO CERTIFY THAT:
*MR. KARIITHI FRANCIS MUTURI*
of LAIKIPIA UNIVERSTY, 0-20100
nakuru,has been permitted to conduct
research in *Nakuru County*

on the topic: *ULINGANUZI WA USEMI WA KISIASA KATIKA KAMPEINI ZA URAIS NCHINI KENYA MIEZI MITANO KABLA YA CHAGUZI ZA MWAKA WA 2007 NA 2013*

for the period ending:
*18th October,2015*

Permit No : NACOSTI/P/15/0608/6356
Date Of Issue : 14th July,2015
Fee Recieved :Ksh 2,000



*Applicant's Signature*

*Director General*
*National Commission for Science, Technology & Innovation*